21 MEI, 2026

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Thelathini na Nne — Tarehe 21 Mei, 2026

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:-

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

SPIKA: Katibu.

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Sheila Edward Lukuba. *(Makofi)*

21 MEI, 2026

Na. 400

Ujenzi wa Shule Mpya za Sekondari Mawasiliano na Luhungo

MHE. SHEILA E. LUKUBA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Shule mpya za Sekondari katika Kata za Mawasiliano na Luhungo ili kupunguza msongamano wa wanafunzi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Sheila Edward Lukuba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ina kata 29 ambapo kata 28 zina shule za sekondari isipokuwa kata moja ya Luhungo ambayo haina shule ya sekondari kutokana na changamoto ya kupata eneo linalofaa kwa ajili ya ujenzi wa shule.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2025/2026 Serikali imetenga shilingi milioni 528.99 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya sekondari katika Mtaa wa Mawasiliano uliopo Kata ya Mkundi ili kupunguza msongamano katika shule ya sekondari ya Mkundi Mlimani iliyopo katika Kata ya Mkundi ambayo kwa sasa ina jumla ya wanafunzi 2,228. Ujenzi wa shule hii utawapunguza umbali wa kufuata shule, kwa wanafunzi wanaoishi katika Mtaa wa Mawasiliano na maeneo ya jirani.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha Kata ya Luhungo inapata shule ya sekondari, Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro imeanza kufanya mazungumzo na uongozi wa Jeshi la Wananchi, Kambi ya Mzinga ili kuona uwezekano wa kupata

eneo linalokidhi vigezo kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Kata ya Luhungo, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Lukuba.

MHE. SHEILA E. LUKUBA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninaomba niulize maswali madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tumebakiza mwezi mmoja kukamilisha mwaka wa Serikali wa 2025/2026. Je, lini Serikali itatoa fedha ili kuweza kwenda kujenga shule iliyopo Mtaa wa Mawasiliano?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga mabweni kwenye shule ambazo zimeshajengwa na ambazo zinaendelea kujengwa ili kusaidia wanafunzi hasa wanaotoka maeneo ya mbali? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Sheila Edward Lukuba, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Morogoro kwa namna anavyowasemea na kuwawakilisha vyema sana wananchi wa Mkoa wa Morogoro na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, tayari wiki hii Jumatatu tumeshapeleka *exchequer* ya kupeleka hii shilingi 528,000,000 katika Kata ya Mkundi kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Shule ya Sekondari Mawasiliano. Kwa hiyo, nimhahikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha hiyo itakwenda kabla ya mwisho wa mwezi huu wa Tano ili kazi za ujenzi ziweze kuanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Mpango wa Serikali ni kujenga mabweni kwanza kwenye shule za kidato cha tano na sita kwa sababu zinachukua wanafunzi wa Kitaifa, na pili kwenye shule za *O-level* ambazo zina changamoto za kimazingira. Kwa mfano, kwa maeneo ya wafugaji ambao watoto wanalazimika

kutembea umbali mrefu sana kwenda shule, basi maeneo haya na maeneo mengine yenye sababu za kijiografia, tumekuwa tukitenga fedha kwa ajili ya kujenga mabweni.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kujenga mabweni katika shule zetu na kuhakikisha kwamba watoto wetu wanasoma katika mazingira bora zaidi.

SPIKA: Mheshimiwa Getere.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, toka mwaka 2024 tulikuwa na ujenzi wa Shule ya Sekondari Kurusanga na Mheshimiwa Naibu Waziri alitamka mwenyewe kwamba atawapelekea fedha ya kujenga. Kwa kuwa wananchi wameanza kujenga madarasa matatu sasa hivi, ni lini fedha zitakwenda ili kuwasaidia wananchi kujenga Shule ya Sekondari Kurusanga?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari katika kata ambazo hazina shule za sekondari, na katika kata ambazo wanafunzi wamekuwa wengi kuliko kiasi kinachotakiwa kwa kila shule.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Getere, amefuatilia sana kwa ajili ya ujenzi wa shule hiyo, na pia niwapongeze sana wananchi wa Jimbo la Bunda wakiongozwa na Mheshimiwa Mbunge kwa kuanza ujenzi wa madarasa. Niwahakikishie kwamba katika bajeti zetu tutaweka kipaumbele, kuhakikisha kwamba shule hiyo inapelekewa fedha kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa madarasa na miundombinu mingine. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Kanoni.

MHE. EDIFONSI J. KANONI: Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Ni lini sasa

Serikali itajenga sekondari katika Kata ya Sundu katika Jimbo la Kalambo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kanoni, Mbunge wa Jimbo la Kalambo alishaleta taarifa ya kata ambazo hazina shule za sekondari na kata ambazo shule zake zimekuwa na wanafunzi wengi zaidi kwa ajili ya kutenga bajeti ya kwenda kujenga shule hizo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutafuatilia vigezo vya kata hiyo ili tuweze kuona namna nzuri ya kuanza kutenga bajeti mapema iwezekanavyo kwa ajili ya ujenzi wa shule hiyo ya sekondari katika eneo hilo.

SPIKA: Mheshimiwa Suma.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa swali dogo la nyongeza. Shule ya Sekondari ya Tukuyu Mjini haina bwalo kwa miaka mingi. Ile shule ni kongwe, ina zaidi ya miaka 20, wanafunzi wanakula wakiwa wamesimama na hali ya hewa ya Tukuyu ni mvua na ni baridi kali. Je, ni lini Serikali itajenga bwalo kwa ajili ya Shule ya Tukuyu Sekondari? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, moja ya vipaumbele ambavyo Serikali imeweka katika sekta ya elimu hususan sekondari, ni kuhakikisha kwamba shule zetu zinakuwa na miundombinu muhimu yakiwemo mabwalo ili kuwawezesha watoto kupata chakula katika mazingira bora, nai pia na shughuli nyingine zinazofanyika katika shule zetu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Shule ya Sekondari ya Tukuyu haina bwalo, na ninafahamu kwamba tulishatoa maelekezo kwa Wakurugenzi kuwasilisha maombi kwa ajili ya

ujenzi wa mabwalo katika shule kama hizo. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kumsisitiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kuwasilisha mapema iwezekanavyo maombi ya fedha kwa kadiri ya ramani na *BOQ* iliyoandaliwa ili tuweze kuona namna ya kuanza kutoa fedha hizo kwa awamu, tuanze kujengwa bwalo hilo ili watoto wetu wasome katika mazuri zaidi.

SPIKA: Waheshimiwa, tunaendelea. Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi.

Na. 401

Ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Sandali – Temeke

MHE. MARIAM N. KISANGI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kituo cha Afya katika Kata ya Sandali Jimbo la Temeke?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Jimbo la Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2026/2027 Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, imetenga shilingi bilioni 2.5 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Sandali kwa muundo wa ghorofa. Aidha, wataalamu ngazi ya Mkoa na Manispaa wanakamilisha uandaaji wa michoro na kuwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka kipaumbele cha kukamilisha miradi viporo ya Vituo vya Afya 364 kote nchini ili

viweze kutoa huduma stahiki zikiwemo huduma za dharura za upasuaji, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Kisangi.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaipongeza sana Serikali kwa hatua hiyo na majibu hayo yenye kuridhisha na kuleta matumaini kwa wananchi wa Kata ya Sandali. Ombi langu, ninaomba hayo ambayo yamepangwa au huo mchakato, utekelezwe kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, swali nililonalo sasa, je, kwa kuwa changamoto Kata ya Sandali inayopitia katika Jimbo la Temeke inapitia Kata ya Azimio, na Kata ya Azimio ina wananchi 63,836 kwa mujibu wa sensa, lakini wana zahanati ndogo sana na hawana kituo cha afya, Serikali haioni umuhimu sasa wa kujenga vituo vya afya hasa kwenye maeneo ambayo yana wananchi wengi? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Jimbo la Temeke kwa ufuatiliaji wa dhati kabisa wa ustawi na maendeleo ya Wananchi wa Jimbo la Temeke, na tukuhakikishie tu kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, tutaendelea kukupa ushirikiano kuhakikisha wananchi wa Jimbo la Temeke wananufaika na matunda ya Serikali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, tayari tumeshatenga fedha hii shilingi bilioni 2.5 kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Temeke. Nitumie nafasi hii kurejea kumpongeza Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke, amekuwa Mkurugenzi wa mfano wa kutenga fedha za mapato ya ndani

kwa ajili ya kuboresha huduma katika jamii na wananchi anaowaongoza.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitoa maelekezo mara kwa mara kwamba Wakurugenzi pamoja na fedha za Serikali Kuu watumie pia fedha za mapato ya ndani katika ujenzi wa miundombinu kama zahanati, madarasa na vituo vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Kata hii ya Azimio na maeneo mengine ambayo tutafanya tathmini na kuona vigezo, moja ikiwa idadi ya watu ambayo mmeshaisema inatosheleza; na pili, umbali kutoka kituo cha karibu zaidi ili tuweze aidha kupandisha hadhi ya Zanahati ya Azimio kuwa kituo cha afya kulingana na eneo ambalo litapatikana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, mpongeze na Mkurugenzi wa Ilala. *(Makofi/Kicheko)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, kwa hakika, na siku mbili zilizopita nilimpongeza sana Mkuu wa Wilaya, Mpogolo, na Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Elihuruma, wanafanya kazi nzuri sana ya kutenga fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Dickson Villa.

MHE. DICKSON N. LUTEVELE: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kata ya Isalavanu ni Kata ambayo iko pembezoni sana katika Kata za Halmashauri ya Jimbo la Mafinga Mjini, lakini ndiyo kata pekee kwenye jimbo hili ambayo haina kituo cha afya mpaka leo. Ninaomba kujua Serikali ina mpango gani wa ujenzi wa kituo cha afya kwenye Kata hii ya Isalavanu hasa ukizingatia kwamba wamekidhi vigezo vyote? Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ni kweli Kata ya Isalavanu katika Jimbo la Mafinga Mjini iko pembezoni. Nitumie nafasi hii nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba tutawasiliana na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Mafinga ili wawasilishe rasmi taarifa ya vigezo vya kata hiyo kwa mujibu wa mwongozo wetu; na ikiwa itakidhi vigezo, tutakubaliana kwanza kuanza kutenga mapato ya ndani ya halmashauri kwa awamu, wakati Serikali kuu inatafuta fedha kwa ajili ya kwenda kuunga mkono na kukamilisha ujenzi wa kituo cha afya katika kata hiyo. Ahsante sana.

SPIKA: Ofisi ya Rais, Utumishi, Mheshimiwa Stella Ikupa.

Na. 402

Utekelezaji wa Mwongozo wa Huduma kwa Watumishi wa Umma Wenye Ulemavu

MHE. MARIAM N. KISANGI K.n.y. MHE. STELLA I. ALEX aliuliza:-

Je, Serikali imefikia hatua gani katika kutekeleza Mwongozo wa Ajira na Mazingira ya Kazi kwa Watumishi wenye Ulemavu katika Taasisi za Umma?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma, Toleo la Pili la Mwaka 2008, pamoja na Sheria ya Watu Wenye Ulemavu, Sura ya 183 imeweka masharti kuhusu Ajira na Mazingira ya Kazi kwa Watu wenye Ulemavu katika

Utumishi wa Umma na Sekta Binafsi. Aidha, katika kutekeleza Masharti hayo katika Taasisi za Umma kwa Watumishi wenye Ulemavu, Serikali imepiga hatua mbalimbali zikiwemo:-

(i) Kutunga Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka, 2022;

(ii) Kutunga Kanuni za Uendeshaji wa Shughuli za Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma za Mwaka, 2021; na

(iii) Kuandaa Mwongozo wa Huduma kwa Watumishi wa Umma wenye Ulemavu wa Mwaka, 2008;

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuweka misingi thabiti ya utekelezaji wa Sera, Sheria na Miongozo kuhusu Watumishi wenye ulemavu kwa kutoa elimu, kuhamasisha na kusimamia ujenzi wa miundombinu fikivu na rafiki kwa watu wenye ulemavu katika Utumishi wa Umma ili kuhakikisha mazingira ya kazi yanakuwa salama na wezeshi, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Kisangi.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, na tunaipongeza sana kwa kweli, tumeona jinsi gani wenye ulemavu katika baadhi ya maeneo wanapewa kipaumbele na hata suala zima la miundombinu ya majengo mbalimbali ya Serikali yamezingatia kundi hili maalumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu. Kwa kuwa katika utaratibu wa ajira, hawa wenye ulemavu wanaingia kwenye *interview* ambazo sasa hivi zimewekwa kwa njia mbalimbali ambazo siyo rahisi sana kumtambua mtu mwenye ulemavu, na huyu hana ulemavu, na ukizingatia ulemavu mwingine unatofautiana, je, Serikali imejipanga vipi sasa katika mfumo wa ajira katika utumishi kuwatambua kundi hili la wenye ulemavu? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Spika, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri na muhimu hasa kwa kundi hili la watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka miongozo mbalimbali kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanapata haki sawa kama watu wengine. Kwa kupitia Serikali yetu, chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameweka miongozo mbalimbali kuhakikisha watu wenye ulemavu wanazingatiwa hasa katika mazingira ya ajira.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia hivyo, watu wenye ulemavu wamekuwa wakizingatiwa anapokwenda kwenye usaili, kwanza kupewa usaidizi wa karibu wakati wako kwenye usaili, lakini hata hivyo wamewekewa mazingira rafiki ikiwemo vyumba wanavyoenda kufanyia usaili, vinakuwa rafiki kwao, pia vifaa wanavyotumia kufanyia usaili vinakuwa rafiki kwao, hasa kwa kuzingatia ulemavu wa aina mbalimbali. Kwa hiyo, kwa kutengeneza mazingira hayo, watu hawa wenye ulemavu wamepewa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, hata kwenye mfumo wa ajira, nafasi kubwa imetolewa kwa watu wenye ulemavu wanaposhiriki katika ushindani wa ajira hizi kama ambavyo sera yetu ya menejimenti na ajira katika utumishi wa umma inavyoelekeza kwamba ajira zote zinatolewa kwa ushindani bila ubaguzi. Hivyo, watu wenye ulemavu wamepewa miongozo kuhakikisha kwamba wanapoingia kwenye usaili, basi na kipaumbele wanapewa watu wenye ulemavu hata pale ambapo wanapopata tu zile alama za kuingilia basi kipaumbele watapewa kwanza wale watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninapenda kumhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa mazingira ni rafiki, na yameendelea kuboreshwa siku hadi siku. Vilevile Serikali imeendelea kupitia miongozo ili kuboresha zaidi watu wenye ulemavu wapewe kipaumbele, lakini waweze kushiriki katika usaili, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Viwanda, Mheshimiwa Dkt. Charles Sungura.

Na. 403

Kiwanda cha Kuchakata Nyama na Maziwa – Handeni

MHE. DKT. CHARLES J. SUNGURA aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga viwanda vya kuchakata nyama na maziwa katika Jimbo la Handeni kwa kuwa lina wafugaji wengi wa ng'ombe, mbuzi na kondoo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, ninaomba sasa kujibu swali Na. 403 kama lilivyoulizwa na Mheshimiwa Charles Jacob Sungura Mbunge wa Handeni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Handeni Mjini, kuna Kiwanda kimoja kidogo cha kuchakata na kusindika maziwa kiitwacho *Bin* Maweni *Fully Milk Processing*. Kwa sasa Serikali imeshatenga maeneo kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vingine vya kuchakata mazao ya mifugo. Maeneo hayo ni Kwamagome, Ngugwini na Mabanda. Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta wawekezaji mahiri kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo ikiwemo nyama na maziwa. Ninaomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Sungura.

MHE. DKT. CHARLES J. SUNGURA: Mheshimiwa Spika, ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Kiwanda cha Maziwa cha Tanga *Fresh* ambacho kilikuwa mkombozi mkubwa kwa wananchi wa Handeni pamoja na mkoa wa ujumla, lakini sasa hivi uzalishaji umesimama. Je, Serikali ina

mpango gani sasa kuhakikisha kwamba kiwanda hicho kinarejea katika uzalishaji ili kiwe mkombozi kwa ajili ya wananchi wa Handeni na Mkoa wa Tanga kwa ujumla? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa maeneo ya Segera Kabuku na Kwamgwe katika Jimbo la Handeni yanasifika sana kwa kilimo cha machungwa. Ninaomba kauli ya Serikali, ni lini sasa itajenga kiwanda cha kuchakata machungwa katika maeneo haya kwa sababu 50% ya machungwa yanayolimwa katika maeneo haya yanakuwa yakioza shambani kwa kukosa soko, na pia kwa kukosa viwanda vya kusindika machungwa hayo? Ninashukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, kwanza, nikiri kwamba Mkoa wa Tanga ni moja ya mikoa ambayo imebarikiwa sana kwa mazao ya mifugo. Kuhusiana na Kiwanda cha Tanga *Fresh,* ninaomba nikiri kwamba ni kweli kuna changamoto za kiuendeshaji wa kiwanda hicho. Kiwanda hiki kina uwezo wa kuzalisha maziwa lita 120,000 kwa siku na ndiyo soko kuu na la uhakika kwa ajili ya bidhaa za maziwa kutoka Tanga na mikoa ya jirani.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Serikali, kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Chama cha Ushirika wa Wazalishaji Maziwa Mkoa wa Tanga *(TDCU),* Hazina na Wizara ya Kilimo, wako kwenye mchakato wa kuona namna bora ya kufufua shughuli za kiwanda hiki na kuimarisha uzalishaji wa maziwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali, kupitia Mrajis wa Vyama vya Ushirika, Tume ya Maendeleo ya Ushirika, ameunda timu ambayo inaandaa ripoti na Jumatatu itaiwasilisha ripoti hiyo ili kuona namna bora ya kuimarisha shughuli za uzalishaji na kuzindua ama kuhamasisha shughuli za uzalishaji. Hata hivyo, tunahamasisha sekta binafsi kuendelea kujitokeza kuongeza idadi ya viwanda kwa ajili ya kuongeza thamani ya maziwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la matunda, ni kweli, tathmini imefanywa miongoni mwa mazao ya uhakika mkoani Tanga ama maeneo ya kimkakati ambayo tunaweza tukaweka viwanda pamoja na kuongeza thamani ya bidhaa za nyama na maziwa katika mkoa huo, na pia, bidhaa za matunda katika Wilaya ya Korogwe na Muheza. Hivyo, hamasa inaendelea kwa sekta binafsi kushirikiana na Serikali katika uwekezaji wa kimkakati katika mkoa huu, hasa katika maeneo ya kuongezea thamani mazao ya matunda. Ninaomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Ado.

MHE. ADO S. ADO: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali ilitoa ahadi katika Bunge hili, kupitia swali la msingi nililoliuliza kwamba inao mpango wa kuhakikisha Kiwanda cha Kubangua Korosho Tunduru maarufu kama Kiwanda cha Bias, kitaanza kufanya kazi katika msimu wa mavuno ya korosho wa mwaka huu; na kwa kuwa imebaki miezi michache kwa msimu wa mavuno ya korosho kuanza, ni ipi kauli ya Serikali juu ya hatua iliyofikiwa ili kuhakikisha kwamba ahadi hii inatekelezwa kwa vitendo? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, ni kweli kulikuwa na ahadi ya huyu mwekezaji kuanza uzalishaji wa kubangua korosho katika msimu huu. Tumemwita Wizarani ili atuambie amefikia wapi? Kwa sababu kuna *commitment* ambayo tumeweka na wananchi wanasubiria kule kuona kwamba uzalishaji wa korosho unaendelea, na pia *commitment* yake inaheshimiwa. Ninaomba kuwasilisha.

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa tuendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Abubakar Mohammed Mussa.

Na. 404

Ku-*Print* Vitambulisho vya *NIDA* - Zanzibar

MHE. ABUBAKAR M. MUSSA aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ku-*print* Vitambulisho vya *NIDA* Zanzibar kama ilivyo *Passport* ili kurahisisha upatikanaji wa vitambulisho hivyo kwa Wananchi?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Abubakar Mohammed Mussa, Mbunge wa Jimbo la Mtoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa Vitambulisho vya Taifa nchini hufanyika katika Kituo Kikuu cha Uchakataji wa Taarifa *(Data Centre-DC)* ambapo taarifa zote za usajili na utambuzi wa watu wote waliosajiliwa huchakatwa kwa ajili ya kuzalisha Namba ya Utambulisho *(NIN)* na Vitambulisho. Kituo hicho kina miundombinu mbalimbali ya kuwezesha utambuzi wa mwombaji na ulinganifu wa alama za vidole *(Automated Fingerprint Identification System)* ambao unamtambua kipekee mwombaji wa Kitambulisho cha Taifa.

Mheshimiwa Spika, uchapishaji wa Vitambulisho vya Taifa hufanyika kwa mfumo wa jumla *(Centralized System)* ili kuhakikisha usalama, udhibiti madhubuti wa ubora, pamoja na usimamizi thabiti wa taarifa muhimu za wananchi wanaosajiliwa na kutambuliwa. Uchapishaji wa vitambulisho katika kituo kimoja chenye ulinzi na udhibiti husaidia katika ulinzi wa taarifa za kibayometriki, mifumo ya usimbaji *(encryption)* na vifaa maalum, na hivyo kupunguza hatari ya udanganyifu, uvujaji wa taarifa na au utengenezaji wa vitambulisho bandia *(fraud)*, uwezekano wa kutofautiana kwa ubora wa vitambulisho, pamoja na ongezeko la gharama za uendeshaji kutokana na hitaji la mitambo na rasilimali

watu katika maeneo yatakayoanzishwa vituo. Ninaomba kuwasilisha, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Mussa.

MHE. ABUBAKAR M. MUSSA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza. Nina swali moja tu. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, je, haioni haja sasa kuanzisha kituo kidogo cha ku-*print* vitambulisho hivyo Zanzibar, ambacho kitakuwa na hadhi sawa za kiusalama, kama hicho kilichopo huku Tanzania Bara? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ninamshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Abubakar kwa hoja yake hiyo ya msingi na muhimu. Serikali inaona haja ya kufanya hivyo, lakini inazingatia zaidi dhana ya usalama, udhibiti wa ubora na kuepusha udanganyifu.

Mheshimiwa Spika, hii ni kutokana na umuhimu wa Kitambulisho cha Taifa kwani, Kitambulisho cha Taifa kina utofauti mkubwa na hati ya kusafiria *(passport)*. Kitambulisho cha Taifa ndicho kinacholinda Utanzania na uasili wetu. Kwa hiyo, ni kitu ambacho kiukweli siyo cha kuchezea hata kidogo. Kwa mnasaba huo, pale ambapo haja na hoja itaonekana ya kufanya hivyo, Serikali itafanya hivyo. Ahsante sana.

SPIKA: Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Festo Sanga.

Na. 405

Ujenzi wa Barabara ya Nkenja – Usalimwani, kwa Kiwango cha Changarawe

MHE. REBECA S. NSEMWA K.n.y. MHE. FESTO R. SANGA aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Nkenja – Usalimwani inayounganisha Kata ya Mfumbi na Kitulo kwa kiwango cha changarawe?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa Barabara ya Nkenja – Usalimwani (kilometa 42.7) kwa kiwango cha changarawe unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Hadi sasa matengenezo makubwa yamefanyika katika sehemu korofi za maeneo ya vitongoji vya Nkenja na Ikuwo. Aidha, Serikali imepanga kuendelea na kazi za kuweka changarawe katika maeneo ya mlima yaliyopo Kitongoji cha Usalimwani na maeneo mengine yaliyobaki, ili kuhakikisha barabara hiyo inapitika majira yote ya mwaka, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Rebeca.

MHE. REBECA S. NSEMWA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali. Kwa kuwa, hali ya barabara hiyo kwa sasa ni mbaya sana kutokana na mvua nyingi zilizonyesha, je, ni nini kauli ya Serikali ya kufanya matengenezo ya dharura kwa barabara hiyo, ili wananchi wa Wilaya ya Makete waendelee na shughuli zao za kiuchumi, ukizingatia hao ni wakulima hodari na wafanyabiashara maarufu nchini Tanzania?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Mkandarasi anayejenga Barabara ya Matamba Mjini kilometa moja na meta 800, ameondoka *site* muda mrefu, licha ya kuwa amelipwa fedha zake. Je, ni nini kauli ya Serikali kwa mkandarasi huyo? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ni kweli eneo ilipo barabara hii ni la miinuko na lina mvua nyingi. Barabara hii ndiyo kwanza imepanda hadhi kuja *TANROADS*. Kwa hiyo, tunachofanya, kwanza, ni kuhakikisha kwamba tunaitoa katika hali iliyokuwa na kuileta kwenye viwango vya *TANROADS*. Ndiyo maana tumeamua kwanza kukarabati na kutengeneza yale maeneo korofi ili iweze kupitika, lakini mpango ukiwa ni kuitengeneza barabara yote.

Mheshimiwa Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge na ninatoa maelekezo hapa kwa Meneja wa *TANROADS* kwamba, mvua imepungua sana katika maeneo hayo, aweze sasa kuitembelea hiyo barabara ili yale maeneo yote ambayo yanafanya wananchi wasiweze kupita kwenye hiyo barabara, basi aweze kuyatengeneza kwa sababu, mkandarasi ambaye amepangiwa hiyo kazi, yupo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Barabara ya Matamba – Mjini; kwa kuwa, mkandarasi amelipwa na nina hakika mvua imepungua, Meneja wa Mkoa wa Njombe ahakikishe kwamba, mkandarasi anarudi na kukamilisha hiyo kazi ambayo amepewa na Serikali, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Kapoma.

MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA: Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Wilaya ya Gairo, Mkoani Morogoro, wanashukuru sana kwa kupatiwa Madaraja ya Chakwale na Nguyami yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 24, lakini sasa tuna Daraja dogo sana la Matare ambalo linaunganisha Idibo na kuelekea Kilindi, Tanga na kata nyingi za Gairo, ambalo tumeliomba kwa muda mrefu sana. Ni lini Serikali itatukumbuka kukamilisha ujenzi wa daraja hili? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika mpango wa kutengeneza yale madaraja ambayo yalikuwa changamoto

miaka yote, na yale aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge, ya Chakwale na Nguyami, yamekamilika na sasa wananchi hao wanapita.

Mheshimiwa Spika, hiyo barabara tunavyoongea sasa hivi ipo kwenye mpango wa kusanifiwa, ikiwa ni pamoja na hilo daraja. Ninamwelekeza tu Meneja wa Mkoa wa Morogoro aweze kwenda kwenye hilo eneo, ili wakati tunakamilisha usanifu, basi tuweze kupata mahitaji na kuona uwezekano wa kulitengeneza hilo daraja kwa muda; kwa sababu, madaraja yale makubwa yametengenezwa, basi na hilo tuweze kuliangalia kama linaweza likatengenezwa kwa udharura, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Kija Ntemi.

MHE. KIJA L. NTEMI: Mheshimiwa Spika, ninapenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri swali. Barabara ya kutoka Chibingo kwenda Chigunga kwenda Bukondo iko chini ya *TANROAD,* lakini kwa kiwango cha changarawe. Barabara hiyo ni mbovu sana kwa sasa na wananchi wetu wanapata shida kupita katika ile barabara. Je, kwa kuwa mvua imeisha, nini kauli ya Serikali kwa sasa ili watu wetu waweze kupita vizuri katika ile barabara? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, barabara ambazo ni za changarawe katika kipindi cha mvua huwa zinakuwa na changamoto maeneo mengi, na baada ya mvua kukatika wakandarasi wanarudi *site*. Ninamwelekeza Meneja ahakikishe kwamba hiyo barabara mkandarasi arudi *site* aweze kuitengeneza, na hasa akianza na yale maeneo ambayo yameharibika zaidi ili wakati anatengeneza barabara yote wananchi waendelee na maisha yao ya kawaida, ahsante.

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng'anzi.

Na. 406

Ujenzi wa Barabara ya Makutano ya Kiomomi hadi Mlingano

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara inayoanzia Makutano ya Kiomomi hadi Makutano ya Mlingano – Tanga kwa Kiwango cha lami?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi, kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS),* inaendelea na kazi ya usanifu wa Barabara ya Makutano ya Mlingano – Mjesani – Pande – Kiomomi pamoja na barabara ya Geza – Pongwe – Pande *(Tanga Bypass),* kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Baada ya kazi ya usanifu kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa *Engineer* Ulenge.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Spika, ninaishukuru Serikali walau kwa kuanza usanifu na upembuzi yakinifu wa Barabara ya *Bypass* ya Tanga. Ninayo maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, lengo la ujenzi wa Barabara za *Bypass* ni kuzipunguzia msongamano barabara kuu, sambamba na kuhakikisha barabara zinakuwa katika hali nzuri, je, nini mkakati wa Serikali kumaliza Barabara ya Tanga – Pangani ili kufikia malengo tarajiwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Barabara niliyoitaja ya Tanga – Kiomoni – Mlingano iko *parallel* na Barabara ya Tanga – Segera. Je, ni nini mkakati wa Serikali wa kuipanua Barabara ya Tanga – Segera, ambayo sasa imezidiwa? Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali kukamilisha Barabara ya Tanga – Pangani upo pale pale na unaendelea. Hii barabara inajengwa kwa kiwango cha lami, kilometa 50, ambapo sasa hivi tuko zaidi ya 50%. Ninamhakikishia Mheshimiwa Ng'anzi Ulenge kwamba, hiyo barabara tutaikamilisha ikiwa ni mpango wa kuunganisha Tanga hadi Makurunge (Bagamoyo). Ujenzi unaendelea kwenye *lots* nyingine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Barabara ya Tanga – Segera, tunavyoongea sasa hivi, nadhani hata kwenye bajeti tumeelezea kwamba, tuko kwenye hatua ya kumtafuta mhandisi mshauri ili aweze kuisanifu hiyo barabara tuweze kuipanua, na hasa kufuatia mafanikio makubwa sana ambayo Bandari ya Tanga inayo. Pia, ndiyo inayosababisha kutengeneza *hiyo bypass,* lakini *bypass* hiyo lazima iendane na upanuzi wa Barabara ya kutoka Tanga kwenda Segera, ahsante.

SPIKA: Waheshimiwa tutaendelea na Wizara ya Uchukuzi. Mheshimiwa Bazilio Kapunda Mbwilo.

Na. 407

Kuanza Kazi Meli ya Liemba na Mwongozo

MHE. BAZILIO K. MBWILO aliuliza:-

Je, lini Meli za Liemba na Mwongozo zitaanza tena kutoa huduma ndani ya Ziwa Tanganyika?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Bazilio Kapunda Mbwilo, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Meli za *MV Liemba* na *MV Mwongozo* zitaanza kutoa huduma za usafiri katika Ziwa Tanganyika baada ya ukarabati kukamilika. Kwa sasa ukarabati wa *MV* Liemba unaendelea na upo katika hatua ya ufungwaji wa vifaa muhimu baada ya kupokelewa na inatarajiwa matengenezo hayo kukamilika mwezi Juni, 2026 na kukabidhiwa kwa *TASHICO* mwezi Julai, 2026, kwa ajili kuendelea kutoa huduma za usafirishaji ndani ya Ziwa Tanganyika. Aidha, taratibu za kuanza ukarabati mkubwa wa *MV* Mwongozo unaendelea kukamilishwa ili kuanza matengenezo hayo hivi karibuni.

SPIKA: Mheshimiwa Mbwilo.

MHE. BAZILIO K. MBWILO: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Ninayo maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, ili hizi meli ziweze kujiendesha kwa faida, zinahitaji abiria wa kutosha na kivutio kimojawapo cha abiria kutumia meli hizi, ni pamoja na bandari. Sasa bandari mbili zilizoko ndani ya jimbo langu, Bandari ya Kipili na Kabwe, zote zimezama. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha bandari hizi zinakuwa nzuri ili zivutie watu wengi zaidi kutumia usafiri huu wa meli?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Watu wengi sana wa mwambao wanafanya biashara na nchi jirani ya Congo na husafirisha mizigo, hasa kwa kutumia maboti ambayo yamesababisha vifo vya mara kwa mara kwa hawa wafanyabiashara. Je, Serikali itaweka ratiba ya walau mara mbili kwa mwezi; moja ya hizo meli iweze kwenda Congo, Mji wa Moba na Kalemie, ili wawe salama zaidi? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji na maswali yake ya nyongeza, ambayo ameuliza. La kwanza, ameuliza kuhusiana na upatikanaji wa abiria. Ni kweli, Serikali inatambua kwamba meli hii na nyinginezo ambazo zinajengwa ni kwa ajili ya kusaidia abiria pamoja na mizigo. Kimsingi abiria wapo, na changamoto kubwa, ambayo imeipata nchi yetu kwenye takribani maziwa yote matatu ni kujaa kwa maji.

Mheshimiwa Spika, tayari tupo na mkakati wa muda mfupi ambao tunaendelea nao kupitia *TPA*. Pamoja na mkakati wa muda mrefu wa kuhakikisha kwamba yale maji ambayo yamejaa kwenye Bandari zetu karibu zote kuanzia Kabwe, Kasanga mpaka kule Kigoma zinaweza kuondolewa, kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa kwamba, tunalifanyia kazi jambo hilo kwa lengo la kusaidia wananchi wetu ambao baada ya kutokea maji haya, kwa kweli wanashindwa kusafiri kwenye bandari hizo.

Mheshimiwa Spika, hoja yake ya pili, tuichukue kama ni ushauri. Meli itakapokamilika kupitia mpango wa kibiashara, tutatazama, kupitia *TASHICO,* kuona wapi iende kulingana na uhitaji utakaokuwepo, ikiwa ni pamoja na ushauri wake anaoutoa kwenda kwenye nchi jirani, kupitia Bandari ya Moba, Kalemie, pamoja na maeneo mengine.

SPIKA: Mheshimiwa Arif.

MHE. ARIF S. PREMJI: Mheshimiwa Spika, Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ya 2025/2030 imeainisha ujenzi wa meli katika Mkoa wa Mtwara ambayo itatoa huduma kati ya Mtwara na Comoro. Je, ni lini utekelezaji huu utaanza?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Arif kwa swali lake la ziada ambapo anataka kufahamu mpango wa Serikali hii katika kujenga meli kwenye ukanda wa mwambao, pamoja na Wabunge karibu

wote wanaopakana na Bahari ya Hindi, wamekuwa wakiuliza maswali haya mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa nijibu kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri mpango wa Serikali. Hatua ya kwanza iliyofanyika ni kutaka kufahamu, je, hali ya biashara na mahitaji katika Bahari ya Hindi ikoje?

Mheshimiwa Spika, tayari tumeshakamilisha tathmini hiyo na kwa mwaka wa fedha 2026/2027 na kwa bajeti ambayo imepitishwa hapa, tunakwenda kuanza kujenga meli kwa ajili ya kusafirisha abiria pamoja na mizigo kwenye ukanda wa bahari ikiwa ni pamoja na Mtwara, Tanga pamoja na maeneo jirani kama vile Mombasa, Comoro, Sychelles na maeneo mengine kadri itakavyoonekana inafaa.

SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Mohamed Mussa Utaly.

Na. 408

Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Kiwanja cha Ndege cha Lindi

MHE. MOHAMED M. UTALY aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga na kukarabati miundombinu ya Kiwanja cha Ndege - Lindi ili kukidhi haja ya uwekezaji wa mradi wa kuchakata gesi ya *LNG*?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Mussa Utaly, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Lindi ili kukidhi haja ya uwekezaji wa mradi wa kuchakata gesi kuwa kimiminika (*LNG)* pamoja na

kuchechemua shughuli nyinginezo za kiuchumi na kijamii. Aidha, ujenzi wa kiwanja hicho uliahidiwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kampeni za uchaguzi wa mwaka 2025. Hivyo, ujenzi wa kiwanja hicho ni kipaumbele cha Wizara yetu na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, tayari imeshaingia mkataba na kampuni ya *China Railway Construction Engineering Group* kwa ajili ya ukarabati na maboresho ya kiwanja hicho cha ndege cha Lindi utakaochukua muda wa miezi 24. Ukarabati huo utahusisha ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, barabara ya kiungio, maegesho ya ndege pamoja na maegesho ya magari.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2026/2027. Aidha, Serikali itaendelea kutenga fedha ili kuendeleza kiwanja cha ndege cha Lindi pamoja na viwanja vingine vya ndege vya mikoa kulingana na mpango wa uendelezaji wa viwanja vya ndege nchini Tanzania.

SPIKA: Mheshimiwa Utaly.

MHE. MOHAMED M. UTALY: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Serikali imeingia mkataba na mkandarasi huyu tarehe 22 Julai, 2024 na sasa yapata miezi 15 bado mkandarasi huyu hajalipwa malipo ya awali jambo ambalo limemfanya ashindwe kuanza kazi, je, ni lini Serikali italipa malipo ya awali kwa mkandarasi huyu ili aweze kutekeleza wajibu wake katika kujenga kiwanja hiki?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa Serikali tayari imesaini mkataba wa miezi 24 wa utekelezaji wa ujenzi wa kiwanja hiki, je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kulieleza Bunge hili kwamba ni kiasi gani cha fedha kimetengwa katika bajeti ya mwaka huu 2026/2027 kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa kiwanja hiki cha ndege cha Lindi? Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Mohamed Utaly kwa kufuatilia Uwanja wa Ndege wa Lindi ambao ni muhimu sana na una historia kubwa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kulitambua hilo, ilishafanya hatua mbalimbali sambamba na kumtafuta mkandarasi, kama ambavyo nimezungumza kwenye jibu la msingi, uwanja huu unajengwa kwa zaidi ya shilingi bilioni 120. Kwa hiyo, unaweza kuona jinsi ambavyo Serikali imebeba kwa uzito mkubwa sana uwanja huu wa Lindi.

Mheshimiwa Spika, maswali yake mawili yameuliza, lini na kiasi gani kimetengwa? Kutokana na umuhimu wake katika mwaka huu wa fedha, na bajeti iliyopitishwa hapa, Mheshimiwa Waziri baada ya kupokea maelekezo ya viongozi wakuu, tunafanya maboresho ndani ya bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, awali tulitenga shilingi 3,800,000,000 lakini tayari tunatafuta fedha nyingine karibu shilingi 70,000,000,000 ambazo zitakwenda kwenye maeneo manne. Moja, kwa ajili ya kulipa fedha za malipo ya awali kwa ajili ya uwanja wa ndege wa Mwanza uanze kujengwa kama ambavyo tulisikia wote mjadala unavyoendelea, na pili, ni kwa ajili ya kuhakikisha uwanja wa ndege wa Mtwara ambao tulishapata mkandarasi, na alikuwa hajalipwa fedha za malipo ya awali.

Mheshimiwa Spika, tatu, kuhakikisha uwanja wa ndege wa Lindi ambao tulishapata mkandarasi na hakulipwa fedha za awali na yeye aanze kulipwa mwaka wa fedha unaoanza uanze kujengwa. Nne, kuendeleza kasi ya maandalizi ya ujenzi wa uwanja wa ndege wa Njombe.

Mheshimiwa Spika, hivyo, ninamsihi Mheshimiwa Utaly atupe nafasi, tukishaanza utekelezaji, kazi hii inakwenda kuanza kama ilivyoahidiwa kwenye kampeni na Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule, uliza swali lako.

Na. 409

Mikakati ya kuwasaidia Wahitimu kupata Mitaji ya Uwekezaji

MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia wahitimu wa vyuo kutumia vyeti vyao kama dhamana kupata mikopo ya kuanzisha miradi ya uwekezaji?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninaomba kujibu swali la Dkt. Neema Peter Majule, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, benki na taasisi za fedha hutumia aina mbalimbali za dhamana katika utoaji wa mikopo kwa watu binafsi. Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Sura ya 113, dhamana inayotambuliwa kwa kiwango kikubwa ni ile inayohusiana na mali zisizohamishika hususan ardhi na majengo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mali zinazohamishika Serikali ipo katika hatua za mwisho kuandaa sheria ya dhamana kwa mali zinazohamishika yenye lengo la kutambua rasmi mali hizo kama dhamana katika utoaji wa mikopo. Aidha, mali hizo zinazotarajiwa kusajiliwa kupitia Benki Kuu ya Tanzania ili kuimarisha usimamizi, uwazi na ufuatiliaji wake. Miongoni mwa mali zinazopendekezwa kufanyiwa tathmini ni vyeti vya taaluma vya wahitimu wa vyuo, kwa lengo la kuchunguza uwezekano wa kuvifanya vitumike kama dhamana katika upatikanaji wa mikopo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inaendelea kuwashauri vijana wanaohitimu vyuo kutumia fursa zilizopo kupitia mifuko na

programu mbalimbali zinazosimamiwa na Serikali, mfano mifuko ya vijana ambayo hutoa mikopo yenye riba nafuu ili kuwawezesha kuanzisha na kuendeleza shughuli zao za kiuchumi. Ninaomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Neema.

MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE: Mheshimiwa Spika, nitakuwa maswali mawili ya nyongeza. Vyuo vikuu vingi duniani sasa hivi vinaandaa wahitimu ambao wanaenda kuajiri wengine, yaani wenyewe wanakuwa waajiri ili waajiri wengine; na wameanzisha *Career Development Department* ambayo kazi yake ni kuwa-*groom* hawa wawekezaji vijana ili watakapotoka, wafungue miradi mikubwa kuanzisha miradi na kuajiri wengine.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ya nchi yetu ipo tayari sasa kuanza kubaini wawekezaji wakiwa bado wapo chuoni na kuweza kuwapa mikopo mikubwa ili wakafungue miradi mikubwa na kuweza kuajiri wengine?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Serikali itaanza lini sasa huu mpango wa kutumia vyeti kama dhamana, kwani uwekezaji ni kitu kikubwa, na kinahitaji mtaji mkubwa?

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ipo tayari kutoa mitaji mikubwa ya kuanzisha na kufanya uwekezaji kwa kutumia vyeti, au watahitaji dhamana nyingine? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA): Mheshimiwa Spika, kwanza ninampongeza sana Dkt. Neema kwa uwezo wake mkubwa sana wa kuweza kujenga hoja hapa Bungeni. Pia, ninaendelea kuwashukuru wanawake wa Mkoa wa Dodoma kwa kutuletea mtu kama huyu hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, kwanza ni kweli kabisa Serikali ya Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, imeendelea kuwawezesha vijana kiuchumi na kujiajiri. Mfano mkubwa ni

shilingi bilioni 200 ambazo tayari zimeshatolewa. Pia kupitia asilimia 10 ambazo zinaendelea kutolewa nchi nzima na programu nyingine zinazotoa mikopo kwa vijana kwa riba nafuu kabisa.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba asilimia kubwa ya wanafunzi wanaomaliza vyuo vikuu wanakuwa hawana misingi ya kufanya biashara kubwa na uwekezaji mkubwa, lakini pia wanakuwa hawana elimu ya kufanya uwekezaji mkubwa pamoja na sifa zinazoendana na hizo. Kwa maana hiyo, pamoja na mawazo mazuri ambayo sasa wanakuwa nayo hawa vijana wetu wanaomaliza vyuo vikuu, bado misingi hii hawana.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana sisi kama Serikali, tunashauri ni lazima tuone mwendelezo wa biashara tangu biashara inapokuwa ndogo mpaka inapofikia kuwa kubwa kufanya *investment* ya shilingi milioni zaidi ya 600, shilingi milioni 800 na kuendelea. Kwa maana hiyo, sisi tunashauri kwamba vijana hawa pia lazima tuangalie *trend* ya biashara wanazozifanya na mitaji yao.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana kuna biashara za aina nyingi kidogo hapa, kuna biashara ambazo ni ndogo kabisa ambazo tunaziita ni *micro business* ambazo mtaji wake ni kama zinaanzia shilingi milioni tano ambazo na zenyewe zinaweza kuajiri vijana kuanzia mmoja mpaka wanne.

Mheshimiwa Spika, pia kuna biashara ambazo ni ndogo, *small businesses* ambazo zenyewe zinaanzia mtaji wa shilingi milioni tano mpaka shilingi milioni 200 ambazo zina uwezo wa kuajiri kuanzia vijana watano mpaka vijana 49. Pia tunazo biashara nyingine ambazo ni hizi za kati ambazo mtaji wake ni kuanzia shilingi milioni 200 mpaka shilingi milioni 800 ambazo zinaweza kuajiri vijana kuanzia 50 mpaka 99.

Mheshimiwa Spika, mwisho, tunao wale wafanyabiashara wakubwa ambao na wenyewe wanaanzia mtaji wa shilingi milioni 800 na zaidi ambao wanaweza wakaajiri watu kuanzia 100 na kuendelea. Kwa maana hiyo, vijana hawa ambao wanatoka

vyuo vikuu, hawana misingi mikubwa na elimu ya biashara mpaka kufikia kutoka biashara ndogo kwenda biashara kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi kama Serikali tunaendelea kuwahimiza lazima tuone *trend* ya biashara ya mtu huyu anayetoka chuo kikuu, tumwezeshe kupata elimu ya uwekezaji na namna ya kufanya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunashauri kwamba tutaona *trend* baada ya kumwezesha sasa kuanza biashara ndogo, *micro* mpaka *large,* tuone *trend* ya biashara inaendaje na baada ya hapo, tuko tayari kuwasaidia vijana ambao sasa *trend* yao ya biashara watakuwa wanakua kutoka biashara ndogo kwenda biashara kubwa kupitia taasisi zetu za kifedha. Ninaomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na ninashukuru kwa majibu ambayo Serikali imetoa. Kwa kuwa, tafiti zinaonyesha kuwa zaidi ya 60% ya wahitimu wa vyuo hukosa ajira rasmi na hili ni kundi muhimu sana na kubwa sana kwa jamii, sasa ninataka kujua, Serikali ipo tayari kuanzisha *Graduate Credit Guarantee Scheme* ambao utakuwa ni mfumo utakaowawezesha wahitimu hawa kutumia taaluma zao na vyeti vyao kama dhamana ili waweze kupata mitaji kwa ajili ya kuanzisha biashara na viwanda vidogo vidogo? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA): Mheshimiwa Spika, kwanza niseme Waziri Mkuu ameshatoa tamko hapa na amesema kwamba Serikali bado inaendelea kutengeneza taratibu na miongozo hiyo na ikishakamilika, miongozo na kanuni hizo zitaletwa hapa Bungeni kama Muswada, na sisi kama Wabunge tukishaupitisha maana yake itakuwa ni sheria. Vijana hawa ambao wanatoka vyuo vikuu, vyeti vyao vitatumika kama dhamana kupata mitaji na mikopo kutoka kwenye taasisi zetu za kifedha. Ninaomba kuwasilisha.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha. Sasa ni kipindi cha wageni.

Wageni waliokaa Jukwaa la Spika ni wageni tisa wa Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Msongwe Kasekenya, Naibu Waziri wa Ujenzi, ni familia yake kutoka Jijini Dodoma, ambao ni Ndugu Subilagha Kasekenya, mke wa Mheshimiwa Naibu Waziri; Ndugu Anna Msongwe, dada wa Mheshimiwa Naibu Waziri; Ndugu Lolonce Kasekenya - mtoto wa Mheshimiwa Naibu Waziri; Ndugu Lujeko Kita, shemeji wa Mheshimiwa Naibu Waziri; Ndugu Neema Mtawa, shemeji wa Mheshimiwa Naibu Waziri; Ndugu Peter Mtawa, shemeji wa Mheshimiwa Naibu Waziri; Ndugu Seif Kaduguda, dereva wa Mheshimiwa Naibu Waziri; na Ndugu Boniface Myalla, Katibu wa Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

Pia, yupo mgeni wa Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, Waziri wa Madini, Ndugu Ramadhani Ngoda, ni mtangazaji wa mpira wa *Azam TV* kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibu yupo juu hapa. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge ni wageni watatu wa Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, Waziri wa Ujenzi, wadogo zake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wengine wageni wawili wa Mheshimiwa Deus Clement Sangu ambao ni wapiga kura wake kutoka Kwela Mkoani Rukwa. *(Makofi)*

Pia, wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati kutoka Wilaya ya Ubungo, Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, ambao ni wajasiriamali kutoka Ilala Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunao wageni 13 wa Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera, wanafunzi wa Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini kutoka Jijini Dodoma.

Pia wapo wageni saba wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, ni wanamaombi kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni wanaotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni Maaskofu na Wachungaji 20 kutoka Kanisa la *AICT* Dayosisi ya Kati na wageni wao kutoka Marekani na Makao Makuu Mwanza. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 130 na Walimu Nane kutoka Shule ya Sekondari ya Wavulana Tengeru Jijini Arusha. *(Makofi)*

Wengine ni wanafunzi 90 na Walimu 10 kutoka Shule ya Sekondari ya Wasichana ya *St. Ursula* Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 50 na walimu 10 wa Shule ya Msingi *Mount Camel* kutoka Kata ya Olorieni Jijini Arusha. *(Makofi)*

Tunao wafanyakazi 20 kutoka *Inuka Microfinance Limited* kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa ninamwita Naibu Spika aendelee na ratiba zinazoendelea.

Hapa Naibu Spika (Mhe. Daniel B. Sillo) Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Katibu.

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI

HOJA YA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, na muda wetu ni dakika sita. Kwa hiyo, tutumie vizuri dakika zetu sita.

Waheshimiwa Wabunge, nitaanza na Mheshimiwa Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, atafuatiwa na Mheshimiwa John Stephano Luhende na Mheshimiwa Masanja Kungu Kadogosa, ajiandae.

Mheshimiwa John Stephano Luhende.

MHE. JOHN S. LUHENDE: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Bukene na nitumie muda huu kushukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na uchache wa muda, naomba nijielekeze kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi ukurasa wake wa 90 na ukurasa wa 99, amezungumzia barabara mbili za Jimbo la Bukene ambazo ni barabara ya Nzega – Itobo – Kagongwa na barabara ya kutoka Tabora – Mambali – Bukene – Itobo. Pia ametenga fedha shilingi milioni 800 na shilingi milioni 500 kwa ajili ya maandalizi kuelekea ujenzi wa lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru sana watu wa Bukene, lakini fedha hizo shilingi milioni 800 hazitoshi. Shilingi milioni 500 kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa barabara hizo hazitoshi na hitaji letu kwa sasa wananchi wa Jimbo la Bukene ni barabara ya kutoka Nzega – Itobo – Bukene ili barabara hiyo sasa ikatuunganishe na mradi mama mkubwa wa *SGR* unaoendelea kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Wizara ya Uchukuzi, *SGR* inatarajia kukamilika eneo hilo mwaka 2028. *SGR* hiyo tutaitumia wananchi wa Wilaya ya Nzega na Wilaya ya Igunga ambao Wilaya mbili zote hizo zina Majimbo Matano. Wananchi wa Nzega na Igunga ni wakulima wakubwa sana, tunazalisha mpunga, pamba, tumbaku na tunazalisha mazao mbalimbali. Pia, tunazalisha matunda aina ya maembe ambayo mara nyingi huwa tunauza katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ukamilishaji wa barabara hiyo itatusaidia kusafirisha mazao hayo kuelekea kwenye mradi wa *SGR* ili tuweze kufanikisha usafirishaji wa mazao hayo kuelekea mikoa mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii nimeipitia, lakini barabara za vijijini ni barabara ambazo zina changamoto kubwa sana kwa sababu zimejengwa kwa kiwango cha changarawe na ukarabati wa barabara hizo Serikali inatumia gharama kubwa sana. Kwa mfano, barabara ya kutoka Nzega – Itobo – Mambali na kutoka Itobo – Kagongwa, mwaka huu tu wa fedha uliomalizika tumetumia zaidi ya shilingi milioni 800 kuzikarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukinunua vifaa vya ukarabati ambavyo ni *grader*, *roller*, *excavator*, pamoja na *tipper* angalau mbili, tuna uwezo wa kutumia shilingi bilioni 1,449. Sasa ukija kuangalia, ununuzi wa vifaa ni shilingi bilioni 1.449, lakini ukarabati tu kwa mwaka mmoja tumetumia shilingi milioni 800. Kwa hiyo, ni afadhali Serikali ijikite kwenye ununuzi wa vifaa vya ukarabati wa barabara zetu za vijijini kwenye kila halmashauri ili tuweze kupunguza gharama na tuweze kutimiza lengo letu la kuhudumia wananchi wetu katika barabara za kiwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija kuangalia nchi yetu hii ina halmashauri takribani 184. Halmashauri 184 ukizidisha kwa shilingi bilioni 1.449, unapata shilingi bilioni 266.6. Fedha hizi, shilingi bilioni 266 zinaweka zikawa mwarobaini wa kuleta suluhisho la kudumu kwenye changamoto za barabara tulizonazo kwenye majimbo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaishauri sana Wizara ya Ujenzi kwa kushirikiana na Wizara ya TAMISEMI kupitia *TARURA*, wanunue vifaa vya ujenzi kwenye kila halmashauri ili tuwe tunaweka *diesel* kwenye vifaa hivyo na kusaidia kujenga barabara zetu kwa gharama nafuu kuliko ambavyo iko kwa sasa hivi tumejikita kwenye utumiaji wa kandarasi. Tunatumia fedha nyingi kuwalipa wakandarasi na wakandarasi hao wanaweka riba kubwa matokeo yake kila mwaka tunakuwa na lawama juu ya barabara hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya sana ukija kuangalia, nchi yetu ina uhitaji mkubwa wa barabara, ndiyo maana ukiangalia asubuhi hapa maswali mengi kwa TAMISEMI yanahusu barabara, maswali mengi pia yanahusu *TANROADS*, na maswali mengine huwa yanahusu Wizara ya Maji. Kwa hiyo, ukija kuangalia, hitaji kubwa la Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa nchi hii, ni barabara; na barabara ni uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka kujua kwamba usafirishaji ndiyo uchumi pekee, angalia juzi ilivyotokea hapo Iran, wamefunga ule mfereji wa Hormuz, mafuta yamepanda kila mahali duniani. Hata sisi wananchi tunaoishi kule vijijini, barabara zinapokatika wakati wa masika ama wakati wa kiangazi tunapata tabu kubwa sana katika usafirishaji wa mazao yetu na usafirishaji wa abiria.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa muda wako umeisha, ninaomba umalizie.

MHE. JOHN S. LUHENDE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba kumalizia kwa kuiomba Wizara ya Ujenzi, wanapokuja kutoa mrejesho wa mwisho, watueleze, kama hawajatenga fedha za ujenzi wa Barabara ya Nzega – Itobo – Bukene, watueleze *alternative* barabara tutakayoitumia sisi watu wa Igunga na Wilaya ya Nzega kuelekea kwenye *SGR* pale itakapokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante sana. Mheshimiwa Masanja Kungu Kadogosa, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwantumu Mzamilu Zodo, Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, ajiandae.

MHE. MASANJA K. KADOGOSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Kwanza, ninaanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika miundombinu kwa ujumla, siyo kwa barabara tu katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa ujumla, kwa hotuba nzuri sana ambayo anaonesha mpango wa Wizara katika mambo ambayo kwa kweli Waheshimiwa Wabunge wamekuwa *concerned* nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nimpongeze sana *Eng.* Besta, *engineer* wetu wa *TANROADS*, *CEO* wetu wa *TANROADS* kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Taifa hili. Vilevile nimpongeze Meneja wetu wa Simiyu, *Eng.* Mkumbo kwa kazi kubwa anayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Simiyu ni mkoa mpya, una takribani kama miaka 14 hadi sasa hivi, na una *square meter* za mraba 25 *plus*. Pia, kwa upande wa barabara kwa sasa hivi *TANROADS* haina *network* kubwa sana Simiyu, wana takribani kama kilometa 200 *plus*. Kwa maana nyingine tunahitaji Mheshimiwa Waziri atusikilize katika hili, kwamba tunahitaji upendeleo kidogo katika mikoa hii mipya ambayo inajaribu kutafuta maendeleo kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua barabara yetu ambayo inaanzia Lamadi – Maswa inaenda mpaka Mwigumbi Mheshimiwa Rais alitufungulia miaka kama miwili iloyopita, barabara ya kutoka Bariadi – Maswa. Tumepata bahati ya kufanyiwa ukarabati barabara yetu ya kutoka Bariadi kwenda Lamadi. Kwa hiyo, kwa hambo hilo tunaishukuru sana Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua kwamba wanaendelea na *study* kwa ajili ya barabara ya kutoka Bariadi – Salama – Magu. Tuna imani kwamba hii stadi itaisha kwa sababu imeanza kitambo sasa. Pia barabara nyingine ya kutoka Nyashimo – Gasamo – Dutwa ambayo inaenda kwenye Jimbo la Bariadi Vijijini, na hiyo tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ambayo inazungumza na Waheshimiwa Wabunge wengi sana ya kutoka Karatu – Imbutu – Haydom – Sibiti – Meatu – Lalago inaenda Maswa. Nyingine inakuja Bariadi inaenda mpaka Mwanza.

Barabara hii ni muhimu sana, na ninajua iko katika mipango yao, lakini vilevile iko katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, Simiyu ni Mkoa mpya kama mikoa mingine, kama Katavi. Kwa hiyo, tunahitaji sana barabara zetu kuimarishwa, na ndiyo maana tunapeleka maombi mengi sana kuhusu kuongeza barabara za *TANROADS* ndani ya Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara mojawapo ambayo Mheshimiwa Waziri tulishazungumza, ni ile ya mzunguko ya kutokea Somanda inaenda Nkololo, inaenda hadi Matongo *then* inakuja Igego. Barabara ile ni umuhimu sana kwa sababu tunapakana na Mbuga ya Serengeti, *almost stretch* ya kilometa 80. Vilevile tuna mapori mawili tengefu *Maswa Game Reserve na upande* mwingine Kijereshi ambayo tunaihitaji sana kwa ajili ya uwindaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninataka kuzungumzia mambo ya Kitaifa. *TANROADS* imeanza Julai, 2000. Ukiangalia kwa namna yoyote ambayo wanaweza wakatumia *method* ya ujenzi *whether* ni *rigid or flexible pavement, obviously lifespan* ya barabara inakuwa kati ya miaka 10 hadi 40, kutegemea na ujenzi ulivyofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ukiangalia barabara nyingi zimejengwa kati ya mwaka 2000 hadi 2026. Maana yake nini? Katika *logic* ya kawaida, ni lazima barabara nyingi kati ya 30% hadi 40% zimeshamaliza *life circle* yake. Maana yake nini? Wanapokuwa wanatengeneza *plan* kwa ajili ya matengenezo ya barabara, maana yake barabara nyingi zinahitaji ku-*overhaul*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kwamba, tusipochukua hatua ndani ya miaka miwili au mitatu, tutakuwa kwenye *crisis*. Kwa sababu ukipita kule, na kwa bahati nzuri Waheshimiwa Wabunge wanapita kule, barabara nyingi nyingi zinalia, zinahitaji *maintenance,* na nyingine zinahitaji *overhaul*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa maana yake ni nini? Tusipochukua hatua, maana yake ni kwamba tutajikuta tunaanza kufanya ujenzi ambao *is extremely expensive*. Tunahitaji kuunganisha barabara sasa hivi kwa badhi ya mikoa iliyobakia, lakini tunahitaji ku-*maintain* hizi barabara zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kwamba, tusipoziba, kama unaweka maji kwenye ndoo, na kuna matobo chini, maana yake hatuwezi kufikia hayo malengo. Tunahitaji kuunganisha na mikoa, *then* twende kwenye wilaya. Kwa hiyo, ninaungana na ripoti yetu iliyotolewa na Mheshimiwa Mwenyekiti wetu, lakini vilevile tunahitaji Wizara kuchukua hatua za haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengine ambayo ninataka kushauri, hii fedha ya *ring fencing*, hii siyo tu kwa barabara; reli, maji, kule tunaihitaji kwa sababu ni sheria. Ujue *ring fencing* ilitokana na sababu ambazo wakati ule waliziona Waheshimiwa Wabunge, ndipo tukaanzisha hii sheria. Kwa hiyo, tusipotii sheria hizi maana yake ni kwamba tunarudi kule tulikokuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Mheshimiwa Waziri amezungumzia kuhusu *alternative financing*. Unapozungumzia *bond,* ku-*issue,* ni lazima kuwepo na *base* ya asset, na ndiyo maana ni muhimu sana kuifanya *TANROADS* kuwa Mamlaka ili iwe na *base* hata ya ku-*issue bond*. *Otherwise* sijui kama Wizara wanaweza waka-*come up* hata na *guarantee* ya Serikali kwa ajili ya ku-*issue* hizo *bond*.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo ninataka kuzungumza…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, muda wako umeisha.

MHE. MASANJA K. KADOGOSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimalizie.

NAIBU SPIKA: Malizia sekunde 30.

MHE. MASANJA K. KADOGOSA: Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunazijenga barabara, hali ya reli haikuwa nzuri, lakini sasa hivi tunapoenda, baada ya miaka mitatu, mitano inayokuja, reli itakuwa na hali nzuri. Ni lazima wakae na Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi na yeye wakubaliane mizigo gani inaenda kwenye reli, nao watakuwa wamesha-*establish trend* mpaka sasa hivi ni mizigo ipi inatuharibia barabara zetu? Mizigo hiyo iende kwa reli, aidha kwa sera au kwa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo, ninaomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama anawatangazia Wajumbe wote kuwa kutakuwa na kikao saa 5.00 kwenye Ukumbi wa Kamati. Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, saa 5.00 kwenye ukumbi.

Tunaendelea na Mheshimiwa Mwantumu Mzamilu Zodo, atafuatiwa na Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, na Mheshimiwa Prof. Sospeter Muhongo, ajiandae.

MHE. MWANTUMU M. ZODO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia. Jana nilisikiliza vizuri sana hotuba ya Mheshimiwa Waziri pamoja na Taarifa ile ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote, ninaomba kuunga mkono hoja ili nisije nikasahau mwishoni. Kwa sababu ya muda ninaomba niende moja kwa moja kwenye barabara zetu. Sisi wananchi wa Mkoa wa Tanga kwa majimbo yote 12, kipaumbele chetu cha kwanza ni barabara ya Handeni – Kibirashi – Chemba – Singida. Kwanza, barabara hii ni ya kimkakati kwa sababu inaenda kupunguza *jam* ya malori yanayotoka bandarini kuja kwenye mikoa mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ni ya uzalishaji. Sisi katika Mkoa wetu wa Tanga, tunapata chakula kutoka Wilaya ya Kilindi na Handeni ambako ndiko barabara hii inakopita. Kwenye Taarifa ya Kamati walieleza kwamba wenzetu wa *PPP* wameonesha nia ya kutaka kuijenga barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Wizara, wakae na wenzetu wale wa *PPP* kujaribu kuangalia namna gani watajenga barabara hii. Barabara hii ni kilio cha wananchi wa mikoa takribani minne; Mkoa wa Tanga, Mkoa wa Singida, Mkoa wa Manyara na Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ni kilio cha viongozi wa dini. Ni juzi tu Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa na ziara na pale Chemba alifanya mkutano; na Shehe wa pale alipewa kufungua mkutano pale kwa dua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka kujua barabara hii ni kilio cha watu wengi, baada ya dua Shehe alithubutu kuomba barabara hii kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Barabara hii ni kilio cha Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Madiwani. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja zake, kipaumbele cha kwanza kwa mkoa wetu wa Tanga iwe ni barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya pili ni Barabara yetu ya Tanga – Segera – Chalinze. Wote tunafahamu bandari imepanuliwa, na sasa hivi malori ni mengi, na barabara ile imezidiwa. Barabara ile ni chakavu, Barabara ya Tanga – Chalinze ina viraka barabara yote, kuanzia mwanzo mpaka mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri, nilimsikia akieleza kwamba wanakwenda kutanua kwa njia nne, lakini sasa alieleza kutoka Chalinze mpaka Segera kuelekea Arusha, hakueleza nini watafanya kutoka Tanga – Segera.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja, atueleze mkakati uliopo na ndugu

yangu hapa Mheshimiwa *Eng.* Ulenge ameuliza swali hilo asubuhi hii. Ni mkakati gani watafanya kuendelea kuondoa ile *jam* kutoka Tanga mpaka Segera? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hayo, kuna barabara yetu inayotoka Handeni – Mzia – Turiani. Barabara hii imeelezwa na Ilani zaidi ya moja na barabara hii ilishaanza kwa kipande cha pale Magole – Turiani lakini ikaishia hapo, imesimama. Hatuelewi ni nini hatma ya kipande hiki cha kutoka Turiani – Mziha – Handeni kipande cha kilometa 108.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Taarifa ya Mheshimiwa Waziri, tumeona imetengewa shilingi milioni 500, kilometa 108. Mheshimiwa Waziri atakapokuja atuambie, ni upi mkakati wa barabara hii ambacho kipande cha kwanza awamu ya kwanza kilishaanza na ni muda mrefu, je, upi mkakati wao wa kwenda kumalizia hiki kipande cha pili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo barabara yetu ya kutoka Mabokweni – Maramba – Old Korogwe, inaenda mpaka kule Mlalo kwa ndugu yangu Mheshimiwa Shangazi. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, tumepewa kilometa 10, barabara hii ina kilometa zaidi ya 127. Nimwombe Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake, atueleze hatma ya barabara hii ambayo ni kilio cha muda mrefu.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. MWANTUMU M. ZODO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana, ahsante.

NAIBU SPIKA: Nimemtaja Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, atafuatiwa na Mheshimiwa Prof. Sospeter Muhongo, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso ajiandae.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru na mimi kwa kunipatia nafasi ya kuweza kutoa

mchango wangu kwa Bajeti ya Kumi na Moja ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu nimeingia Bungeni mwaka 2015 na Bajeti yangu ya kwanza ilikuwa ya mwaka 2016, nilisimama kuzungumzia barabara ya kutoka Tanga – Kibirashi – Handeni – Kiteto – Chemba – Kwa Mtoro Singida. Mimi barabara hii kila Bajeti nimekuwa nikiichangia, lakini kipekee niwashukuru sana Wahehsimiwa Wabunge wa Bunge hili la Kumi na Tatu, wameona kilio change, na wameamua kunishika mkono kuhusiana na hii barabara, ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii siyo tu Mheshimiwa Kunti anaisema, barabara hii imeandikwa kwenye vitabu vya Serikali miaka na miaka. Tunavyozungumza, huu ni mwaka wa 26 iko kwenye vitabu vya bajeti, inaandikwa kila leo. Wanachokifanya Serikali, mnabadilisha tu maneno; la mbele linakuja katikati, la katikati linaenda nyuma, la nyuma linaenda mbele; ni maneno wanatugeuzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeuliza maswali zaidi ya 30 ya barabara hii. Bajeti ya mwisho tulipokuwa tunahitimisha Bunge la Kumi na Mbili mwaka 2025, Serikali ilituambia kwa maana ya Wizara kwamba tumetoka kwenye *EPC + F* tunakwenda kwenye *PPP,* na tukaambiwa kwenye *PPP* tunakwenda kuchukua wenzetu na Wizara ya Uchukuzi, kwa maana ya Taasisi ya Serikali, *TPA*, watakwenda kujenga ile barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ya mwisho wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha, na swali langu nililowauliza mwezi huu wa Tano, nimejibiwa kwamba mazungumzo bado yanaendelea. Nikawa ninajaribu kujiuliza, kama sisi tu ndani ya nchi mazungumzo yanakaa zaidi ya miaka mitatu, nini sababu inayofanya Serikali washindwe kukubaliana? Serikali moja, nchi moja? Ni kitu gani kinachokwamisha hayo mazungumzo ili wananchi hawa waweze kupata huduma ya barabara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ndiyo inayopeleka wanawake kwenda hospitalini kuongeza viongozi wa kesho ndani

ya Taifa letu. Wanawake wa Wilaya ya Chemba wanafia njiani kwa sababu ya barabara hii. Mvua inaponyesha, Mto Songolo hakuna mwanamke anayeenda kujifungua akavuka kwenye ule mto. Ukija Goima, na kwa mvua za mwaka huu daraja limekatika pale, watu wamekaa siku tatu hawana njia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatamani Serikali ikija ituambie na kwenye bajeti kitabu cha Waziri, imetengwa shilingi bilioni nane. Nikawa najaribu kutafakari, hivi shilingi bilioni nane inaenda kujenga barabara ipi? Hizo kilometa 20 ambazo tumeanza kuimbiwa miaka na miaka haziishi. Kila kitabu, kila bajeti inayokuja tunakutana na kilometa 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama imeshindikana ujenzi wa hii barabara, siyo vibaya tukaambiwa kwamba jamani barabara hii imeshindikana, kuliko kuwa tunawekwa, wanatupa matumaini kila mwaka lakini barabara haijengwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao Mto Bubu ambao unapita kwenye Daraja la Bubutole, umeua zaidi ya watu wanne. Barabara hii ikijengwa, wananchi wangu hawatakufa, Serikali watuonee huruma. Sisi Uchumi wa Wilaya ya Chemba barabara hii ikijengwa ndiyo hatima ya ukusanyaji wa mapato na kujitegemea kwa halmashauri na kusukuma maendeleo kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapolia na barabara hii, hatutamani tu rangi ya barabara ibadilike, bali tunatamani maendeleo ya wananchi wetu yaweze kusonga mbele. Ninatamani Serikali ikija, Waziri wa Ujenzi, kaka yangu Mheshimiwa Ulega anafanya kazi kubwa ya kumsaidia Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais alipokuwa ziara Tanga alitoa maelekezo kuhusiana na hii barabara, kwamba barabara hii iende ikajengwe ili tuweze kusaidia mizigo ya kutoka Bandari ya Tanga inayokwenda nchi za jirani ipite ile mizigo kwenye barabara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachelewesha uchumi wa nchi hii kukua. Twendeni tukafungue milango, tujengeni hiyo barabara.

Mheshimiwa Ulega akija atuambie ni lini wanakamilisha mazungumzo na *TPA* ili barabara ya kutoka Handeni – Kibirashi – Tanga – Kiteto – Chemba mpaka Kwa Mtoro – Singida inakwenda kuanza kujengwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu la pili ni Ujenzi wa Daraja la Kelemasimba. Daraja hili limekaa zaidi ya miaka 15, bovu limekatika. Kibaya zaidi barabara hii ilisainiwa mkataba mwaka 2022, limekaa mpaka leo mkandarasi akaamua ku-*terminate* mkataba kwa sababu tu ya kukosa fedha kwa ajili ya kwenda kujenga lile daraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2025 niliongea nikawaambia Mawaziri, mmekuwa mkienda mnabeba na mbuzi za watu, mnakula; hii ni laana. Huwezi kwenda kuwapa wakina mama wa watu wamejinyima, wamekupa Zawadi, wameona matumaini, unawaambia tunakuja kujenga daraja, halafu matokeo yake watu wanaendelea kufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kule hatuna vyombo vya Habari. Tungekuwa mjini, mngeona wananchi wetu wanavyokufa. Vyombo vingekuwa vinarekodi, mngeona namna watu wanavyokufa kwa ajili ya hizi barabara. Ninaomba Serikali ikija iniambie kuhusu daraja la Kelemasimba ambalo nimeimba miaka yote. Tunaona raha gani kwenda na bahasha za kutoa rambirambi wakati tulikuwa na uwezo wa kuhakikisha kwamba tunawatengenezea mazingira rafiki wananchi wetu na kuokoa maisha ya Watanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa muda wako. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mheshimiwa Dickson Nathan Lutevele Villa ajiandae.

MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa muda. Ninadhani malalamiko ni makubwa.

Kwa hiyo, unipatie muda niwapatie na sehemu ya kutafuta fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge…

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Profesa Muhongo ni dakika sita kwa kila Mbunge, orodha ni ndefu sana…

MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, kwa hiyo, nenda kwenye hoja moja kwa moja.

MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wawili wameshasema wananipa muda wao. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wote hapa tukifanya utafiti kwenye Majimbo yetu sasa hivi, Serikali imefanya makubwa sana. Watu wanachokiomba sasa hivi kwenye kila Jimbo: moja ni maji; pili, umeme; na tatu, ni barabara. Bajeti yetu hii ya shilingi trilioni 62 hata tukitoa kwenye hivi vitatu tu hazitoshi. Kwa hiyo, tatizo hapa ni fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kwangu Musoma Vijijini. Sisi tuna barabara moja kuu inaunganisha kata 21, vijiji 68, vitongoji 374. Barabara moja tu, lakini hatuna lami. Tumeshajengewa kilometa tano, *tender* zimetangazwa mbili. *Tender* ya kwanza aliyeshinda alikuwa mtu bingwa kweli kweli wa Uganda nilimfuatilia; lakini kosa walilofanya *TANROADS* ni kuchukua mkandarasi mmoja ambaye majadiliano yao yalichukua muda mrefu kwa sababu alijua yuko peke yake, lazima wafuate matakwa yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sasa imetangazwa tena. Hii barabara imetangazwa *tender* mara ya pili. Kwenye bajeti iko ukurasa wa 83, ukisoma pale hata yule wa kilometa tatu hajalipwa, na hizi kilometa 40 kwa makadirio tunahitaji shilingi

bilioni 100. Kwa hiyo, tatizo hapa ni fedha. Sasa yanakuja mapendekezo yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimalizie tu kwa kusema, watu wa Musoma Vijijini tumetangaziwa *tender* mara ya pili, hivyo tunaishukuru Serikali kwa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yangu, na ndiyo maana ninachukua muda wa hawa wenzangu hapa. Kitu cha kwanza, barabara zetu tuzijenge kwa taratibu ambazo zinatumika pengine pote duniani. Ni lazima; ninaomba nisisitize, ni lazima Tume ya Mipango ihusike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi barabara siyo kila mtu anakuja tu na mipangilio yake. Hii mipango tuitunze kisheria. Kwa mfano, ni lazima tukubaliane kwamba tuunganishe mkoa kwa mkoa. Barabara zinazounganisha mkoa kwa mkoa mapendekezo yangu, ziwe ni mbili mpaka tatu. Zinaenda mbili au tatu, zinarudi mbili au tatu *(lanes* nne mpaka sita). Sasa hizi ziwepo kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Tume ya Mipango, ndiyo itaboresha hata matumizi ya fedha, tuunganishe wilaya kwa wilaya na penyewe ziwe zinaenda *lanes* mbili, zinarudi *lanes* mbili (*lanes* nne).

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kuunganisha halmashauri zetu na makao makuu ya wilaya, ambapo zinaenda barabara mbili, zinarudi mbili. Kwa hiyo, hizo ni *lanes* nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la pili ni matengenezo *(road mantainence)*. Ndugu zangu fedha nyingi sana tunapotezea kwenye *repair* na *maintenance*. Sasa wataalamu, ndiyo maana nilichelewa kidogo mzee, nilikuwa nasubiria *engineer* mmoja anipe kitu kabla sijaja Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani ni kwamba usipofanya *routine maintenance,* inahitajika kati ya miaka mitatu mpaka mitano ile *preventive* lazima ifanyike. Halafu kuna *periodic*

ambayo unaweka lami *re-surfacing* na *sealing*. Unaziba pale lami ili barabara isipokee maji. Hiyo ni kati ya miaka sita mpaka minane. Halafu barabara imeharibika kabisa, unahitaji *rehabilitation re-construction*. Hiyo ni kati ya miaka 15 mpaka 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya sisi hatuyafanyi haya, ndiyo maana gharama za ujenzi wa barabara zinakuwa kubwa, tunarudia mle mle. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa gharama za kutofanya matengenezo haya kwa wakati, ukidharau ikapita miaka mitatu, gharama zake zitakuwa mara sita kama ambavyo ungewahi. Ukiiacha miaka mitano, tena huyu ndio *engineer* wa mwisho ameniambia asubuhi; gharama zake zinaweza kwenda mara 18. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la tatu. Vyanzo vya fedha. Kitu cha kwanza ni Bajeti ya Serikali. Bajeti yetu ndugu zangu za miradi ni shilingi trilioni 2.5, Mfuko wa Barabara umetoa shilingi trilioni 1.05, Mfuko wa Serikali umetoa shilingi bilioni 500 na fedha za nje zilikuwa shilingi bilioni karibu 920. Kwa hiyo, hicho ni chanzo cha kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, chanzo cha pili ni kutokana na rasilimali zetu; migodi… *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, ninakuongezea dakika moja…

MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, inabidi mnivumilie, haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua mfano zile kampuni zilizoingia mikataba, hata wengine hatujaingia huko Wizarani; mwaka 1995 bei ya dhahabu *ounce* moja ilikuwa dola 390. Miaka 30 baadaye, mwaka 2025 bei ya dhahabu *ounce* moja ilikuwa dola 4,000. Je, kwa nini tusitafute fedha kutokana na mikataba yetu ya madini hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni *soft loans* (mikopo laini). Hii inatoka *IMF, World Bank* na *African Development Bank* na nchi. Halafu hizi riba yake ni kati ya sifuri mpaka asilimia tatu, na *grace period* ni miaka mitano mpaka 10. Halafu *repayment periods* ni miaka 15 mpaka 45. Kwa hiyo, twende kwenye mikopo kama hii *(soft loans). (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namba nne, *sovereign wealth funds.* Madini yetu na gesi yetu. Lazima tutunze fedha kama wanavyofanya Norway, na hizi fedha tutatumia *sovereign bonds* kuweza kupata mikopo. Duniani hapa anayeongoza mwenye mfano mzuri ni Norway ambaye ya kwake imefika shilingi trilioni 1.1 na juzi mwezi Aprili, 2026 Canada wameanzisha kama hii, na tayari wamewekeza dola bilioni 25. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni *PPPs (Public Private Partnership).* Hii ni sawasawa kama Barabara ya Kigamboni. Mwisho, ninamalizia, ni kwamba *infrastructure investments* mifano mingine duniani, na hii ni muhimu sana ulisikilize hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kwanza, China wanatumia asilimia tano nukta tano ya pato lao la Taifa kwenye *investments* za *infrastructure.* India ni asilimia tano mpaka sita, Vietnam asilimia karibu sita, Seychelles ambayo ni nchi tajiri Barani Afrika inatumia asilimia sita, Mauritius ambayo inafuata kwa utajiri, inatumia karibu asilimia nne ya *GDP* yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninamalizia kwa kusema kwamba, hii bajeti tunayoiongelea kama na sisi tungeiga nchi nyingine tukatumia asilimia tano *of our GDP, GDP* yetu sasa hivi ni dola bilioni 95, *five percent of 95 billion US dollars* ni dola bilioni 4.75 ambayo ni sawasawa na shilingi trilioni 12.35…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa ahsante sana…

MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sasa hivi tulikuwa tunapaswa kujadili bajeti ya shilingi trilioni 12, siyo ya shilingi trilioni mbili. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Profesa.

MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Nilimtaja Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, atafuatiwa na Mheshimiwa Dickson Nathan Lutevele Villa, Mheshimiwa Mecktridis Fratern Mdaku ajiandae.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu ambayo ni Bajeti ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya katika sekta hii. Vilevile, nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi ambazo zinaendelea kufanyika na zinaonekana zimefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba tunapojenga barabara zetu kwa kiwango cha lami, ndivyo ambavyo tunachochea ukuaji wa uchumi wa eneo husika, na uchumi wa nchi kwa ujumla. Ni muhimu sana Serikali ikaipa vipaumbele barabara zote ambazo zinaenda kusaidia na kuchochea ukuaji wa uchumi wa eneo husika na hasa zile barabara za kimkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wetu wa Arusha ni mkoa wa kitalii, lakini ni mkoa ambao unaandaa mashindano ya *AFCON* itakapofika 2027. Tunatambua kwamba kuna jitihada zinaendelea na tayari kuna mikataba imeshasainiwa ya barabara zinazoelekea kwenye uwanja kujengwa kwa kiwango cha lami. Matumaini yetu sisi Wabunge wa Mkoa wa Arusha ni kwamba barabara hizo zitakamilika kwa wakati ili ziweze kuendana na mashindano hayo ya *AFCON* katika mji wetu wa Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika Wilaya ya Karatu tuna barabara muhimu tatu ambazo zinasimamiwa na *TANROADS,* tuna barabara ambayo sasa inatumika ya Makuyuni kuelekea lango la Ngorongoro ambayo ni barabara ya muda mrefu na bado ina hali nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Barabara ya Karatu – Mbulu kwa kilometa 75 na tuna Barabara ya Njia Panda - Mang'ola kuelekea Lalago yenye urefu wa kilometa 129. Hizi zote ni barabara ambazo zinahudumiwa na *TANROADS* mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kwa kweli kumpongeza sana Meneja wa *TANROADS* Mkoa, pamoja na timu yake. Wamekuwa wakijitahidi kufanya matengenezo ya mara kwa mara na ninajua hata sasa matengenezo yanaendelea kwa kiwango cha changarawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na uhitaji wa muda mrefu wa barabara hizi kujengwa kwa kiwango cha lami, na tumekuwa tukiahidiwa muda mrefu kwamba barabara hii itajengwa. Pia, mara nyingi tumeuliza Bungeni, tunaambiwa upembuzi yakinifu, usanifu umekamilika lakini bado hatujaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumaini yetu sisi wananchi wa Karatu hasa kwa hii Barabara ya Njia Panda - Mang'ola kwenda Lalago sasa itajengwa kwa kiwango cha lami. Umuhimu wa hii barabara labda nieleze ili tuone ina umuhimu kiasi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ni muhimu kwa uchumi wa Wilaya yetu na uchumi wa Mkoa kwa ujumla. Kwanza ni barabara ya kitalii, ndiko ambako wageni wetu wengi wanaenda kuangalia kabila maarufu la Wahadzabe ambao wako hapa nchini ambapo kama tunavyowajua hao kina Chabba wako kule. Kwa hiyo, barabara hii inatumika sana kwenda kwenye eneo hilo na watalii kufika katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii barabara pia ndiko ambako inaelekea Hospitali ya Wilaya. Hapa sasa nichukue nafasi hii kwa

kweli kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake. Nimeona kwenye bajeti wametenga kilometa tano ambayo itaenda mpaka Hospitali ya Wilaya kujengwa kwa kiwango cha lami. Tunawashukuru sana kwa hili, na hii ndiyo maana halisi ya kazi na utu. Wamezingatia utu kwa wananchi wetu wa Karatu wanapoenda kupata huduma katika Hospitali yetu ya Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, barabara hii ndiko ambako kuna kilimo kikubwa cha umwagiliaji. Wananchi wa eneo husika wanalima vitunguu maji na vitunguu hivi vinasafirishwa nje ya nchi. Wanunuzi wetu wakubwa ni watu wa Kenya, Uganda, na *South Sudan*. Kwa hiyo, barabara hii pia ni muhimu sana kwa uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kuwa tumepata kilometa tano, bado kilometa 45 angalau ifike mpaka eneo la Mang'ola. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri azingatie tuweze kupata hizo kilometa zilizobaki kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii pia ndiko ambako sasa hivi wanaendelea na utafiti chini ya shirika letu la *TPDC* kutafuta mafuta. Utafiti unaendelea na hatua imeshafanyika nzuri. Kuna uwezekano mkubwa wa kupata mafuta katika eneo hilo katika Ziwa Eyasi. Kwa hiyo, tunaona umuhimu wa barabara hii, tunaomba sana Serikali iizingatie na kufikiria kukamilisha hizo kilometa chache tuweze kupata kwa kiwango cha lami barabara husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nitoe shukrani na pongezi kubwa kwa Serikali kwa upanuzi wa uwanja wa *Lake Manyara Airport*. Tumeona kazi inaendelea na kazi inafanyika. Kwa kweli kwa upanuzi wa uwanja huo ni uthibitisho kwamba utachangia kwa kiwango kikubwa ongezeko la utalii au watalii katika eneo letu la Karatu ambao wanaenda kufanya utalii katika Hifadhi ya Ngorongoro na Serengeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kazi inaendelea. Ni matumaini yangu kwamba kazi ile haitaweza kusimama,

itaendelea na uwanja ule utakamilika na utaanza kutumika ikiwa ni kichocheo muhimu sana cha utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tuna barabara hii ya kuanzia Singida kwenda Katesh – Dareda mpaka Babati. Ile barabara sasa hivi ukipita ina mashimo makubwa mno, barabara imeharibika, haipitiki. Tuna imani barabara ile sasa itatengenezwa na itaweza kupitika kama ambavyo ilikuwa inapitika huko kwa kuwa ni barabara muhimu sana, inaunganisha Mkoa wa Singida, Mkoa wa Manyara kuelekea Mkoa wa Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, ninaomba kusisitiza sana umuhimu wa ubora wa barabara zetu. Kwa kweli tunaongea hapa, tunaomba na tunasisitiza na fedha zinatengwa, unaona kabisa fedha inatengwa barabara inatengenezwa lakini ile *life span* ya barabara huwa hazifiki. Kwa hiyo, ni muhimu sana Serikali ikazingatia ubora wa barabara tunazotengeneza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Profesa Muhongo ameeleza hapa vizuri jinsi ambavyo tutatengeneza ubora wa barabara kwa kiwango kinachotakiwa, ndivyo ambavyo barabara hiyo itadumu zaidi na ndivyo ambavyo sasa Serikali itaelekeza nguvu kujenga barabara nyingine, na hii ikaendelea kudumu. Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba Serikali itazingatia jambo hili na barabara zetu zitakuwa bora na zitadumu kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi, na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Cecilia Paresso kwa kutumia muda vizuri. Mheshimiwa Dickson Nathan Lutevele Villa atafuatiwa na Mheshimiwa Mecktridis Fratern Mdaku, Mheshimiwa Pascal Lucas Lutandula ajiandae. *(Makofi)*

MHE. DICKSON N. LUTEVELE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangie kwenye Wizara hii

muhimu. Kusema ukweli ninaomba nielekee moja kwa moja kwenye uchangiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kwa kuzungumzia barabara tatu na nitatumia muda wangu vizuri sana. Sisi katika Wilaya yetu ya Mufindi tunayo barabara ya kimkakati, barabara inayotoka kwenye Jimbo langu la Mafinga kwenda Mgololo. Barabara hii ina kilometa 81.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii Wabunge wenzetu kwa kipindi cha miaka 20 humu ndani wameshiriki kupitisha bajeti za barabara za nchi hii ikiwemo barabara yetu ya Mgololo, lakini hivi ninavyozungumza barabara ya Mgololo hata kilometa moja haijawahi kujengwa. Jambo hili linatufedhehesha na linatusikitisha sana sisi Wanamufindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipokuja tarehe mbili kwenye ziara wilayani kwetu alitoa maagizo kwa Wizara kwamba anatoa wiki mbili awe mkandarasi amepewa *advance payment* kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii, pamoja na barabara ya Nyololo, Igowole kwenda Mtwango. Hayo ni maelekezo ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, barabara hii ilikuwa na maagizo ya Mheshimiwa Rais. Sasa kwa sababu wiki mbili zimeshaisha tangu tarehe mbili, ninaomba Waziri atakapokuja atuambie je, huyu mkandarasi tayari yuko *site,* ama amepuuza maagizo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu? Jambo hili Mheshimiwa Ulega atakapokuja ninaomba atuambie. Sisi Wanamufindi kusema ukweli jambo hili halitupi furaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ni barabara ya kutoka Kinyanambo kwenda Madibila. Hii barabara ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwamba tutengenezewe kiwango cha lami kilometa 20. Tuliishukuru na kuipongeza Wizara, walianza kwa kutengeneza kilometa 1.2, maelekezo ya Mheshimiwa Rais ni kilometa 20, lakini wakaanza kilometa 1.2. Nayo kilometa 1.2. ninavyoongea leo, mimi tangu nimeingia humu Bungeni, nimeanza kudai hii barabara kwa sababu imefumuliwa, watu

wanapata vumbi wakati wa jua, wanapata tope wakati wa mvua. Kilometa 1.2 mpaka leo haijafanyiwa chochote na mkandarasi hayupo *site*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu Mheshimiwa Waziri aniambie, furaha ya kuunga mkono bajeti hii inatoka wapi kama kilometa 1.2 nalo limekuwa tatizo? Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atuambie tatizo ni nini? Sisi watu wa Nyanda za Juu Kusini tuna shida gani, kama barabara ya kilometa 1.2 nayo inakuwa shida? Ninaomba sana mambo haya atakapokuja Waziri atuambie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, sisi tunaamini kwamba kauli ya Mheshimiwa Rais ni kauli ya mwisho. Mheshimiwa Rais akitoa kauli ni kauli ya mwisho, na wananchi wanashangilia kweli kweli. Kwa nini Wizara inakuwa haitekelezi barabara hizi za kimkakati?

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Mafinga kwenda Madibila ni barabara ambayo ndiyo sehemu ya skimu ya chakula inayolisha Mji wa Mafinga. Mpaka leo barabara ile siyo nzuri, wakati wa mvua haipitiki kabisa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atakapokuja atuambie.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, iko barabara inayotoka Kinyanambo kwenda Itimbo, inapita mpaka kwenda Kisusa mpaka Mlimba. Barabara hii tumeambiwa imefanyiwa upembuzi ya kinifu. Sasa, umeanza upembuzi yakinifu, ndizo lugha alizotoka kuongea Mheshimiwa Kunti hapa. Itakuwa upembuzi yakinifu, sijui mtaala elekezi, sijui hali ya hewa, miaka 20 inaisha. Tunaomba Wizara hii pamoja na kazi wanazozifanya, wawe na kauli ambazo zinatekelezeka. Vinginevyo Wabunge tutalaumiwa, lakini ukweli ni kwamba kule majimboni hali ni mbaya na tunashindwa kufanya ziara wakati wa masika kwa sababu unaweza ukapigwa mawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ni mbaya, hata hizo zilizotengenezwa kwa kiwango cha changalawe hazipitiki. Ametoka kuzungumza Mheshimiwa Paresso hapa, ubora wa

barabara ni kitu muhimu sana, barabara zetu hata hizo za changarawe hazitengenezwi kwa ubora. Wewe mtu *culvert* anakwenda kuweka mlimani wakati maji yanajaa bondeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana barabara zitengenezwe kwa ubora. Hapa ndani hata kama tutapongezana vipi, kama hali halisi kule haiwezi kuwa nzuri tutakuwa tunadanganyana. Tunaiomba hii Wizara kwa sababu ndiyo inayobeba uchumi wa nchi, wakandarasi na watu wetu wanaofanya kazi kule wafanye kazi kwa kutumia weledi na uzoefu walionao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kaka yangu Mheshimiwa Ulega yeye anajua, ninampenda sana, lakini leo kwenye hoja ya barabara, kama hatatoa majibu ya haya niliyoyasema, nakamata shilingi kwa sababu bila kufanya hivyo nami 2030 hapa ndani sitarudi. Ninaomba sana jambo hilo alizingatie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kushikilia shilingi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa. Nilimtaja Mheshimiwa Mecktridis Fratern Mdaku, atafuatiwa na Mheshimiwa Pascal Lucas Lutandula, Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete ajiandae.

MHE. MECKTRIDIS F. MDAKU: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia bajeti wa Wizara ya Ujenzi ya Mwaka huu wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Morogoro ni mkoa unaochangia kwa asilimia kubwa sana pato la Taifa, lakini mkoa huu umekuwa na changamoto kubwa za barabara. Waheshimiwa Wabunge wenzangu jana walikuwa wametangulia kusema na kuongelea barabara zote za Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, nami nimeona nianze na hili kwa Serikali iweze kutupa kipaumbele Mkoa wa Morogoro ili zile barabara ziweze kurekebishwa na nyingine kujengwa, ili

Morogoro iendelee kuwa kitovu cha uchumi wa Taifa hili kwa sababu pato la Taifa linachangiwa kupitia sekta ya kilimo, lakini pia utalii, madini, lakini pamoja na maliasili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuongelea Jimbo langu la Malinyi. Jimbo la Malinyi limekuwa kisiwani, tuseme pembezoni, lakini ni kama bakuli, linapokea maji kutoka maeneo mbalimbali ya miinuko. Mvua zinanyesha kwingine, Malinyi tunapata mafuriko. Hali hii imeathiri sana barabara zetu za *TARURA* na *TANROAD* kule Malinyi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi ni shahidi, alikuja kule Malinyi mwaka 2025 mwezi wa Nne akaona hali halisi ya mafuriko, lakini akaona Madaraja ya Namhanga pamoja na la Mto Fuluwa likiwa limesombwa na maji. Aliahidi kuwa mwezi wa Saba mwaka 2025 lile daraja lingekuwa limeanza ujenzi, lakini mpaka leo ni mwaka sasa na miezi minne, ujenzi wa Daraja la Mto Fuluwa haujaanza, wala pale Namhanga, walianza kidogo lakini wamekwama. Mkandarasi haonekani *site*, hamna kingine chochote kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, madaraja haya yamekuwa ni changamoto kubwa sana kwa usafiri na usafirishaji wa mazao, na pindi tunapopata misiba, wananchi wamekuwa wakipata shida sana, kwa sababu Daraja la Mto Fuluwa linaunganisha kata nne; Kata ya Sofi, Kata ya Mtimbila, Kata ya Igawa pamoja na Kata ya Biro. Wananchi wanapata misiba, lakini wanashindwa jinsi ya kwenda kuzika, inabidi wengine wazikwe huko huko upande mwingine, ng'ambo nyingine, wengine wazikwe huku.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana Serikali iangalie suala hili la haya madaraja. Ninashukuru Mheshimiwa Waziri ameniahidi, amesema kuwa akimaliza bajeti hii atafika kule Malinyi na kusema ule ujenzi utaanza lini na kuzungumza na wananchi wa pale Malinyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuongelea na barabara ya lami kilometa 112 kutoka Ifakara – Lupiro – Mtimbira. Hii barabara imekuwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi,

zaidi ya ilani sita. Pia bado kwenye kitabu cha bajeti cha Wizara ya ujenzi imekuwa ikitajwa kila mwaka. Leo tena nimeona kwenye *page* ukurasa wa 26 imeelezwa kuwa wanaenda kujenga barabara ya lami kilometa 112 kutoka Ifakara – Lupiro – Malinyi na mkandarasi yupo anajipanga ili kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, haya yanakuwa ni maneno tu. Nami ninaiomba Serikali, kwa wananchi wa Malinyi ambao ni wilaya inayozalisha kwa kiasi kikubwa mazao ya ufuta, mpunga, korosho, pamoja na mazao mengine, na bado yana mazao mengine ya kimkakati, barabara hii ni muhimu sana. Kujengwa kwa barabara hii kutafungua fursa nyingi katika Wilaya ile ya Malinyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba barabara hii ipewe kipaumbele cha aina yake. Katika Mkoa wa Morogoro, Wilaya ya Malinyi ndiyo wilaya ya kwanza inayozalisha chakula kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia kuongelea barabara ya kutoka Malinyi – Luchemba – Londo – Namtumbo. Barabara hii ni miaka mingi inawekwa kwenye ilani, na barabara hii pia ni miaka mingi inazungumziwa. Barabara hii inaenda kuunganisha Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Ruvuma, lakini bado haipewi kipaumbele kinachostahili. Barabara hii itakapokwenda kufunguliwa fursa nyingi zitafunguka. Tutafungua fursa za biashara, uwekezaji, utalii, madini, kilimo, pamoja na kuongeza thamani ya mazao yanayozalishwa katika pande hizi mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba sana Serikali yetu iweze kwenda kufungua hii barabara, kwani ni muhimu kwa mikoa yote miwili pamoja na watu wengine watakaotumia barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, bado Malinyi tuna tatizo la kivuko ambacho ni barabara ile inayounganisha Malinyi kwenda Wilaya ya Mlimba, Kivuko cha Kikove. Huu mradi umeanza mpaka sasa ni miaka tisa, lakini haujakamilika mpaka

sasa. Kila siku kunakuwa na changamoto hizi na zile. *Gutter* zinajengwa miaka minne, mitano, wanajenga *gutter* tu. Kivuko nacho mara kimekamilika mara bado hakijakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Wizara ya Ujenzi kufanya tathmini ya kina kujua tatizo la huu mradi, kwa nini unakwamba mpaka leo unaenda mwaka wa 10 na kitu? Kilichobaki ni kidogo tu. Sidhani kama hata shilingi milioni 400 inafika kukamilisha ule mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali pia kupitia Wizara ya Ujenzi kwenda kukamilisha huu mradi wa Kivuko cha Kikove pamoja na kinachounganisha Wilaya ya Malinyi pamoja na Mlimba.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. MECKTRIDIS F. MDAKU: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi anapohitimisha bajeti yake hapa, atuambie, ni lini barabara hii ya kilometa 112 na barabara ya kuunganisha Malinyi – Namtumbo zinakwenda kujengwa? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, ahsante sana.

MHE. MECKTRIDIS F. MDAKU: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Pascal Lucas Lutandula, atafuatiwa na Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga ajiandae. Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote ninaomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Hatimaye ninamshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kumpongeza kwa kazi kubwa na nzuri

anayoifanya katika maeneo yote, na hasa kwenye eneo hili la sekta ya barabara. Hongera sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, ninampongeza Waziri na Katibu Mkuu na viongozi wale wote. Ninampongeza Waziri kwa uwasilishaji wake ambao umegusa maeneo yote katika Wizara yake. Sambamba na hili, wakati anaeleza, ameeleza vipaumbele sita katika kuwasilisha hii bajeti ya Wizara yake ya Ujenzi. Vipaumbele hivyo ni kama vifuatavyo:- *(Makofi)*

(i) Kuendelea na ujenzi wa barabara;
(ii) Kuendelea na barabara zinazounganisha mikoa; na
(iii) Kuendelea na kuimarisha usafiri wa miundombinu pamoja na vivuko na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, nikianzia na suala zima la barabara, ni kama ambavyo wachangiaji wengi wamezungumza kuhusu barabara za mikoa na barabara zinazounganisha mkoa mmoja na mkoa mwingine na barabara zile za kimkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi ninataka nieleze kwamba, kipaumbele chetu au kipaumbele ukienda ndani ya Mkoa wetu wa Lindi, hii ni barabara inayounganisha mikoa zaidi ya minne. Ni barabara inayounganisha Taifa hili na Taifa lingine. Hii ni barabara ya Lindi – Kibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara hii ya Lindi – Kibiti ni muhimu sana katika uchumi na ustawi wa maisha ya watu. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, tulipata kadhia kubwa ambayo haijawahi kutokea katika maisha tunayoyafahamu kwa karne nyingi. Ikatokea mafuriko, mafuriko yale yakaharibu miundombinu ya barabara hii yote kuanzia Dar es Salaam mpaka unafika kule Lindi. Kilwa ndiyo ilikuwa usiseme, iliharibika yote na watu walikaa njiani kwa muda kadhaa. Hawavuki kutoka Pwani kuelekea Lindi hatimaye kuelekea Mtwara, hatimaye kuelekea Ruvuma hatimaye hata wale wanaoelekea *Mozambique* hawakuweza kuvuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, alitoa fedha nyingi, na yale madaraja yote yakajengwa. Baada ya ujenzi wa madaraja yale, hawakumaliza tu kujenga madaraja, halikadhalika hata taa za barabarani zilifanyaje? Ziliwekwa katika madaraja yale isipokuwa daraja moja tu. Wamejenga hatimaye taa za barabarani hazikuwekwa. Hili ni Daraja la Mbwemkuru. Sasa sijui hakukuwa na bajeti au hakukuwa na nini sijui! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri atambue na ajue ya kwamba, barabara hii ya Lindi – Kibiti ndiyo barabara pekee ya tumaini, na ndiyo barabara pekee ya uchumi, na sisi hatuna njia nyingine yoyote ya usafiri zaidi ya barabara hii ya Lindi – Kibiti. Ukitaka kwenda Lindi, kama daraja moja likiharibika ina maana hufiki Lindi, na haufiki sehemu yoyote ndani ya Mkoa wa Lindi, hata Mkoa wa Mtwara hata Mkoa wa Ruvuma hata huko *Mozambique* huwezi kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nini tunachohitaji? Tunachohitaji pamoja na yote, barabara imejengwa, madaraja yamejengwa vizuri, basi kuwe na njia mbadala, tusiwe na barabara moja tu. Tunahitaji hata kama isipokuwa kesho au keshokutwa, tunahitaji Mkoa wa Lindi na mikoa yetu ya Kusini kuwe na *SGR*. *SGR* ni muhimu sana kwetu. Mtengeneze mazingira, ama sivyo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wamezungumzia asubuhi kwenye swali kuhusu suala la uwanja wa ndege. Ule uwanja wa ndege upo miaka mingi, lakini mpaka leo umeachwa. Tunazungumzia suala la *LNG; LNG* haiwezi kuwepo bila kuwa na uwanja wa ndege wa Mkoa wa Lindi. Ninaomba Mheshimiwa atakapokuja kuhitimisha, hili ni muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, ninaenda kwenye jimbo langu la Mchinga.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba univumilie kwa dakika moja. *(Kicheko/Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ninakuongeza dakika moja.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ninakushukuru kwa hiyo dakika moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye Jimbo langu la Mchinga kama siku zote ambavyo ninasema, Jimbo la Mchinga ni jimbo pekee ambalo nikisema, hatimaye huko wataandika. Waandike tu, nami nimechaguliwa kwa ajili ya kuwatetea wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Mchinga halina lami hata kidogo. Hata pale kilometa moja sijui nukta mbili kwenda kwenye shule ya wasichana imejengwa hivi karibuni. Leo ninapata taarifa daraja lile lime-*sink*. Sasa, huu ni ujenzi wa aina gani? Ninataka hii barabara ijengwe, lakini ninataka lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia kuunganisha makao makuu ya mkoa, hatuunganiki sisi. Jimbo la Mchinga limejifunga. Ninataka Mheshimiwa Waziri akija hapa anipe uhakika jinsi ya kuliendeleza Jimbo la Mchinga ambalo halina lami hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha tumepatiwa. Baada ya kupatiwa fedha hizo, sijui wanasema kuna mikataba gani haijaenda vipi! Ninataka nielezwe, aidha anieleze hapa au nitamtafuta huko aniambie kitu gani kinachokwamisha fedha zile zilizotolewa na Serikali, mikataba ile isiwe sawasawa na wakaanza kujenga? *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa kweli ninachohitaji, Barabara yetu ya Lindi ijengwe kwa kiwango, ifumuliwe yote, hatimaye ijengwe upya. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Edward Kisau Olelelaita, na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma ajiandae.

MHE. JANETH E. MAHAWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na mimi ninashukuru kwa nafasi hii ya kuchangia Wizara hii ya Ujenzi. Kwanza kabisa, nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa maono yake na dhamira yake ya kuendelea kuijenga na kuboresha Mkoa wa Dar es Salaam, kupitia uwekezaji wa miundombinu ya barabara zinazoendelea kwenye mkoa wetu. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya uongozi wake, tumeona ujenzi unaoendelea Dar es Salaam, umebadilisha mwonekano na umeendelea kuboresha ubora wa mkoa ule, kwa sababu Dar es Salaam ndiyo mkoa unaobeba sura ya Taifa letu la Tanzania, kazi kubwa imefanyika. Bado kuna upungufu, lakini kwa hiki kilichofanyika, hatuna budi kushukuru na kuipongeza Wizara na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nimpongeze Waziri wa Ujenzi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu nzima, kwani wanafanya kazi nzuri, sisi wananchi wa Dar es Salaam tumeona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi unaoendelea Dar es Salaam, umesaidia kupunguza foleni, kwa sababu barabara za ndani zimeboreshwa. Tumeona taa zimewekwa ambazo zinasaidia kuongeza uchumi wa wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam. Sasa hivi wananchi wa Dar es Salaam wanafanya biashara mpaka usiku. Kama tunavyofahamu, Mkoa wa Dar es Salaam, *nature* yake ni biashara. Kuna wanaofanya biashara asubuhi, lakini wengine wanafanya biashara usiku kwa sababu ya miundombinu iliyoboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ukishuka hata stendi ya Magufuli usiku, pembezoni mwa barabara utaona biashara zinaendelea, hususan wanawake wajasiriamali wamekuwa wakiuza pipi, karanga, na matunda usiku. Haya yote yamefanyika kutokana na ujenzi ulioendelea, miundombinu iliyoboreshwa ndani ya mkoa wetu wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi ule umeongeza hadhi ya mkoa wetu. Mtu aliyeondoka Dar es Salaam, miaka 10 iliyopita akirudi leo lazima anaona mabadiliko makubwa na anaweza hata akapotea. Kwa hili, hatuna budi kuishukuru Serikali na kuipongeza Wizara kwa kazi inayoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa miundombinu hii umesaidia pia kuongeza thamani ya maeneo ya Dar es Salaam. Leo hii watu wanapungua Dar es Salaam na kupunguza msongamano, wanakwenda pembezoni kununua viwanja, kujenga, lakini hata vile viwanja ambavyo watu walikuwa wanauza kwa bei rahisi, sasa hivi thamani imepanda kwa sababu ya miundombinu. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali iendelee kuboresha barabara za Dar es Salaam, kwa sababu Dar es Salaam ndiyo mkoa wenye wananchi wengi kuliko mikoa yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanaingia Dar es Salaam kila siku, ongezeko ni kubwa. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali, miundombinu iendelee kuboreshwa ili watu waendelee kuja, waendelee kutengeneza fedha, kwa sababu Dar es Salaam ndiyo mkoa unaoingiza uchumi mkubwa na unaongeza pato kubwa la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiacha shughuli za Uchumi, lakini tuna maombi ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam. Kazi kubwa imefanyika, lakini kuna vitu bado tunaomba. Tunaomba uboreshaji wa miundombinu ya barabara za ndani uongezeke kupunguza msongamano wa barabara kuu ambazo zinatumika na watu wanaoingia na kutoka mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dar es Salaam watu wote asubuhi wanatoka wanatawanyika kwenda kutafuta vipato, jioni watu

wote wanarudi. Kwa hiyo, tena barabara nyingi za ndani ili kupunguza msongamano na watu wafanye shughuli zao kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba pia kufunguliwa kwa barabara ambazo ujenzi unaendelea, barabara zile nyingi zimefungwa. Kwa hiyo, zilizokuwa zimekamilika waruhusu watu wapite kupunguza msongamano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, tunaomba taa za barabarani. Ni kweli taa zimewekwa, lakini kuna maeneo mengine tumeona taa zimewekwa, lakini bado hazina ubora. Ukiangalia mfano barabara ya Chuo Kikuu kupita Makongo – Goba kumeanza kuwekwa taa. Taa zile zimewekwa mbalimbali sana ukilinganisha na maeneo mengine, lakini bado ni taa ambazo hazina mwanga wa kutosha, kwa hiyo, inakuwa kama hazisaidii. Tunaomba mkandarasi anayeweka taa zile aboreshe, ziwekwe taa zenye viwango ambazo kweli zilete thamani ya taa za barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba pia uboreshaji wa mifereji katika ujenzi unaoendelea ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam, kwa sababu Dar es Salaam, ikinyesha mvua ndogo tu mafuriko. Kukishakuwa na mafuriko ndani ya barabara zile tayari inaleta msongamano mkubwa sana. Inakuwa changamoto kubwa kwa watoto wanaokwenda shuleni na hata watu wanaokwenda maofisini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi unaoendelea Dar es Salaam kwenye barabara nyingi umeinua vipato vya wananchi wa Dar es Salaam. Mama Lishe na Baba Lishe waliokuwa wanapika kilo tano kwa siku, sasa hivi wanapika mpaka kilo 30. Vijana wanaouza vinywaji (maji, juisi, na soda) walikuwa wanauza katoni mbili, tatu, sasa hivi wanauza mpaka 10. Kwa hiyo, tunaomba ujenzi uendelee. Tunatamani ujenzi uendelee, huku tunatamani ujenzi uishe, kwa sababu unavyoendelea, uchumi unaongezeka, ukiisha pia utakuwa na faida kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Wizara, tuna Barabara ya Kimara Mwisho kupitia Bonyokwa hadi Kinyerezi. Barabara hii tunaomba ijengwe kwa viwango cha lami kama Serikali ilivyokuwa imetaka ifanye, kwa sababu toka mwaka 2024, mkandarasi ametoa vifaa pale, wananchi wale walikubali kupisha kwenye maeneo yale bila kulipwa fidia, kitu ambacho ni kikubwa na kizuri sana. Sasa hawaoni kinachoendelea, wanaacha kufanya shughuli zao za kiuchumi, hawaendelezi maendeleo yoyote na hawana taarifa yoyote nini kinaendelea, toka mwaka 2024 mpaka leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikali iangalie barabara hii, imekuwa na msaada mkubwa sana na ina tija sana kwa wananchi hawa na ndiyo maana kwa hiyari yao wakapisha bila fidia. Tunaomba Mheshimiwa Waziri, hili lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tuna Barabara ya Msongola – Kivule – Kitunda - Banana na Barabara ya Majohe kwa Warioba na Majohe Ngozoma. Barabara hizi zimeharibika sana kutokana na mvua zinazoendelea ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Wizara, katika ukarabati unaoendelea, Mheshimiwa Waziri hapa alisema, ujenzi utaendelea baada ya mvua kwisha. Tunaomba hizi zifanyiwe haraka sana, zimekwamisha uchumi wa wananchi wa maeneo haya, watu hawafanyi shughuli zao, watoto wanashindwa kwenda shule na kufika kwa wakati. Mtoto anatoka nyumbani asubuhi saa moja, anafika shuleni saa nne, amepitwa na vipindi. Tunaomba hizi barabara ziangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna changamoto ya malori njia ya Bandari kwenda Kigamboni. Wananchi wanahama, wanaacha nyumba zao kwa sababu ya changamoto hii.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. JANETH E. MAHAWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru, na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, na Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, ajiandae.

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi, na kwa sababu ya muda tutapongezana baadaye. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Manyara ni mkoa wa nane Tanzania Bara kwa ukubwa na barabara za *TANROADS* ni kilometa 1,657. Zenye lami peke yake ni 259, na barabara kuu kati ya hizo ni 207, barabara za mkoa ni kilometa 52 peke yake ndiyo zenye lami. Sasa rafiki yangu Mheshimiwa Waziri Ulega, haiwezekani Mkoa wa Manyara, mkoa wa nane kwa ukubwa iwe na kilometa 52 peke yake, haiwezekani! *It is a big job*. Kwa hiyo, kwa kweli Wizara ikakae vizuri ilete fedha kwa ajili ya barabara za Mkoa wa Manyara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za *EPC+F* tulisaini mikataba tarehe 16/6/2023. Barabara ya Kongwa – Kiteto – Simanjiro - Arusha ilikuwepo kati ya barabara ambazo tulisaini mikataba na sifa zake mnafahamu. Barabara ya Kongwa inaunganisha Mkoa wa Dodoma, Manyara na Arusha. Sisi tumekubaliana hapa kwamba sera yetu, tuunganishe barabara za mikoa kwa mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Handeni – Kiberashi – Kibaya – Njoro – Chemba - Singida ilikuwepo kwenye barabara hii ya *EPC+F,* tulisaini mikataba tangu tarehe 16/6/2023. Tulifahamishwa kwamba kulikuwa na tatizo kwenye *EPC+F* na tukaelewa, lakini bajeti iliyopita walisema wameyeyusha mikataba na kwamba barabara hizi zitajengwa. Kwa ushauri wa kisheria wa bure kabisa, unaposaini mikataba, ni sharti uzijenge barabara hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameweka historia kuwa Rais wa kwanza aliyeweka fedha nyingi sana kwenye kilimo. Ni shilingi trilioni 1.2 bajeti ya mwaka 2025 na shilingi trilioni 1.1. Sasa hii maana yake nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, anataka kuacha *legacy* kwenye kilimo, lakini bila barabara inayotoa mazao hatutaweza kuwa tumemtendea haki Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuacha *legacy* ya barabara hiyo. Kwa hiyo, hizi barabara mbili za Tanga - Manyara mpaka Singida ni barabara za wakulima, ni barabara zitakazochochea kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wale Mawaziri kama hawataki kuelewa na ninaomba nimnukuu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, hapa alipokuwa Tanga, akizungumzia Barabara ya Kiberashi – Kiteto - Chemba mpaka Singida ninanukuu: "*Barabara hii ni muhimu sana kwa maendeleo yetu ya bandari. Nimezungumza na Waziri, hii barabara tuifanye kwa PPP, tusiwaachie Wizara ya Ujenzi, hii barabara haitakwenda haraka.*" Sasa kitu gani hakieleweki hapa, nukuu nzito sana, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan analifahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, anataka barabara hii ijengwe kwa haraka na kaagiza Wizara mbili: Ujenzi na Uchukuzi sasa kwenye bajeti ukurasa wa 217, Mheshimiwa Ulega bado anatuambia eti hii barabara ipo kwenye *PPP*, *it is not enough*. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alishatoa na hii kauli ni ya maelekezo. Rafiki yangu, huo ni ushauri mwingine wa kisheria. Tofauti ya ahadi na maelekezo, ushauri wa kisheria huo, *take it or leave it,* lakini ni ushauri. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, alivyokuja Mheshimiwa Waziri Mkuu na tumpongeze sana, alitumia barabara hii ya Kongwa mpaka Arusha karibu kilometa 453. Mwenyezi Mungu alitusaidia na mvua ikanyesha vizuri sana, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema hivi: "Nikirudi Dodoma nitaitisha kikao cha dharura haraka sana kwa ajili ya hii barabara." Mheshimiwa Ulega, hata hii kauli huielewi? Haya ni maelekezo, sawasawa! Yaani hapa leo

ningesema tutakamata shilingi, ninadhani hata Waziri Mkuu ataniunga mkono kwa sababu ya kauli hii. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua sisi ni waungwana sana, sasa msitake tuwe wakorofi. Jambo lingine la kisheria, unajua mimi na Mheshimiwa Ulega ni marafiki, sasa na kisheria huwa urafiki pia unakuwa *reviewed* ikiwa kama haueleweki eleweki hivi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunataka sana baadaye utupe kauli kuhusu barabara hizi mbili. Kwa hiyo, kwa kweli ninaunga mkono *with condition* kwamba utatupa baadaye kauli nzuri ya kuridhisha, ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Olelekaita.

Mheshimiwa Waziri, Barabara ile ya Dareda ndiyo haya anayoyasema. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa, Joseph Musukuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera, ajiandae.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Kwanza ninakupongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa ujenzi unaoendelea kwenye jimbo langu, kilometa 20, tunashukuru sana kwa sababu mkandarasi yupo *site*.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nimejaribu kusikiliza wachangiaji toka jana, kwa kweli kuna tatizo. Mimi ni Mbunge wa awamu ya tatu, Sheria hii ya *Road Fund* tulikuwemo mwaka 2019, ya ulinzi wa zile fedha za *Road Fund*. Sasa mara nyingi huwa tukisema tunaonekana kama hatueleweki, kwamba yalikuwa ni mawazo mazuri sana, watu walifanya *research* na sisi wengine wenye elimu za kawaida tukaungana na Mawazo, tukaweka ile sheria ya kulinda fedha zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kujiuliza, ikiwa mimi sijatoka Bungeni toka mwaka 2019, nimetoka tu kipindi cha uchaguzi 2020 na cha juzi, ni lini Bunge lilikaa likabadilisha hiyo

Sheria ya *Road Fund*? Kama kweli huu mhimili tunauheshimu? Tulitunga wenyewe, tunaweza kubadilisha wenyewe. Ni nani ameingilia mamlaka ya kwenda kutoa Mfuko wa *Road Fund* kutokupeleka fedha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunatoka vijijini na ninataka niwape stori moja. Samahani sana mdogo wangu Mheshimiwa Makonda, nina *message* hapa Mheshimiwa nitakufowadia. Jana kuna gari imepasua matairi pale kwenye mlima Saranda, mtu mmoja nadhani ni *fan* wangu, akanitumia *message* ile gari ilivyo na matairi yake *michelin* yalivyopasuka. Halafu akaniambia ninyi Wabunge, yaani sisi tunahangaika na mashimo, ninyi mnatuletea Rio Ferdinand, ndiyo nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kujiuliza, hivi vitu, ndugu zangu leo hii hebu ondoka hapa nenda Mwanza uone hii barabara, ukitoka tu hapa kwenda kupata kwao Waziri Mkuu, ukisalimika kupasua tairi una bahati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ondoka Singida nenda Arusha; ondoka Arusha nenda Tanga; ondoka Dodoma nenda Morogoro; ondoka Dodoma nenda Mbeya, nenda Songea. Ndugu zangu kama tulikaa wenyewe humu ndani tukapitisha shilingi bilioni 956 mpaka leo tunaenda kumaliza mwaka mmepeleka shilingi bilioni 212 na fedha mmeshakusanya zote. Sasa tuzungumze nini sisi Wabunge? Tuzungumze nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Rais, kama anatusikiliza, apange ziara ya kupita kwa mguu pengine labda wanampitisha kwenye ndege haoni huku chini. Mimi ningekuwa ninaweza kuwa-*convince* Wabunge, tunge-*cancel* mipango yote ya mwaka huu tukarabati kwanza hizi barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, mimi nimekuwa dereva miaka sita, ninaendesha basi kutoka Mwanza kwenda Dar es Salaam, wakati huo wa *rough road*. Sasa hivi kutoka Mwanza kwenda Dar es Salaam ni sawa na *rough road*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais, kafanya kazi nzuri ya kuifungua bandari yetu, tuna mizigo, tuna kila kitu, watu wote wanajua barabara za Tanzania ni nzuri. Ninataka niwaambie Watanzania na ndugu zangu Wabunge, ikiwa hizi nchi jirani zitatulia vurugu zilizonazo, watu wengi sana watatukimbia kwa sababu ya ubovu wa barabara kwenye bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni vizuri sisi kama Bunge, tuna uwezo, na tuna maamuzi, hatumshikii shilingi Mheshimiwa Ulega, maana hizi shilingi mwisho tutammalizia zote. Ningeshauri Wabunge, sisi kama Bunge, leo tukipumzika saa saba, Waziri Mkuu ni wa kwetu humu ndani, Waziri wa Fedha yupo humu, wakakae waje hapa wakati wa ku-*wind up* Waziri atatuambia fedha zinaenda lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa fedha wameshakusanya, wanazo shilingi bilioni 956, wanapeleka shilingi bilioni 211, haiwezekani. Haiwezekani, mtuhurumie! Tunaenda kujimwaga wote kutengeneza treni, ni jambo zuri sana, lakini wamefanya tathmini watu wangapi wanapita kwenye treni na watu wangapi wanapita barabarani?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajivuna tuna ndege, tunajenga *airport,* sawa. Watanzania wangapi wana-*afford* kupanda ndege? Wengi wapeni ambao wanapita kwenye barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuomba sana kwenye hili tusichukulie kama michango ya kawaida. Bunge tuna uwezo wa kusema tunahitaji majibu ya Serikali. Huyu Mheshimiwa Ulega hana fedha. Mwenyekiti, kasema jana tutamgawana, mpelekeeni fedha halafu tum-*sue* humu ndani. Mimi ni mwaka wa 15 sijawahi kuona Wizara ya Ujenzi inasulubiwa kama kipindi hiki tulichonacho kwa leo. Kwa nini hampeleki fedha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha wanakusanya, sheria tumetunga, halafu fedha haziendi! Ukienda kwenye akaunti ya *Road Fund,* leo kuna shilingi bilioni 56 mwezi wa Sita, mnatoboa tu

kidogo mnataka kuzipiga au mnataka kufanya nini? Achieni pesa tukatengeneze barabara za wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri, tusikubali kabisa kuipitisha hii bajeti kabisa, kwa sababu najiuliza, mimi ni mwana CCM, wapi tumefungwa kusema ukweli? Lazima tuwaombe kama mnamshauri vibaya Mkuu wa Nchi, basi mshaurini tunahitaji fedha. Sisi tunaoishi maisha ya barabarani tunajua shida tulizonazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ukisoma ukurasa wa 50 nimeona Mheshimiwa Ulega amekuja na hati fungani. Mimi ninamshauri siyo suluhisho. Tulikuwa na *Bond* ya Mama Samia, ilifanya vizuri kwa 170%. Ipo wapi *performance* yake? Leo tena amekuja na karatasi nyingine; niwashauri sana Waheshimiwa Wabunge, Serikali itusikilize; na Mheshimiwa Waziri Mkuu, saa saba mkakae hili ni suala ambalo linaumiza watu wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jaribu kutoka hapa leo kwenda kwako kule Babati Mzee Sillo uone barabara zilivyo. Tumetoka kwenye milima inayoua watu, tukaweka lami tukajisifu, tuziache tena jamani ziharibike hizi barabara! Tuliweka Sheria ya *Road Fund* ya kazi gani? Niwaombe sana Wabunge, tukaze ili leo tupate majibu kabla ya kumsulubu ndugu yetu Mheshimiwa Ulega hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, ninataka kutoa ushauri wa kitaalamu, mimi nimebobea kwenye usafirishaji. Mheshimiwa Waziri ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba dakika moja kama Profesa maana mimi ni daktari.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, malizia sekunde 30.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninafanya kazi ya *transport*, ninauliza kwenye mizani tunaongoza

Tanzania kwa foleni, lakini nimepita juzi ninafanya tathmini tu kwamba, wenzetu mlifikiria nini? Ninachukua mfano, gari za mafuta; ukinunua gari ya mafuta, lazima upeleke kupima *calibration* na Serikali ndiyo inapima. Huwezi kupakia zaidi ya *calibration* iliyoandikwa pale kwenye *depot* yenyewe ina mashine yake ambayo inapakia kufuata *calibration*. Imepimwa na Serikali, ina kibali cha Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu unaenda tena kwenye foleni, unaenda unapanga tena foleni masaa sita. Vile ni vitu vya mlipuko na ukijiuliza, nimekaa jana mzani mmoja ninajiuliza ngoja nione leo zinazozidi kama watashusha mafuta. Hakuna tanki, hakuna madramu, mnaweka foleni, jamani, mnahitaji akili ya ziada!

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Musukuma, tunashukuru.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, kama wanashindwa, waniazime mimi niwarekebishie haya mambo ili tuweze kwenda sawa. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Nilimtaja Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera, na Mheshimiwa Jesca David Kishoa, ajiandae.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu. Nimesimama hapa kwa heshima kubwa na taadhima kuomba kuhusu barabara yangu ya Kolandoto kwenda Mwang'ongo, maana dakika zenyewe ni chache.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii imekuwa ikiwekwa kwenye ilani tangu mwaka 2020. Vilevile tangu Mwaka 2020 imekuwa inatengewa fedha kidogo za bajeti, hata hivyo hakuna kitu chochote ambacho kimefanyika. Barabara hii ni ya muhimu sana kwa uchumi wa Jimbo langu la Kishapu na Wilaya yetu ya Kishapu, kwa ujumla ni barabara muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri. Yapo mambo mengine ambayo yako ndani ya uwezo wa Waziri na yako ndani ya uwezo wa *TANROADS*, lakini bado kuna mambo mengine ambayo kidogo yanakuwa yako nje ya uwezo wao. Ninamshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, alikuja kwenye barabara ile akaitembelea, akaikagua na kuona hali halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo ambalo lilikuwa halijawahi kutokea, hakuna Waziri ambaye ameshawahi kufika pale akafanya ukaguzi wa ile barabara akaona. Barabara hii inaunganisha wilaya kwa wilaya, lakini mpaka sasa, barabara ile ilikuwa haijawahi kuwekwa lami. Tuseme, kwa ujumla wake kwa historia, barabara ile haijawahi kuwekwa lami tangu uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana *TANROADS,* licha ya kazi nzuri ambazo inafanya, inafungua nchi, inasimamia barabara, hebu Mheshimiwa Waziri barabara yetu hii ya *TANROADS* ya kutoka Kolandoto, kupita Kishapu kwenda Mwangongo, ambayo ina kilometa 52.7 iweze kuwekwa lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wangu wamekuwa wakilalamika sana, wafanyabiashara wanabeba rangi zinamwagika, wafanyabiashara wa ujenzi wananunua *gypsum*, wanasafirisha kwenye barabara hii mbovu, *gypsum* zinavunjika. Hasara ambazo wamekuwa wakizipata, wafanyabiashara wengi wa aina mbalimbali, ni hasara kubwa sana. Ninaomba sana Wizara hii iichukulie barabara hii kwa uzito unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alipita kwenye jimbo langu mwaka 2025, tarehe 19 akasema, baada ya kusikiliza historia hii kwamba, barabara hii haijawahi kupata lami tangu uhuru, sasa hivi inakwenda kujengwa kwa lami. Ninaomba kwa heshima na taadhima, *TANROADS,* na Wizara hii ya Ujenzi, iweze kutimiza wajibu wake kwa kujenga barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo barabara nyingine ambayo ni ya muhimu sana kwa uchumi wa Kanda ya Ziwa. Barabara hii inakwenda kuwa muhimu kwa mikoa zaidi ya sita kwenye Kanda

ya Ziwa; hiyo ni Barabara ya Igunga – Igurubi – Manonga – Ukenenge, kupita Kolandoto, yenye urefu wa kilometa 90. Barabara hii, endapo kama ikitokea changamoto yoyote maeneo ya Igunga na Nzega, ndiyo *alternative*. Ninasikitika kwamba, barabara hii haipo kwenye mpango. Ninaomba Wizara iiweke barabara hii kwenye mpango ili iweze kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kwa heshima zote na mapenzi yote tumpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akiifanya kwa kutenga fedha nyingi kwenye barabara. Nchi hizi za kimaskini, hasa za Kiafrika, ambazo zinakuwa na changamoto na *priorities* nyingi wakati, mwingine tunaweza tukalaumu kwamba, hiki hakijafanyika na hiki kimekwenda hivi. Mambo ni mengi, matatizo ni mengi na kila kitu ni cha muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tukizungumzia *SGR*, ni ya muhimu, tukizungumzia hiki ni cha muhimu. Tukizungumzia umuhimu wa barabara, kila mtu atasema Dodoma ni muhimu, mwingine atasema huku ni muhimu. Kwa hiyo, ninaomba Waheshimiwa Wabunge leo tumpitishie Mheshimiwa Ulega, mambo huwa yanakwenda na maendeleo huwa yanafanyika taratibu. Tupitishe hii bajeti, hata, hivyo kama ni kusikia Serikali imesikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana, kwa heshima zote na mapenzi yote, kama ni kusikia, kama ni kupigwa nondo wamepigwa za kutosha; kama ni kusemwa, wamesemwa vya kutosha na kwa kweli, ambaye atakuwa hajasikia atakuwa ana matatizo ya uziwi. Ahsante sana.

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Sitaki taarifa zako na wewe! Hebu kaa chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea kumalizia jambo moja kwa sababu, muda hautoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine ambalo ninapenda kuzungumzia.

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lucy, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Sigrada Mligo.

TAARIFA

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumpa taarifa mzungumzaji kwamba, yeye sio mamlaka ya kuizungumzia Serikali, itakuja itazungumza yenyewe. Yeye azungumze matatizo yake na asitushawishi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lucy, Taarifa unaipokea?

MHE. LUCY T. MAYENGA: *Mheshimiwa Naibu Spika, huyu hajitambui, hata kumjibu nitapoteza muda. Ninataka nizungumzie jambo moja.* **[MANENO HAYA SIYO SEHEMU YA TAARIFA RASMI ZA BUNGE]**

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba…

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lucy kwa kusimamia kanuni...

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei. Ni kwamba, jambo hili, sisi ni Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, hatuwezi kusema kwamba, hatuwezi kuizungumzia Serikali, pale ambapo inatakiwa kuzungumzwa lazima tuseme. Ni lazima tuseme, hatuwezi kunyamaza tu hivi hivi, kimyakimya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ninapenda kumalizia ni suala la ubora wa barabara. Wananchi wengi, hasa Wabunge, wamezungumza kwa machungu makubwa sana kwamba, ubora wa barabara kwa kweli unasikitisha. *Lifespan* ya barabara imekuwa ya muda mfupi, nadhani hili lingezingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja, bajeti itapita, mambo yatakwenda na kazi ziendelee. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lucy ameshamaliza muda wake wa kuchangia.

Sasa ninamwita Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera, atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Kishoa. Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoa, ajiandae.

MHE. MGORE M. KIGERA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Ninapenda dakika chache hizi, kwanza nitoe pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaifanya kuhakikisha miundombinu ya barabara inaendelea kuimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana tumesikia hapa kilometa 1,495 zimeweza kujengwa kwa kipindi cha Awamu ya Sita, na hapa bado ana miaka mingine minne mbele. Ninaona Mheshimiwa Rais anakwenda kuvunja rekodi katika ujenzi wa barabara za lami nchini Tanzania. Tumesaini juzi mkataba wa kujenga barabara ya njia sita kutoka Dodoma kwenda mpaka Chamwino. Hiyo ni kazi nzuri inayofanywa na MheshimIwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ninawapongeza Wizara ya Ujenzi, chini ya Waziri wetu Mheshimiwa Ulega, pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Kasekenya, Katibu Mkuu na Naibu wake na watendaji wote wa *TANROADS* Tanzania nzima wakiongozwa na Mtendaji Mkuu, kaka yangu Besta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamesimama hapa wakiongea kuhusu barabara. Ni kweli kitovu cha uchumi wa nchi yetu ya Tanzania ni barabara. Wakulima wanatumia barabara ambazo ni *gravel* na tunazo barabara za lami, hata hivyo barabara zote, ili ziweze kuendelea

kuimarika, tunahitaji tupate fedha. Huyu Mheshimiwa Ulega huyu, watashika shilingi, watamkata masikio, lakini bila fedha kwenda Wizara ya Ujenzi, hakuna kitakachoweza kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia mwaka 2025/2026 shilingi bilioni 945 zilitakiwa zitoke kwenye Mfuko wa Barabara, zimetoka shilingi bilioni 418, sawa na 44% tu, 56% fedha hazijaenda. Utekelezaji wa miundombinu utafanyikaje? Siyo ujenzi wa barabara mpya, wala siyo kufanya *maintenance* ya barabara zetu; ni kweli barabara ni mbovu sana, tunahitaji fedha. Ninaomba Serikali ipeleke fedha Wizara ya Ujenzi, fedha zinavyokusanywa ziende zilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamekuja na mpango wa kusema kwamba, inatakiwa asilimia tano iende kwenye maeneo mengine. Mimi sijawahi kuona mtu anaenda kuomba jamvi msibani; yaani wewe una msiba, mtu anakuja kukuomba jamvi! Wizara ya Ujenzi hapa inapumulia mashine, tena itolewe asilimia tano iende maeneo mengine. Sidhani kama hii ni sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itafute maeneo mengine ya kutoa *fund* iende kusaidia maendeleo mengine na fedha za Mfuko wa Barabara ziachwe kama zilivyo, ili ziendelee kutengeneza barabara zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ametoka kuongea hapa Mheshimiwa Musukuma, ni kweli, kutoka Dodoma mpaka ufike Jimboni kwangu Musoma, kama haujapasua tairi mbili, una Mungu ndani yako. Ni kwa sababu, Wizara ya Ujenzi haina fedha, wanashindwa kufanya chochote. Ninaomba Serikali ipeleke fedha Wizara ya Ujenzi, na hili ninalisisitiza, tunaomba fedha ziende Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niongee kuhusiana na madeni ya wakandarasi. Katika watu wenye matatizo dunia hii, hasa nchini Tanzania, ni wakandarasi tena wa ndani. Wakandarasi wa ndani wanadai fedha nyingi sana, na yote inatokana na fedha kutokwenda kwa wakati, ndiyo maana wakandarasi wanakuwa wanadai.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisikia *depression*, wakandarasi; *pressure*, wakandarasi; sukari, wakandarasi; vifo, wakandarasi; watu kuuziwa mali zao, wakandarasi; kwa sababu, wanafanya kazi hawalipwi. Ninaomba Serikali ije na mpango mzuri wa kuona ni wapi itaenda kupata fedha, na Serikali yetu inaaminika, hata kama ni kwa kukopa waweze kuwalipa wakandarasi madeni yao yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ujenzi inashindwa ku-*perform* kwa sababu, fedha inaingia *for instance* shilingi trilioni moja, katika trilioni moja inayoenda kufanya *projects* ambazo ni *current,* unakuta ni shilingi bilioni 300, 400; shilingi bilioni 600, 700 inaenda kulipa madeni. Tutawezaje ku-*execute* kazi vizuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, madeni ya wakandarasi yaje na mpango mzuri waweze kulipwa, tuokoe maisha ya wakandarasi. Tunapoteza *dignity* ya wakandarasi wetu wa ndani kwa sababu yao, leo mkandarasi haaminiki, huwezi kwenda sehemu kukopa akakubalika. Wanajua hata wakimkopesha, kuja kulipa ni changamoto. Serikali ilizingatie hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niweze kuchangia kwenye upande wa Jimbo langu la Musoma Mjini. Mimi kwanza ninaishukuru Serikali, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kutuletea shilingi bilioni 35 ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Musoma, ujenzi wetu umefika 67%. Ninaomba sasa Waziri atusaidie, huyu mkandarasi ana *certificate* yake ya shilingi bilioni 1.9, amlipwe, ili hizi 33% zilizobaki zikamilike na uwanja huo uweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea pia kuomba kuhusiana na Jimbo langu la Musoma Mjini. Barabara ya lami ninayo kutoka Nyabange mpaka Musoma Mjini, ila kwenye Kona ya Nyasho tuna changamoto ya mafuriko. Kila mvua ikinyesha wananchi wa Musoma Mjini wanateseka na mafuriko makubwa pale Kona ya Nyasho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Daraja la Kona ya Nyasho liweze kufanyiwa ufumbuzi, watujengee daraja pale ili

tuepukane na mafuriko katika eneo hilo. Ninaomba pia, hili lielekee upande wa *TEMESA*. Mheshimiwa Waziri tuna Kivuko chetu pale cha Kinesi, kile kivuko kwanza kina injini moja, *anytime* mnaweza mkasikia maafa yametokea katika Jimbo la Musoma Mjini na Rorya kwa sababu, kivuko kile siyo rafiki. Tumeshaomba na tuliahidiwa kwamba, tutaletewa kivuko kingine, mpaka leo kivuko hakijaja. Wananchi wanapata changamoto kubwa kuhusiana na kuvuka kutoka ng'ambo ya Musoma kwenda Kinesi na kutoka Kinesi kuja Musoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Mheshimiwa Waziri, kaka yangu, nina imani bajeti yake itapita vizuri kwa sababu, changamoto ni fedha huletewi, ila ninachoomba akija ku-*wind up* hapa, atuambie maafa yanayoweza kutokea *anytime* pale Kinesi, anakuja kuya-*rescue* vipi, kwa sababu, tunahitaji kivuko, kwa ajili ya wananchi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni walioko Bungeni asubuhi hii. Tunao wageni 50 wa Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule. Hawa ni Wanafunzi na Walimu wa Shule ya Awali na Msingi Rhema ya Jijini Dodoma. Karibuni sana Bungeni.

Wageni 35 wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, ambao ni Wanakwaya wa Umoja wa KKKT kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana Bungeni.

Wageni waliotembelea Bunge, kwa ajili ya mafunzo. Tunao wanafunzi 92 na waalimu nane wa Shule ya Sekondari Elishadai kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana Bungeni.

Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Jesca David Kishoa, atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma. Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, ajiandae.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa

nguvu na afya njema, mpaka leo nasimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuchangia hotuba hii ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, kama ambavyo wengi wetu wametangulia, kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika Taifa hili na kutuongoza kwa umaridadi mkubwa sana. Pia, ninachukua fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa kaka yangu, Mheshimiwa Ulega, Waziri wa Ujenzi, kwa hotuba yake nzuri iliyosheheni mambo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pekee nimefurahishwa sana na Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi mimi pamoja na wananchi wangu wa Wilaya ya Mkalama, Jimbo la Iramba Mashariki, baada ya kuona barabara yetu kilometa 89 kutoka Iguguno kupitia Nduguti na kuendelea imetajwa kwenye bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara yetu ile ndiyo moyo wa wananchi wa Mkalama. Barabara ile ndiyo uti wa mgongo wa wananchi wa Mkalama. Nimefurahi sana kuona imetajwa, na ninasema tu, hivi karibuni nimepata ujumbe kutoka kwa Meneja wa *TANROADS,* Mkoa wa Singida, ambaye ni mchapakazi kweli kweli. Amenijulisha kwamba, siku chache zijazo anakwenda kutangaza upya tenda za kilometa 10 ambazo zinakwenda kuvuruga kwa mkeka mweusi *centre* ya Nduguti, Wilaya ya Mkalama. Naishukuru sana Serikali, naishukuru sana Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi letu ni moja tu. Tunaomba jambo hili, mchakato huu, uwe kwa haraka, usisuesue kwa sababu, tunahitaji sana barabara hizi. Sina wasiwasi kabisa na Mheshimiwa Waziri; sina wasiwasi na watendaji wake wote akiwepo Mkurugenzi wa *TANROADS* Tanzania; ninaamini kabisa mambo haya yatakwenda kufanyika, ujenzi huu utakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutumia fursa hii kuipongeza sana Kamati ya Miundombinu. Hotuba hii ni nzuri na imetupa mwanga sisi Wabunge kuweza kuishauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja ya Kamati inayotaka mfuko. Inapendekeza fedha za mfuko wa barabara zielekezwe kwenye matumizi yaliyokusudiwa kwenye barabara, yaani tusiwe na *reallocation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiruhusu *reallocation* kwenye fedha hizi, hiyo asilimia tano ni wazi kabisa *TANROADS* itakufa na haitaweza kujisimamia. Ni muhimu sasa Serikali ikaona umuhimu wa kuifanya *TANROADS* kuwa na *full financial autonomy*, ikawa na mamlaka kamili ya kifedha, ili kuweza kuiwezesha kutekeleza shughuli zake za ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili sisi hatutakuwa wa kwanza. Nimetazama nchi mbalimbali, ziko nyingi, lakini kwa sababu ya muda, nitataja nchi mbili. Mfano, *South Africa* wana shirika lao linaitwa *SANRAL,* yaani *South African National Roads Agency Limited*. Shirika hili lina *full authority*, lina uhuru kamili wa kifedha. Shirika hili linakusanya ushuru na kupokea fungu la matengenezo bila kupitia urasimu wa hazina yake. Hii ndiyo imesababisha barabara nyingi za *South Africa* zinakuwa na ubora zaidi Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi hatutakuwa wa kwanza, kuna nchi ya *New Zealand*, hii inaitwa *'The Gold Standard'*. Wao wanatumia mfumo unaitwa *NLTF,* yaani *National Land Transport Fund*. Sheria yao waliyoitunga inakataza kabisa Wizara ya Fedha, pamoja na Hazina kuingilia kwa vyovyote vile makusanyo yanayogusa fedha za barabara. Wanakusanya kwenye kodi ya mafuta na wanapeleka moja kwa moja kwenye mfuko wao, hawataki kabisa mfuko ule uguswe. Kwa nini sisi tusifanye hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, nimeangalia ripoti, inaonesha Tanzania imewahi kuwa kwenye rekodi kubwa miaka 20 iliyopita kwa kupeleka makusanyo ya bajeti kwa kiwango kile kile kilichokusanywa kikapelekwa kwenye Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma ripoti ya *Road Fund Board Secretariat* ya Mwaka 2005 na ninayo. Ripoti hii ilikuwa ina lengo la kuonesha mwenendo wa kibajeti wa kifedha toka mwaka 1997 mpaka 2004. Ripoti inaonesha kwa miaka mitatu ya

fedha, mfululizo, kuanzia mwaka 2001/2022 bajeti, mwaka 2022/2003, 2003/2004 Wizara ilipeleka kiasi chote, 100% ya kiasi kilichokuwa kinatengwa kwa ajili ya barabara. Sasa ni kwa nini sasa hivi tunashindwa kufanya hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi zinakusanywa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, muda umeisha, malizia.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja, lakini ninaiomba Serikali, fedha zote za Mfuko wa Barabara zipelekwe kwenye vipaumbele, zisipelekwe kwenye vipaumbele vingine. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, Mheshimiwa Jonas William Mbunda ajiandae.

Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa.

MHE. AGNES M. MARWA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kwa kuwashawishi wenzangu kwamba tumpitishie Mheshimiwa Waziri Ulega bajeti hii kwa sababu kwanza amekuwa ni Waziri wa kwanza ambaye anajituma, anakwenda Wilaya kwa Wilaya, Jimbo kwa Jimbo na anapambana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tunatakiwa tujue kwamba haya mambo ameyarithi tu, ameyakuta na kikubwa ni kwamba hapewi fedha za kutosha. Kwa hiyo, niseme tu viboko wamekutandika sana Mheshimiwa Ulega na wewe ukiingia kwenye vikao, basi nenda ukawe mkali. Wamekuchapa sana, wamekutandika sana, lakini hata tukikutundika, haina maana. Maana yake ni kwamba tusipokupitishia, na hizi ndogo au chache zilizopo, basi kazi zisifanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niende moja kwa moja kwa kusema, ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge wangu wa

Musoma Mjini Mheshimiwa Muhongo, ameiongelea sana jamani barabara yake ya Musoma - Makojo - Busekera, hadi imefika hatua yaani sasa, ninaona kama anaona huzuni hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama Mbunge wake, na mwananchi wake wa Musoma, ninaomba sana Serikali iiangalie hii barabara kwa jicho la huruma. Kati ya barabara zote nchi nzima, Mheshimiwa Rais alizosema kwamba ziunganishwe Wilaya kwa Wilaya, imebakia Wilaya ya Musoma Vijijini na Wilaya ya Musoma Mjini peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ndiyo ambao hazijaunganishwa barabara na barabara, pamoja na kuwa Mheshimiwa Rais amefanya kazi nzuri sana na baadhi ya maeneo mkoani kwetu Mara kwa kweli, amefanya mambo mazuri sana tunampongeza na barabara zipo baadhi ya maeneo, lakini kwa eneo hili la Musoma Vijijini basi tuonewe huruma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hizi kilometa 92 jamani kilometa tano tu! Ni kweli kwamba wengine wanapata mpaka barabara za vichochoro, wanapata barabara za kuunganisha mpaka barabara hizi zinazotoka Benki ya Dunia. Jamani, sisi hii barabara moja tu basi angalau tujaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Rais huko aliko, aniangalie mtoto wake, binti yake Bungeni pekee, mtoto wa Chifu Hangaya, barabara inayokwenda nyumbani kwetu Musoma Vijijini Majita, Mheshimiwa Rais, ninaomba angalia mama, kwenye mfuko tu wa ziada, basi angalau na mimi binti yako niwe ninaenda kwetu ninajitapa au ninatamba kwamba mtoto wa Rais nimekuja Musoma Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna hili daraja la Nyasahungu na daraja la Suguti. Juzi Mkuu wetu wa Mkoa imebidi ashuke atembee kwa miguu, bahati nzuri Mheshimiwa Mtambi, Mkuu wetu wa Mkoa ni Mwanajeshi, yuko vizuri, ikabidi apite pale. Hili daraja limeleta maafa mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwomba sana Waziri, rafiki yangu Mheshimiwa Ulega, ndugu yangu, yeye ni mchapakazi, basi angalie. Ninaamini kabisa bajeti siyo msahafu, inaweza ikarekebishwa na baadhi ya maeneo, wakatuongezea fedha basi na sisi tukajengewa hata madaraja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Waziri Ulega anakumbuka juzi juzi amekuja Tarime, katika msafara wake kuna gari yake ilipata pancha katika barabara zetu, angalia hii barabara ya Tarime - Mugumu. Hii barabara kwetu sisi ni barabara ya kiuchumi, pia inaleta watalii, inapitisha watalii, lakini ni barabara mbovu. Hii ndiyo barabara ambayo hata Mheshimiwa Musukuma juzi alitucheka. *Imagine*, mpaka Wabunge wenzetu wanatucheka jamani Mkoa wa Mara! Kwani sisi tuna matatizo gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika kwetu ndiyo ametoka Mwasisi wa Taifa hili Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Kwa kweli najisikia uchungu, nataka hata kulia. Roho inaniuma sana kuona kwamba sisi tulimtoa Mwasisi wa Taifa hili, lakini pia bado miundombinu kwetu inakuwa ni migumu. Jamani, Mkoa wetu wa Mara ndiyo ungekuwa kivutio, Mkoa wetu wa Mara ndiyo ungekuwa wanasema kwamba jamani, tunataka kwenda kuangalia Mkoa wa Mwasisi wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana Wizara zituangalie, tunaomba na sisi pia tuangaliwe ndugu zetu, basi na sisi angalau tuonekane tumetoka Mkoa wa Mara. Tunajitahidi sana kama mnavyotuona angalau kupambana kuogaoga hivi, lakini kwetu kule tunaoga vumbi. Barabara bado ni vumbi jamani. Sisi tutajitapia nini tuliotoka kwa Mwasisi wa Taifa hili? Kwa hiyo, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri Ulega nenda kaangalie na Wizara yako basi mrekebishe hizi barabara angalau zipitike.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Wabunge wenzetu wanatucheka, tunajisikia vibaya. Juzi ilibidi twende tukajifungie pamoja Wabunge wa Mkoa wa Mara tulie, kwa sababu haya mambo kwa kweli tulikuwa tunaongea kwa uchungu sana. Kwa hiyo, niwaombe sana ndugu zangu mtusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kuna hospitali yetu ya Kwangwa, ile ni hospitali ya rufaa. Hospitali ambayo Mama yetu Samia Suluhu Hassan katenga fedha nyingi sana, lakini ndiyo hospitali ambayo haipitiki. Ukienda pale hospitalini, juzi mwenezi CCM wa Taifa Ndugu Kihongosi alikuwa na ziara, akiwa na ziara hata hajafika mwisho, gari ya mwisho ikapata pancha katika gari zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri aangalie jinsi ya kurekebisha mambo haya kwa sababu bajeti siyo msahafu, inaweza ikarekebishwa na sisi Mkoa wa Mara tunatamani kujulikana kwamba Mwasisi wa Taifa hili ametoka Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nimemtaja Mheshimiwa Jonas William Mbunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Chacha Mwita Wambura na Mheshimiwa Christina Solomon Mndeme ajiandae.

MHE. JONAS W. MBUNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika bajeti hii ya ujenzi. Awali ya yote, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na afya njema, na leo nimepata nafasi ya kuchangia bajeti hii ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana mtani wangu, Mheshimiwa Ulega kwa hotuba nzuri ambayo ameiandaa pamoja na wasaidizi wake na ina mambo mengi, lakini changamoto ninayoiona kubwa ni namna gani anawezeshwa ili kuhakikisha kwamba anaitekeleza hiyo bajeti yake? Kwa hiyo, niwaombe Wabunge wenzangu tushirikiane tuiagize Serikali itoe fedha ziende katika Wizara ya Ujenzi ili Mheshimiwa Ulega aweze kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu kuna barabara ya kutoka Mbinga - Myangayanga – Litembo. Barabara

hiyo ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais. Barabara hiyo ni barabara muhimu sana kwa sababu wakulima wa maeneo ya Litembo na maeneo mengine wanalima kahawa na hiyo barabara ni kama barabara inayosaidia sana kuhakikisha kwamba mazao haya yanafika katika eneo la Mji wa Mbinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri katika mikakati yake na mipango yake yote kuhakikisha kwamba barabara hiyo inajengwa na itakuwa imekidhi na kutimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kuna barabara ya kutoka Mbinga - Pachani – Longa kilometa 10. Kipande hicho kinaleta changamoto kwa sababu ukitoka Longa kwenda Rundumato, barabara hiyo imejengwa kwa kiwango cha lami, lakini kutoka Pachani mpaka Longa barabara hiyo ni ya vumbi na inasumbua sana wakati wa kipindi cha mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wananchi wa Mbinga wamenituma nimwombe Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba barabara ile inajengwa ili wananchi wale waweze kupata neema na matunda ya uhuru wa nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2025 nilipata bahati nikawekewa baadhi ya taa za barabarani pale Mbinga Mjini. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri katika mikakati yake ahakikishe kwamba Mji wa Mbinga unaendelea kumeremeta kwa kuwekewa taa za barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ni muhimu sana kwa Wananchi wa Mkoa wa Ruvuma ni Barabara ya kutoka Songea - Njombe hadi Makambako. Barabara hiyo ilijengwa mwaka 1984 na kampuni ya *Balfour Beatty* na ina umri wa miaka zaidi ya 30 inaelekea 40, lakini barabara hiyo inatumika kwa ajili ya kusafirisha makaa ya mawe, mazao mbalimbali ya kahawa na mahindi, na sasa hivi imeharibika na inaleta ajali nyingi sana katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Ulega katika mikakati ambayo imewekwa, tunajua kuna mpango wa kuanza kujenga kilometa 100, lakini mpaka sasa hivi, kazi hiyo haijaanza. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali, kuweka msisitizo kwa kuhakikisha kwamba barabara hiyo inaanza kujengwa ili wananchi wa Mkoa wa Ruvuma waweze kuitumia kwa kusafirisha makaa ya mawe, kusafirisha kahawa, mahindi na mazao mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ambayo ipo kwenye Wizara hii ya ujenzi ni Taasisi yetu ya *TEMESA* huwa inashindwa kulipa wazabuni. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, pamoja na mikakati yote aliyonayo, ahakikishe kwamba wazabuni wanalipwa ili waendelee kutuhudumia na kutoa huduma nyingi katika maeneo yetu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Jonas William Mbunda kwa kutumia muda vizuri sana. Nimemtaja Mheshimiwa Chacha Mwita Wambura, atafuatiwa na Mheshimiwa Christina Solomon Mndeme, Mheshimiwa Kakulu Burchard Kakulu ajiandae.

MHE. CHACHA M. WAMBURA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara yetu hii ya ujenzi. Awali ya yote nianze kumshukuru Mungu kwa kutupa uhai sisi sote humu ili basi tuweze kutimiza hili jukumu ambalo tumepewa na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee sana nimpongeze na nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi ambavyo ameendelea kusimama na kutuongoza Tanzania na hata hizi barabara ambazo tunaziongelea leo zimeendelea kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wote humu ndani wamezungumzia barabara; na kilio cha Watanzania walio wengi

ni barabara. Siyo *TANROADS* na siyo *TARURA*, kote huko ni barabara zimetenganishwa tu, lakini ukiangalia Tanzania kilio kikubwa ni barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatambua kwamba mkate wa Taifa ni mdogo na kwa sababu mkate ule tunagawana kidogo kidogo, wakati mwingine hautoshi. Hautoshi kufikia malengo yale ambayo kila mbunge aliyeko humu ndani angetamani kwenye Jimbo lake kiweze kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane sana na Kamati na niipongeze Kamati kwa kazi kubwa ambayo imeifanya. Hamna muujiza utakaotendeka kutengeneza barabara zote zile kama hatuna fedha. Hatuwezi tukapiga magoti tukaomba kesho yake barabara zikawa zimetengenezwa; tutatengeneza barabara hizi iwapo tu tutakuwa na fedha za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa nini ninaungana na Kamati? Kamati ushauri mmojawapo ilioutoa ni kufikiria na kugundua vyanzo ambavyo vitaongeza mapato ili barabara zetu ziweze kutengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sisi ni Watanzania, lakini pia ni Wabunge. Tukubaliane kwamba, ni lazima tutafute vyanzo, na vyanzo hivyo wakati mwingine vitaumiza, wakati mwingine vitaongeza gharama, lakini tutaangalia kipaumbele tunataka nini? Tunayo bandari, tunakusanya fedha huko kwenye bandari, tunazo sehemu nyingi ambazo tunaweza tuka-*adjust* kidogo tu, changamoto zikipatikana, lakini tuta-*solve* tatizo. Hatuna mtu wa kutusaidia, ni sisi Watanzania tunatakiwa tujisaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kupata vyanzo vya mapato na kuongeza, hizo fedha tukizipata na kwa sababu ni kwa ajili ya barabara, tuweze kuzilinda ili ziweze kwenda kufanya kazi iliyokusudiwa. Kama tutakusanya na tukalinda zikafanya kazi iliyokusudiwa, kiukweli tutapiga hatua kiasi; tunaweza tusimalize leo, lakini kesho na keshokutwa tukamaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, tunashauri na Kamati nayo imeshauri kwamba tuwe na uwezekano, miradi ambayo imeshaanza tusikusanye mingi. Tunakusanya halafu mwisho wa siku hatuna bajeti. Tutengeneze ile ambayo imeshaanza, tutengeneze ile ambayo tulishasaini mikataba, ili basi ikamilike hata kitu kionekane, kuliko kuwa tunafanya vipande tunaachia njiani, vipande tunaachia njiani, matokeo yake kila sehemu ni kelele na hakuna kilichofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona nchi nyingine kuna barabara zipo za kulipia. Hii *PPP* ambayo tunasema tuiitekeleze kwa vitendo, ili mwisho wa siku tusiwe tunasema tu. Tukija hapa tunasema, lakini hakuna mradi ambao tunaufanya wa hizi *PPP*. Tutafute watu wenye fedha ambao wanaweza kushirikiana na Serikali. Sehemu zile ambazo kunaweza kufanyika kibiashara hizi barabara tujenge kwa *PPP* ili mwisho wa siku, tuweze kuipunguzia mzigo Serikali na tuweze kupata barabara nyingi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali watakapokuwa wanakuja kuhitimisha, watupe *commitment* ya kutafuta vyanzo ambavyo aidha vinaumiza kidogo au haviumizi ambavyo vitaongeza mapato twende tukatengeneze barabara. Vilevile Mheshimiwa Waziri atupe *commitment* ya kulinda hizi fedha ambazo zinakusanywa kwa ajili ya Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kidogo kuhusu Geita. Nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa daraja kubwa ambalo alilikamilisha la Kigongo – Busisi, angalau sasa hivi una uhakika wa kutopanga foleni sana unapokwenda Mwanza, lakini sisi Geita hatujawahi kuunganishwa na Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo barabara ambayo toka mimi nakua, tumekuwa tukiambiwa inatengenezwa kwa kiwango cha lami, lakini mpaka sasa hivi tunavyozungumza haijatengenezwa. Tarehe 1/10/2025 ulisainiwa mkataba wa kuitengeneza ile barabara. Ukiangalia kutoka Kahama mpaka Kakola, mwekezaji ametengeneza, lakini kutoka Kakola mpaka

Geita hiyo barabara haijatengenezwa. Mkataba umesainiwa, fedha za kumlipa mkandarasi *advance* imekosekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba *commitment* ya Serikali, hizi fedha ni lini zitaenda kulipwa ili ile barabara kiukweli itengenezwe ili na watu wa Geita waweze kunufaika na hizi barabara zinazounganisha Mkoa na Mkoa.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwambura muda umeisha.

MHE. CHACHA M. WAMBURA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana, kwa kunipa nafasi, ninaunga mkono hoja na ninaomba *commitment* ya Serikali kwenye hayo ambayo nimeyaongea.

MHE. ADO S. ADO: Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ado, mwongozo wa Spika kwa kifungu gani?

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. ADO S. ADO: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa Kanuni ya 79 inayowapa nafasi Wabunge kuomba Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa endelea.

MHE. ADO S. ADO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Kama nilivyoitaja Kanuni hiyo inatupa nafasi ya kusimama muda wowote kuomba mwongozo kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama linaruhusiwa ama la.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda mfupi uliopita, Mbunge Sigrada Mligo alitoa taarifa na wewe ulimwelekeza mchangiaji

Mheshimiwa Lucy Mayenga kama anaipokea au haipokei taarifa hiyo, badala yake Mheshimiwa Mayenga alisema kwamba Mbunge Mligo hajitambui.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka Mwongozo wa Spika kwa kuzingatia kwamba Bunge hili pamoja na mambo mengine linaongozwa na mahitaji ya lugha ya kibunge. Iwapo kauli hiyo kwamba Mbunge hajitambui inaruhusiwa katika Bunge hili na kama inakidhi masharti ya Kanuni ya 74(1)(j) ambapo pamoja na mambo mengine inazuia Mbunge yeyote kumsema vibaya Mbunge mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Ado Shaibu akiomba Mwongozo wa Spika kwa kutumia Kanuni yetu ya 79, kuhusu Mheshimiwa Sigrada alipotoa taarifa kwa mchangiaji Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga.

Waheshimiwa Wabunge, kama utakumbuka Mheshimiwa Mbunge wakati Mheshimiwa alipopewa taarifa, nilimwuliza kama taarifa hiyo anaipokea au haipokei, lakini alisema taarifa haipokei. Kwa hiyo, Mwongozo wa Kiti ni kwamba baada ya kusema kauli hiyo, alihojiwa na Kiti kwa mujibu wa Kanuni, taarifa anaipokea au haipokei na Mheshimiwa Mbunge alisema taarifa haipokei.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo Mwongozo wa Kiti. Tunaendelea. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilimtaja Mheshimiwa Christina Solomon Mndeme, atafuatiwa na Mheshimiwa Kakulu Burchard Kakulu, Hija Hassan Hija ajiandae.

MHE. CHRISTINA S. MNDEME: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuboresha miundombinu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto za miundombinu ni nyingi na mahitaji ni mengi, lakini Mheshimiwa Rais wetu anafanya kazi kubwa kuhakikisha kuwa barabara, madaraja, makalvati, mifereji na kila kitu kinakuwa sawa kulingana na uwezo. Tunampongeza sana Rais wetu. Tanzania ya leo siyo Tanzania ya jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kubwa kwa Mheshimiwa Waziri Ulega pamoja na timu yake yote. Ninampongeza sana kwa kazi kubwa anayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais wetu kipenzi na chaguo la Watanzania. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wake wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru sana Serikali yetu pendwa kwa kutuboreshea miundombinu Mkoa wa Tabora, kwani Tabora ya leo siyo Tabora ya jana. Sasa Tabora inafikika kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka mingi Mkoa wa Tabora ulikuwa haujaunganishwa na barabara za lami, ilikuwa ni vigumu kuufikia mkoa wetu, lakini sasa hivi kwa siku moja unaweza ukafika ndani ya Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Tabora haukuwa na hata taa za barabarani. Sasa hivi taa za barabarani tunazo. Tabora tulikuwa tuna matatizo sana ya barabara ambazo zilikuwa hazipitiki kwa mwaka. Sasa hivi kiwango kimeongezeka. Zipo ambazo tumeongezewa, zinapitika kwa mwaka mzima. Tumeongezewa madaraja, tumeongezewa makalvati, tumeongezewa mtandao wa barabara ya lami ndani ya Mkoa wetu wa Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, palipo na mafanikio hapakosi changamoto. Ninaomba kuishauri Serikali kufanya mambo yafuatayo. Pale ambapo hali itaruhusu ili kuendelea kuboresha miundombinu ya barabara ndani ya Mkoa wa Tabora na kurahisisha usafiri na usafirishaji, nami kwa namna ya pekee ninawashawishi Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuipitishe bajeti hii ili yale ambayo tunayaomba yakatekelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba tuweze kujengewa barabara ya lami ya mchepuo *(bypass)* kutoka Kigwa – Ibili ambayo ni Wilaya ya Uyui, ili kupunguza msongamano wa malori na magari mengine yanayokwenda mikoa mingine na nchi jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, tunaomba kuzibiwa mashimo yaliyochimbika katikati ya barabara yaliyosababishwa aidha na mvua na changamoto nyingine ili kupunguza ajali na kuharibika kwa vyombo vya moto. Vilevile, tunaomba kurudishiwa taa za barabarani na alama za barabarani maeneo ambayo zimetoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tunaomba ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Ipole mpaka Lungwa kupitia Kata ya Ngoywa – Kitunda – Kiloli - Kilumbi na Kipili. Pia ni barabara muhimu sana kwa utalii wa Mbuga ya Mpemba Mpazi, ipo wilaya ya Sikonge na pia inaunganisha Mkoa wa Tabora na Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba kujengewa barabara kwa kiwango cha lami ili kuunganisha Mkoa wa Tabora na Singida kutoka Tura - Maguliati na Iyumbu. Tunaomba kujengewa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Tabora – Mambali kupita Bukumbi – Shitage - Ushetu na Kahama. Hii itasaidia kuunganisha Mikoa ya Kagera – Shinyanga - Tabora, Katavi na Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba kujengewa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Nzega – Itobo – Igusule – Gongwa, Mkoa wa Shinyanga. Tunaomba barabara kwa kiwango cha lami kutoka Kahama – Ushetu – Ulyankulu – Kaliua na Ugala, Mkoa wa Katavi. Tunaomba kujengewa barabara kutoka Tabora – Ibili – Ulyankulu ambapo upembuzi yakinifu umekamilika; tunaomba ujenzi uanze.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba barabara kwa kiwango cha lami kutoka Puge – Ziba – Choma kwa kiwango cha lami ambapo kuna Hospitali ya Rufaa ya Nkinga. Hii ni hospitali

ambayo barabara inapokuwa imeharibika wanaopata changamoto kubwa ni akina mama na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba maombi haya yote. Ujenzi huu wa barabara uwe wa ubora wa hali ya juu ili ziweze kudumu kwa muda mrefu. Ninapomalizia maombi haya, niwashawishi wenzangu tuiunge mkono hotuba hii, ili maombi haya sasa yaweze kufanyiwa kazi kwa kuwa changamoto ni nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Kakulu Burchard Kakulu, atafuatiwa na Mheshimiwa Hija Hassan Hija, Mheshimiwa Faraji Buriani Nandala, ajiandae.

MHE. KAKULU B. KAKULU: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi hii. Nianze kwa kuipongeza Serikali kwa mageuzi makubwa ya miundombinu ya barabara hasa Barabara Kuu ya Kilwa katika Jimbo la Mbagara na kwa ukamilikaji na kuanza kwa shughuli za mwendokasi kuanzia mjini kwenda Rangi Tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi pia kwa Serikali yetu na kwa Rais wetu na wanaomsaidia katika upanuzi wa barabara ya kutokea Rangi Tatu kuelekea Kongowe na ujenzi wa daraja kubwa katika Mto Mzinga, ambao tunaamini utaenda kumaliza tatizo la mafuriko pale Mto Mzinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, nijielekeze kwenye jambo moja mahususi lililoko jimboni kwangu, ambalo ninafikiri pia linahusu Jimbo jirani la Kigamboni, kuhusu Barabara itokayo Kongowe kwenda Kivukoni kule Kigamboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi na upanuzi wa Barabara ya Kongowe kuja mpaka Rangi Tatu utakuwa na maana sana kama ile barabara inayotokea Kongowe kwenda Feri itafanyiwa upanuzi au kufanyiwa marekebisho makubwa. Ni muhimu

tukubaliane, Mheshimiwa Waziri yuko hapa ni jirani yangu pale tunapakana mipaka Jimbo la Mkuranga na Jimbo la Mbagala. Barabara ya Kongowe kwenda Feri ni barabara ambayo imeharibika vibaya mno. Ninafikiri ujenzi wake sasa hivi ni kama miaka 40 tangu kujengwa. Imekuwa ikifanyiwa ukarabati kwa muda mrefu, lakini hali ni mbaya zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kiwango cha upanuzi wa viwanda na ujenzi wa viwanda unaotokea kwenye eneo la Kisarawe II kule Kigamboni na viwanda vinavyoendelea kuongezeka kule eneo la Mkuranga ambako ndiko Mheshimiwa Waziri anapotokea, barabara ile haiwezi kuhimili tena kiwango cha mizigo inayopita kwenye ile barabara. Kwa hiyo, imeharibika kiasi kwamba usumbufu kwa wananchi ni mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwenye hili la barabara ya Kongowe kwenda Feri, inabidi tuzungumze zaidi na Mheshimiwa Waziri, kwa sababu vinginevyo wakati wa kupitisha kifungu kwa kifungu tunaweza tukatofautiana, pamoja kwamba ni jirani yangu mwema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba kusisitiza kwamba barabara hii ifanyiwe na kupewa kipaumbele mahususi kwa sababu ni barabara muhimu kiuchumi na kwa matumizi ya wananchi. Pia ni barabara ya mchepuko kwa wananchi wanaoenda kusini, wanaoenda Mikoa ya Mtwara na Lindi. Kwa hiyo, ni muhimu sana hili jambo nilisisitize mbele yako na Mheshimiwa Waziri ambaye ni jirani yangu ninafikiri ananisikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nitazungumza, ni la kisera kidogo, lakini pia ni jambo la miundombinu. Dar es Salaam kwa sasa hivi ilipofikia inaelekea ku-*jam*. Pamoja na upanuzi mkubwa wa barabara inayofanyika kwenye maeneo makubwa na mengi pale, lakini bado kuna tatizo kubwa sana la foleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kama tukitaka Bandari yetu ya Dar es Salaam ambayo tumeifanyia mageuzi makubwa sana; makadirio ya bandari yetu kati ya sasa na 2030 inatarajiwa kuwa ita-*handle* mizigo ya zaidi ya tani milioni 58. Katika hali ya

kawaida kwa hali ya foleni iliyoko Dar es Salaam, bandari yetu tunaweza tusiifaidi kama hatutafanya upanuzi wa kutosha wa barabara. Hatutafaidi matunda yanayotokana na bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, upanuzi wa barabara inayotokea bandari kwenda Ubungo na kutoka nje ya Dar es Salaam unatarajiwa kuwa wa njia sita. Katikati mwendokasi, na njia nne, mbili upande mmoja na mbili upande mwingine; lakini ukiniuliza mimi nitakwambia Dar es Salaam ilipofikia hata upanuzi huo hautatutosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafikiri mtazamo sasa ubadilike. Mheshimiwa Waziri ananisikiliza, kwamba zile barabara sasa hivi inabidi tufikirie kuzijenga kwa upana zaidi kuliko kubaki na njia nne zile ambazo bado haziwezi kutusaidia sana kuondoa msongamano pale bandarini na kwenye Mji wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya miundombinu ya Dar es Salaam kama tukiendelea kuitazama kama ilivyo bila kufikiria upanuzi mkubwa, bado tutaendelea kuwa na tatizo kubwa zaidi. Kwa mfano, upanuzi wa barabara inayotokea mjini kwenda mpaka Bunju wa njia sita. Njia mbili za kawaida na njia mbili za katikati za mwendokasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafikiri kwa sababu bado barabara ina nafasi ya kutosha tungeweza kupanua zaidi ya hapo ili barabara sasa tusiende kulazimika tena miaka mingine 10 kufanya mageuzi makubwa tena ya ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dar es Salaam, kwa uzoefu wangu, kwa mfano barabara ile ya Kilwa tuliipanua wakati wa Mheshimiwa Rais Kikwete kuwa njia nne. Imetutumia miaka 15 kwenda kurudi tena pale kuipanua tena kwa mara nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninafikiri mtatazamo uwe mkubwa zaidi, tupanue zile barabara ili bandari iweze kuwa na manufaa zaidi, kwa sababu vinginevyo kama hali ndiyo ile hatutaondoa tatizo. Kwa mfano leo tunapozungumza eneo la Jimbo la Mbagara foleni imekuwa mbaya zaidi kuliko ilipokuwa

kabla. Kwa nini? Kwa sababu ongezeko la *ICDs* na ongezeko la shughuli za bandari zimefanya ile barabara sasa hivi inapata usumbufu mkubwa sana. Kwa hiyo, unakuta malori yame-*pack* kandokando ya barabara, hali ya usumbufu ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi lori lilianguka pale Mto Kizinga kabla ya kufika Mbagala, magari yamesimama pale na wananchi wametembea kwa mguu kwa zaidi ya masaa sita. Kwa hiyo, huu ni msisitizo. Mheshimiwa Waziri yuko hapa, kwamba tukubaliane kwamba kuna haja ya kufanya mageuzi makubwa katika ukubwa wa barabara zinazotoka Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia jambo moja la mwisho kuhusu fidia za wananchi wangu pale Mbagala. Zaidi ya wananchi 536, wanadai zaidi ya shilingi bilioni 21. Walibomolewa nyumba tangu mwaka 2002 hadi leo wanadai, na hatujapata majibu ya kuridhisha kutoka kwa Serikali kuhusu ni lini wananchi hawa watafidiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hili ninaomba tupate majibu ya kuridhisha ili tuweze kumuunga mkono Mheshimiwa Waziri. Nitaunga mkono hoja hii kama nitapata majibu ya kuridhisha kuhusu hizo hoja nilizozitoa hasa kuhusu barabara ya Kongowe – Feri na fidia kwa wananchi wetu wa Mbagala.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kakulu, ahsante sana. Nimtaja Mheshimiwa Hija Hassan Hija, atafuatiwa na Mheshimiwa Faraji Buriani Nandala, Mheshimiwa Sigrada Wilhem Mligo ajiandae.

MHE. HIJA HASSAN HIJA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, na ninaomba nichangie kwa ufupi sana kwenye hoja hii ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu. Kwanza ninaomba niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri, na niwaombe Waheshimiwa Wabunge

wenzangu tumuunge mkono Mheshimiwa Waziri ili bajeti yake ipite ikafanye kazi ya kuwatetea wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamezungumza hapa, tutaendelea kulalamika na kumlaumu Mheshimiwa Waziri, lakini hoja ni kwamba Wizara hii ina tatizo la ukosefu wa fedha. Hoja ya pili, Wizara hii ina tatizo la kundi kubwa la madeni ya wakandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niendelee kuiomba Serikali kwamba kama tunahitaji Wizara hii ifanye vizuri na Watanzania wapate barabara kama inavyohitajika, basi tulinde fedha za Mfuko wa Barabara kama ambavyo wenzangu wamezungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Serikali ikubali sasa kubeba madeni yote ya wakandarasi chini ya Wizara hii. Laiti kama Serikali itabeba madeni yote, nina uhakika kwamba Wizara hii itafanya vizuri na malalamiko ya Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa Tanzania yataondoka kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, Serikali ikubali tu kubeba madeni ili kupunguza mzigo kwa Wizara hii ili Mheshimiwa Waziri na Wizara yetu ifanye kazi vizuri kwa ajili ya kuwatetea wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisikiliza malalamiko ya Waheshimiwa Wabunge wote, sisi ambao hatuna barabara; mimi ninaishi Zanzibar, lakini ninaiona hisia ya wenzangu wa Tanzania Bara. Ukweli ulivyo, siyo kwamba Waheshimiwa Wabunge wana nia mbaya, ni kwa sababu wanayabeba maono ya wananchi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, njia ya pekee ya kuwasaidia wananchi wa Tanzania ni kuongeza fedha kwenye Wizara hii na kulinda fedha za Mfuko wa Barabara ili Watanzania wapate barabara kama ambavyo Serikali na Mheshimiwa Rais amedhamiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hili njia pekee ninaomba nikumbushe kwamba ni njia nne tu. Ya kwanza ni kulinda fedha ya Mfuko wa Barabara. Njia ya pili ni kubeba madeni ya Wizara ya

Miundombinu ili Serikali ibebe madeni haya na fedha ya maendeleo ya Wizara hii, ibakie kwa ajili ya ujenzi wa barabara zetu. Njia ya tatu ni kutafuta vyanzo vipya vya mapato ambavyo vitaangalia maslahi ya wananchi na havitaumiza wananchi wetu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa mikoa yote, wa kanda zote tumsaidie Mheshimiwa Waziri, hii bajeti yake ipite. Mheshimiwa Waziri ni msikivu mbele ya Kamati, amekuwa akitusikiliza na Kamati yetu imebeba maoni ya Wabunge wote kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wa Tanzania. Kwa hiyo, ninaunga mkono hoja hii, ninaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuunge mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hija Hassan Hija, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Faraji Buriani Nandala, atafuatiwa na Mheshimiwa Sigrada Mligo, Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga ajiandae.

MHE. FARAJI B. NANDALA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ili nami niwe miongoni mwa wachangiaji wa hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia nichukue nafasi hii pia kumshukuru na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa dhamira yake ya dhati ya kuona kwamba barabara za Kitanzania zinapitika muda wote na zinakuwa rafiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tuliiona mapema tu tangu alivyoingia kuwa Rais Awamu ya Sita. Tumeona mchakamchaka mkubwa wa ujenzi wa barabara. Mimi ni Mbunge kutoka Mtwara kutoka Jimbo la Ndanda. Sisi kutoka Mtwara, tumeona maendeleo makubwa

sana ya barabara. Nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitamshukuru yeye na Waziri mwenye dhamana hii ya ujenzi, kaka yangu Mheshimiwa Abdallah Ulega. Amefanya kazi kubwa sana Mtwara na Wanamtwara wanamkubali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wanamtwara tumeshuhudia fedha nyingi zimemwagwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara. Tumeona fedha zaidi ya shilingi bilioni 268 kwenye ujenzi wa barabara kutoka Mtwara – Mnivata – Tandahimba – Newala kuja Masasi. Pia hawakutuacha hapo, wakatupatia fedha nyingine zaidi ya shilingi bilioni 400 kwenye ujenzi wa barabara kutoka Mtwara – Mingoyo – Ndanda kuja Masasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wananchi wa Mtwara tunakubali sana jitihada za Serikali na tunaona jitihada hizi ni za kuungwa mkono na za kupongezwa, kwa sababu asiyeshukuru kwa kidogo, hata ukimpa kwa kikubwa hawezi kushukuru kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mazuri hayo, bado kuna changamoto moja ambayo sisi wananchi wa Masasi, hasa Jimbo la Ndanda, tumekuwa tukilalamikia sana kuhusu barabara ya kutoka Masasi – Nachingwea – Liwale. Barabara hii imekuwa na changamoto nyingi, kwa sababu iliwekwa katika mpango wa bajeti ya *EPC+F*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kufanya *analysis* ya barabara zote zile saba ambazo ziliwekwa katika mkataba huu, ufanisi wake umekuwa siyo mzuri. Sisi kule hii barabara moja ya kutoka Masasi – Nachingwea – Liwale imekuwa ikipigwa danadana sana, na kwa muda mrefu sana na kuwafanya wananchi kuwa na malalamiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii wananchi walifanyiwa uthamini na tathmini tangu mwaka 2013, Serikali iliwaahidi kuwalipa fidia. Cha kustahajabisha, hadi leo hii wananchi hawajalipwa fidia, lakini pia hata ujenzi wa ile barabara bado haujaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Jimbo la Ndanda, Masasi, Nachingwea na Liwale wameniagiza nije nimwulize Waziri na Serikali, ni lini hasa ujenzi wa barabara hii kutoka Masasi – Nachingwea – Liwale utaanza ujenzi wake? Pia wameniomba niiulize Serikali ni lini fidia itakwenda kulipwa kwa wananchi? Hawa wananchi watalipwa fidia kwa *rate* ipi? Kwa *rate* ya mwaka 2013 au kwa *rate* ya mwaka huu wa 2026. Kwa sababu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ardhi inasema, ukitoa ardhi ya mwananchi, lazima ulipe fidia na ulipe fidia kulingana na *current price* ya ile ardhi. Leo hii ni zaidi ya miaka 15, wananchi hawajalipwa fidia kwenye ile barabara na barabara haijaanza. Kwa hiyo, wameniagiza nije kuuliza, ni lini hasa hawa wananchi watalipwa fidia ili waweze kuendeleza yale maeneo?

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wale wamekaa zaidi ya miaka 15, na msingi mkubwa kwao ni ardhi. Leo hii wameshindwa kuendeleza ile ardhi kwa sababu Serikali imewazuia wasifanye chochote kwenye ile ardhi kwa kuwaahidi kwamba watawalipa fidia. Miaka mingi imepita, wazee wengine wanafariki, vitukuu pia vinakufa, lakini bado fidia kutoka kwa Serikali haijalipwa na hata barabara bado haijaanza kutengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe kaka yangu Mheshimiwa Abdallah Ulega atakapokuja kufanya hitimisho ya hotuba yake hii atuambie, ni lini wananchi wa Masasi, hasa kata ya Lukuledi watalipwa fidia zao na wananchi wote mpaka kuelekea Jimbo la Masasi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Sigrada Mligo, atafuatiwa na Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, ajiandae.

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kidogo kwenye hii Wizara. Sisi Mkoa wa Njombe tuna barabara kubwa

nne ambazo ni miaka 20 sasa zinaingizwa kwenye bajeti na zinawekwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa barabara ambayo imekuwa ndiyo changamoto kuliko barabara nyingine zote ni Barabara ya Ludewa – Njombe maarufu kama Itoni – Lusitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kuwapa picha ya hii barabara kwa sababu Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini, kaka yangu Mheshimiwa Deodatus Mwanyika hataki mgogoro na Serikali, ndiyo maana hata alivyoizungumzia hakuweza kuingia kiundani zaidi. Mimi Sigrada Mligo sina cha kupoteza, ninataka niseme ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mwaka wa tatu sasa, barabara imesimama. Mkataba unasema ilitakiwa barabara hiyo ikabidhiwe mwaka huu mwezi wa tano.

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sigrada kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

TAARIFA

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, haki lazima isemwe na isemwe wazi. Mheshimiwa Mwanyika, kwanza jana amechangia vizuri sana juu ya Barabara ya Itoni - Lusitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata juzi wakati tunaposhangilia Mei Mosi, Mheshimiwa Mwanyika akiwa na Mheshimiwa Villa na Mheshimiwa Kihenzile na wengine katika eneo hili la Iringa na Njombe, walinialika rasmi kabisa, akiwa na Mheshimiwa Sanga wa Makete. Walinialika rasmi nitembelee ikiwa ni pamoja na kuiona barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, kwa kuwa wananchi watakuwa wanafuatilia Bunge Tukufu, ninaomba nitoe taarifa ya

kuwa Mheshimiwa Mwanyika, Mbunge wa Njombe ni kipaumbele chake namba moja, juu ya barabara hii na zingine nyingi katika Mkoa wa Njombe. Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sigrada taarifa unaipokea?

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipokea kwa sababu ameniunga mkono na anaungana na mimi kwamba Mheshimiwa Deo anaipambania hii barabara. Sasa kuna vitu ambavyo hawezi kuzungumza, nitazungumza mimi. Kwa hiyo, ninaipokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko hivi, kama nilivyosema, barabara hii ilitakiwa ikabidhiwe mwezi Mei mwaka huu. Mpaka ninavyozungumza hivi….

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sigrada kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Neema Mgaya, taarifa ya mwisho hiyo.

TAARIFA

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nilikuwa ninapenda kumpa taarifa, Mheshimiwa mzungumzaji kwamba, katika Wabunge ambao wamepambania barabara ile tangu mwanzo na ile barabara imeanza kujengwa kipindi ambacho Mheshimiwa Deo Mwanyika ameingia madarakani, ndiyo mwanzo wa kujengwa barabara ile na mpaka sasa hivi inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hakuna kitu chochote ambacho anaogopa kukiambia Serikali. Amezungumza mambo mengi na ndiyo maana barabara ile imeanza kujengwa ndani ya uongozi wake Mheshimiwa Deo Mwanyika. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Sigrada taarifa unaipokea?

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo siipokei kwa sababu yeye ndiyo hana taarifa. Hatuna lami hata sekunde moja, hata nusu meta hakuna. Kwa hiyo na yeye hana taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninataka kusema kitu kimoja, hii barabara ni mwaka wa nne sasa hatuna hata meta moja ya lami. Mkandarasi alipewa mradi, akafika *site,* akatifua ile barabara, halafu baada ya hapo akaondoka. Mpaka ninavyozungumza hivi, barabara ile imesimama, miaka minne sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tumerudi kwenye kampeni mwaka jana, mimi nilikuwa mgombea pia na Mheshimiwa mwenzangu Deo Mwanyika, tulikubaliana kwamba, Mungu akitujalia tukafika Bungeni, lazima tusimame wamoja. Msije mkafikiri mimi na Mheshimiwa Deo hatuzungumzi; poleni sana. Tusimame wamoja ila kila mtu aongee kwa mipaka yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyozungumza hivi, mhandisi mshauri ana miaka miwili analala *guest*. Kama mimi mwongo nishtakiwe. Ninavyozungumza hivi, mkandarasi aliondoka toka mwaka 2023 yuko Kigoma hajawahi rudi. Ninavyozungumza hivi, hii barabara ilivyoshindikana kupitika mwaka jana wakati wa kifuku, ikabidi Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Njombe atafute mkandarasi wa ziada ampeleke *site*. Ndipo mkaona kuna picha na waandishi wa habari wamesema Barabara ya Ludewa - Njombe mkandarasi yuko *site*.

Mheshimiwa Naibu Spika, yule siyo mkandarasi wa ile barabara, yule alichukuliwa kwa muda, kunusuru wakazi wa Njombe na Ludewa ambao kuna watu walijifungulia njiani. Ndiyo maana nikasema ninataka mpate picha pana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi nimehudhuria mkutano wa *RCC* ambao Mheshimiwa dada yangu Neema hajahudhuria. Nimesoma kabrasha la Meneja wa *TANROADS,* Mkoa wa Njombe, anasema, mradi ule kwenye makabrasha yake ni wa shilingi 109,000,000,000. Mkandarasi alilipwa shilingi 21,000,000,000,

anadai zaidi ya shilingi 70,000,000,000 na ndiyo maana mkandarasi yule, sasa hivi tunasingizia watu kwamba, mvua, mvua. Mvua Njombe ilishakwisha. Yule mkandarasi hawezi kurudi *site,* kwa sababu anachodai ni kikubwa kuliko kile ambacho tumemlipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kila atakayesimama anakwambia, tuliambiwa mvua. Kwani mwaka jana hatukuwa na mvua na kiangazi? Mwaka juzi hakukuwa na mvua na kiangazi? Mwaka 2022 hakukuwa na mvua na kiangazi? Kwa nini, tusiambizane ukweli?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mbunge mmoja alichangia hapa, *sometime* ni bora kuwaambia wananchi ukweli kwamba, hii barabara kwa sasa hatutajenga, kwa sababu hatuna bajeti na siyo kusingizia mvua na Mwenyezi Mungu anawaona. Wanasingizia mvua, wakati mwaka jana kulikuwa na kiangazi, mwaka juzi kulikuwa na kiangazi. Hivyo viangazi vya mwaka jana na mwaka juzi walijenga wapi? Ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea na hoja yangu nyingine. Hoja nyingine, kuna Mbunge mmoja hapa alitoa hoja ya msingi sana, ni namna gani tunaweza kwenda mbele. Akasema tunaweza kununua lami kwa *bulk procurement.* Hoja ya msingi sana. Sasa, kwa sababu sisi vitu kama hivyo hatutaki kusikia, niliona hakuna anayempigia makofi ila ukiongea mambo fulani ndiyo unapigiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ile laiti tungejua umuhimu wake sisi kama Wabunge na alitoa hesabu zake kwamba, tuna uwezo wa kununua lami na kujenga kilometa moja ya lami kwa shilingi 900,000,000 na akatoa namna gani tunaweza kujenga lami kwa shilingi 900,000,000. Mimi nilimpigia makofi, lakini mimi sitaki kupigiwa makofi kwa sababu, siku nitakayoanza kupigiwa makofi na CCM, ujue hali yangu ni mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia sitaki kupigiwa makofi kwa sababu mimi siyo hela. Anayependwa na kila mtu ni hela tu. Ahsante baba yangu. *(Makofi/Kicheko)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa. Waheshimiwa, nilimtaja Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga na Mheshimiwa Mohamed Mussa Utaly ajiandae.

Waheshimiwa Wabunge, tujadili kwa sauti ya chini tafadhali.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia niseme kidogo kwa mchangiaji wa mwisho dada yangu aliyemaliza kusema. Bunge hili ni chombo Tukufu sana na ni chombo ambacho tunategemea kukidhi matarajio ya Watanzania kwa kuisimamia Serikali. Tukifanya kama *debate* za shule za msingi, zile ambazo tulikuwa tunafanya wakati huo, si sawa. Mbunge unasimama kuanza kuchambua hotuba ya Mbunge mwenzako. Sidhani kama ni kazi ya Kibunge kuchambua, mpaka unajua alishiriki *CC*, unajua mkandarasi amelala *guest*, sasa sidhani kama hii ni kazi ya Kibunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilifikiri, chombo hiki kingetusaidia kushauri Serikali ili tutoke hapa tulipo. Baada ya kusema hayo, sasa nijikite kwenye hoja zinazohusu Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, Mheshimiwa Waziri ninamshukuru sana. Katika Jimbo letu la Hai umefanya kazi kubwa, amejenga *culverts* pale *KIA* akatuwekea na taa. Tunakushukuru sana na kwa kweli wananchi wa Hai wamenituma nimshukuru Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo tunasema tunashukuru au tunasifia tu, tunataja na vitu vilivyofanyika, imejengwa *culvert* na taa za barabarani zimefungwa. Hakuishia hapo, pale Bomang'ombe ameweka taa za kuongozea magari. Tangu tumepata uhuru, tangu dunia imeumbwa hazijawahi kuwepo, ndiyo zimekuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini, tusimsifie Mheshimiwa Rais? Ndiyo uungwana huo na niliwahi kusema humu jamani, wale Wakristo tulifundishwa kwamba, hata namna ya kusali, ombeni Baba yetu uliye Mbinguni, jina lako litukuzwe, utukufu wako, halafu baadaye ndiyo utupe leo riziki yetu. Kwa hiyo, ni *formula* tu ya kidunia na mtu akifanya jambo ashukuriwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hapa ninazungumza, Mheshimiwa Waziri amejenga Daraja la Makoa, japo halijakamilika, lakini tunamshukuru. Anajenga Daraja la Kitafu, kwenye bajeti hii nikisoma, ninaona miradi. Barabara ya Sadala kwenda Lemira kilometa 16, zimo humu. Daraja letu la kisasa la Kitafu limo humu. Sasa nimwombe Mheshimiwa, pamoja na mambo hayo mazuri ambayo ametuwekea huku, niweze kukushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, Mheshimiwa Waziri amalizane na mimi kuhusu viporo vilivyobaki. Kiporo cha kwanza ni pale Kwasadala. Wananchi wamekubali kuondoka, tunaomba, tunajua mchakato umeenda na kila wanapofanya kikao pale, bahati nzuri Naibu Waziri wake ni maarufu sana kule Hai, wanamjua. Wanasema yule baba mnene kila siku anakwambia tutalipwa, tutalipwa. Sasa ifike mahali, ile fidia iweze kulipwa na daraja lile lijengwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kiporo kingine kule Kitafu Juu, ambapo Kalali na Uswaa ilitakiwa iunganishwe. Juzi hapa Naibu Waziri ameniambia mkandarasi ameshalipwa. Tunamwomba nikitoka hapa akanikabidhi huyo mkandarasi, kwa sababu ameshachukua mzigo wa Mama Samia, nimfuatilie ili aweze kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kwenye zile kalavati walizojenga, zinapeleka maji kwenye nyumba za watu kule *KIA* na Mheshimiwa Waziri alikuja pale aliona jambo hili. Nimwombe sana chonde, chonde, atusaidie namna ya kujenga mitaro ili maji yale yasifike kule. Bahati nzuri nilitembea na Meneja wa *TANROADS,* tukaenda kuona namna ambavyo wananchi wanapata tabu kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Waziri jambo lingine kubwa sana na kwa sababu ya *AFCON* inayokuja nchini kwetu; tuna Barabara ya Bomang'ombe - Chekimaji - *TPC* kwenda mpaka Tarakea. Barabara hii ni barabara muhimu sana na ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, lakini majuzi hapa Waziri Mkuu alikuja kuweka jiwe la msingi kilometa tatu, kuanzia Bomang'ombe kwenda kule Rundugai. Ninamwomba sana, Waziri Mkuu alisema washirikiane *TANROADS* na *TARURA* kujenga barabara hii. Ninamwomba washirikiane *TANROADS* ili barabara hii iweze kujengwa kwa kiwango cha lami yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana *RAS* wa Kilimanjaro ameandika barua kumkumbusha Mheshimiwa Waziri, kupitia Katibu wake Mkuu. Katibu Mkuu ninamwamini sana, mama mchapakazi yule. Niombe waifanyie kazi barua hiyo, ili barabara hii iweze kupitika. Hii ndiyo barabara ambayo ni *diversion road*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Arusha - Moshi imeshajaa, kipindi cha *AFCON* hapo tutashindwa, alisema Mheshimiwa Nassari hapo. Nimwombe pia, kiko kipande kidogo cha barabara kutoka kwa Mengi kwenda Kiaria. Hili Katibu Mkuu wa Wizara analifahamu vizuri, kupitia kwa Askofu Shoo pale. Ninaomba kipande hiki tumeshaahidiwa sasa asukume kiweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nishauri jambo moja hapa kabla sijagongewa kengele. Amezungumza Profesa Muhongo hapa, mambo mazuri kabisa, kwamba tuna mikataba ya madini iliyosainiwa kipindi cha Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kwenye uongozi wake. Mikataba hii haijafanyiwa *review,* kama tukiweza wao wenyewe ingekuwa hii mikataba inawapa hasara, wangekuja Serikalini kuomba kufanyiwa *review*. Sasa sisi kwa kuwa wanapata faida na bei ya dhahabu imeongezeka, ifanyiwe *review* iwe ndiyo eneo ambalo tunaweza tukapata pesa ya kuongeza kwenye ujenzi wa barabara. Niombe sana hayo wayafanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, Tume yetu ya Mipango ifanye utafiti, aina ya barabara ambazo tunapaswa

kujenga kwa mazingira yetu. Mheshimiwa Waziri ni mjanja, mtoto wa mjini. Ninasikitika sana kila akitembea barabara kuu hizi anakuta watu wana vitoroli na mchanga, wanafukia mashimo, kesho wanarudi pale pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini, tusijenge barabara ambazo ni za kiwango, tukijua tumejenga, tuondoke hapo. Kama kuna barabara kama alivyosema Mheshimiwa Kadogosa hapa, zimeshapitwa na wakati tuweke bajeti, kuliko hiki tunachoendelea. Ukisoma kitabu cha Waziri, utaona pesa za *maintenance* ni nyingi kuliko za kujenga barabara mpya. Kwa hiyo, Tume ya Mipango ikae chini, ije na *draft* ya kwamba, barabara zetu suluhu ni nini kuliko hivi tunavyokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe pia, kuna Barabara ya Machame kwenda Kiaria. Barabara hii kumekuwa na mgogoro, ninajua kuna kesi za Mahakama, lakini wananchi wanashindwa kujenga kwa sababu kuna wakati walipewa *stop order* ya kuendelea. Hebu wafike mwisho watuambie, wananchi waendeleze barabara zao? Serikali itoe tamko, kuliko sasa hivi watu hawajui wajenge au wasijenge.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na kumalizia kiporo kingine cha taa za barabarani, pale mjini ametuwekea taa vizuri kabisa. Ninajua na eneo la Kwasadala atatuletea, lakini yeye mwenyewe alivyokuja kwenye ziara yake alituahidi kutuwekea barabara hii na yeye anaijua ni ya kimkakati. Nimwombe kaka yangu amalize jambo hilo ili tuweze kufikia malengo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana na ninaunga mkono bajeti hii kwa 100% na haya tuliyomshauri Waziri akayafanyie kazi. Mungu ambariki sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Mussa Utaly na Mheshimiwa Patrick Adkin Mwalunenge ajiandae.

MHE. NJALU D. SILANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii nzuri sana

ya mtani wangu Mheshimiwa Ulega. Jana kila akitaja alikuwa akitaja Wasukuma, akasema amepigiwa na mama Bogohe, akasema msukuma mmoja tena amelala kwenye barabara ya lami pale Busisi. Tunamshukuru, lakini tunamshukuru sana kwa kuendelea kutupangia fedha kwenye bajeti yake hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote tunayoyazungumza katika Bunge lako Tukufu, bila kuwa na pesa hakuna kitakachofanikiwa. Waziri atakuja na mbwembwe hapa, atasema kila aina ya maneno na Mheshimiwa Waziri hatukufundishwa hivyo kwenye Umoja wa Vijana. Lazima tufike sehemu tuwe wakweli, tusimamie Serikali, tuipe ushauri zitoke fedha tufanye kazi. Kama kuna tatizo lijulikane wananchi tuwaambie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho kingine ni kibaya kabisa, Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa wanapofanya ziara wanapotoa ahadi mbele ya wananchi, halafu baadaye utekelezaji unakuwa ni shida, tunaingia kwenye matatizo kama viongozi na tunaingia kwenye matatizo kama Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombeni sana Wizara ya Fedha itoe fedha ili kusudi watu wafanye kazi. Hakuna chombo ambacho kilikuwa kinasifika kama *TANROADS* na ni chombo ambacho, kwa ukweli usiopingika kilitufanya Chama Cha Mapinduzi tuwe na nguvu ya kusimama mahali popote na kusema utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe sana Waziri; iko Barabara ya kutoka Mkoa wa Arusha – Karatu – Mbulu – Singida – Sibiti – Meatu – Lalago – Kolandoto mpaka Mwanza. Wamekaa Mheshimiwa Olelekaita amezungumza hapo kwamba, wananchi wamekusanyika na mahema yakawepo, wakatia sahihi kwamba, sasa mipango inaenda kufanyika, mpaka leo utekelezaji wako hujafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukirudi kule tunawaambia nini? Ifike mahali sisi kama viongozi, sisi kama Taifa, mambo ya msingi

tuyape kipaumbele. Tunajua tuna mambo mengi ya kufanya yanahitaji fedha, lakini kupanga ni kuchagua kwamba, ni kitu gani kilichoko mbele yetu. Tukifanya hivyo, matarajio na kujenga nchi si kwa siku moja, kila Mbunge aliyeko humu anahitaji maendeleo, ni jambo ambalo ni la muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Waziri kuhusu Barabara yetu ya kutoka Bariadi - Kisesa, ambayo inakuja na kukutana na Sibiti, inakuja kukutana na Singida, ameitengea kwenye upembuzi sasa, kilometa 102. Ziko kilometa 20 pale Itilima, kwa mwaka ni mara nne wanapitisha sijui ule wembe, (wanasema kitaalam sijui kufanya nini) imechoka na magari yameongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kwenye Mikoa hii ya Simiyu ni wakulima, kwa hiyo, mazao yetu yanayotoka kwenye Vijiji vya Laini, Migato, Chinamili kwenda kuuzwa kwenye *NFRA*, pale Ikindilo hayatafikika. Maana yake, tunarudi kwenye umachinga wa kawaida, watu watakwenda kununua mazao kwa bei ya chini, halafu tunarudi kuanza kulalamika huku hatujasimamia uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe sana, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Wizara ya Fedha, hapa ni eneo moja tu, Wizara ya Fedha itoe pesa. Wataalam wa *TANROADS* wana uwezo mkubwa mno. Tuna *engineers* wazuri sana, wana uwezo mkubwa sana wa kufanya mambo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyinyi ni mashahidi, pale Ubungo wame-*design* viongozi wa *TANROADS,* ukienda pale *TAZARA, TANROADS* imefanya hiyo kazi. Hatuna sababu ya kuwa na mashaka na chombo hiki. Yawezekana sasa Mawaziri, wanapoingia kwenye vikao hawasimami imara, wanakuwa na uswahili, uswahili, unaosababisha wataalam wetu wasifanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, jambo hili alifanyie kazi. Akumbuke alifanya ziara na Mheshimiwa Rais kwenye eneo letu. Mheshimiwa Rais alisema aweke mataa katika Wilaya ya Itilima, ili wale watu wasiwe

wanapitapita usiku. Ninadhani alisimama na akasema, tayari atafanya hiyo kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru, amefanya hiyo kazi. Kilometa 118 ameziweka kwenye mpango wake za Barabara ya kutokea Luguru kwenda Madirana, kwenda Migato, kwenda Longalombogo, inakuja Ndolelezi, inakuja kuungana na Mheshimiwa Kadogosa na Mheshimiwa Kundo. Ni jambo la msingi sana, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri tusimamie fedha. Hata vyanzo hivi tunavyovizungumza kuviongeza kila kukicha, kama hatusimamii tulichokipitisha toka mwanzo, tutakuwa ni watu wa ajabu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili Bunge ni Bunge la Tatu. Wizara ya Ujenzi ilikuwa ikisimama ni makofi na kupongeza na kuondoka, lakini hii ni ishara Wizara hii na Mheshimiwa Waziri, watu tunampenda na Wabunge wanampenda. Wanataka sasa aende akatekeleze kazi kwa vitendo. Jambo hili ni la muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, ujenzi wa barabara zetu kwa sasa ninashindwa kuelewa. Sijui utaalam umepungua, au yawezekana magari yameongezeka zaidi kuliko zamani. Barabara inajengwa ndani ya miaka miwili, mitatu inakuwa inafanyiwa *maintenance* kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Barabara ya kutoka Shinyanga - Maswa - Lamadi, ni fedha nyingi sana zinazotumika. Pale *tender* inapotangazwa kwenye maeneo yale, kuna wakandarasi, kuna washauri, wanajengewa nyumba nzuri sana za kushauri kwamba, ni namna gani watakavyojenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi barabara Mheshimiwa Musukuma amezungumza tu kwamba, kuna mtu mmoja, Mheshimiwa Kiswaga tu huyu hapa tairi nne zilipasuka siku moja kwenye gari yake, zikapiga shimo kaa! Safari ikaishia hapo, hapo. Hata jana usiku kule Lamadi, jamaa mmoja akasema, hivi kuna Mbunge kwenye Mkoa huu wa Simiyu? Imepiga ikapasuka. Kwa hiyo jambo hili ni muhimu sana wataalam wabadilishe kusimamia mipango yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja, ili mtaalam aende akafanye kazi yake. Wabunge niwaombe tupitishie bajeti yake ili akafanye kazi zake, hizi hizi ndogo, zimsaidie. Huyu bwana ana maneno mengi sana na Wazaramo kazi kwao hawaiwezi, lakini sasa tunaamini ataiweza. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mohamed Mussa Utaly, atafuatiwa na Mheshimiwa Patrick Adkin Mwalunenge na Mheshimiwa Dr. Charles Jacob Sungura ajiandae.

MHE. MOHAMED M. UTALY: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika bajeti hii. Kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuweza kusimama leo kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, wakati ambao tulikutwa na majanga ya *El Nino* katika nchi nzima kuna miradi 81 ya ujenzi wa madaraja ambayo yametekelezwa katika mikoa 22 na zimetumika pesa jumla ya shilingi bilioni 556.93 na miongoni mwa madaraja hayo ni pamoja na madaraja yaliyojengwa katika Barabara ya Kibiti - Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, niseme jambo moja tu kwamba madaraja haya ili tuweze kuyafikia ni lazima barabara iweze kujengwa. Hapa ninakusudia kuzungumzia Barabara ya Kibiti – Lindi - Mingoyo ndiyo barabara ambayo ninaizungumzia. Barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa mikoa minne na mikoa miwili iliyokuwa mwishoni ndiyo inanufaika zaidi. Barabara hii ilijengwa kwa kiwango cha lami kwa awamu kuanzia mwaka 1994 mpaka mwaka 2008, ambapo kipande cha mwisho cha Malendegu ndiyo kilikamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ni miaka 18 tangu barabara hii imejengwa. Nikichukua maelezo ya Mheshimiwa Profesa Mhongo maana yake barabara hii sasa hivi kipindi chake cha kuishi kimekwisha tangu zamani, kipindi cha kuishi kimezidi miaka minane.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii iliposanifiwa ilikuwa hakuna magari mazito yanayopita kwenye barabara hii ilikuwa ni barabara ambayo inapita mabasi tu na magari madogo madogo. Sasa hivi kuna mizigo mizito ambayo inapita, ni barabara hii tunayoitumia kusafirishia makaa ya mawe, ni barabara hii tunayoitumia kusafirishia mawe ya jasi ambayo yanaenda katika maeneo mbalimbali katika viwanda vya *cement,* ni barabara hii tunayoitumia kusafirishia bidhaa mbalimbali zinazotoka katika Bandari ya Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa sababu ya mizigo mizito barabara hii imechakaa, imechakaa, imechakaa mno katika kiwango ambacho huwezi kuikarabati kwa sababu katika maeneo ambayo yanaharibika sana sasa hivi ni maeneo yale ambayo tunajaribu kuyakarabati.

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mohammed kuna taarifa kutoka Mheshimiwa Katani Katani.

TAARIFA

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nimetoka Mtwara leo usiku nikiwa ninapita kwenye barabara hii tairi zangu zote nne zimepasuka, gari imechakaa kabisa. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mohamed, taarifa hiyo unaipokea?

MHE. MOHAMED M. UTALY: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hiyo ninaipokea kwa mikono miwili. Sasa hivi ukitembea katika barabara ile huwezi kujua kiraka ni kipi barabara mpya ni ipi kwa sababu kiraka kinazidi barabara iliyokuwepo. Tunaiomba sana Serikali itusaidie watu wa Kusini hali yetu ni mbaya, hali ni mbaya sana. Mheshimiwa Mbunge yeyote akisimama hapa asipoitaja barabara ya Kusini haturudi, hili ndilo jambo ninataka nilizungumze wazi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba barabara hii ijengwe na barabara hii ina ahadi nyingi sana, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipokuja kwenye kampeni alisema barabara hii itajengwa kilometa 477 kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi wa safari hii tumeambiwa barabara hii itajengwa kilometa 166. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya uchaguzi wa Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Lindi, Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema mkeka utatandikwa kuanzia Dar es Salaam - Lindi - Mingoyo. Leo tunakuja kwenye bajeti hii hatuoni kiasi kilichotengwa kwa ajili ya Barabara, inatusikitisha, inatuhuzunisha, inatuumiza. Tunaomba, imefikia mahali sasa hivi wawekezaji hawawezi kuja Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa juzi tumezungumzia habari ya umeme ambayo ni nyenzo nzuri sana ya kuhakikisha wawekezaji wanakuja, jambo lingine ambalo ni tatizo kwetu ni barabara, barabara ni tatizo kubwa sana na sasa tunakwenda katika *LNG*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana niliuliza siku ile hivi ni kweli tuna uhakika kwamba sisi tunakwenda ku-*sign LNG* au hatuna uhakika, kwa sababu kama tuna uhakika barabara hii ingewekwa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba barabara hii ijengwe na suala langu la kuunga mkono hoja litakuja baada ya Mheshimiwa Waziri kusema kwamba barabara hii ameitengea kiasi chochote cha pesa.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. MOHAMED M. UTALY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Nilimtaja Mheshimiwa Patrick Adkin Mwalunega atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Charles John Jacob Sungura. Mheshimiwa Kinjekitile Ngombale Mwiru ajiandae.

MHE. PATRICK A. MWALUNENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara yetu ya Ujenzi. Kwanza kabisa ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa maono yake na kutupa barabara kile kipande cha njia nne pale Mbeya Mjini kuanzia Jimbo la Uyole mpaka Ifisi, ninampongeza sana kwa niaba ya Wanambeya, ninaomba Waheshimiwa Wabunge tumpigie makofi sana Mheshimiwa Rais kwa sababu barabara ile ni barabara ya uchumi karibu 60% ya mizigo inayotoka bandarini inapita kwenye ile barabara. Kwa maana yake ni kwamba kama ni pesa tunazitafuta basi ziko kwenye barabara ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri na nimeona kwenye vitabu vyake amesema, ameiongelea hiyo barabara na Wanambeya wamekusikia, basi *flow* ya pesa iendelee kwenda pale ili mkandarasi asitoke kwenye *site*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa fedha alizozitoa shilingi 27,000,000,000 za fidia kwa waliopisha ujenzi wa barabara ya mzunguko. Ninakumbuka Mheshimiwa Waziri alikuja Mbeya na yeye mwenyewe akasema nikirudi tu bajeti ya mwaka jana ile na akasema hizi fedha nitazitoa wakati huo Mheshimiwa Mbunge alikuwa ni dada yangu Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson na shilingi bilioni 27 zilishalipwa fidia kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hii ni dhamira njema ya Mheshimiwa Rais kwamba anataka kutukwamua Wanambeya kuepukana na foleni, lakini na ajali ambazo zinatokea mara kwa mara kutokana na jiografia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up* atufahamishe Barabara ya njia ya nne hiyo ambayo inaanzia Igawa mpaka Tunduma ni lini itaanza kujengwa? Ili kukamilisha hicho kipande chote kiishe lakini na zile barabara zinazoilisha hiyo barabara ya njia ya nne ya Mbeya. Tunazo barabara ambazo zinazounganisha mikoa; iko Barabara ya kutokea Makongolosi kwenda Rungwa

ambayo inaunganisha Mikoa mitatu Singida, Tabora na Mkoa wa Mbeya, lakini kwa bahati...

MHE. MASACHE N. KASAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Patrick kuna taarifa kutoka Mheshimiwa Kasaka.

TAARIFA

MHE. MASACHE N. KASAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kumpa taarifa mchangiaji pamoja na maneno mazuri anayoendelea kuyasema, lakini barabara hii aliyoitaja ya Makongolosi kwenda Mkiwa ni barabara ya kimkakati ambayo inaunganisha na kwenda kufungua fursa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini pamoja na mikoa ya kati. Hivyo ni muda mwafaka sasa Serikali itoe fedha ili barabara hii iweze kwenda kutengenezwa. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Patrick taarifa unaipokea?

MHE. PATRICK A. MWALUNENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipokea taarifa hiyo kwa sababu ninajua hawa ni wachimbaji wa madini na matajiri wengi wa Tanzania sasa hivi wanakimbilia kule Makongolosi na Chunya. Kwa hiyo, ni hii barabara ina umuhimu mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine tunayo barabara nyingine kwenye Mkoa wetu wa Mbeya na Mheshimiwa Waziri anaelewa kwa nini ninazitaja barabara zote za Mkoa wa Mbeya. Tunayo Barabara pia ya Mbeya Vijijini ya Mbarali - Shigamba na yenyewe imetajwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie hiyo barabara ianze kujengwa, kwa kuwa Mbeya Vijijini ndiyo wilaya pekee nchini inayolima zao la pareto na ni zao la kiuchumi kwa nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo Barabara ya Kyela inayoanzia Ibanda – Kajunyumbele - Itungi Port. Ile barabara tayari ilishakuwa na mkandarasi ambaye mkataba wake ulivunjwa, kwa hiyo siyo barabara ambayo inaanza usanifu upya, lakini tunashangaa mpaka leo hii hakuna mkandarasi kule *site* na sijui itakuwaje. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, watu wa Kyela wanamsikiliza kwa sababu ni wakulima wakubwa wa kokoa na Serikali inapata fedha nyingi za kigeni kupitia zao lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wameongea hapa na malalamiko makubwa ni upatikanaji wa fedha. Hata hivyo, ninaweza kusema jambo moja, Sheria yetu ya Manunuzi ndiyo imekuwa ni kansa kubwa sana kwenye Wizara ya Ujenzi. La kwanza inashawishi mianya ya rushwa na ndiyo maana unakuta barabara nyingi zikijengwa ndani ya miaka miwili mitatu zinakufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine linaongeza gharama kubwa sana ya ujenzi; nitoe mfano leo hii, ni mkandarasi nina tenda, ninatangaza kwenye *NeST* maana yake tunashirikisha dunia nzima, watu washiriki kwenye zile tenda, anashinda mtu kutoka nje ya nchi anakuja na begi lake anasaini mkataba. akishasaini sisi tunamtafutia *advance payment* na tunasema tuna shida ya fedha, wakati ilitakiwa wale watu waliotoka nje waje na mitaji yao ili wakandarasi wetu wa ndani tuwajengee uwezo ikiwezekana hao ndiyo wapewe *advance payment. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini mtu umpe pesa? Kwa mfano miradi ipo mitano kila mkandarasi anataka shilingi 25,000,000,000, maana yake ni shilingi 100,000,000,000 inatumika kwa *advance payment.* Kwa nini Wizara isipeleke zile fedha kwenye benki zetu za ndani wale wakandarasi wakawa wanapewa mikopo kupitia benki zetu za ndani na mwisho wa siku Wizara inatoa *guarantee* tu pale kwenye mabenki kwamba huyu ni mkandarasi fulani, amejenga barabara imekaguliwa kilometa 10 apewe malipo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii unampa *advance payment* mkandarasi ya shilingi 25,000,000,000 yuko hapa ndani miaka zaidi ya mitano, ukimuuliza shilingi 25,000,000,000 umejenga wapi barabara anasema hii pesa ni *mobilization,* amejenga mabanda na kununua magari ya wafanyakazi halafu anajenga barabara kilometa 10 labda *certificate* ya shilingi 10,000,000,000 pesa inachukua mwaka mzima hajalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii tunafanya nini sisi, hii sheria ipo kwa ajili ya kum-*favor* nani? Ninaomba Mheshimiwa Ulega ninajua ni mtu makini na ana Mheshimiwa Naibu Waziri mzuri, ni injinia hebu aiangalie vizuri hii sheria inatu-*favor* sisi kama nchi au inawa-*favor* watu wengine. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuomba uniongezee hata dakika mbili nimalize.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa malizia muda wako umekwisha.

MHE. PATRICK A. MWALUNENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mimi ni mtu wa mwisho, ninaomba dakika mbili tu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, bado bado kuna wachangaji wengine, malizia sekunde 30.

MHE. PATRICK A. MWALUNENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Jambo lingine tunao sisi wasomi wetu hapa ndani ambao ni wataalam, tuwajengee uwezo, wafungue makampuni wale vijana wetu ili wao ndiyo wawe wanajenga hizo barabara na tuwape hizo *advance payment*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi imekuwa ni tabia kampuni za nje zinakuja kufungua kampuni hapa nchini zinajifanya ni *local company* ambayo tunaangalia *local content* kumbe ni kampuni za nje, wanapewa *advance payment* zinakwenda nje, ndiyo wanaamua shilingi ngapi zije kujenga

barabara. Hatuwezi kufikia malengo na kumsaidia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. PATRICK A. MWALUNENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri aliangalie sana. Ninaunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Charles Jacob Sungura, tutamalizia na Mheshimiwa Kinjitile Ngombale Mwiru.

MHE. DKT. CHARLES J. SUNGURA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Ujenzi. Kwanza nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu Mkoa wa Tanga umetengewa takribani shilingi 78,000,000,000 kwa ajili ya ukarabati wa uwanja wetu wa ndege. Fedha hizi zitasaidia katika upanuzi wa uwanja ule kwa sababu mpaka dakika hii eneo la kutua na kurukia ndege ni meta 1,268 ambazo zilisababisha mpaka ndege kubwa zitakuwa hazitui pale Tanga lakini kwa fedha hizi tayari itaweza kuongeza mpaka meta 2,500 takribani kilometa 2.5 ambayo itawezesha kutua kwa ndege kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, fedha hizi pia zitasaidia katika ujenzi wa eneo la kuegesha ndege, pia ujenzi wa jengo jipya la abiria pamoja na mnara wa kuongozea ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu utakapokamilika utasaidia sana wananchi wa Mkoa wa Tanga hasa katika kukuza utalii pamoja na kuchochea biashara katika Mkoa wetu wa Tanga. Kwa maana hiyo ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa sababu ya fedha hizi shilingi 78,000,000,000 ambazo zitakwenda kusaidia kukuza utalii pamoja na biashara katika mkoa wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa nijikite katika barabara zetu za kimkakati. Ukiangalia Mkoa wa Tanga tuna hii

Barabara yetu ya Tanga – Segera - Chalinze. Barabara hii ni mshipa mkubwa sana katika maendeleo ya Mkoa wetu wa Tanga na Jimbo la Handeni. Kwa sababu barabara hii si kwamba tu inaunganisha mkoa na mkoa, lakini pia inaunganisha Tanzania na Nchi ya jirani ya Kenya, kwa maana hiyo ni barabara muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano sasa hivi ukiangalia Bandari ya Tanga imetanuka, kutanuka kwa Bandari ya Tanga kunaongeza msongamano mkubwa wa maroli katika Barabara yetu ile ya Segera - Tanga - Chalinze. Kwa maana hiyo ninamwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa aje na maelezo yaliyonyooka ya kwamba ni lini miradi hii itaanza ili kuhakikisha barabara hii inaongezeka, lakini pia inatanuliwa kutoka njia mbili kuwa njia nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ninaomba Waziri atambue kwamba Ukanda wetu wa Pwani kuanzia Chalinze, Mkata, kwa Msisi, kwenda Kwedizinga, Kabuku, Segera mpaka Tanga ni ukanda ambao una viwanda, ni ushoroba ambao una viwanda vingi. Katika kongani za viwanda za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anakwenda jenga viwanda vingine zaidi katika ukanda ule kwa maana hiyo tutegemee kuongezeka kwa malori mengi sana mbali na haya ambayo yanatoka katika bandari zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo ninaomba kumsisitiza Mheshimiwa Waziri, atakapokuja atupe uhakika namna gani hii barabara itaenda kujengwa na lini itaenda kujengwa. Barabara hii ni *East African Highway* nilishasema mwanzo inaunganisha Nchi jirani ya Kenya kupitia Handeni kwa maana hiyo bado umuhimu wake ni mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, mbali na hapo barabara hii inaruhusu magari yanayotoka upande wa kaskazini kwa maana ya Kilimanjaro na Arusha yanapita katika njia ile, hivyo msongamano bado ni mkubwa zaidi. Ninaomba atakapokuja pia atupe maelezo yaliyonyooka, sina lengo la

kushika shilingi, lakini nataka maelezo yaliyonyooka. Ni lini barabara hii itajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo Barabara nyingine kutoka Handeni - Mziha - Turiani yenye kilometa 108. Barabara hii ni *shortcut* ya usafiri wa mizigo kutoka Bandari ya Tanga kama nilivyosema, lakini pia na maeneo mengine ya kaskazini kwa maana ya Arusha na Kilimanjaro barabara hii itasaidia kurahisisha usafiri wa mtu ambaye anazunguka kupitia Chalinze mpaka Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, barabara hii ikitengenezwa inakuwa ni *shortcut*. Kwa mfano mtu anayetoka Handeni apitie Chalinze mpaka Morogoro mpaka Dumila atatumia takribani masaa sita na nusu, lakini kama itawekwa lami mtu atatoka Handeni mpaka Dumila atatumia masaa mawili na nusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo tuiangalie hii barabara kwa jicho la kiuchumi kwa sababu ni barabara muhimu sana na pia itachagiza sana mizigo inayotoka kwenye Bandari yetu ya Tanga itapita katika barabara hii lakini pia itaenda maeneo mengine ya Iringa na maeneo mengine ya Nyanda za Juu Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo barabara nyingine ninaomba niizungumzie, ipo barabara inayotoka Mkata - Pozo - Kwa Msisi. Barabara hii inasikitika kwamba ni miongoni mwa barabara za *RISE* za *World Bank,* lakini mpaka dakika hii sijaona Wizara kama wameitangaza. Kwa hiyo, ninaomba anapokuja kwenye majumuisho atuambie ni lini atatangaza barabara hii ili zabuni itangazwe na iweze kujengwa wananchi wangu wa Kwamkata Kwamsisi na Pozo waweze kunufaika. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. DKT. CHARLES J. SUNGURA: Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwisho kabisa…

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, muda wako umekwisha malizia.

MHE. DKT. CHARLES J. SUNGURA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana. Lipo Daraja la Mto Mligazi, daraja hili linaunganisha Kata ya Kwasunga pamoja na Kata ya Miono. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa sababu ameshalitembelea na nimeshamletea *BOQ* ya shilingi 989,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba sasa kwenye majumuisho yake aniambie kama mwaka huu kama alivyoahidi atalijenga daraja lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu ni Mheshimiwa Kinjekitile Ngombale Mwiru.

MHE. KINJEKITILE N. MWIRU: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo kunifikisha hapa niweze kuongea. Pili ningependa kumshukuru Mheshimiwa Rais wangu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu, kwa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi ya kisasa katika Wilaya yetu ya Kilwa ambayo ni jambo ambalo watu wa Kilwa wanamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ningependa kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia, kwa madaraja, sasa hivi kusini na wilaya yangu ya Kilwa hakuna tena mambo ya daraja kuvunjika, watu kulala njiani, mambo hayo yamekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijikite kwenye hoja zangu tatu. Kwanza ni Barabara yetu ya kutoka Dar es Salaam kwenda Mnazi Mmoja – Lindi. Hii barabara haifai, haifai kabisa yaani imekwisha. Haiwezi hata kuwa *repaired* tena, Mheshimiwa Dkt. Samia ametujengea madaraja mazuri sana, lakini barabara haifai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoka Makao Makuu ya Wilaya ya Kilwa mpaka Dar es Salaam ni kilometa 330, basi linatumia masaa nane mpaka tisa, jamani wananchi wanateseka sana. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri aangalie huko kwenye jungu kuu tunaweza tukaanza vipi kuitengea hela hii barabara. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, atupe maelezo yanayoeleweka kuhusu Barabara hii tunafanya nini kuanza kuirekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya pili Mheshimiwa Waziri anaifahamu sana Barabara ya Nangurukulu Zinga - Liwale. Mheshimiwa hii barabara haifai jamani kama mnabisha naombeni wabunge twende tufanye ziara kule watu wanateseka mpaka leo miaka yote ya uhuru watu wanalala njiani. Mimi mwenyewe Mheshimiwa Mbunge ninalala njiani, haifai kabisa ile barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, ninajua nimepata lami kilometa 72 zinaanzia Liwale lakini tuangalie huku Ngea – Miguruwe - Njinjo tunafanya nini ili watu wapite mwaka mzima wakati tunatafuta pesa za kuimalizia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya mwisho ni Barabara ya kutoka Tingi Njianne kwenda Kipatimu. Hii barabara juzi ndiyo imeweza kufunguka kuwa na mabasi ya kufika Kipatimu. Mabasi yalikuwa yanaishia Chumo na Mheshimiwa Waziri anajua kule kuna wazee, kuna wagonjwa, unavyoanza kusema kwamba wapande boda boda au wabebwe kichwani mpaka Chumo ndiyo wapande mabasi ni tatizo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anaifahamu sana Kilwa nikigombea naye anaweza akanishinda kwa vile anavyojulikana katika Wilaya ya Kilwa, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, aifikirie hii barabara iweze kupitika wakati ule utaratibu wetu wa lami unakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ninamwomba Mheshimiwa Waziri taa katika kata zangu za Kilwa; Kata ya

Mingumbi, Chumo na Mayuni Kipatimu, Njinjo na Miguruwe ninamwomba Mheshimiwa Waziri basi hata watu waone wakitembeatembea hivi wakati wanasubiri mambo mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsanteni sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, ahsante sana. Waheshimiwa tumefikia mwisho wa Shughuli yetu ya Bunge kwa mchana huu. Kipindi cha jioni tutaendelea na wachangiaji wafuatao: Mheshimiwa Asia Abdulkarim Halamga, Mheshimiwa Patali Shida Patali, Mheshimiwa Yohana Stephen Msita, Mheshimiwa Profesa Pius Zembe Yanda na tutaendelea kutaja orodha jinsi tunavyoendelea kuchangia.

Kuna tangazo kutoka Katibu wa Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi anawakumbusha Waheshimiwa Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi kwamba tutakuwa na kikao saa 7.30 katika Ukumbi huu wa Msekwa leo hii.

Baada ya tangazo hili ninasitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 7.02 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)

Mwenyekiti (Mhe. Cecilia D. Paresso) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae.

Katibu.

NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

(Majadiliano yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano ya hoja iliyopo mbele yetu ambayo ni bajeti ya Wizara ya Ujenzi.

Sasa ninamwita Mheshimiwa Asia Abdulkarim Halamga, wajiandae Mheshimiwa Patali Shida Patali na Mheshimiwa Yohana Stephen Msita.

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu na baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, nichukue nafasi hii kumpongeza na kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo ameendelea kufanya mageuzi ya kiuchumi nchini kwetu, lakini katika kuhakikisha tunaendelea kuunganisha mikoa kwa kiwango cha barabara za lami lakini pia tunaunganisha kupitia reli pamoja na anga. Haya ni mageuzi makubwa na hatua kubwa kabisa katika Nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri kweli nimeamini; umoja wa vijana ni tanuri la kupika na kuoka viongozi na ndiyo maana leo Mheshimiwa Waziri Abdallah Ulega ameiva katika Wizara hii na katika kuhakikisha kwamba anatutumikia sisi Watanzania na kutusikiliza sisi wawakilishi wa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri bila kusahau Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na watumishi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nichukue nafasi ya kumpongeza sana Meneja wetu wa Mkoa ndugu yetu Masele kwa kazi kubwa ambazo anazozifanya: Meneja wa *TANROADS* Mkoa pamoja na timu nzima ya *TANROADS,* Mkoa wa Manyara, bila kumsahau Meneja wa *TARURA* Mkoa pamoja na Meneja wa *TARURA* na watumishi wote wa *TANROADS* pamoja na *TARURA* katika Mkoa wa Manyara na hususani Jimbo la Hanang.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Manyara una takriban ya barabara zinazosimamiwa na *TANROADS* kilometa 1,657 lakini katika kilometa hizi tuna kilometa 257. Kati ya kilometa hizi 257 sisi kama Mkoa wa Manyara tuna kilometa 52 pekee za lami. Kilometa 257 ni kilometa zinazounganisha Mkoa wa Manyara, Babati - Dodoma, Babati - Singida, Babati - Arusha zinasababisha kuwa na kilometa 257, lakini ukiingia ndani ya mkoa tayari sisi tuna kilometa 52.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Manyara tuna uchumi wa kutosha. Tuna imani sisi Wanamanyara na wananchi wametutuma hapa tuje tuipishe Serikali bajeti hii, lakini tuombe kwamba watuondoe kwenye kilometa 52 za barabara watuongezee tuwe na mtandao mkubwa wa barabara na sisi tunufaike na mema ya Nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo barabara ya muhimu sana inayopita katika Mkoa wa Manyara. Barabara inayounganisha Mkoa wa Manyara na mikoa yote ya Tanzania, lakini Mkoa wa Manyara, Nchi ya Tanzania pamoja na nchi zingine za jirani. Kipande cha Barabara ya Dareda mpaka Gehandu yenye kilometa 82 kwa sasa kipande hiki kimeharibika, kimechakaa, tumekwishafanya marekebisho ya mara kwa mara, tumekwishaweka viraka mara kwa mara, lakini na viraka kwa sasa vimekataa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna imani tunakwenda kupitisha bajeti tunaomba tupewe fedha tukaikomboe barabara hii ya msingi na ya umuhimu katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo Bandari ya Tanga ambayo kwa sasa hivi inatuletea fedha za kigeni, lakini fedha zenyewe za nchi yetu ya Tanzania. Kama haitoshi Mkoa wa Manyara hususani Wilaya ya Hanang tunapokea magari ya kutosha kwa ajili ya mazao. Tuna chumvi ya kutosha, dhahabu pia ipo na uchumi mkubwa. Tunaomba sana ndani ya Wizara ya Ujenzi leo akianza Dar es Salaam, aje Tanga, aje Kilimanjaro, aje Arusha, aje Manyara atoke aende Singida mpaka Mwanza hakuna kipande kibovu kilichoharibika zaidi kama kipande cha kilometa 82, kipande cha kutoka Dareda mpaka Gehandu. Mheshimiwa Ulega *is my brother*, yeye ni *Youth League* mwenzangu ninamhakikisha siwezi kuishika shilingi yake kwa sababu ninahitaji fedha, wananchi wa Hanang wamenituma, akina mama, akina baba, vijana, wazee, lakini viongozi wote wa dini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Hanang wamenituma wanaomba sana, wana mapenzi mema na Serikali yao, wanatambua kazi ambazo zimefanyika kwenye vituo vya afya, elimu, maji na miundombinu mingine na sasa ni zamu yetu tukitengeneze kipande hiki ili tuweze kuupata uchumi na watu wetu wapite kwa masaa yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kabisa ukiachana na hiki kipande cha *national road* ambacho kinaunganisha Mkoa wa Manyara na mikoa mingine lakini Mkoa wa Manyara na nchi zingine. Sisi Wanahanang tuna kipande cha barabara kinachoitwa Mogitu - Haydom chenye kilometa 68. Kipande hiki cha barabara kipo katika awamu zote kwenye Ilani za uchaguzi na hata sasa nje ya Ilani ya Uchaguzi bado imekuwa ni ahadi ya viongozi wetu wakuu wa nchi. Tunaiomba sana Serikali, kipande hiki mwaka 2016 upembuzi yakinifu ulianza; 2016 mpaka sasa 2026 ni takriban miaka 10. Tumeona tumewekwa kwenye mpango lakini mwendelezo wa upembuzi yakinifu. Tunaomba sana kwa mara ya kwanza na sisi tupate hata lami kilometa moja ya kuanzia licha ya 68 ambazo tunazihitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upembuzi yakinifu umekwishachukua takribani miaka 10, sasa wananchi wa Hanang wanasubiri lami kwa heshima na unyenyekevu mkubwa sana kwa sababu ni wakulima wazuri, wana uchumi mkubwa wa nchi hii, magari yanaingia ya kutosha na sisi katika Taifa letu tuweze kuchangia mapato yale ili yaweze kufanya kazi ya kufanya maendeleo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo barabara ya kimkakati. Wanaposimama hapa Wabunge kuongelea habari ya Barabara ya Sibiti inayokwenda Simiyu, barabara hii ni nyepesi sana. Kuna Barabara ya kutoka Nangwa - Gisambalang kuja Daraja la Munguri, Mkoa wa Dodoma, Jimbo la Kondoa. Hii ni barabara nyepesi sana itakayounganisha Mkoa wa Dodoma, Mkoa wa Manyara pamoja na mikoa ya Kanda ya Ziwa kwa maana ya Simiyu, Mara na mikoa mingine. Barabara hii ina jumla ya kilometa 79. Tunaomba sana imekuwepo kwenye Ilani, imeanza upembuzi yakinifu, ni ahadi ya viongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa barabara hii iweze kufanyiwa kazi...

MHE. MARIAM D. MZUZURI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Asia Halamga kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mariam Ditopile.

TAARIFA

MHE. MARIAM D. MZUZURI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Ninaomba kumpa taarifa Mheshimiwa Asia Halamga, Mbunge wa Hanang.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara anayoizungumzia inayounganisha Jimbo la Hanang kwa maana Mkoa wa Manyara na Jimbo la Kondoa Mjini kwa maana ya Mkoa wa Dodoma ni kweli pamoja na kilometa hizo 70 pia linajumuisha daraja ambalo ni la msingi na daraja hili limevunjika miaka 15 iliyopita, Daraja la Munguri B.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atakapojibu na taarifa ninamwongezea tu kwamba upembuzi yakinifu tayari na vilevile Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshatoa kauli kule kwamba daraja hili na barabara hii litajengwa kwa kiwango hicho cha lami.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Asia unaipokea taarifa hiyo?

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ni lazima niipokee kwa mikono yote miwili na mimi ninaendelea kupiga dua kwamba fedha zipatikane, tupitishe hapa bajeti na tuweze kujenga barabara hii ni kiunganishi kikubwa sana cha uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi nilichotaka kuomba ni Barabara ya Mogitu - Haydom kilometa 68, lakini Dareda - Gehandu kilometa 82, lakini Nangwa kwenda Daraja la Munguri kilometa 79. Bila kusahau mkoa wetu una kilometa 52 tu, tuna mapenzi makubwa, tuna imani kubwa na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. Mheshimiwa Rais amejenga vituo vya afya, amejenga majengo kama uyoga, hatuna hofu wala shaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukishapitisha bajeti hapa ninamwomba sana Mheshimiwa Ulega, wananchi wa Hanang wapo tayari kupokea mema ya nchi na wanapenda chama hiki na wanapenda Serikali hii na wanampenda Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tuna imani kubwa kwa matunda ambayo ametupatia miaka mitano iliyopita, hatuna hofu na 2026/2030. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Patali Shida Patali, ajiandae Mheshimiwa Yohana Stephen Msita.

MHE. PATALI S. PATALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa kupata fursa hii ya kuchangia hotuba ya bajeti hii muhimu ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasaa huu na dakika hizi katika wakati wote tukiwa kwenye hivi vikao vya bajeti, leo hii Jimbo la Mbeya Vijijini takriban wananchi 500,000 wamenyamaza kimya kusikiliza juu ya mustakabali wa barabara zao za kimkakati, barabara tatu. Nami ninaomba niseme kwa niaba yao. Barabara ya Mbalizi - Shigamba nimepitia bajeti vizuri barabara hii ipo, ninaishukuru Serikali. Barabara ya Isyonje - Kikondo mpaka Makete nimepitia vizuri bajeti hii barabara hii ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Mbalizi - Chang'ombe inayoenda Mkwajuni - Makongolosi mpaka kuunganisha mikoa ya karibu Singida mpaka Tabora nimepita vizuri bajeti hii barabara hii ipo. Kwa heshima kubwa ninaomba niiombe Serikali kuwepo kwenye bajeti barabara hizi ni jambo moja. Sasa baada ya Wanambeya Vijijini kusubiri kwa zaidi ya miongo mitatu, niisihi sana Serikali yangu barabara hizi zikajengwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hizi Barabara, lakini ninaomba niseme jambo moja, niliuliza swali la nyongeza kupitia Wizara hii ya Ujenzi; Barabara ya Mbalizi Shigamba. Nikajibiwa kwamba mwaka huu tumepewa kilometa 10. Ninaomba Mheshimiwa Waziri kaka yangu Ulega, sina shaka naye na yeye ndiye Waziri pekee ambaye ameapishwa tu amefika jimboni kwangu Mbeya Vijijini pale Songwe. Kwa hiyo, sina shaka na utendaji wake, ninaomba hizi kilometa 10 zianze haraka vile inavyowezekana twende tukawafute vumbi Wanambeya Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na barabara hii Mkoa wa Mbeya, mkoa ambao ni mkoa wa tatu kwa kuchangia pato la Taifa, nyuma ya Mkoa wa Dar es Salaam na Mwanza, barabara zake zimekuwa katika hali mbaya sana. Ninaomba nichukue fursa hii kwa moyo wa unyenyekevu mkubwa kumshukuru sana Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, baada ya kelele nyingi za Wanambeya Vijijini ametufuta mavumbi, ametupatia fedha zaidi ya 4,000,000,000 ambazo zimemrudisha mkandarasi *site*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu la msingi kwenye jambo hili. Ninaomba Mheshimiwa Waziri mkandarasi huyu asimamiwe asiondoke *site* tena ikiwa ni pamoja na kumaliza

certificates zake anazodai zaidi ya shilingi 4,000,000,000 zingine ili aongeze kasi ya kutengeneza barabara hii Wanambeya waondokane na hii adha ya vumbi ambayo wameipata kwa zaidi ya miezi minne sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nishauri hapa Jiji la Mbeya lina barabara moja tu, ile *highway* ambayo ni *TANZAM*. Mheshimiwa Waziri kwa kuwa wamekuja kupitia *TANROADS* na mpango wa kutengeneza barabara ya mchepuo; na hapa nimpongeze sana *Engineer* Bishanga, Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Mbeya kwa usimamizi wake makini sana. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri ile barabara ya mchepuo kutoka Uyole kupitia Kata ya Swaya inaenda kutokea Songwe ianze sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, ile barabara ikianza itapunguza msongamano katikati ya Jiji la Mbeya. Jambo la pili, itaharakisha matengenezo ya barabara sababu magari pale katikati yatakuwa machache; na jambo la tatu na la muhimu, itafanya hizi barabara zidumu kwa sababu yale malori makubwa yatapita kwenye hii njia ya mchepuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba nishauri jambo lingine la msingi. Serikali hii tunatambua jitihada kubwa zinazofanywa kuwaletea maendeleo Watanzania hususani hapa kwenye uwekezaji wa miundombinu kwenye nchi yetu hasa barabara zaidi ya 40,000,000,000,000 sasa zimewekezwa. Ni dhahiri kwamba uwekezaji huu uende sambamba na maono ya usimamizi wa *quality* ya hizi barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri jambo moja; ninaomba Serikali ione haja ya kutenganisha majukumu ya usimamizi wa *quality* ya barabara pamoja na majukumu ya utengenezaji wa barabara. Niishauri Serikali kuona haja ya kuunda chombo mahsusi kinachojitegemea cha usimamizi wa *quality* za hizi barabara zinazojengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto kubwa na Waheshimiwa Wabunge watakubaliana na mimi, barabara zetu

zinatengenezwa baada ya muda mfupi zinaharibika. Sasa tuliondolee jukumu hili la usimamizi wa *TANROADS*. *TANROADS* ibaki na jukumu la utengenezaji wa Barabara, lakini usimamizi wa *quality* wa zile barabara kuwepo kuna *agency* inayojitegemea na hii *agency* iwe na watumishi ambao ni *well vetted* na hawana mashaka yoyote na uzalendo wao wa juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba nihitimishe na jambo moja la msingi na kwa kifupi sana kwa dakika moja. Miaka ya 1990 ninakumbuka magari yote nchi yetu yalikuwa yanasajiliwa kimkoa, lakini nimebahatika kutembelea Nchi ya *South Africa* nimeona magari yanasajiliwa *GP, Gauteng* yanasajiliwa kimkoa au ki-*province*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo ninalolitazama.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako muda wako umekwisha.

MHE. PATALI S. PATALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninaomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Nilimtaja Mheshimiwa Yohana Stephen Msita; Mheshimiwa Pius Zebhe Yanda na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, wajiandae.

MHE. YOHANA S. MSITA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii adhimu sana. Nianze kwanza kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo ametukumbuka sana watu wa Jimbo la Itigi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Itigi kwangu Mjini tuna kilometa 10 za barabara ya lami. Jambo ambalo kwa kweli hapo nyuma lilikuwa ni hadithi. Nikushukuru sana Mheshimiwa Rais, nikushukuru sana Waziri wa Ujenzi kwa kazi kubwa ambayo

imefanyika pale, mabilioni ya fedha yamelala pale kwenye Jimbo langu la Itigi pale mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru pia maana nisiposhukuru nitakuwa ninajifunza roho mbaya na mimi bado kijana. Tuna kilometa 25 ambazo zinatoka Noranga mpaka Itigi, hii Barabara kubwa ya kwenda Rungwa mpaka Makongolosi. Tayari kilometa 25 zimekamilika na mkandarasi saa hizi yupo *site* anafanya *finishing* kumalizia ile barabara. Tunashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninataka nizungumzie Barabara hii ya kutoka Mkiwa - Itigi kuelekea Rungwa - Makongolosi ambayo kwa kweli barabara hii ndiyo imebeba uchumi mkubwa, ndiyo imebeba siasa kubwa sana ya Jimbo la Itigi. Hii barabara ya kutoka Mkiwa mpaka Makongolosi takriban kilometa 356. Ni kipande kidogo tu cha kilometa 25 ndiyo kimekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimeona kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri kwamba, wametenga bajeti, kwa ajili ya mwaka huu wa fedha takribani shilingi 6,000,000,000, lakini bado fedha hii haitoshi kwa sababu, hii barabara inaunganisha Mikoa karibu sita ya Singida, Tabora, Katavi, Songwe, Mbeya. Ili tuweze kutengeneza uchumi lazima tuhakikishe hii barabara yenye urefu wa kilometa 356 ikamilike kwa kiwango cha lami; imekuwepo kwenye ilani karibu awamu tatu tangu 2015, 2020 na sasa 2025 kwenda 2030, bado barabara hii imekuwa ni kizungumkuti, haijakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema tu, Itigi pale ndiyo kitovu hasa, watu wanaotoka Tabora, watu wanaotoka Mbeya, watakutana pale, kwa ajili ya kupanda treni ya mwendokasi kwa sababu, Stesheni kubwa sana ya *SGR* pale inakwenda kujengwa. Kwa hiyo, tunakwenda kuifungua nchi yetu kutoka Nchi za Zambia, Malawi na kadhalika na ile mikoa ya Nyanda za Juu Kusini yote itapita kupitia Itigi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema tu, kama barabara hii itakamilika maana yake ni kwa miaka mitano tutakuwa tumeokoa

takribani shilingi 40,000,000,000 kwa sababu, mtu anapotoka Mbeya akazungukia hii Barabara ya Iringa kuja Dodoma anakuwa ametembea zaidi ya kilometa 300 mpaka 400, wakati angepita hii ya kutokea Makongolosi kuja Itigi angeokoa kilometa 300. Sasa ukifanya *rate* utakuta gari moja likitembea kilometa 300 litatumia karibu lita mia moja za mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukitumia lita 100 za mafuta unazungumzia karibu shilingi 450,000. Hiyo ni kwa lori moja, maana yake ni ukiwa na malori 50 kwa siku, unazungumzia umepoteza fedha shilingi 22,500,000 kwa mwezi tutakuwa tumepoteza shilingi 675,000,000. Kwa mwaka tutakuwa tumepoteza shilingi 8,100,000,000 kwa miaka mitano tutakuwa tumepoteza jumla ya shilingi 40,500,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunatenga shilingi 6,000,000,000, lakini tunakwenda kupoteza shilingi 8,000,000,000 kwa mwaka. Ninadhani hii barabara sasa, Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa kuhitimisha, atuambie Barabara kutoka Noranga kuelekea Rungwa kuelekea Makongolosi, bado hatuna mkandarasi pale. Imefanyiwa upembuzi, imefanyiwa usanifu, lakini bado hayupo mkandarasi wa kujenga ile barabara. Sisi barabara ile ndiyo imeibeba uchumi, ndiyo imeibeba siasa ya Jimbo la Itigi. Ninaiomba sana Serikali, hii barabara tuitazame kwa macho mawili, ili tuitengee fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema tu hapa na tunakubaliana na Wabunge wenzangu kwamba, Wizara ya Fedha hata tungesema mpaka jioni hapa, kama Wizara hii haiongezewi fedha! Tukate matumizi mengine mahali pengine, ili tuiongezee fedha, shilingi trilioni 2.5, bado haitoshelezi kwenye ukarabati wa ujenzi wa barabara za nchi hii. Ninaomba sana Wabunge wenzangu tuungane pamoja, ili tuweze kuiambia Serikali iongeze fedha kwenye Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha nasema tu kwamba, sisi tunaunga juhudi za Serikali mkono, jinsi ambavyo inaendelea kupambana na ujenzi wa barabara na marekebisho ya barabara. Wabunge wote tunakubaliana hapa kwamba,

upitaji wa barabara umekuwa ni mgumu sana, barabara zimechimbika, kuna mahali barabara hazipitiki. Leo mazao yanashindwa kusafirishwa, watu wanapata changamoto barabarani, wagonjwa wanapoteza maisha, changamoto kubwa ni hii barabara. Nchi ili iweze kukua kiuchumi ni lazima ihakikishe miundombinu ya barabara inapitika vizuri, ili uweze kwenda kwenye uchumi mkubwa ambao tunautarajia kwenye Dira ya 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti baada ya maneno hayo, ninakushukuru sana kwa nafasi, lakini ninaomba tujifunze kwa Mataifa mengine katika kusimamia matumizi ya fedha za barabara zinazopelekwa kule kwa wakandarasi na kuzingatia ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo, ninakushukuru sana, ninaamini Itigi baada ya mwaka mmoja sasa inakwenda kung'aa. Ninaunga mkono hoja. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Ninamwita sasa Mheshimiwa Pius Zebhe Yanda.

MHE. PIUS Z. YANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nichangie hiyo hotuba ya bajeti ya ujenzi. Awali ya yote ninaomba kwanza, nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuwezesha kufungua Mkoa wa Kigoma na kuwezesha miundombinu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka wakati wa ziara yake ya kugombea uchaguzi uliopita, aliweza kutamka neno moja muhimu sana. Akasema, mikoa ya pembezoni siyo ya pembezoni tena, ni mikoa ambayo ni ya kimkakati kwa hiyo, yuko tayari kuweza kuifungua, ili kwa kweli, iweze kuchangia katika maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hilo kwa sababu, ule ulikuwa ni mkoa ambao kwa kweli, tukizungumzia miundombinu, mkoa ule ulikuwa katika hali mbaya sana. Kwa mara ya kwanza ni

kipindi ambacho tulianza kupata Barabara kutoka Tabora kwenda Kigoma mpaka Kasulu, lakini barabara ya pili, ambayo tuliipata hivi karibuni inatoka Nyakanazi – Kibondo – Kasulu mpaka mpakani mwa Tanzania na Burundi. Hiyo barabara imeweza kufungua milango mikubwa sana huko, lakini kana kwamba haitoshi, kuna ujenzi ambao unaendelea pia, wa Kituo cha Forodha cha pamoja ambacho na chenyewe kitafungua milango ya kiuchumi kati ya Tanzania na Burundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uwekezaji huo bado kuna changamoto chache ambazo tunahitaji kuziangalia. Kwa mfano, ile Barabara ya Nyakanazi mpaka mpakani mwa Burundi, kupitia Buhigwe, maeneo makubwa hayajawa na barabara na taa za barabarani, ikiwemo Buhigwe *Center* na vijiji vyote kandokando ya hiyo barabara, lakini changamoto nyingine ni vijiji vilivyoko jirani na Buhigwe; kwamba ile barabara ina mifereji mikubwa sana, hawajaweka matoleo ya wananchi kuweza kutoka barabarani kuvuka kwenda kwenye makazi yao. Kwa hiyo, inabidi wazunguke eneo kubwa sana, mbali, ili kuweza kuvuka ile mifereji. Sasa ni ombi langu kwa Wizara husika kuwezesha hilo liweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa ziara ya kampeni ya kuomba kura kwa wananchi, Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya ujenzi wa Barabara ya Kalela – Buhigwe mpaka Muyama – Mugera na kuelekea Kibondo. Juzijuzi wananchi waliona kibao kikubwa kimewekwa, kwa ajili ya ujenzi wakafikiri sasa ule ujenzi wa lami unaanza na walianza kusherehekea, kesho yake nikawaambia wapige picha wanitumie, lakini walipotuma tukakuta kwamba, kumbe ni ukarabati wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walinyong'onyea pamoja na kwamba, jana yake walikuwa wanasherehekea. Sasa ombi langu, kwa niaba ya Wanabuhigwe, ile ni barabara ya kimkakati, ambayo inaunganisha kata zaidi ya 10 kati ya 20 na inakuja kuungana na Wilaya ya Kibondo na Kakonko. Kwa hiyo, ninaomba pia, Wizara iweze kufikiria na kuona ni jinsi gani inaweza kuwezesha hilo jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Barabara ambayo inatoka Makere na kwenda kuungana na hiyo barabara nyingine. Hiyo pia, tutafurahi kuona kwamba, inaanza kufikiriwa kuwekewa lami, ili wananchi waweze kupata nafuu ya kutembea kutoka maeneo mengine kwa shughuli za kiuchumi na za kijamii pia. Itakuwa ni rahisi kwa wananchi kwenda kupata huduma kwenye vituo vya afya na pia, hata hospitali kubwa za wilaya. Sasa maombi yangu kwa Wizara husika ni waangalie ni jinsi gani waweze kulifanyia kazi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ni kubwa zaidi ni, tunazungumza barabara zinajengwa, kesho yake zinaanza kuharibika. Kuna sababu moja ya msingi ambayo inabidi pia tuifikirie, mabadiliko ya tabianchi yanabadilisha mfumo wa mvua. Kwamba, mwaka hadi mwaka kiasi cha mvua kinachonyesha ndani ya muda mfupi kinazidi kuwa kingi, sasa maji yakituama kwenye barabara ambayo imejengwa, ya lami, kwa vyovyote vile lazima ibomoke. Sasa ninachotaka kupendekeza ni kwamba, tufike mahali tusitumie *design* ya *business as usual* kwenye *design stage,* tuanze kufikiria *business unusual,* ambapo suala la mabadiliko ya tabianchi liweze kuhusishwa kwenye *design* za barabara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwa nimesema hayo, ninaunga mkono hoja iliyoko hapo mbele yetu. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, wajiandae Mheshimiwa George Natany Malima, Mheshimiwa Zuberi Yahya Mfaume na Mheshimiwa Mabula Johnson Magangila.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi. Ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutuona watu wa Tarime, Mugumu, Serengeti kupata barabara ya kilometa 87; barabara imeanza ujenzi, imefika Makao Makuu ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amefika hivi karibuni akaona, yule mkandarasi anadai shilingi bilioni 4.8 na kule

Serengeti mkandarasi aliweka *camp* na imedondoka, ametoka *site*. Basi ninaomba atakapopata fedha apeleke, hii kazi iweze kufanyika, tuunganishe Wilaya ya Tarime pamoja na Wilaya ya Serengeti. Watalii wanapata shida sana kutoka kule Mugabili – Nginjanginja; unashangaa namna ambavyo wanachangia mapato, tena *in terms of dollar,* lakini barabara zetu ni mbovu kiasi kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo machache ninataka nipitie kwa harakaharaka kwa muda ambao amenipa. Tunazo barabara zetu za Mkoa wa Mara; Barabara ya Musoma – Makojo – Busokero, kwa Mheshimiwa Profesa Muhongo. Barabara ya Musoma – Bunda, ambayo inamuunganisha Mheshimiwa Bulaya na kule Mheshimiwa Kangi Lugola. Barabara ya kutoka Tarime – Serengeti, ambayo nimeitaja mimi na Mheshimiwa Esther Bulaya, Barabara ya kutoka Utegi kwenda mpaka Shirati na Barabara ya kutoka Makutano kwenda Mugumu, Serengeti, ambayo inapita Butiama kwa Baba wa Taifa; hizi ni barabara muhimu sana, zikifunguliwa zitasaidia sana watu wa Mkoa wa Mara kuwasiliana kufanya shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa ambayo nimeisoma hapa, *summary* ya Kamati, Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba, wenyewe wameandika 70% ya barabara zetu ni mbovu, 30% tu ndiyo zina afadhali, lakini 39.4% barabara hizi zimezeeka. Maana yake ni kwamba, haya mambo ambayo wenyewe wataalam wameandika anapokwenda kutafuta fedha ajue kwamba, kuna kazi kubwa ya kufanya ku-*maintain* barabara hizi ziweze kupitika. Siwezi kurudia kwa sababu, Waheshimiwa Wabunge wametaja kila mkoa na kwa kweli, maeneo haya ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri ana kazi ya ziada hapa, ziko barabara, kwa mfano Barabara kutoka Iringa – Dodoma, barabara hii hata kabla ya muda wake kwisha imeharibika. Barabara kutoka pale Mwigumbi – Maswa – Bariadi, mkandarasi hatoki *site*, haifanyi kazi, achilia mbali hii shida ya Singida – Babati – Arusha. Sasa Mheshimiwa Waziri hawa watu ambao wanajenga

hizi barabara, zinaharibika kabla ya muda, unachukua hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, unapeleka fedha kujenga barabara, kabla hajaikabidhi, barabara ni mbovu na hatujawahi kuona mtu amepelekwa mahakamani, amewajibishwa au ametaifishwa mali. Wanapoteza fedha za wananchi, lazima Bunge hili liweke mpango mkakati, watu ambao wanajenga barabara chini ya kiwango. Tusiishie kutafuta fedha na kupeleka, watuambie kwa nini wanajenga barabara chini ya kiwango?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawawajibishwe, watoe mfano kwa mtu mmoja tu. Mtu akafilisiwa kwa kuharibu fedha za Watanzania watashika adabu na mtu akipewa kazi atafanya. Barabara zingine zipo, kwa mfano kutoka pale Bunda mpaka Sirari, miaka nenda miaka rudi utafikiri imejengwa jana; hawa wakandarasi wapo na hii inazua maswali mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo ninataka niiseme hapa ni tunayo Sheria ya Mwaka 2019 ile, ambayo inazungumzia Mfuko wa Barabara. Tufanye mambo mawili; moja ni, kama kuna mianya, kuna matobomatobo pale tuyazibe, fedha ile ikitengwa iende moja kwa moja kwenye kazi ambayo tumekusudia hapa kutenda. La pili ni, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, fedha zote ambazo zilitakiwa ziende Mwaka 2024/2025 walipeleka 35%. 35% hii iende ikajenge barabara zetu! Mwaka 2025/2026 ni 44%, kuna 54% haijaenda! Fedha hizi zikienda zitasaidia sana hizi barabara ambazo kila Mbunge anataka barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mapendekezo, ile habari ya kuchukua asilimia tano ikafanye kazi zingine, mimi siungi mkono, fedha hii yote iende kwenye barabara. Mapendekezo ya Kamati yote ninayaunga mkono, lakini hili la tozo! Sasa hivi kuna mambo haya ya mafuta, maisha yamekuwa magumu, wananchi wanalalamika, hatuwezi kuongeza mambo ya tozo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, *TRA* kwa taarifa zao wenyewe hawajafikisha 60% ya makusanyo kwa vyanzo halali. Ninauliza Waheshimiwa Wabunge humu ndani, wanafanya manunuzi, wangapi wanapewa risiti na wangapi wanadai risiti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda hapo *center* tu, mtu ananunua simu ya shilingi 3,000,000 au 4,000,000, hakuna risiti. Maana yake ni kwamba, hapo kodi ya Serikali haipo, kwa hiyo, kuna mianya mingi ya usimamizi wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Fedha na watumishi wake na *TRA* wanakusanya kodi. Kodi ikikusanywa shida pia ya Watanzania, tupunguze mambo ya anasa, maneno ya mzahamzaha kwa matumizi ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ikikusanywa Watanzania wanataka kuona, tumesema tunajenga barabara, kusanya fedha, jenga barabara. Kama ni fedha ya umeme, kusanya fedha, nenda kwenye umeme. Watanzania wakigundua kama fedha yao wanayotoa inafanya kazi iliyokusudiwa, hawatapinga mipango ya Serikali, watatuunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumeenda hata Marekani pale, mama ntilie tu anauza chipsi ana *computer,* anatoa risiti ya mashine, analipia na usipolipia kodi wanakuona wewe ni mkosefu. Sisi hapa mtu asipolipa kodi ndiyo mjanja, anayelipa kodi analalamika, hatuwezi kuwa na *double standard*. Kila mtu ambaye anapaswa kulipa kodi, alipe kodi na fedha ikikusanywa ifanye kazi ambayo tumekusudia, tuwaondoe Watanzania kwa mambo ya mzahamzaha haya, itatusaidia sana.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sekunde moja nimalizie. Ninaomba nimpe kazi Mheshimiwa Waziri, hii habari ya madeni na riba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mianya, wanatengeneza mikataba, wanawaambia nikichelewa kulipa fedha nitakulipa riba! Mikataba hii wanatengeneza wenyewe, wabadilisheni mikataba ile. Hii habari ya madeni na riba inaweza ikawa ni uchochoro fulani, 10% mikataba ya uongo uongo ibadilishwe.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa George Natany Malima, ajiandae Mheshimiwa Zuberi Yahya Mfaume.

MHE. GEORGE N. MALIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja hii iliyoko mezani. Kwanza ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye ametupa uhai na afya, tunaendelea na shughuli zetu mahali hapa. Pili, ninampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye anafanya kazi kubwa sana, pamoja na ufinyu wa bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Waziri wa Ujenzi, ndugu yangu Mheshimiwa Ulega, yeye ni Waziri mzuri. Ni Waziri ambaye anafaa, anafikika. Mara nyingi nimemtafuta, nimempata, amenipa matumaini hata kama ujenzi wa barabara yangu haujaanza, lakini nina matumaini mengi kwa sababu ya usikivu wake, lakini ninampongeza sana Naibu Waziri wake, hata anapojibu maswali hapa Bungeni, utafikiri ni Kamusi ya Barabara na Vichochoro vya nchi hii, hakuna barabara asiyoijua. Tafsiri yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake ni kwamba, huyu mtu kwanza anazunguka kutembelea barabara, lakini anazijua zote na mwisho anapenda kazi yake. Ninampongeza sana Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza kuchangia. Sisi wa Mpwapwa tuna shida ya barabara mbili; ya kwanza ni Barabara ya kutoka Kongwa kwenda Mpwapwa, yenye urefu wa kilometa 32 na ya pili ni Barabara ya kutoka Mpwapwa kwenda Kibakwe. Barabara hizi ziko katika majimbo yetu mawili; Jimbo la Mpwapwa Mjini na Jimbo la Kibakwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Barabara hii ya kutoka Kongwa kuja Mpwapwa tayari tuna mkandarasi kwenye *site,* ambaye amekaa pale zaidi ya miaka miwili, lakini kazi haijaanza sababu hajalipwa fedha yake ya awali shilingi bilioni 5.3. Ninataka nikwambie ukweli Mheshimiwa Waziri, uchumi wa wananchi wa Mpwapwa unategemea sana barabara hii. Wananchi wa Mpwapwa wanaishi maisha magumu sana, bei ya vitu madukani iko juu kwa sababu ya usafirishaji wa kutoa bidhaa Dodoma au Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malori mengi yanayoleta bidhaa hayakubali kufika Mpwapwa kwa sababu ya ubovu wa barabara kwa hiyo, tunaishi maisha ya umaskini kwa sababu ya barabara hiyo, lakini tuna kilimo kule. Wananchi wa Mpwapwa wanalima sana vitunguu na mazao mengine ya biashara, lakini hawawezi kupeleka kwenye masoko kwa sababu, barabara yetu ni mbovu, wasafirishaji hawawezi kuleta magari yao kwenye barabara mbovu na pia, hata wawekezaji hawawezi kuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwenye Wilaya ya Mpwapwa hatuna *interaction* ya watu wengi kwa sababu ya ubovu wa barabara kwa hiyo, ninasimama hapa kueleza, Mheshimiwa Waziri, Wananchi wa Mpwapwa wanamwangalia Waziri leo, wanamtegemea sana kwamba atawakomboa. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri, akamlipe mkandarasi wa barabara hii, mkandarasi huyo ni mzawa, lakini ni mtu mmoja bora sana katika kazi yake, anajua kazi yake, anachosubiri ni malipo yake ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani kubwa sana na Mheshimiwa Waziri na sikusudii kushika shilingi yake, lakini ninaomba sana ajenda hii ya barabara hizi mbili, Barabara ya kutoka Kongwa mpaka Mpwapwa, Mpwapwa mpaka Kibakwe, ziwekwe katika hesabu. Ninaomba sana, atakapo-*wind up* jioni hii tafadhali awaambie wananchi wa Mpwapwa, barabara hii ni lini itaanza kujengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata habari njema kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, huko nyuma tulikuwa na kazi nyingi za miradi mikubwa ya kimkakati ilikuwa bado

itekelezwe na akatuambia sasa mingi imekwisha, kwa hiyo tunakokwenda huko hali itakuwa tofauti, ninaomba Mheshimiwa Ulega aikumbuke sana barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama yetu Samia anapambana kuboresha Jiji la Dodoma na sisi watu wa Dodoma tunamshukuru sana, lakini ubora wa Jiji hili hauwezi kukamilika kama Wilaya mojawapo katika Wilaya saba za Mkoa wa Dodoma kuwa haina barabara ya lami inayounganisha kutoka wilayani kuja Makao Mkuu ya Mkoa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ulega ajue kwamba ni Wilaya ya Mpwapwa tu ndiyo haijaunganishwa kwa barabara ya lami kutoka Mpwapwa kuja Makao Makuu ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la pili, tunalo Daraja maarufu la Godegode. Mheshimiwa Naibu Waziri tuliwahi kufika pamoja, wananchi wakatushangilia wakaona kwamba sasa mwanga umeonekana, lakini toka wakati ule hawajaona chochote. Nimpe taarifa Mheshimiwa Waziri kwamba, baada ya mvua zilizonyesha miaka miwili au mitatu eneo lile alililoliona sasa limeongezeka kuharibika, limepanuka sana hata *survey* iliyokuwa imefanyika itabidi ifanyike upya kwa sababu tumechelewa kwenda kulijenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, daraja hili ni muhimu sana kwa Majimbo yetu yote mawili ya Jimbo la Kibakwe na Jimbo la Mpwapwa. Kule Jimbo la Kibakwe kuna wakulima wengi wanaolima mazao ya biashara ya vitunguu, ufuta na mambo mengine, lakini hawawezi kuyaleta Mpwapwa, Dodoma au Dar es Salaam kwa sababu ya daraja hilo. Ikifika masika mawasiliano yanakatika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi huwezi kupita pale maji yanaendelea kupita, lakini wanafunzi wanaacha shule hawawezi kuvuka kwenda shuleni wanakaa nyumbani miezi minne mpaka mitano. Daraja hili tuliambiwa liko kwenye hatua ya manunuzi, lakini mpaka leo hatuoni kinachoendelea.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako.

MHE. GEORGE N. MALIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri azingatie hicho kitu na anapo-*wind up,* basi atuambie sisi wa Mpwapwa tunategemea kusikia kutoka kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa. Nilimtaja Mheshimiwa Zuberi Yahya Mfaume, ajiandae Mheshimiwa Mabula Johnson Magangila.

MHE. ZUBERI Y. MFAUME: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuchangia katika Wizara hii ya Ujenzi. Kwanza, nianze kwa kuipongeza Wizara yenyewe kwa kazi nzuri inayoifanya, lakini zaidi kwa ushirikiano inaotoa kwa sisi Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niweke historia sawa. Sisi Jimbo letu la Morogoro Kusini lina sifa moja, Rais wa Kwanza wa Tanganyika na baadaye Tanzania ndiye aliyekuwa Mbunge wetu wa kwanza. Kwa hiyo, aliingia katika utumishi wa Serikali kuwatumikia wananchi akiwa anatokea Jimbo la Morogoro Kusini japo ni mzaliwa wa Butiama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wa kwanza mwanamke wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yeye ni mkulima kutoka Jimbo la Morogoro Kusini. Kwa hiyo, tuna historia ya kuweka viongozi wawili wa kwanza ni Rais wa kwanza akitokea kule kama Mbunge lakini na Rais mwanamke wa kwanza akitokea Morogoro Kusini kama mkulima wa kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Morogoro Kusini tuna kauli mbiu inayosema kila jambo na wakati wake. Mheshimiwa Rais alipokuja kwenye kampeni pale Ngerengere mwaka jana alituahidi kutujengea Barabara ya Bigwa - Kisaki na ndani ya siku 100 tumeona *site clearance* na kazi ikawa imeanza. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa juhudi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa ninataka niseme kwamba sisi sote Wabunge hapa tunajua juhudi kubwa anazozifanya Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha kila sekta inapata fedha za kutosha, siyo katika elimu, afya na mawasiliano. Ninawaomba tupitishe bajeti hii kwa moyo mmoja na kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia atakuwa wa mwisho kuona barabara za nchi hii zinaharibika na hazitengenezwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwe na uhakika kwamba tunakwenda kupata pesa za kutosha kutokana na juhudi zake. Baada ya kusema hayo niiombe sasa Wizara ya Ujenzi kilio chetu kikubwa ni Barabara ya Bigwa – Kisaki, Mheshimiwa Rais ameliona hilo na ndani ya siku 100 ujenzi wa Bigwa – Kisaki umeanza, tumeona pia katika bajeti tuna 2% ya ujenzi. Nimwombe ndugu yangu Mheshimiwa Ulega waende wakaongeze kasi sasa, wananchi wa kule wanalia sana hawana barabara na kwa miaka yote tumekuwa watu wa vilio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuna barabara niliyoielezea jana, Barabara ya Msalabani - Tawa, ninaomba wakaharakishe hiyo *feasibility study* ili waweze kuitafutia pesa na barabara hii ikaanze. Pia, kwa kuwa ninatoka katika Jimbo katika Wilaya ya Morogoro, tuna Barabara inayotoka Ubena Zomozi - Ngerengere, Ngerengere - Tununguo, Tununguo – Mvuha, tunaomba pia barabara hii wakaiangalie. Mkandarasi yuko pale lakini kwa kweli anasuasua. Kazi yake inakwenda polepole sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Mabula Johnson na Mheshimiwa Kija Limbu Ntemi na Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng'anzi Ulenge wajiandae.

MHE. MABULA J. MAGANGILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninapenda nimshukuru na kumpongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, Waziri Ulega na Naibu Waziri *Engineer*

Kasekenya kwa kutupatia Barabara ya lami kilometa 75, Kahama - Kakola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hiyo mpaka sasa hivi tayari imekwisha jengwa kwa kiwango cha lami kilometa 25 na mkandarasi yuko *site* anaendelea, lakini tunashukuru kwa sababu barabara ile ni matokeo ya usimamizi mzuri wa sera ya *CSR*. Barabara ile inafadhiliwa na *Barrick* kwa 100%. Kwa hiyo, tuna uhakika barabara ile itakwenda kukamilika bila kusuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwenye barabara hii, ninaomba barabara hii ikamilike kwa viwango vyote kama ilivyokuwa *designed*. Tunaomba taa zote ziwekwe kwenye vijiji vyote ambavyo barabara hii inapita kama ilivyokuwa kwenye mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizi, ninaomba nishukuru kwenye mpango huu wa bajeti wa Wizara ya Ujenzi. Nimeiona barabara ambayo ni barabara inaunganisha Kata Saba, Barabara inayotoka Didia – Chana – Mwankima – Mwakuhenga – Ngaya - Busangi - Ntobo Makao Makuu. Barabara hii kwa mara ya kwanza imeweza kutengewa pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe barabara hii ni muhimu sana kwa wananchi wetu, hizi kata nilizozitaja zote ni kata ambazo zina wakulima wakubwa. Ndizo kata zinazochangia 50% ya mchele katika Mkoa wa Shinyanga. Kwa hiyo, ujenzi wa barabara hii ni wa muhimu sana kwa ajili ya kukuza uchumi wa Mkoa mzima wa Shinyanga, lakini kwa wananchi wa Msalala pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingine ambayo nimeona kwenye mpango huu ni Barabara ya Kahama – Bulige - Solwa na yenyewe tumeweza kutenga pesa. Barabara ya Nyambula – Chela - Nyang'olongo na yenyewe tumeweza kutenga pesa kilometa 95.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, tunayo changamoto kubwa ya upelekaji wa pesa. Bajeti hii tunayotekeleza Mkoa wa Shinyanga ulitengewa shilingi 12,000,000,000, pesa zilizopelekwa ni

shilingi bilioni 1.7 tu mpaka sasa. Kwa hiyo, tunapotenga pesa tutapitisha bajeti hapa, lakini niiombe Wizara ya Fedha wapeleke pesa Wizara ya Ujenzi. Hatuisaidii Wizara ya Ujenzi kwa kuipitishia bajeti halafu tusipeleke pesa kwa ajili ya kutekeleza miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunapopitisha bajeti hapa tunalia kuhusu pesa nyingi kwa ajili ya matengenezo ya barabara zetu, lakini ninajiuliza ni kwa nini, ni kitu gani kinachotusababishia mizigo yetu yote ya *transit* ambayo inakwenda Nchi za Rwanda, Burundi, Congo na Uganda, kwa nini malori yanaifuata Dar es Salaam wakati tunayo Bandari Kavu pale Isaka na ilishawahi kuwa hivyo huko nyuma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunaendelea kutumia gharama nyingi za matengenezo ya barabara kipande hiki? Mabilioni na mabilioni tunatenga kila mwaka ya kutengeneza barabara wakati tunazo bandari kavu ambazo zinapunguza msongamano wa malori kwenye barabara zetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kwa nini Wizara ya Uchukuzi - *TRC* hawaioni hii fursa. Reli ya Kati inafika pale kwenye ile bandari kavu na *SGR* inapita pale kwenye bandari kavu. Kwa nini Serikali sasa haifikirii kupunguza mzigo kwenye barabara zetu kwa kuanza kutumia bandari kavu ya Isaka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msongamano wa malori, hivi kweli! Malori kutoka Rwanda, Burundi yanafuata nini Dar es Salaam? Kama waliwahi kukosea huko nyuma walikuwa ni babu zetu, sasa hivi sisi ni vijana tuko kwenye Bunge hili, Serikali ichukue mawazo yetu sisi vijana na sisi tuweze kuokoa Taifa hili, tutumike na sisi kwa wakati wetu wa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutumie njia mbadala ili kuokoa gharama kubwa tunayotumia kwenye matengenezo ya barabara zetu ili sasa pesa yetu tutakayokwenda kuiokoa twende tukaongeze mtandao wa lami kwenye barabara zetu nyingi ambazo sasa hivi ni za changarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi kwa kweli kwa barabara hizi ambazo nimepatiwa nimeona kwenye bajeti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Kija Limbu Ntemi, ajiandae Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng'anzi Ulenge.

MHE. KIJA L. NTEMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninakushukuru sana kwa nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyosaidia kuifungua nchi yetu barabara zote ambazo zinapitika kwa sasa. Pia niipongeze Wizara ya Ujenzi ikiongozwa na Mheshimiwa Waziri Ulega mwenyewe. Mheshimiwa Ulega ni mtu mzuri, mwaminifu na msikivu, anayeshirikiana na mtu yeyote na anasikiliza mawazo ya kila mmoja, hicho ndicho ninachompongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anapokea na mengine anayafanyia kazi na yasiyowezekana anasema atalifikisha kwenye Wizara ili waweze kulichambua, ninampongeza sana. Nimekuwa nikimfuata kila siku, nina Barabara yangu ya kutoka *STAMICO* kwenda CCM, angalau basi kilometa tatu amenitia moyo sana, amenishauri vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea mawazo yake, lakini ninamwomba atakapopata fedha, ameniambia kuna kilometa 47 kutoka Ushirombo kuja Katoro na kule Ushirombo walishaanza kujenga japo walisimama kwa wakati, basi ninamwomba atakapoweka bajeti zake vizuri, aje aanzie pale Katoro anipe kura zangu maana atanipotezea kura. Aje pale Katoro anisaidie kuanzia Katoro, anitoe tu kidogo, watu wale wanapata vumbi sana. Ninaamini Waziri atafanya kwa sababu yeye ni mtendaji mzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemshukuru sana Waziri Ulega amenikumbuka kwenye Barabara ya Chibingo - Chigunga –

Bukondo, amenitengea fedha za kurekebisha ile barabara na watu wangu walikuwa wanapata shida sana na walikuwa wanasubiri hii bajeti wajue, je, watapewa fedha kwa ajili ya marekebisho ya ile barabara. Nitamuunga mkono Waziri Ulega kwa asilimia zote 200 ili apitishiwe bajeti ila nimwombe kitu kimoja, nimekubali safari hii kwa sababu mimi ni *Engineer,* yule mkandarasi atakayemleta nitakwenda kumsimamia. Maana barabara zetu zinaharibiwa na wakandarasi, wanatujengea barabara za kiwango cha chini kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana hata barabara zetu za lami zimekuwa na changamoto hizo kwa sababu wale tunaowapa kazi, yaani mimi huwa ninashangaa sana anakuwepo mtu anaitwa *consultant* ila ukiangalia *consultant* anachoshauri baada ya miezi sita alichoshauri ni nini mbona barabara imeharibika? Nimwombe Mheshimiwa Waziri, baada ya bajeti yake, akae na wataalam, tunataka sasa anapokwenda kuanza kufanya kazi mwaka huu barabara zetu zitakazojengwa zote ziwe kwenye kiwango kinachotakiwa.

(Hapa Mhe. Kija L. Ntemi aliongea lugha ya Kisukuma)

MHE. KIJA L. NTEMI: *Olo udumha, nikharibishage onhe nakoghunane nanhe, nadolile. Obhebhe olo odumha hange nikharibishege nakoghunane nang'ho ili tujelhaneje pyabhose bhapamoja.* **[MANENO HAYA SIYO SEHEMU YA TAARIFA RASMI ZA BUNGE]**

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kija kwa mujibu wa Kanuni zetu ni lugha mbili tu zinatumika ambazo ni Kiingereza na Kiswahili.

MHE. KIJA L. NTEMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana ninarekebisha.

MWENYEKITI: Hivyo, *Hansard* ifute haya maneno uliyoyataja.

MHE. KIJA L. NTEMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme kwamba nilikuwa nasema hivi, Mheshimiwa Ulega baada ya bajeti hii aniite na mimi tusaidiane ili twende pamoja ili tutafute

watu wanaotujengea barabara zetu kwa kiwango cha chini tuwaondoe. Tunataka kiwango cha lami *standard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Barabara kutoka Kahama kwenda Runzewe malori yote yanayotoka bandarini yanapita miaka yote katika ile barabara, ile barabara sijajua nani aliyeijenga ni barabara bora miaka yote, haijawahi kuharibika, kwa nini? Barabara zingine zimekuwa na changamoto sana. Kwa hiyo, tunaomba yule mkandarasi aliyejenga wataalam wako hapa, wamtafute, yule aliyejenga Barabara kutoka Kahama kwenda Runzewe, wampe tenda na wampe fedha atutengenezee barabara zetu zote zilizoharibika ili ziweze kuwa imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kurudiarudia kila mwaka tunarudi nyuma, yaani miezi sita umerudia, miezi sita umerudia, hatuwezi. Tunamuunga mkono Waziri, lakini kwenye timu yake tunaomba akawarekebishe, akawaambie wajipange kwa ajili ya kutengeneza barabara vizuri ili barabara zipitike vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, ninaiomba sana Wizara inapokwenda hata kuziba ile mitaro ambayo imeshatokea, ninaomba jambo hili, watakapokwenda kuanza kuziba zile barabara watafute lami sahihi ya kuziba, siyo kutuwekea mchanga. Mheshimiwa Waziri tunaumia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi juzi kidogo nife, nilikuwa ninatoka Bariadi ninaenda *airport* nimechelewa, nikapiga shimo, yaani kui-*control* gari ni kazi sana nikasema sasa mimi Mbunge ningekufa leo halafu na miezi nane wananchi wangu wangefanyaje, lakini ni kwa sababu barabara mbovu. Tuanze tena uchaguzi leo tu kwa sababu ya mashimo? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana ili tuishi vizuri na tuendelee vizuri na watu wengi wamezungumza humu zile barabara nyingi ndiyo maana unatuona tunazungumza hivi kwa sababu barabara zetu nyingi zina changamoto. Namwomba Mheshimiwa Ulega baada ya kutoka hapa babu yangu, yaani yeye ni babu yangu kabisa, lakini ninamwomba atuhakikishie

barabara zetu zinakuwa salama kwa muda wote na watu wetu wapite kwa usalama na hata Mheshimiwa Musukuma, msafishaji wa mabasi asafirishe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninamuunga mkono Mheshimiwa Waziri Ulega, bajeti yake ipitishwe kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, wajiandae Mheshimiwa Beng'i Mazana Issa, Mheshimiwa Haidary Hemed Sumry na Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwenye enzi na utukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa wanayoifanya katika sekta hii ya ujenzi. Kiukweli kabisa kazi kubwa imefanyika katika Taifa letu, hilo halipingiki, ukichukulia zero ya barabara zote nchini pale *Clock Tower* Dar es Salaam mpaka Kigoma unakwenda bila kukanyaga vumbi, ni mapinduzi makubwa na tuipongeze Serikali kwa kazi kubwa inayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ya ujenzi katika sera yake ya mwaka 2003 ilishazungumza suala la ushirikishwaji wa wanawake na vijana katika shughuli za ujenzi. Miaka yote hiyo hatua kadhaa zimekuwa zikifanyika, lakini tumpongeze Dkt. Samia Suluhu Hassan, *significant impact* imekuja kutokea awamu hii ya Dkt. Samia Suluhu Hassan na Katibu Mkuu mwanamke *Eng.* Aisha Salim Amour.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya wanawake wakandarasi imetengwa kwa kiwango cha shilingi 40,000,000,000 na zaidi, haijawahi kutokea. Huko nyuma mimi binafsi nilishiriki sana kuwa-

train wakandarasi wanawake, lakini hili jambo lililotokea kipindi hiki ni jambo kubwa na ni jambo la kupigiwa mfano. Hongera sana Mheshimiwa Waziri Ulega kwa kusimamia jambo hili kuweza kutokea. Hongera sana *TANROADS* kwa utekelezaji wa jambo hili. Mimi nina hakika wataiona tofauti. Wakandarasi wanawake wakipewa fedha hawazipeleki sehemu nyingine, fedha yote inarudi barabarani, hongera sana Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kusema kwamba kuanzia mwaka 1980 mpaka 1990, Taifa letu lilikuwa linatekeleza ujenzi wa barabara kwa kutumia mfumo wa *nationalization of the budget;* kwamba, fedha yote inawekwa katika kapu moja. Haya yanayotokea sasa barabara kuweza kwisha muda wake na zikawa na hali mbaya yaliwahi kutokea mwaka 1980 mpaka 1990.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo sababu ilianzishwa *Road Fund Board* mwaka 2000. Ilionekana kwamba, haiwezekani kuweka fedha pamoja, utahakikisha tu unajenga, unajenga, unasahau *maintenance*. Ndiyo sababu ulianzishwa Mfuko huu mwaka 2000. Hiki kinachotokea sasa hivi ina maana tunarudi miaka ya 1980 na 1990. Barabara kweli zilifunga na tukaanza kujenga upya. Hiki kinachotokea sasa hivi ina maana tunarudi tena kule nyuma. Maana yake ni nini? Tunataka kuiua *Road Fund Board* ambayo imeanzishwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingi za Afrika wapo walioanzisha Mfuko wa Barabara na ukafa kwa sababu hii na mmojawapo ni Ethiopia. Kwa hiyo, kama Taifa tunataka kurudi kule kujenga tena barabara upya kama tulipotokea miaka ya 1980 hadi 1990, basi tuendelee kuzichanganya hizi fedha katika Mfuko mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme kwamba, licha ya kwamba Serikali imefanya kazi nzuri kwa wakandarasi; nami ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alipoingia tu madarakani, yeye ndiye aliyetunga kanuni kwa ajili ya ile sheria ya kubaini matatizo ya kodi, ile taasisi ya kushughulikia malalamiko ya kodi. Hii iliwasaidia sana wakandarasi wa ndani kwa sababu walikuwa na changamoto nyingi; na yeye tunampongeza sana

kwa jambo hilo. Hata hivyo, sasa ukweli ni kwamba ni lazima wakandarasi hawa tuwaangalie kwa jicho la pekee hasa wakati huu ambao mafuta yamepanda bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkandarasi anayetekeleza mradi sasa hivi wakati ali-*tender* mafuta yakiwa ni lita shilingi 2,000 sasa hivi mafuta ni shilingi 4,000, hali ya mkandarasi huyu kiukweli ni kwenda kufilisika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri sekta hii ilishaliona jambo hili muda mrefu kimataifa na kitaifa; *FIDIC Condition of Contract Red Book*, huu ni mkataba wa kimataifa wa utekelezaji wa kazi za ujenzi; unazungumza vizuri kwenye *clause* ya 13.7, suala la *cost adjustment* iwapo tu Serikali inapotangaza kupanda kwa bei ya mafuta. Vilevile, *PPRA* yenyewe kwenye mikataba yetu ya ndani Kifungu Namba 17.8 kinazungumza suala la *cost adjustment* iwapo tu Serikali imetangaza kupanda kwa bei ya mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala la kutafuta fedha kwa ajili ya kuiongezea wizara hii *is inevitable*; ni lazima fedha zitafutwe kuweza kusaidia kuinusuru sekta hii ya ujenzi. Kwa suala la kutafuta fedha ninaunga mkono kwa asilimia mia moja, shemela (shemeji) wangu Mheshimiwa Ulega kuhusiana na suala la hatifungani. Kitu ambacho kilichelewa tu kufanyika ni kuja kutupiga semina hapa ndani. Watu wanachanganya mambo, hatifungani ni tofauti kabisa na *EPC + F*, ni vitu viwili tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kupata elimu na kulielewa jambo hili vizuri. Hatifungani inaelekea katika ile sera ya Serikali ya kufanya uchumi fungamanishi na uchumi shirikishi; kwamba wananchi wenyewe tunashiriki kujenga barabara zetu wenyewe kwa kutumia fedha zetu na halafu tunapata faida.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE … kwa hiyo, suala hili tupate kuelewa zaidi, lakini ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie, kwamba sishiki shilingi kwa sababu lililokuwa likitugombanisha katika Barabara ya Kiomoni limeanza kufanyiwa kazi na mkandarasi yuko kazini. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa. Nilimtaja Mheshimiwa Beng'i Mazana Issa na Mheshimiwa Haidary Hemed Sumry ajiandae.

Mheshimiwa Haidary Hemed Sumry.

MHE. HAIDARY H. SUMRY: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na afya. Niendelee kuwa pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa ambayo imeendelea kuifanya ya kujenga miundombinu kwenye nchi yetu hii ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nitajikita kwenye fidia. Nimesoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri, naomba ku-*declare interest;* Mheshimiwa Waziri ni *youth league* mwenzangu, kwa hiyo sitachukua shilingi yake; lakini nitaelezea ukweli wa mambo jinsi yalivyo katika jimbo langu na kwenye Mkoa wangu wa Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Barabara ya Stalike – Mpanda – Mpanda Ndogo. Barabara hii ilianza ujenzi wake mwaka 2015 na imekwishakamilika; lakini hadi leo wananchi walio kandokando ya barabara hiyo, hawajalipwa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, tumefanya ziara na Mheshimiwa Waziri Mkuu, hoja za wananchi zilijitokeza kwenye mikutano; na majibu ya Wizara ya Ujenzi ilikuwa ni kwamba katika bajeti hii watatenga pesa ili uthamini ukafanyike upya kwa sababu uthamini huu umefanyika kwa muda mrefu. Nimwombe sana ndugu yangu, kaka yangu

Mheshimiwa Ulega, tunaomba wananchi wale waende wakafanyiwe uthamini na ikiwezekana waanze kulipwa fedha zao kwa sababu jambo hili limekuwa ni la muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba jambo hili linawa-*cost* wanasiasa kwa sababu Serikali inaahidi lakini hili jambo halitekelezeki; na tukienda kwa wananchi, wananchi wanashindwa kutuelewa. Kwa hiyo, ninamwomba sana; hilo la kwanza liko kwenye jimbo langu, liko kwenye jimbo la Mheshimiwa Lupembe - Nsimbo, lakini liko pia kwenye jimbo la Mwenyekiti wa Kamati hii, Mheshimiwa Kakoso huko Tanganyika. Kwa hiyo ninamwomba sana alichukulie uzito unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kwa sisi watu wa Mpanda na watu wa Tabora maeneo ya Kaliua, tunayo barabara ya kuanzia Mpanda mjini – Ugala – Kaliua – Kahama. Barabara hii imeanza kuwekwa kwenye Ilani tangu mwaka 2015, lakini mpaka leo nimesoma kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri sijaiona hii barabara. Hiyo siyo shida kwa sababu bado tuna miaka minne ya utekelezaji wa Ilani ya chama chetu. Ningemwomba sana Mheshimiwa Waziri, kwenye maeneo mengine, ninatolea mfano Barabara ya Sumbawanga ilivyoanza kujengwa, yalianza kujengwa kwanza madaraja kabla ya barabara ya lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe ndugu yangu Mheshimiwa Ulega, kwamba tunataka Daraja la Ugala lenye urefu wa meta 150 lijengwe ili tuanze kuona picha ya hiyo Barabara sasa ya kutoka Mpanda – Kaliua – Kahama itakuwaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wamekwishaanza kazi pale, wameweka fedha, wamejenga *box culverts* nne, lakini sasa zile *box culverts* walizozijenga pale kama hamna la Ugala zile *box culverts* zilikuwa na maana gani ya kujengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, chonde chonde, tunaomba Daraja la Ugala. Ninataka majibu kwamba Daraja la Ugala litajengwa lini. Ndiyo, Ugala si jimbo langu, lakini ninatoka jimbo la mjini pale katikati ambazo

barabara zote zinazojengwa kwenye Mkoa wa Katavi mimi ndiye mnufaika namba moja kwa sababu jimbo langu ndilo jimbo la mjini. Kwa hiyo ninamwomba sana ndugu yangu atusaidie kwenye hilo Daraja la Ugala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona amelieleza kwenye ukurasa wa 11 wa hotuba yake, lakini tunataka majibu ya kina tuone ni namna gani sasa wananchi wa Katavi watafunguka. Katavi imekaa kwenye jiografia ambayo inaunganika na mikoa zaidi ya minne na kote huko kuna barabara. Nimwombe barabara ya Kigoma imeongelewa na nimeona kwenye bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ni moja kwenye hizi barabara ambazo zinakaa muda mrefu. Hii pengine Waheshimiwa Wabunge ni lazima tufahamu. Kwa mfano Barabara ya Kibaoni, toka ilivyotangazwa kilometa 50, leo hii ni mwaka wa nne. Hivi yule mkandarasi aliyeko pale *site* kwa miaka minne ile gharama ya shilingi 52,000,000,000 ndiyo itakuwa hiyo hiyo ya kwenda kumlipa atakapokamilisha hii barabara? Jibu ni kwamba siyo, tutakwenda kumlipa zaidi ya shilingi 100,000,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nini tutekeleze hii miradi kwa gharama ambazo zilikuwa zinawezekana, lakini kwa kuchelewesha mradi unakwenda unaongeza gharama kubwa zaidi kwenye mradi? Vivyo hivyo kwa Barabara ya Kigoma. Nimwombe sana ndugu yangu, barabara hizi ni muhimu kwa uchumi wa Mkoa wetu wa Katavi, lakini na mikoa ya ukanda huo wa Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme machache tu…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, muda wako umekwisha Mheshimiwa.

MHE. HAIDARY H. SUMRY: Mheshimiwa Mwenyekiti, sekunde chache tu. Mkoa wa Katavi ndiyo mkoa uliobaki ambao

haujaunganishwa na mikoa mingine. Sisi watu wa Mkoa wa Katavi tumelikosea nini hili Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Simon Songe…

MHE. HAIDARY H. SUMRY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Emanuel Qambaji Nuwas, ajiandae.

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi nichangie hotuba ya Waziri wa Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo barabara ambazo zina mashimo makubwa sana. Tunayo Barabara inayotoka Nyanguge – Lamadi na kutoka Lamadi – Maswa. Barabara hii ya Nyanguge – Lamadi imeharibika. Kama ni *depreciation* zilishakataana. Ninatamani hata kuomba vitabu vya *TANROADS* ili nianze kuangalia kama hii barabara bado iko kwenye vitabu vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika barabara iliyoharibika yenye mashimo makubwa makubwa ni pamoja na Barabara ya kutoka Nyanguge – Lamadi. Ukipita barabara hii ni *option* yako tu ya kufanya, unatamani kuingia kwenye shimo kubwa au shimo dogo, kwa sababu barabara yote imejaa mashimo. Yanatofautiana tu aina ya mashimo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuchukulie *serious* barabara hii iliyojaa mashimo kutoka pale Nyanguge – Lamadi. Imefikia sehemu hata huyu Mheshimiwa Mbunge Ntemi alipokuwa anazungumza hapa kwamba alitaka kupata ajali ni kwenye hiyo barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima Mheshimiwa Waziri aje na *commitment* wakati anakuja kuhitimisha hoja yake. Nimeona kwenye randama yake, ameweka shilingi bilioni 2.5 kwa ajili ya maandalizi ya ukarabati. Sasa sijaelewa maandalizi ya ukarabati, sijui ndiyo anataka kuandika *proposal?* Yaani mimi sijaelewa hapo maandalizi tunataka kufanya ni yapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni lazima iingie kwenye mpango kwa sababu ni barabara ya kiuchumi. Ni barabara inayokufikisha Mwanza, ni barabara inayokupeleka Mara, ni barabara inayokupeleka Simiyu, ni barabara inayokupeleka Geita. Ni lazima tuichukulie maanani ili barabara hii iweze kutengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo moja. Ilipofika hali ya barabara hii waendesha magari, nikiwemo mimi, tunatamani hata kupita njia ya *rough road* kuliko kupita kwenye ile lami ya kutoka Nyanguge – Lamadi kwa sababu imejaa mashimo. Ukipita barabara ile kwa sasa hivi uwe tu na bajeti ya kupasua tairi mbili wakati wowote. Pamoja na kupasua tairi muda wowote watu pia wanapata ajali kupitia barabara hizi ambazo sasa zina mashimo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tumepita hapa na Mheshimiwa Kiswaga, Mbunge wa Magu, mbele tu ya wapi hapa kabla ya kufika Manyoni, lori moja limeingia kwenye shimo limekita, tairi limepasuka, likaenda kulia likagonga gari, watu watatu wakafa. Hapo tu Manyoni, hata kabla hujafika Manyoni. Kwa nini, kwa sababu ya shimo. Sasa wale waliokuwa na lile lori lililopata ajali na sisi tukakita, tukapasua tairi mbili tukaanza kupeana pole. Ni lazima tuyaangalie mashimo makubwa ambayo yanasababisha ajali kwa Watanzania. Nilitaka kusema hili ili tuone namna ya kuitengeneza Barabara ya kutoka Nyanguge – Lamadi iliyojaa matatizo makubwa kwenye barabara ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo tatizo kubwa la *quality* ya barabara. Barabara zinazotengenezwa sasa hivi hazikidhi viwango vinavyotakiwa. Nimekuwa nikifikiria, hivi huyu mkandarasi aliyejenga Barabara ya kutoka Igoma – Nyanguge mbona

alijenga kiwango kikubwa ambacho sijui hata ile barabara itaharibika lini? Huyu aliyejenga Barabara ya kutoka Maswa – Lamadi kwa nini hakutujengea vile?

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

TAARIFA

MWENYEKITI: Mheshimiwa Songe, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Emmanuel Cherehani.

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampa taarifa Mheshimiwa Mbunge, kwamba hata ile barabara inayotoka Manyoni inayokwenda mpaka Tabora, barabara mpya haijamaliza miaka mitatu, nayo sasa ina mashimo yamechimbika ambayo ni makubwa na ni hatari zaidi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Simon Songe, unaipokea Taarifa hiyo?

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea na ile barabara niliipita mwezi Machi. Hii Barabara ya Manyoni – Tabora Mjini ndiyo ilikuwa *priority* yangu kupita ile barabara lakini kwa sasa hivi ile barabara muda si mrefu ndiyo itakayoongoza kwa ubovu kuliko barabara zote kwa sababu sasa yenyewe inatengeneza matuta pale katikati, inatengeneza tuta linakuwa hivi, inatengeneza inaenda hivi. Sasa tunashindwa kuelewa huyu mkandarasi alijenga akiwa anawajengea Watanzania kweli au alikuwa analipua kazi za wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakandarasi kama hawa watafutwe ili waweze kurekebisha barabara zetu. Tumetumia fedha nyingi za Watanzania, tumetumia fedha nyingi za walipakodi, ni lazima *quality* ya barabara iweze kuwa nzuri. *Otherwise* kwa sababu mimi siyo *engineer* aje aniambie kuna aina nyingi za barabara, kuna ya kawaida, kuna ya kati na kuna ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kama watani-*convince* kwa *style* hiyo, lakini kama tuna aina moja ya *quality* ya barabara tunatamani tujengewe barabara za aina kama ya kutoka Igoma kuja pale Nyanguge. Ni barabara ya mfano tunatamani hata Barabara ya kutoka Nyanguge – Lamadi – Bunda ijengwe kwa staili hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina tatizo na kuunga mkono hoja, ninaunga mkono hoja, lakini Barabara ya kutoka Nyanguge – Lamadi itengenezwe. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Dkt. Emanuel Qambaji Nuwas na Mheshimiwa Beng'i Mazana Issa ajiandae.

MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wetu katika majimbo yetu wanahitaji mambo matatu; la kwanza wanahitaji maji, la pili wanahitaji barabara na la tatu wanahitaji nishati. Hayo ndiyo mambo matatu ya msingi sana ambayo wananchi wetu wanalilia kule katika majimbo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wetu wa Manyara ambako ndiko Jimbo langu Mbulu Vijijini liliko tuna kilometa chache sana za lami. Kwa haraka haraka barabara ambazo zinahudumiwa na *TANROADS* ni kilometa 1,657. Kati ya hizo ni kilometa 259 tu ndizo za lami. Vilevile, pamoja na hiyo ni 16% tu peke yake za kilometa ambazo zinahudumiwa na *TANROADS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mkoa wetu kwa kweli una kilometa chache sana za lami; na hivyo nimwombe Waziri wetu wa Ujenzi autazame mkoa wetu. Ninaamini kwamba tunalitendea haki Taifa letu kwa kufanya uzalishaji katika eneo la kilimo, eneo la ufugaji, eneo la madini na vilevile na eneo la viwanda. Kwa hiyo, tunahitaji kutazamwa kwa namna ya pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika barabara hizo barabara pekee ukiacha barabara za *TANROADS* ambazo ni takribani kilometa 206, kilometa 52 ndizo ambazo zinaunganisha halmashauri zetu sita. Kwa kuangalia kwa haraka haraka Wilaya yangu ya Mbulu ambako ndiko Jimbo la Mbulu Vijijini liliko, tuna kilometa 12.5 tu za lami na ndiko ambako tunalia kwa namna ya pekee sana. Wananchi hawa wana haki ya kupata barabara za lami na wana haki ya kupata barabara zinazopitika majira yote ili kufanya shughuli zao za uzalishaji hasa katika eneo la kilimo, eneo la mifugo, lakini vile vile na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana, Mheshimiwa Waziri ametenga fedha, ukiangalia zile barabara za changarawe zilizotengewa fedha kufanyiwa *maintenance* kwa mwaka huu wa fedha wa 2026/2027, mkoa pekee ambao unaongoza kwa kuwa na barabara za changarawe na za udongo ni Mkoa wa Manyara; zaidi ya kilometa 1,356. Tofauti na mikoa mingine yote ya Tanzania. Kwa hiyo ninaomba Mheshimiwa Waziri atutazame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana ninakuja kwenye eneo la pili, kwamba tunajua hizi zina athari kubwa sana katika shughuli za uchumi za wananchi. Kwa hiyo, lazima tuone Wanamanyara hatujawakosea lolote, tunaomba tuzingatiwe kwa namna ya pekee. Tunashukuru tumepata fedha, ametutengea kiasi cha fedha katika Barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Lalago mpaka kwenye barabara ile ya *Maswa Road*. Kwa kweli tunashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata kilometa 25 za Barabara ya Mbulu – Garbabi na pia tumepata kilometa 25 za Barabara ya Labay – Haydom, lakini bado kasi ya ujenzi ni ndogo sana. Hadi sasa kwa kipande kile cha Mbulu – Garbabi ni kilometa tatu tu zimekamilika. Je, itahitajika miaka mingapi kukamilisha? Bado tuna safari ndefu sana. Ninaomba Mheshimiwa Waziri aongeze fedha pale; na ninaomba sana nipate maelezo, je, barabara hii itakamilika baada ya miaka mingapi? Tunahitaji kuona barabara hii ikikamilika ili wananchi wakafanye shughuli zao za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna wananchi ambao wamekutwa na ile barabara, bado wanahitaji kulipwa fedha zao kwa ajili ya kupitiwa na barabara ile. Ni takribani miaka mitatu na tayari muda ule wa mkataba umekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba atakaposimama Mheshimiwa Waziri atupe maelezo ya kwamba ni lini barabara hizi zitakamilika lakini pia wananchi hawa watalipwa lini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa Barabara ya Dareda – Dongobesh, tumepata fedha kidogo kwa kilometa chache, tunaomba fedha ziongezewe. Hii barabara ni muhimu, ndiyo inayounganisha Wilaya ya Mbulu kwenda Makao Makuu ya Mkoa. Tunaomba ipate lami ili iweze kukamilika. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri aitazame kwa namna ya upekee. Hatuwezi kwenda kutumia masaa zaidi ya matano au sita kwenda Makao Makuu ya Mkoa ambako ndiyo eneo la kiutawala na wananchi wanahitaji kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata Barabara ya Haydom – Katesh, tunashukuru usanifu umekamilika, imetengewa fedha shilingi 250,000,000 lakini haitoshi. Barabara hii ni muhimu kwa ajili ya hospitali yetu ya Kilutheri ya Haydom ya Rufaa ya Mkoa. Pia, ngano inalimwa kule kwa wingi na ngano haiwezi kutoka kama hatuna barabara nzuri. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri tunaomba barabara hii tuiongezee fedha. Kwa kuwa umesema mwenyewe hapa, ziko barabara mpya ambazo tumesema ziachwe kwanza. Zile ambazo usanifu umekamilika na tayari ziko kwenye mpango zitengewe fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru pia kwa Barabara hii ya Haydom – Ilongero kwenda Singida kilometa karibu 96, imetengewa fedha, pia tunaomba Waziri aiongezee fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kusema mawili ya mwisho. Tuna barabara za mkoa; tuna Barabara ya Babati – Singida ambayo imeharibika, tunaomba itengewe fedha. Ile barabara ni aibu kwa Taifa lakini pia inaangusha biashara.

Tunaomba ifanyiwe ukarabati ili iweze kutumika kwa ajili ya shughuli za kibiashara lakini vilevile kwa shughuli nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna barabara za mkoa; Barabara ya Arusha – Kibaya kwenda Kongwa, ni barabara muhimu sana na ndiyo ambayo inaturudisha nyuma kama mkoa kuwa na kilometa chache za lami. Tunaomba tutazamwe kama Mkoa wa Manyara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuna Barabara ya Handeni – Kibaya – Singida ambayo ni muhimu pia kwa Bandari yetu ya Tanga. Tunaomba Mheshimiwa Waziri atakaposimama, basi atujibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, Mheshimiwa Waziri tumetenga fedha kwenye *Road Fund* kwa ajili ya marekebisho. 35% *TARURA*, 65% kwenda *TANROADS,* lakini bado hatuipati hii fedha. Wananchi wanaochangia, ni wale wanaolipishwa nauli, ni wale bodaboda, ni wale wa bajaji ndiyo wanakatwa kwenye mafuta kila lita. Tunaomba hizi fedha ziheshimiwe na kama ambavyo iko *fenced*, ziweze kwenda kutengeneza barabara. Wananchi wanataka kuona ma-*grader* yakiwa yanatengeneza barabara ili waweze kuendesha maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tozo ya simu hatuwezi kukubaliana nayo kwa sababu inakwenda kugusa maisha ya wananchi wetu. Lazima tutafute vyanzo ambavyo havigusi maisha ya wananchi wetu. Kwa sasa wana maisha magumu kutokana na gharama kubwa za bei ya mafuta, kwa hiyo lazima tuondokane na hiyo. Hata hivyo, ninaunga mkono suala la kuangalia *bond* ili kuona namna ya kupata fedha za hakika ili kutengeneza barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kukushukuru sana na ninaomba kusema, Mheshimiwa Waziri atakaposimama atupe maelezo haya ili tuweze kuunga mkono hoja yake na aweze kwenda kutekeleza. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Beng'i Mazana Issa, wajiandae Mheshimiwa

Emanuel John Khambay na Mheshimiwa Benjamin Lukubha Ngayiwa.

MHE. BENG'I M. ISSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ninapenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema. Vilevile, ninamshukuru Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa juhudi zake kubwa kwenye sekta hii ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchangia Bajeti ya Wizara ya Ujenzi ya mwaka 2026/2027 kwenye maeneo ya miradi ambayo sekta hii ndiyo ambayo inasimamia miradi na vilevile inasimamia wakandarasi. Katika miradi mingi ambayo tukitembelea tunavyoona, kwenye kui-*design* ile miradi kumekuwa na tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta miradi inakuwa haifanyiwi *feasibility study* vizuri na kwa hivyo ninafikiri ni vizuri tuishauri Wizara iweze kuliangalia eneo hili kwa sababu kutofanya *feasibility study* vizuri kumesababisha kuwa na *variations.* Yaani zile bei ambazo zimekubalika kwenye mikataba zinabadilika kutokana na hali hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo inasababisha miradi inakuwa ya gharama zaidi kuliko ambavyo Serikali ilikuwa imejipanga kabla ya hapo. Kwa hiyo, ni eneo ambalo linatakiwa liangaliwe sana kwa sababu katika kila mradi, unakuta kuna mapungufu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni eneo la uratibu. Unakuta barabara inajengwa kwa mfano, katika barabara ile pia litapita labda bomba la maji na vilevile labda itapita njia ya umeme au itapita njia ya simu lakini unakuta barabara inajengwa mpaka inamalizika, hakuna uratibu ambao unafanyika kati ya hizi sekta ambazo zinakuja kuweka hii miundombinu. Baadaye inasababisha barabara ile *either* ikatwe ili kusudi miundombinu iweze kutokea. Kwa hiyo kwa sababu Serikali ni moja, tunashauri kwamba uratibu wakati tunataka kutekeleza hii miradi uwepo katika sekta mbalimbali ili kuondoa adha ya vitu kama hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ninapenda kulizungumzia, ni eneo la usimamizi wa mikataba kwa ujumla katika utekelezaji wa miradi. Wakandarasi wengi au kwa kushirikiana na wafanyakazi wa Serikali unakuta usimamizi umekuwa siyo mzuri kuanzia mambo ya uratibu kama nilivyosema, lakini vilevile kuisimamia hii mikataba vile ambavyo inataka. Kwa mfano mikataba yote inakuwa na *Bills of Quantities*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa hapa Waheshimiwa Wabunge sana tangu asubuhi kwamba thamani au tuseme *value* ya ule mradi inaweza isifanane. Kwamba unakuta barabara inajengwa lakini haifanani na *Bills of Quantities* ilivyokuwa inataka. Kwa maana hiyo inaharibika haraka tofauti na vile ambavyo ilikuwa imekadiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo ninapenda kulizungumzia ni wakandarasi. Sekta hii pia inasimamia wakandarasi na kuna Bodi za Wakandarasi na kuna bodi zaidi ya tatu ambazo zinasimamia masuala ya ukandarasi. Tatizo kubwa ambalo limekuwepo kwa wakandarasi wetu wa Kitanzania, kwanza ni nidhamu ya kufanya kazi, lakini pili hawana mitaji. Wengi wao wamekuwa hawana mitaji na hili limekuwa ni tatizo kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba benki zimetengeneza bidhaa za kukopesha wakandarasi ili waweze kupata, lakini wanakuwa saa nyingine hawana vigezo kwa sababu hiyo hiyo ya kukosa mitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu kabisa kwamba katika Wizara hii kuna Mfuko wa kusaidia wakandarasi ambao unaitwa *Contractor's Assistance Fund* ambao ni Mfuko wa Dhamana. Anatakiwa mkandarasi aombe, halafu benki itamdhamini kwa kupitia Mfuko huo, lakini Mfuko huu una mtaji kidogo. Mtaji wake ni mdogo sana na kwa sababu sisi kama Serikali tumekuja na *program* ya *local content* kwamba tuwape wazawa miradi mingi watekeleze wao, ni lazima pia tuwawezeshe. Miradi mingi ya wazawa ina thamani ndogo kwa sababu ya kukosa mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo ni kwamba Mfuko uboreshwe ili wakandarasi wetu waweze kupata miradi mikubwa yenye thamani kubwa kama ambavyo wanapata wakandarasi wa nje. Kwa sababu ukifanya kwa *assessment* ya haraka haraka, kwenye zabuni zinazotolewa hapa nchini, 20% zinakwenda kwa wazabuni wa nje na 80% zinakwenda kwa wazabuni wa ndani, lakini 80% ya kazi thamani yake ni ndogo sana kulinganisha na ile 20% iliyokwenda kwa wazabuni wa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote hii inatokana kwanza ni kukosa mitaji na vilevile kukosa ujuzi na ujuzi hauwezi kupatikana kama hawapewi nafasi ya kupata uzoefu kwenye maeneo hayo. Kwa hiyo ninapendekeza Wizara iangalie jinsi ya kuboresha Mfuko wa Wakandarasi ili waweze kupata mitaji kupitia mfuko wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa ni suala ambalo ni la kimkataba. Mikataba mingi sana sasa hivi ya wakandarasi inasema wakandarasi watalipwa *advance payment*. *Advance payment* hii imekuwa ni tatizo na ninaona kama imekuwa ni kichaka kwamba kazi haiwezi kuanza bila mkandarasi kulipwa *advance payment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unakuta kazi hazianzi kwa sababu labda mkandarasi hana fedha kabisa. Kwa nini mkandarasi alipwe *advance payment?* Lazima tuiangalie hii sheria. Sheria za zamani zilikuwa kwamba kama unaomba kazi, lazima uwe na uwezo angalau wa kukopeshwa ili uweze ku-*mobilize* kazi yako kwa sababu *mobilization* ya kazi mara nyingine wala haihitaji hiyo *advance payment*. Kwa hiyo tuliangalie hili eneo kwa sababu miradi mingi sana ina-*suffer* kwa sababu ya *advance payment*.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

MHE. BENG'I M. ISSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Emmanuel John Khambay, ajiandae Mheshimiwa Benjamin Lukubha.

MHE. EMMANUEL J. KHAMBAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara yetu hii ya Ujenzi. Awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuweza kusimama mahali hapa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Babati Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliopata nafasi ya kuchangia wa Bunge hili na Waheshimiwa Wabunge wanaotoka Mkoa wa Manyara. Mkoa wa Manyara ni miongoni mwa mikoa mikubwa katika nchi yetu, lakini ni mkoa ambao umekuwa na changamoto kubwa ya barabara. Sasa ni wakati wetu watu wa Mkoa wa Manyara, Wizara hii chini ya ndugu yetu Mheshimiwa Ulega, utupe kipaumbele na sisi walau katika hizi kilometa zaidi ya 1,600 ambazo ziko chini ya *TANROADS*, lakini kilometa 259 ndiyo zenye lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo kilometa ni kilometa zinazotoka kwenye Makao Makuu yetu ya Mkoa kuelekea Dodoma, kuelekea Singida, kuelekea Arusha, lakini kama mkoa wenyewe una kilometa 207 ambazo zinahitaji kuwekewa lami. Mheshimiwa Waziri ndugu yetu Mheshimiwa Ulega, tunatambua kwamba, Wizara hii ni ngumu na inahitaji fedha na fedha alizotengewa bado hazitoshi. Hata hivyo, fedha hizi zilizotengwa, kama zitapatikana na zisiposimamiwa kwa weledi, bado hazitoweza kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia nafasi hii kuungana na wenzangu kama nilivyokwishatangulia kusema, Mkoa wa Manyara hususan Wilaya yangu ya Babati Mjini, tuna uhitaji wa *bypass*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *bypass* ni hitaji muhimu kwa Makao yetu Makuu ya Mkoa ambapo ni Wilaya yetu ya Babati Mjini kama ambavyo Singida ilivyo ina uhitaji wa *bypass*, kama ilivyo

Tabora ina uhitaji wa *bypass*. Kwa hiyo ninamwomba Mheshimiwa Waziri, atakaposimama, sitamani kushika shilingi yake kwa sababu amekuwa ni mtu muungwana, wakati wote tumesema na yeye na amekuwa akitenga muda wake kutusikiliza, hatutamani kushika shilingi yake lakini asimamapo, tunaomba aje na majibu sahihi kuhusiana na suala la *bypass*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona nimetengewa kilometa 15.5 *bypass* ya Babati – Dodoma, lakini kuna mkanganyiko kidogo. Kuna eneo ambalo linaonesha Mhandisi Mshauri amepewa jukumu la kufanya utafiti katika barabara hizi mbili (Barabara ya Babati – Dodoma yaani *bypass* na *bypass* ya Babati – Singida). Hivyo asimamapo, ninaomba anipe uchambuzi sahihi juu ya suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Barabara ya kwetu ya Singe – Kimotorok na Ngoytok. Barabara hii inaunganisha Jimbo la Babati Mjini, Jimbo la Babati Vijijini na Jimbo la Kiteto pamoja na Simanjiro. Mheshimiwa Waziri upembuzi yakinifu umekwishafanyika juu ya barabara hii, lakini na usanifu wa kina umekwishafanyika, hivyo tunamwomba Waziri atusaidie ili barabara hiyo iweze kukamilika kwa sababu ni barabara muhimu katika uchumi wa Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tuna wananchi wetu katika barabara hiyo hususan kwangu Jimbo la Babati Mjini eneo la Hala na maeneo mengine katika barabara hiyo, wananchi wanahitaji kulipwa fidia. Tunaomba wananchi waweze kulipwa fidia kwa sababu taratibu zote zimekwishakamilika ili shughuli hiyo iweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Babati, ina uhitaji pia, kwa sababu ya msongamano wa magari. Sisi watu wa Babati Mjini tuna uhitaji wa *double road. Double road* ya Babati – Singida, *double road* ya Babati – Arusha na *double road* ya Babati – Dodoma kwa sababu barabara ile imezidiwa, magari zaidi ya 600 kila siku yanapita katika barabara ile. Sasa ni wakati sahihi wa wizara kuangalia namna sahihi ya kutusaidia

kuepukana na msongamano wa magari makubwa kwa sababu Bandari yetu ya Tanga imekuwa ikihudumia nchi za jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo barabara yetu imekuwa *busy* kuhudumia usafirishaji wa magari hayo katika kusafirisha mizigo. Hivyo ninamwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie sisi watu wa Babati, watu wa Mkoa wa Manyara kwa sababu tuna uhitaji mkubwa wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kunipa kilometa moja ya Barabara ya kutoka Kiru – Mbulu. Barabara hiyo pia ni muhimu kwa uchumi wa wananchi wa maeneo hayo kwa sababu inaunganisha Jimbo la Babati Mjini, Jimbo la Babati Vijijini na Jimbo la Mbulu. Mheshimiwa Waziri, kilometa moja haitoshi, kwa heshima ya kaka yangu Mheshimiwa Naibu Spika, kutupa kilometa moja bado haitoshi. Tunamwomba, katika bajeti hii ya mwaka huu, atuongezee fedha ili barabara hiyo walau iweze kusogea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ninamwomba kwa Barabara ya Mbuyu wa Mjerumani – Magara – Mbulu. Barabara hiyo pia iweze kukamilika ili kuweza kusaidia wananchi wa eneo hilo. Barabara hiyo pia ni muhimu kwa sababu inatumika pia kwa utalii. Kwa hiyo, ninamwomba, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Mkoa wa Manyara waliotangulia kusimama walivyozungumza, sisi Mkoa wa Manyara tuko nyuma kwenye suala zima la barabara. Tunaomba asimamapo hapa, atuambie ni kipaumbele kipi anatupa katika kutusaidia ili walau barabara hizo ziweze kuboreka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata zile za kiwango cha changarawe zimechakaa. Sisi watu wa Mkoa wa Manyara tuna changamoto kubwa sana. Tunaomba Waziri atusaidie ili suala hilo liweze kwenda sawasawa na wananchi wa Jimbo la Babati Mjini na majimbo mengine ya Mkoa wa Manyara waweze kutufurahia sisi wawakilishi wao kwa majukumu ambayo wametupatia. Kutokutusaidia ni kutuweka katika mtego sisi Waheshimiwa Wabunge wote tunaotoka kwenye Mkoa wa Manyara kutokana na changamoto ambayo tunayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufikia hapo, ninaunga mkono hoja, lakini asimamapo Waziri ninaomba majibu ya kina kuhusiana na *bypass* ninarudia tena. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Benjamin Lukubha; wajiandae Mheshimiwa Japhael Masanja Lufungija na Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani.

MHE. BENJAMIN L. NGAYIWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana pia kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia Bajeti ya Wizara yetu nyeti kabisa ya Ujenzi. Sote tunafahamu kwamba, kama ilivyo katika mwili wa binadamu, barabara zinakuwa kama *blood vessels*, zinapitisha damu katika mwili mzima. Ndivyo ilivyo katika kusafirisha bidhaa na binadamu kwa maana ya abiria katika kukuza uchumi wa nchi yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru sana Serikali na hasa Wizara ya Ujenzi. Nimeona katika bajeti yao na katika makadirio yao, wametenga shilingi 500,000,000 kwenda kukarabati Barabara ya kutokea Kahama, inapita Nyandekwa, inaenda Nyamilangano mpaka Uyogo kwa Mheshimiwa Cherehani, shilingi 500,000,000. Ninaishukuru sana Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, Barabara inayotoka Kahama - Kakola kwenda Bulyanhulu kwa Mheshimiwa Magangila, na yenyewe inatengenezwa kilometa 73. Pia, Barabara kutoka Kahama – Tulole – Muhuridede mpaka huko Mambali, Tabora kilometa 152 imetengewa na yenyewe bajeti ya shilingi 500,000,000 lakini kipande cha kilometa 20 kutoka Kahama kwenda Tulole na chenyewe kimetengewa fedha kwa ajili ya kukarabatiwa. Kwa hiyo ninaishukuru sana Wizara, ninaishukuru sana Serikali ya Chama Cha Mapinduzi chini ya Jemedari Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninajielekeza katika hoja nyingine na Mheshimiwa Abdallah Ulega kaka yangu ninaomba anisikilize hapa, ninaomba ombi hili muhimu sana. Ile barabara ya kutoka Kagongwa unaenda mpaka Nzega yenye kilometa karibu

73, karibu kilometa 65 imejengwa mpaka kufikia tabaka la tatu kwa maana ya lugha ya kitaalamu *G-45* kupitia ufadhili wa kampuni moja ambayo ni ya *EACOP* inayotengeneza mabomba ya mafuta kwa ajili ya Mradi wa *EACOP* kwenda Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kilichobaki ni tabaka la kuwekewa lami tu. Sasa majibu ya Serikali hapa wanasema wanatafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha tabaka la lami. Ninamwomba ndugu yangu Mheshimiwa Abdallah Ulega, afanye juhudi za makusudi kwenda kumalizia tabaka hili la lami kutoka Kagongwa kwenda pale Igusule ili tuiweke lami barabara hii isije ikaharibika. Tukikaa muda mrefu na mvua zikanyesha tena za msimu ujao, barabara zile tabaka la tatu, la pili mpaka la kwanza zitaharibika, tutaanza tena upya kwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumebakiza kipande cha kumwaga lami tu kilometa 18.3, Kagongwa – Igusule. Ninamwomba sana kaka yangu Mheshimiwa Abdallah, sitaki kusema mambo ya kushika shilingi. Ninamwahidi, akinitengenezea barabara hii, kwa kuwa wao ni Waislamu wanaruhusiwa *mathna* na kule tuna Wasukuma wazuri wazuri, aje aniambie tutampatia mke mwingine kutoka kule Kahama. Siyo rushwa lakini ninakuombea mema ndugu yangu Mheshimiwa Abdallah Ulega. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara nyingine ile inayotoka Kahama, inapita Nyandekwa inaenda mpaka Nhwande, Ugalla, Kaliua, inatokezea Ulyankulu mpaka Mpanda. Hii barabara inaunganisha Mikoa hii ya Shinyanga mpaka Mpanda. Ni barabara muhimu, inasafirisha mazao, tumbaku kutoka kwa Mheshimiwa Cherehani, inasafirisha mbao, mpunga, mahindi na alizeti. Ni barabara muhimu sana hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba tena Mheshimiwa Abdallah Ulega, barabara hii amesema kwamba imetengewa fedha shilingi 150,000,000 kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu. Ninamwomba Mheshimiwa Abdallah Ulega, hizi lugha za upembuzi yakinifu, usanifu sijui *feasibility study*, zimekuwa ni lugha

za kawaida sana na hii barabara imekuwa ikitengewa bajeti kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sana Waziri tuanze hata na kipande cha kutokea Kahama tufike Nyamilangano twende mpaka Kaliua huko, Bulyanhulu na twende polepole tuweke lami barabara hii ili wananchi wetu wasafirishe mazao na waweze kusafiri kipindi chote bila kupata shida yoyote. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. BENJAMIN L. NGAYIWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana kwa muda huu. Mheshimiwa Abdallah Ulega ile Barabara ya Kagongwa kwenda Igusule, kilometa 18 tuimwage lami ndugu yangu, nitakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaomba kuunga hoja mkono. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Japhael Masanja Lufungija, ajiandae Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani.

MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi. Lakini nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kunipa uwezo wa kuweza kujadili Hotuba ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri na kauli yake yenye utu tusonge mbele tunaendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana pia Waziri wa Ujenzi na Naibu Waziri, Katibu Mkuu dada yangu Aisha na daktari bingwa sana Dkt. Charles Msonde kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya, bila kumsahau *Engineer* wangu wa Mkoa ndugu yangu Mlimaji kwa kazi nzuri ambazo anazifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuishukuru Serikali kwa kuona imepanga fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu na ujenzi wa Barabara ya kutoka Kahama – Ushetu – Ulyankulu kwenda Kaliua. Barabara hii ni barabara muhimu. Barabara hii ilianzishwa mwaka 2010 na imekuwepo kwenye Ilani zetu muda wote, lakini kwa umuhimu wa barabara hii inaunganisha mikoa zaidi ya kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niitaje barabara hii inaunganisha Mikoa ya Tabora, Shinyanga, Geita, Bukoba, Mwanza na Mara kwa maana ya kanda maalum. Barabara hii itakapojengwa kutokea Mwanangwa itakuja mpaka maeneo ya Kahama na ndiyo barabara inayotoka kwenda huko Mpanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mikoa ya Kusini, barabara hii inaunganisha Barabara ya Tabora, Mkoa wa Tabora, Mpanda, Mkoa wa Katavi pamoja na Rukwa. Barabara hii imekuwa *busy* sana. Kwa takwimu za kawaida, kwa siku barabara hii inatumika na magari makubwa sita mabasi ambayo yanasafiri kila siku. Gari ndogo ndogo kwa maana ya *hiace* ni *hiace* tatu, mabasi ya kati ni mabasi ishirini na tano lakini malori kwa wastani wa kawaida kila siku inapitisha malori mia moja na kumi, ina maana kwa mwaka malori yanayopita ni 39,600. Kwa hiyo, unaweza ukaiona barabara hiyo ilivyo na umuhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ninamwomba Waziri nimeona ameweka *token* pale kwamba imepata kifungu kwa maana ya kuingiziwa fedha. Tumwombe Mheshimiwa Waziri nchi hii imeundwa ikapewa kila eneo na vipaji vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukanda wa kaskazini wenzetu wanategemea mazao mengi yatoke Mikoa ya Kusini. Kwa maana ya wenzetu wa Katavi, Mpanda, Kaliua na Tabora sisi ni wazalishaji wakubwa sana wa zao la tumbaku, mahindi, mpunga, mifugo lakini pamoja na uzalishaji wa asali na misitu. Kwa hiyo, ni barabara ambayo ni ya muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kusisitiza suala hili ili Waziri aipe kipaumbele kuhakikisha kwamba upembuzi sasa uanze, ikimpendeza hata kama ungeanza na Mwamnange - Ulyankulu kwenda Kahama halafu huku atoke Mwamnange kwenda Kaliua ili kuhakikisha kwamba ile barabara inaanza kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Waziri, nimeona Barabara ya kutoka Tabora kuja Ulyankulu kujengwa kwa kiwango cha lami. Ameitengea shilingi 2,000,000,000 nimshukuru na kumpongeza, kwamba barabara hiyo ni ya muhimu, ni barabara inayotuunganisha Mkoa na Jimbo la Ulyankulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisikia tumbaku Tanzania tunazungumza Mkoa wa Tabora, ukisikia tumbaku Tanzania tunazungumza Wilaya ya Kaliua. Siyo Kaliua tu tunazungumza pia Jimbo la Ulyankulu lakini Ulyankulu tunayo madini, tuna mgodi pale Nsungwa, kwa hiyo, tuone umuhimu wa kuifungua barabara hii ili kuhakikisha inachochea uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru nimeona barabara inayotoka Ulyankulu kwenda Urambo kwa mama yangu Margaret Sitta, imepewa *token,* Mungu akubariki sana mjukuu wangu, huyu ni mtu muhimu sana katika maisha yetu, nimwambie mimi sitashika shilingi yake, ninaamini tunapitisha mpango wa *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini kule Ugalla muhimu kabisa ile barabara tukijenga daraja na sisi hatuna matatizo ukanda ule jenga Daraja la Ugalla ambalo miaka ya nyuma liliingiwa mkataba wa kujengwa kwa muda wa miezi 18, lakini fedha hizo hazikutoka. Likijengwa hilo daraja ninaamini litatuunganisha vizuri na mama yangu Mheshimiwa mama Lupembe pamoja na Haidary na ndugu yangu wa kule Mpanda, Katavi na Rukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haitoshi tunayo hii Barabara ya Tabora – Ibiri – Ulyankulu. Sasa kwa sababu tayari kuna madaraja alishajenga ninamwomba hatua nyingine za kuanza kuwafanyia tathmini watu wanaostahili kulipwa, ianze kufanyika ili kuhakikisha kwamba shughuli inafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya kutoka Kahama, limejengwa daraja zuri sana pale Kashishi baina ya Sunga na Kashishi. Barabara ya kiwango kizuri ndiyo hayo ambayo pia Serikali kupitia Waziri Mkuu amekuwa akieleza Serikali imefanya kazi kubwa kuhakikisha kwamba inajenga daraja, kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri ajenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo pia barabara inayotoka Jimbo la Ushetu kwa maana ya Halmashauri ya Ushetu. Barabara hii inatokea Masumbwe inapita Mwabomba inakuja mpaka Ulowa namba nne lakini inakuja kuniunganisha huku na Sungwa. Liko daraja moja limejengwa zuri sana Serikali imewekeza fedha nyingi. Ninaiomba Serikali yetu pendwa, bila kujenga Daraja la Mto Igombe linalotuunganisha sisi na Ushetu bado tutakuwa hatuitendea haki barabara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma ninakumbuka barabara hiyo pia ilikuwa kwenye mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami ili kuwapunguzia watu wanaotoka Mikoa ya Geita na Mwanza wanapotaka kwenda mikoa aidha ya Katavi na Mbeya watatoka wakifika Masumbwe wanakata kupunguza umbali, wakija wanafika Ulyankulu watapita Urambo watakwenda Ipole, wataunga kwenda Mkoa wa Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa hawa wanaohitaji kwenda Mkoa wa Katavi watafika Ulyankulu. Waziri anitengenezee *roundabout* nzuri pale Mwenda Kulima, kwa maana ya Uyowa, aweke *roundabout* nzuri pale Barabara Sita Ulyankulu ili kuhakikisha…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda wako umekwisha…

MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA: …wanaokwenda Urambo watakuwa wanakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani; wajiandae Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mheshimiwa Musa Godfrey Mbuga na Mheshimiwa Dotto Jasson Bahemu.

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu. Asiyeshukuru kwa kidogo hawezi kushukuru hata kwa kikubwa, nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutupa fedha ambayo inajenga Barabara ya Mnivata – Nanyamba – Tandahimba mpaka Masasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia, kwa kutupa fedha pia ya Barabara ile ya Mingoyo – Lindi, Mingoyo – Mtwara na Mingoyo – Masasi lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kumteua ndugu yetu Ulega na baada ya kushika madaraka haya ya Uwaziri ameweza kutembelea barabara tunazozitaja za kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo changamoto kwenye Barabara ya Mnivata – Nanyamba – Tandahimba mpaka Mitesa, mkandarasi aliyepewa barabara China Wu Yi ambao mkataba wake unamalizika tarehe 31 ya mwezi Oktoba mwaka huu. Tunapozungumza leo ameweka lami kilometa nne, mwenzie mwenye kilometa 60 *China Communication* ameweka lami zaidi ya kilometa 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amepata bahati ya kuja kwenye barabara ile na ile ni barabara ya uchumi. Tunapozungumza zao la korosho 60% ya korosho za Tanzania zinatoka kwenye hii Barabara ya Mnivata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, yeye ni mtu mwema sana, tunapomaliza kupitisha bajeti yake twende tukajue changamoto ya mkandarasi yule kama

kuna namna ya kumfukuza, wamfukuze, wamweke mwingine wananchi wanataka barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanamtwara, Wanatandahimba, Wanananyamba, Wananewala, wanataka kuona barabara imekamilika kwa kiwango cha lami. Bahati nzuri fedha ya barabara ile inatoka Benki ya Maendeleo ya Afrika hakuna kona kona ya fedha, hapa pana janjajanja ya mkandarasi. Wenzetu wamesema kazi hizi kubwa zote wanawapa wakandarasi wa nje ya Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila ukisikia mradi mkubwa wa barabara wanawapa watu nje, tunashindwa namna ya kukabiliana nao. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri tukimaliza, ikiwezekana twende tukaangalie changamoto ya barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumza wenzangu hapa, ili ufike Mtwara ni lazima uanze kutoka Mbagala, uende Mkuranga, Kibiti, Muhoro, Nangurukuru, Lindi. Barabara hii tunayoisema Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni amezungumza vizuri kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasi tunaipongeza Serikali kwa kujenga madaraja, imefanya kazi kubwa sana. Tunataka tuone wakati una-*wind up* Mheshimiwa Waziri barabara hii mpango wake ukoje? Ninamwomba sana kaka yangu, nimepita usiku nikiwa ninatoka Mtwara kuja kwenye hili Bunge na kilichonileta hasa juu ya barabara hii nimepasua matairi manne, matairi manne nimeacha gari kwa ubovu wa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba barabara hii tumekuwa na Mradi wa *Cement* wa Dangote, magari yale makubwa yote yamepita kwenye Barabara hii, sasa imekufa. Tumekuwa na Mradi wa Makaa ya Mawe umepita mle barabara imekufa lakini Serikali wakati wote wanazungumza juu ya Mradi wa *LNG*. Mwekezaji gani atakuja akapita barabara mbovu hii akaja kuwekeza Lindi, ni Mwekezaji wa aina gani apite kwenye barabara ile ya kwenda Lindi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wametengeneza pale Kilwa ipo bandari ambayo wamewekeza mabilioni ya fedha. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, ndugu yangu, wakati ana-*wind up* hapo hapo wakati tunataka kupitisha bajeti yake nami nitakaa ndani humu. Nami katika watakaoshika shilingi na mimi ndugu yake nitashika shilingi kama sikusikia maneno mazuri juu ya Barabara ya kutoka Dar es Salaam kwenda Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nami sitafika Mtwara hata kama atanijengea barabara yote ya Mtwara ya mzunguko, lakini kama kutoka Dar es Salaam kwenda Lindi kuna vumbi, kama ile barabara ni mbovu, maana yake sina sababu ya kufika Mtwara kwa sababu njia haipitiki. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda wako umekwisha…

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho wenzetu wametoa mapendekezo hapa juu ya watu kuchangia sijui kwenye simu. Hivi mkulima wa korosho ambaye leo hata vocha ya shilingi mia tano hawezi kuweka, umwambie atozwe fedha eti achangie ujenzi wa Barabara, jambo hili halikubaliki, halikubaliki kabisa, halikubaliki kabisa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda wako umekwisha, unga mkono hoja.

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nilimtaja Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, ajiandae Mheshimiwa Musa Godfrey Mbuga.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza kwa ajili ya muda nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa rehema zake kwetu sote, niishukuru sana Serikali yangu kwa kazi kubwa iliyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda huu ni miaka karibu 10 niko ndani ya Bunge hili na sasa tunaenda awamu ya tatu kazi kubwa imefanyika. Waheshimiwa Wabunge wenzangu wanakumbuka kwamba tulipoanza wakati ule 2015 kazi kubwa imefanyika kwa sekta ya barabara iwe *TARURA,* iwe *TANROADS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa eneo hili ni kwamba, kuna baadhi katika maeneo ya nchi hii kama Wilaya ya Mbulu sisi tuko juu ya Bonde la Ufa, kule ni juu ya Bonde la Ufa, kwa hiyo hakuna jiografia inayofanana na Mlima Magara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawaziri wengi wamekwenda Mbulu, lakini kila tulipofika walisema Mheshimiwa hii ndiyo barabara yako, hakuna barabara nyingine? Kwa kweli tunaipongeza Serikali ilichukua hatua kubwa ikaweka zege kwenye Mlima Magara, pia ikajenga Daraja la Magara. Tunampongeza sana Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipokuja 2015 hatukuwa na Daraja la Magara wala hatukuwa na zege kwenye Mlima Magara kwa sehemu kubwa, kwa hiyo kazi hiyo kubwa ilifanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali ni kwanza kazi zote tulizoanza tuendelee kuendeleza hizo barabara zimekaa muda mrefu. Barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali kwa ujumla alivyokuja, mara baada ya ziara yake nilipokuja kwake hapa Bungeni Serikali ilimlipa yule mkandarasi na lakini bado hajarudi *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kabla Bunge halijakwisha arudi *site*. Baada ya Bunge hili Waziri afanye ziara ya kutembelea Barabara hiyo ya Mbulu – Garbabi na kipande cha Labay kwa sababu eneo hili la barabara limekuwa changamoto kubwa kwa wananchi wa Wilaya ya Mbulu na hali imekuwa mbaya sana, hali ya usafiri na barabara zinajifunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali ni kwamba gharama tunazopata baada ya miradi kukaa muda mrefu, riba

inakuwa kubwa na baadaye tunalipa hela nyingi sana kwa mkandarasi kutokana na hii hatua ya miradi kukaa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, eneo hili wameweka kilometa mbili tu za lami hadi sasa, lakini bado kilometa 23 zimebaki na mkandarasi hayupo *site*. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri atakaporudi atuambie sisi Wabunge wa Mbulu Mkandarasi wa Mbulu – Garbabi atarudi lini *site* kwa sababu tayari Serikali imeshamlipa na hii ni hatua kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Mbuyu wa Mjerumani – Magara kwenda Mbulu usanifu umefanyika kwa takribani miaka miwili sasa, lakini ninachohofu ni kwamba baadaye tutarudi tena kufanya usanifu. Kwenye fedha za mwaka huu wameweka sehemu kidogo ya zege katika Mlima Magara

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali ikamilishe zege katika Mlima Magara na Mheshimiwa Waziri atakapokuja Mbulu, apite barabara ya Magara ndiyo atajua kwamba jiografia ya Wilaya ya Mbulu katika Mlima Magara na Mlima Dabidi, hakuna eneo kama hilo katika Tanzania hii, hakuna mwinuko wa mlima mkali wenye kona 130 ni Mbulu Mjini unapokwenda ambako inatuunganisha sisi na Mkoa wetu wa Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, katika fedha za barabara tunazochanga kwa sasa bado tuendelee kutafuta vyanzo vya mapato. Mimi kwenye tozo ya simu na tozo nyingine mnazosema…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda wako umekwisha…

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti…

MWENYEKITI: Muda wako umekwisha…

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru ninaunga hoja mkono, ahsante kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Musa Godfrey Mbuga, ajiandae Mheshimiwa Dotto Jasson Bahemu.

MHE. MUSA G. MBUGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi hii uliyonipa kuongea kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Kisesa, nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii. Ninampongeza Waziri wa Ujenzi Abdallah Ulega, kaka yangu sana pamoja na Naibu wake *Engineer* Godfrey Kasekenya huyu ni zaidi ya *encyclopedia*, hii ni *encyclopedia* inayotembea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Katibu Mkuu, Balozi *Engineer* Aisha, ninampongeza Naibu Katibu Mkuu Dkt. Charles Msonde, ninampongeza pia Meneja wangu wa Mkoa wa Simiyu *Engineer* Boniface Mkumbo. Nami ni Mjumbe wa Kamati ya *PAC,* tumetembelea miradi mingi ya *TBA,* ninaomba nimpongeze sana Kiongozi Mkuu *DG* wa *TBA* pamoja na taasisi nyingine ambazo ziko chini ya Wizara ya Ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda sitaweza kuongelea kazi za *TBA* na mengine, naomba nijielekeze kwenye upande wa barabara. Ninashukuru Serikali inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa fedha ambazo zimekuja Jimboni Kisesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya ufinyu wa muda nijikite kwenye changamoto zilizopo Kisesa. Ndugu yangu Mheshimiwa Ulega, kuna changamoto kubwa sana ya barabara inayotoka Maswa inakuja mpaka Mwabusalu inaenda Mwandoya inaenda mpaka Sakasaka. Barabara hii ina hali mbaya. Ninaomba atakapokuwa anafanya majumuisho aeleze mkakati ambao alionao pamoja na viongozi wengine walio chini yake kwenye hii barabara inayotoka Mwabusalu mpaka Sakasaka, hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ninapongeza na ninatoa shukrani, nimeangalia kwenye randama nimeiona barabara ambayo inatuunganisha na Singida pamoja na Simiyu, ninaipongeza sana Serikali, Wizara hata tu kwa huu utayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa imeshatengewa fedha ninakuomba ndugu yangu hii Barabara ya kutoka Singida kuja Sibiti kuja Mwanhuzi inakuja mpaka Ng'oboko, Mwandoya mpaka Bariadi, kwetu sisi hii ni barabara ya muhimu sana kiuchumi hata kwenye utalii. Jimbo la Kisesa na Jimbo la Meatu tumepakana na Hifadhi ya Pori la Akiba la Maswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watalii wengi wanapokuja wanapata shida sana. Hata Mheshimiwa Rais amekuja ameona hali halisi ya barabara hii. Hata hivyo, barabara hii imekuwa inawekwa kwenye ilani. Kila ilani unakuta ipo, lakini unakutana na maneno upembuzi yakinifu, upembuzi yakinifu. Ninamwomba ndugu yangu Mheshimiwa Ulega, upembuzi ufikie mwisho. Tumechoka kusikiliza mambo ya *feasibility study*, sasa tunamwomba aje na mkakati wa namna gani anaenda kuikamilisha hii barabara. Kwa hiyo, tunamshukuru kwa sababu ameiweka kwenye bajeti, sasa tunamwomba atekeleze kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ndiyo inafungua mazao yetu ambayo tunalima. Sisi ni wafugaji tunasafirisha mifugo yetu kwenda kwenye minada mbalimbali kwa kupitia barabara hii. Kwa hiyo, tunamwomba sana Waziri, mazao yetu yaweze kwenda kwenye masoko mbalimbali. Atakuwa ameongeza mzunguko wa uchumi kwenye jimbo la Kisesa pamoja na Meatu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa leo sitaki kuwa na mengi sana, ninachohitaji ni Barabara ya kutoka Mwanhuzi kuja mpaka Bariadi. Ninachohitaji ni Barabara ya kutoka Mwabusalu kwenda Sakasaka. Barabara ya kutoka Ng'hoboko kwenda Itinje kuelekea mpaka Lalago.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja ya bajeti hii. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Dotto Jasson Bahemu. Mheshimiwa Morris Joseph Makoi na Mheshimiwa Isack Joseph Copriano, wajiandae.

MHE. DOTTO J. BAHEMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Ninaomba nianze kwanza kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na nitaeleza sababu kwa nini nimeanza kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kusema katika Bunge hili kwamba mimi ni Mbunge wa saba anayetoka katika Jimbo la Ngara ambaye amekuwa akiomba Barabara ya Nyakahura – Kumubuga – Rulenge – Murugalama. Mimi ni Mbunge wa saba. Wabunge wenzangu wote waliopita wamezungumza sana kuhusu hii barabara na huenda ndiyo maana walikuwa hawarudi kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, mimi nikiwa katika Bunge hili nimezungumza mara nne kuhusiana na Barabara ya Nyakahura – Kumubuga – Rulenge – Murugalama. Nimeona katika bajeti ya mwaka huu Mheshimiwa Waziri amezungumza kuhusiana na hii barabara, ambapo kiasi cha shilingi 1,500,000,000 kimetengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira ya kawaida kabisa, ukiwaza kilometa 145 ambapo umetengewa shilingi bilioni 1.5 unaweza ukaona ni kiasi kidogo sana kimewekwa na ukajiuliza kinaenda kufanya nini? Ukirudi kwenye chimbuko la nia ukasema kwamba hata kutengwa kwa hiyo shilingi bilioni 1.5, angalau kutengwa tu, barabara ambayo imezungumzwa kwa zaidi ya miaka 35. Nimezungumza kwamba leo angalau imekumbukwa, imetengewa shilingi bilioni 1.5. Sisi watu wa Ngara tunasema ahsante sana Mwenyezi Mungu, angalau kwa mara ya kwanza tumezungumzwa katika barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mchana nimekutana na Mheshimiwa Waziri pale nje, nikamtania nikamwambia Mheshimiwa Waziri ile barabara nimeona wametupa *1.5 billion*. Hata angetupa shilingi 100,000, kutenga tu kiasi hata shilingi 100,000 sisi tungeshukuru. Tunaona kwamba kuna mwanga mbele unakuja, kwamba angalau ile barabara sasa inakwenda kuanza kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo limewafurahisha sana watu wa Ngara, wameanza kupata imani. Imani yao imerudi baada ya kuwa wameona kwamba kwa muda mrefu wamekuwa wakitengwa kwa sababu ile barabara ilikuwa haipitiki na sasa wanaona kwamba sasa na sisi tumekumbukwa. Yale ambayo tumekuwa tukiyatoa kwa Serikali, Serikali na sisi imekwenda kuturudishia. Kwa hiyo, ndiyo maana sisi watu wa Ngara tunasema tunashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mijadala ya tangu jana mpaka leo, lakini vilevile nilisikiliza taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu ambaye amezungumza kwa kina sana kuonesha ni kwa namna gani ambavyo kuna changamoto ya upatikanaji wa fedha katika maeneo mbalimbali, lakini sisi pamoja na changamoto hiyo ya upatikanaji wa fedha angalau tumepewa hicho kiwango kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wa Ngara tunashukuru sana na Mwenyezi Mungu amlipe Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tunazidi kumwombea azidi kumpa maisha mazuri, maisha yenye afya ili Watanzania waone yale mazuri ambayo anakwenda kuwafanyia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wa Ngara hatuwezi tuka-*complain* kabisa hata kidogo kwenye hii bajeti ya Wizara ya Ujenzi, hata tufanyeje. Kwa sababu, ukiachilia mbali kiwango ambacho kimetengwa kwenye hii barabara, bado vilevile tuna Barabara ya kutoka Kobero kwenye mpaka wa Burundi – Kabanga – Ngara – Nyakasanza. Ile barabara ni mbovu. Wabunge wengine wamekuwa wakizungumza kuhusu barabara ambazo zimeharibika. Ile barabara pia imepitwa na muda wake,

lakini nimeangalia kwenye bajeti tumewekewa shilingi 300,000,000 ya kwenda kufanya ukarabati wa muda ili yale mashimo yaweze kuzibika. Tunashukuru kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, tunayo Barabara inayotoka Lusahunga – Nyakahura – Rusumo. Inapita katika majimbo mawili. Jimbo la Biharamulo kwa ndugu yangu kaka Ezra, lakini vilevile katika Jimbo la Ngara. Ile barabara nayo ilikuwa ni kichefuchefu. Kama ambavyo wamekuwa wakizungumza watu wengine kwamba barabara zao hazipitiki, ile barabara kipindi cha nyuma ilikuwa haipitiki kabisa. Ninaamini ile barabara ndani ya miezi miwili itakuwa ni mkeka, tutakuwa tunateleza kwa sababu iko katika matengenezo makubwa sana. Barabara imetolewa imewekwa barabara nyingine mpya. Sisi tunashukuru sana, hatuwezi ku-*complain*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Kivuko cha Kanyinya – Mayenzi ambacho na chenyewe tumeweka shilingi 200,000,000 kwa ajili ya kwenda kukitengeneza. Chenyewe katikati hapa kilikuwa hakipitiki na nilishawahi kuuliza swali Bunge kwamba kile kivuko hakipitiki, lakini nimeona kuna shilingi 200,000,000 ambazo zimewekwa kwa ajili ya kwenda kutengeneza kile kivuko ili kiweze kupitika. Sisi tunashukuru sana watu wa Ngara. Hatuwezi ku-*complain* chochote kuhusiana na hii bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tumeona kwamba changamoto ni upatikanaji wa fedha, Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema siwezi kurudia, lakini sisi hatuamini katika kuanza kwenda kuwaumiza wananchi kwa ajili ya kwenda kutoa tena tozo kwa ajili ya kwenda kuongeza huku kwa ajili ya hivi vitu vipatikane. Tunaamini maeneo mengine kuna sehemu ambapo fedha zinaweza zikapatikana bila kuwaumiza wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaungana na Wabunge wengine wote ambao wamechangia kuhusiana na *PPP*. Tufanye mradi wa *PPP* na mimi nimefuatilia nimegundua kwamba hapa kwetu changamoto kubwa iko kwenye *PPP* ambao ni urasimu. Sasa sisi tunaomba, kama wawekezaji wamekuja, wawekezaji wamepatikana, tunaamini kuna barabara ambazo ni *potential*

ambazo Serikali hata haiwezi ikaumiza kichwa kwenda kutengeneza, ambapo ukitangaza kwenye *PPP* watu wanajitokeza. Hata tukifanya *PPP* ule urasimu ukatoka hatutakuwa wa kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ndugu zetu hapa jirani zetu wa Afrika Mashariki (Kenya), nao wanatumia *PPP* mambo yanaenda vizuri.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. DOTTO J. BAHEMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaona muda wangu umekwisha, ninaunga tena mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Morris Joseph Makoi. Hayupo, Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando.

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kigoma Mjini na Kigoma kwa ujumla, ninaomba tuwe na moyo wa shukrani kwa kazi iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, chini ya Waziri wetu mzee wangu Mheshimiwa Ulega.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niwahakikishie ndugu zangu Wabunge, Jimbo la Kigoma Mjini tumeteseka sana kwa miaka mingi namna ya kuunganisha kutoka Kigoma Mjini kwenda Tabora, kutoka Kigoma Mjini kwenda Mwanza, kutoka Kigoma Mjini kwenda mikoa ambayo imetuzunguka, lakini Serikali ya Awamu ya Sita imefuta hicho kilio kwa wananchi wa Kigoma Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa ukitoka Kigoma Mjini kwenda Tabora itakugharimu saa 13, lakini sasa hivi Mheshimiwa

Dkt. Samia Suluhu Hassan amemaliza hilo tatizo na kutoka Kigoma Mjini kwenda Tabora ni saa nne peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka Kigoma Mjini kwenda Mwanza ilikuwa inatugharimu saa 17, lakini sasa hivi Serikali ya Awamu ya Sita imemaliza hilo tatizo na sasa hivi ni saa nane tu peke yake. Lazima tuwe na moyo wa shukrani. Siku zote tumekuwa tunaomba, lakini pale ambapo tumetendewa mambo mazuri, lazima wananchi wangu wa Kigoma Mjini Mbunge wenu ninashukuru kwa niaba yenu hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimwambie mzee wangu Mheshimiwa Ulega, maneno yote yaliyosemwa haya ninaamini yeye ni jembe na anaweza kupambana nayo. Ninauamini uwezo wake alionao na ndiyo maana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alimpa nafasi ya pili kwenye Wizara hiyo hiyo. Ingekuwa ni mtu ambaye hana uwezo wa kutosha angehamishwa hamishwa au angetolewa angewekwa mtu mwingine. Maneno yaliyozungumzwa na Wabunge wengi hapa yachukuliwe kama changamoto ili aende akawasaidie kwa sababu wao wanaongea kwa niaba ya wananchi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mimi hapa leo hii katika Jimbo la Kigoma Mjini hatuna shida kubwa sana na barabara za *TANROADS*. Kazi kubwa ameifanya, kazi kubwa ameimaliza. Nimesikia kuna Wabunge hapa wanaomba kilometa 85, kilometa 20, kilometa 30, mimi nina vitu vidogo sana, vichache mno vya kumwambia Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza, tumeleta maombi ya kubadilisha barabara mbili ambazo tunataka zitoke kwenye *TARURA,* tumtue mzigo Mheshimiwa Profesa Shemdoe, nitammaliza. Tumtolee Mheshimiwa Profesa Shemdoe kidogo tukuletee wewe ili tuwe tunapambana vizuri. Barabara ya kutoka Katosho kupitia Kibirizi Sokoni kutokea kwenye ma-*tank*. Maombi yako mezani kwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya pili, ni barabara kutoka kwa Mkuu wa Wilaya pale Kigoma Mjini kwenda Katonga,

tunaomba Waziri atusaidie. Barabara ambayo tumeipa jina la *Kasulu Road* ambayo itawapunguzia mzigo watu wa Ujiji wasizunguke kwenda mjini wakitaka kwenda kwenye nyumba zao. Tunaomba, ni kilometa chache chache sana hazifiki hata kilometa 13. Tunaomba sana tusaidie apitishe hayo maombi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la mwisho, ninaomba anipe heshima ya kupata barabara ya juu katika Jimbo la Kigoma Mjini. Nimeongea na Waziri wa Uchukuzi, kuna sehemu ambapo *SGR* inapita. Mama anatuletea *SGR* Kigoma Mjini, *SGR* inapita. Mkandarasi wa *SGR* anataka kujenga tuta, yaani aikate Kigoma Mjini katikati kwa tuta iwe kama ardhi na mbingu. Hatukubaliani na hicho kitu, tunaomba atutengenezee barabara ya juu, magari yapite juu, treni ipite chini ili wananchi wa Kigoma Mjini kwa mara ya kwanza waweze kupata *flyover. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili, tumeomba; Kigoma Mjini ukienda Ujiji kuna sehemu panaitwa Darajani. Tumeomba tupate Daraja kama lile la Manzese. Maandiko yako ofisini kwake. Tunataka wananchi wapite juu, magari yapite chini kwa sababu imekuwa ndiyo sehemu ambayo wanagongwa mara kwa mara katika Soko la Buzebazeba. Amenileta *engineer* mmoja machachari sana, yuko vizuri sana Edward. Ninamkubali sana kwa sababu ya *idea* alizonazo zinaendana na spidi niliyo nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *engineer* aliyekuwepo mzee wangu Choma alikuwa anafanya kazi vizuri sana, lakini huyu wa sasa hivi tutaendana kwa sababu ni kijana mwenzangu. Nikimwambia weeh na yeye anasema weeh! Tunaondoka kwa pamoja mambo yanakuwa mazuri sana. Tunaomba sana Wizara ya Ujenzi waende wakatafute hela kwa ajili ya kutimiza hii miradi ya Wabunge wengine wote walioongea. Kwangu mimi nataka kilometa 13 tu peke yake.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo machache ninaomba nishukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa Mzee, Mheshimiwa Ulega na

ninamuunga mkono wala asife moyo. Mwenyezi Mungu amsaidie tunamuunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Hapa Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti

SPIKA: Mheshimiwa Morris Joseph Makoi. Mheshimiwa *Engineer* Fadhili Sandali Chilombe ajiandae.

MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwenye Jimbo la Tunduru Kusini iko barabara moja inayotoka Tunduru – Nalasi – Mtwara Pachani. Nimeongea ndani ya Bunge hili kama mara tatu mara nne kuhusiana na barabara hii na Jimbo la Tunduru Kusini kwa ujumla, kwamba, Jimbo hili ni moja kati ya majimbo machache ambayo hayana lami kabisa.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, amekuwa mkweli. Alipokuja Tunduru kwenye kampeni alitoa ahadi ya kuijenga barabara ile kwa kiwango cha lami na nimeangalia kwenye randama za Mheshimiwa Waziri barabara ile ipo. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, tunamshukuru Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara. Barabara hii kwetu sisi ni muhimu mimi na mwenzangu Mheshimiwa Dkt. Homera. Ninajua yeye anashindwa kusema kwa sababu alivyo, lakini angeweza kuisemea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kuwa tayari Serikali imeshaamua kuchukua hatua kwenye barabara ile, zetu sisi ni shukrani. Ila ninaomba kidogo; sisi watu wa Tunduru Kusini tuna kipande hicho cha barabara peke yake chenye urefu wa kilometa 300, lakini kuna kipande cha barabara ambacho kinahudumiwa na *TANROADS* ambacho kinatoka Nalasi kwenda eneo moja linaitwa Chamba, ni kama kilometa 17 hivi.

Mheshimiwa Spika, pia, kuna kipande kingine kinahudumiwa na *TANROADS* kinaanzia pale Azimio – Lukumbule kina urefu wa kilometa 65. Ombi langu, wakati mpango wa kutengeneza hii barabara ambao unaenda kuanza muda mfupi ujao, ninatamani

vipande hivi vingechukuliwa kabisa ili sisi tumalizane na *TANROADS* moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, ombi langu la pili, nimesikia hapa Wabunge ambao wana barabara za lami kwenye maeneo yao. Iko miradi imekaa muda mrefu sana. Wananchi wa Tunduru wanataka kuona lami ikipita kwenye maeneo yao. Kwa hiyo, ninaomba mradi utakapoanza basi uende kwa spidi itakayowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi watu wa Tunduru maisha yetu tunategemea sana Dar es Salaam. Bidhaa nyingi au zote zinatoka Dar es Salaam na tuna *alternative* mbili za kufika Dar es Salaam. Aidha, tupite Mkoa wa Lindi ambako ni kilometa 708 kutoka Tunduru au tupite Songea – Iringa ambako ni kilometa 1,239.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kawaida unaona kabisa njia yetu ambayo tunaitumia mara kwa mara ni hii ya Mkoa wa Lindi. Kwa sababu hiyo basi, ninaomba niungane na Wabunge walionitangulia wa Mkoa wa Lindi na Mtwara kuomba Serikali iipe kipaumbele barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, madhara tunayoyapata sisi watu wa Tunduru ni kwamba, bidhaa ikitoka Dar es Salaam kwenye barabara mbovu ile, licha ya kupanda kwa gharama zinazotokana na kupanda kwa mafuta ndani ya nchi, lakini na ubovu wa barabara pia wale watu wanatutoza. Kwa hiyo, barabara hiyo ikiendelea vile, basi mwananchi wa kawaida ambaye yuko mpakani kule anateseka zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kuwa Serikali hii ni sikivu na Wabunge wameongea kwa uchungu mkubwa na wameonesha hisia zao, matumaini yangu ni kwamba Serikali hii inaenda kuchukua hatua. Waziri Mkuu tunamwona yuko hapa na ni mtu ambaye amekuwa akifanya kazi na akitembelea kwenye maeneo hayo yote. Kwa hiyo, tunaamini haya mambo au hiki kilio cha watu wa Kusini kitafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu la tatu, Mji wa Tunduru unakua sana. Tayari Serikali ilishauona kwamba mji ule unakua na unahitaji kuendelezwa. Sisi tunayo *proposal* ya barabara ya *bypass* na upembuzi yakinifu ulishafanyika. Ile barabara inaanzia kwenye eneo moja linaitwa Mkapunda, inapita nje kwa nje inaenda kutokea kwenye eneo linaloitwa Masonya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara ile upembuzi yakinifu ulishafanyika siku nyingi, lakini nimeangalia kwenye kitabu cha mtani wangu Mheshimiwa Ulega sijaona akiongea kitu chochote kuhusiana na barabara ile.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba, ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE: ... anapokuja ku-*wind up* atueleze kuhusiana na hiyo *bypass*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Isack Joseph.

MHE. ISACK J. COPRIANO: Mheshimiwa Spika, ninachukua nafasi hii kukushukuru kwa kupata nafasi ya kuwa sehemu ya wachangiaji kwenye Wizara.

SPIKA: Jiandae Naibu Waziri.

MHE. ISACK J. COPRIANO: Mheshimiwa Spika, kwanza ninachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa na nzuri aliyoifanya kama Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyosema, kwamba madaraja zaidi ya 81 yameshajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninataka nishauri jambo dogo tu. Watu wamelia sana na barabara nyingi na barabara nyingi ni kweli zimeharibika. Ninawaomba kwanza *TANROADS*, hii biashara ya

barabara zilizokufa kuanza kuziba mashimo, hebu iishe. Kama ni hizo fedha chache Mheshimiwa Waziri zinazopatikana, afadhali hata ijengwe kilometa moja kuliko kuziba mashimo ambayo yanaharibu magari ya Watanzania. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, lazima mrudi kwenye Sheria yetu ya Manunuzi, muiangalie upya Mheshimiwa Waziri. Kwa sababu sheria hizi za kutaja mtu ambaye ni *lowest* ndiyo apewe kazi, ndiyo inatupelekea sisi Watanzania kupata kazi chafu na ambazo hazina ubora. Lazima turudi tuangalie kwenye upande huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitaki kusema sana leo kwa sababu kwanza nimepata bahati, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwamba anakwenda kulijenga lile Daraja la Mto Athumani kutoka Selela – Ngaruka; Ngaruka – Oldoinyolengai; na Oldoinyolengai – Loliondo. Wote waliona fika kipindi fulani lile daraja lilichukua mpaka magari ya wananchi. Juzi nilipokuwa jimboni nimepita nimekuta wataalamu wameshaanza kazi yao nzuri ya upembuzi pale kwa ajili ya ujenzi wa daraja lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, ninajua wameshatangaza *tender* ile ya kilometa 23 kwenda kwenye ujenzi wa Kiwanda cha Magadi kule Selela na Engaruka, basi mkataba usainiwe, ili ile kazi ikaanze. Tuna Barabara ya kilometa 11 kutoka Monduli Mjini kwenda Mfere, kwenda mpaka Monduli Juu kwa Sokoine, naomba ikaanze.

Mheshimiwa Spika, leo siombi lami nyingi, ninataka nimwombe Waziri; wengi wameomba lami, mimi ninaomba barabara za changarawe. Kwa hiyo, nipo tofauti kabisa, ninaomba barabara ya changarawe. Sasa akininyima tena hiyo Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu ananisikia hapa na *TANROADS* wote wananisikia. Ninampongeza sana Meneja wangu wa *TANROADS,* Mkoa wa Arusha, ni meneja msikivu na tunamwomba Mheshimiwa Waziri, tunapomsifia mtu siyo ndiyo umhamishe. Ni meneja msikivu, ukimpigia simu wakati wowote, panapotokea tatizo lolote kwenye barabara zile za vijijini, sekunde amefika. Ni

meneja wa mfano sana Ndugu yetu Masawe, *salute* kwake kwa kazi kubwa anayoifanya ndani ya mkoa wetu.

Mheshimiwa Spika, mimi ninaomba Barabara ya kutoka Monduli Juu – Mfereji; Mfereji – Ol Doinyo Lengai mpaka Engaruka kilometa 123, mimi niwekee changarawe wananchi wangu wapite kwa amani, mimi siombi lami hiyo. Barabara ya kutoka Meserani – Naalarami – NAFCO mpaka Lolkisale na kwenda kukutana na barabara ya kwenda kule kwa wenzetu Simanjiro. Mheshimiwa Waziri aniwekee changarawe ipitike, wananchi wangu waache kupata kero kwa sababu, ndiyo pekee ambayo ninaona wengi hawajaomba.

Mheshimiwa Spika, ninaomba hiyo na ninaamini atakapokuja kusimama hapa ataniambia kilometa 20 hizo ataniwekea changarawe, ili wananchi wangu waendelee kupita niondokane na kero. Mimi lami nitakuja kumwomba huko mbele, kwa sasa ninaomba anitengenezee barabara ya changarawe wananchi wangu wapate *access* ya kuingia na kutoka kwenye maeneo yale.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kwa Mheshimiwa Waziri, kuna mwananchi wangu amefanya kazi na yeye, hebu amwangalie, tangu 2023; *TEMESA*, *Zawadi Company Limited,* hela ndogo sana. Akalipwe hela zake, ni mwananchi, nyumba yake inauzwa na benki!

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninashukuru kwa kunipa nafasi, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ninajua kilometa 22, zinaenda kusainiwa na tunapata lami. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungi anayetujalia uzima na kutujalia amani katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayotufanyia Watanzania. Hakika Rais wetu amefanya mambo mengi na makubwa sana katika Taifa letu. Leo karibu barabara zote kuu zimejengwa kwa kiwango cha lami. Hongera sana. Tuliona kama ni hadithi au ndoto ya mchana kuwa Watanzania tungeweza kusafiri kutoka Mtwara mpaka Kagera kwa kutumia gari ndogo (Toyota Mark II, IST, Corola, Carina na kadhalika). Waheshimiwa Wabunge, ndoto hii leo imekuwa kweli. Tunawashukuru sana viongozi wetu wakuu kwa kazi hii waliyoifanya na wanayoendelea kuifanya.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana vilevile Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya. Wameyapokea maelekezo na maono ya Mheshimiwa Rais na kuyaweka katika vitendo hakika wameitendea haki Wizara hii. Niwapongeze zaidi kwa kuwa wanyenyekevu na wasikivu kwa wananchi na husasani kwa Wabunge, hii imetupa moyo sana.

Mheshimiwa Spika, tunajua bado kuna kazi kubwa ya kufanya, lakini tunasema safari ni hatua kuna siku nchi yetu itakuwa na barabara nzuri kama matamanio ya Watanzania ambayo wangependa.

Mheshimiwa Spika, hii nchi ni kubwa, tuna mtandao mrefu wa barabara zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi ambao wa urefu wa kilometa 37,734.41 hii sio kitu chepesi kwamba tutalala, tuamke tukiwa tumezimaliza barabara zote kwa kiwango cha lami siyo jambo jepesi. Hata hivyo, tunaipongeza Serikali kuona kila sehemu ya nchi ina barabara za lami. Kiasi cha kilometa 12,225.26 zimeshajengwa kwa kiwango cha lami. Hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi ikamilishe barabara kuu zinazounganisha mkoa na mkoa ikiwemo Barabara ya Ipole-Rungwa mpaka Mbeya na Sikonge-Kiloleli-Kipili mpaka Singida. Kujengwa kwa barabara hizo kwa kiwango cha lami unaenda kufungua uchumi wa Mikoa ya Tabora, Singida na Mbeya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, sasa nilete kilio cha wananchi wa Mkoa wa Tabora na hususani wananchi wa Sikonge.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Ipole-Rungwa yente urefu wa kilometa 172.4 ni kati ya barabara kuu *(truck road)* iliyobaki bila kujengwa kwa kiwango cha lami katika Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa barabara hii kwa kiwango cha lami kwa zaidi ya miaka 30 sasa. Aidha, imekuwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi zaidi ya ilani tano na kwa nyakati tofauti tofauti viongozi wetu wakuu wametoa maelekezo ya kuitengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya barabara hii bado haijajengwa. Hata hivyo turejee semi za wahenga wetu kwamba; "yaliyopita si ndwele, tugange yaliyopo." Wana-Sikonge tunampenda sana Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan na yeye anatupenda sana na tunaamini barabara hii ataijenga kabla kipindi chake hakijaisha.

Mheshimiwa Spika, sauti za watangulizi wangu Bungeni; nawashukuru sana watangulizi wangu waliokuwa Wabunge wa Jimbo la Sikonge akuwemo Mheshimiwa Said Juma Nkumba ambaye kwa sasa ni Mwenyekiti wetu wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Tabora. Katika kipindi chake chote cha Ubunge kwa miaka 15 ameisemea sana barabara hii na kuzitamka waziwazi faida za kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, vilevile Mheshimiwa George Joseph Kakunda, katika kipindi chake cha miaka 10 amepaza sauti sana kuhusu ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Spika, ni nani sasa aje aisemee barabara hii ndiyo ijengwe? Mheshimiwa Waziri, nikukumbushe maandiko matakatifu kutoka Kitabu cha Injili ya Luka Mtakatifu Sura ya 16:19 – 31 kwa kifupi; "Ni habari ya Tajiri, Lazaro na Nabii Ibrahimu. Kwamba Tajiri alipoona mbinguni kuna moto mkali sana

alimwomba Nabii Ibrahimu atume watu kutoka mbinguni ili wakawaambie ndugu zake waliokuwa duniani kuwa waache dhambi, wasije wakapata mateso kama yeye aliyokuwa anayapata. Nabii Ibrahimu akamwambia wasipokuwasikiliza." Mwisho wa maneno matakatifu.

Mheshimiwa Spika, Waziri Ulega ni msikivu nina hakika ataitendea haki barabara hii na hana sababu ya kumsubiri malaika kutoka mbinguni kwa ajili ya ujumbe wa barabara hii.

Mheshimiwa Spika, nina imani sana na Mheshimiwa Waziri kwa sababu ameshaahidi kuitembelea barabara hii mara baada ya Bunge hili ili kuwasikiliza wananchi wahanga wa barabara hii wakiwemo Kata za Ngonywa, Kitunda, Kiloli, Kilumbi, Kipili na wenzao wa Singida na Mbeya. Hii inanipa matumaini sana kwamba sasa Rais wetu Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan anaenda kuandika historia nyingine ya kutujengea barabara yetu hii hata kabla ya kipindi chake kuisha.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mungu wa mbinguni awaongoze katika kutafuta fedha ya barabara hii na barabara zingine za Watanzania wenzangu ili tuzidi kuwakumbuka katika historia ya maisha ya Wanasikonge na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, barabara hii ni ufunguo wa uchumi katika mikoa ya Tanzania pamoja na nchi jirani na hususani nchi za Maziwa Makuu. Barabara ya Ipole - Rungwa inaunganisha Mkoa wa Tabora na Mikoa ya Mbeya na Singida. Hivyo kujengwa kwa barabara hii kwa kiwango cha lami itawezesha wafanyabiashara wa Tabora, Mbeya na Singida kufanya biashara zao kwa urahisi na ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Tabora tuna mazao mengi ya misitu ikiwemo asali na mbao, lakini tuna mazao ya kilimo yakiwemo mahindi, karanga, mpunga na kadhalika ambayo tungependa kuyauza Mikoa ya Kati na ya Nyanda za Juu Kusini na hata nje ya nchi ikiwemo Malawi, Zambia na hata Afrika Kusini. Hii itawezekana tu kama barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo juu kuwa barabara hii (Ipole-Rungwa) inatoa wepesi na kupunguza gharama za usafiri wa wananchi wa Mikoa ya Kanda ya Ziwa ikiwemo Shinyanga, Mwanza, Mara, Geita, Kagera na Kigoma. Kwa vile wanaposafiri kwenda Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na watalazimika kupitia Dodoma - Iringa hadi Mbeya kwani *route* hii ina urefu kilometa 970, lakini kama kipande cha Barabara ya Ipole - Rungwa kitajengwa kwa kiwango cha lami umbali wa Tabora hadi Mbeya ni kilometa 562 tu; tofauti ya kilometa zaidi ya 400. Hivyo watapunguza muda, uchovu wa safari na kupunguza gharama za mafuta.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika wasafiri kutoka nchi jirani za Rwanda, Burundi DR Congo na kadhalika wanaosafiri kwenda Kusini mwa Afrika watatumia barabara hii kwa sababu nilizozisema hapo juu. Tunaomba Serikali ione haja ya kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Sikonge – Kiloleli – Kipili; wananchi wa Sikonge wanatambua majibu ya Serikali wakati wa majibu ya Swali Namba 81 pamoja na swali la nyongeza. Majibu ya Serikali ni kwamba Serikali itaanza kuifanyia barabara hiyo upembuzi yakinifu ili kuona namna ya kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Wana-Sikonge wanaomba kuona sasa watalaam wanaanza kuifanyia barabara hiyo upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu; kama nilivyosema hapo juu, nchi yetu ni kubwa na inahitaji fedha nyingi kukamilisha ujenzi wa barabara zetu kwa kiwango cha lami. Mheshimiwa Waziri kuna watu huko duniani wana fedha nyingi sana na wanatafuta mahali pa kuziwekeza. Mimi nashauri kaeni na Wizara ya Fedha ili muingie makubaliano na wenye fedha duniani kuwa watujengee barabara zote kwa makubaliano kuwa kila mwaka tutawalipa sehemu ya fedha zinazotengwa kwa ajili ya barabara; tuseme angalau shilingi trilioni moja kwa mwaka ambazo ni sawa na wastani *USD million 400* zinazotokana na bajeti yako, watakubali tu! Hii itafanya changamoto za barabara kuisha na wananchi wetu watakuwa na barabara nzuri na deni lao tutalilipa kwa namna tutakavyokubaliana na wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

MHE. SHAFFIN A. SUMAR: Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalamu wote Wizarani kwa kazi nzuri mnayoifanya.

Mheshimiwa Spika, nashauri tuongeze kidogo tozo kwenye mafuta, lakini pia tozo ambazo zimekuwepo zipatikane kwa wakati. Kuna utaalam mpya na wenye gharama nafuu unatumika *South Africa* ambao tukiutumia itasaidia sana kuziba mashimo barabarani kwa gharama nafuu. Wizara ifanye juhudi za kuujua na kuujaribisha katika barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, tuombe mkopo wenye gharama nafuu kutoka kwa *African Development Bank* mahsusi kwa ajili ya barabara zetu na kiwango cha lami kiwe na maisha zaidi ya miaka 15.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana kuna ahadi ya Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba Wilaya ya Uyui barabara iliyopo chini ya *TARURA* kutoka Magiri kupitia Nsimbo kufika Kigwa kilometa 27 itapandishwa hadhi kuwa chini ya *TANROADS* na kujengwa kwa kiwango cha lami. Ninaomba sana tulinde heshima ya Rais.

Mheshimiwa Spika, jimbo langu la Uyui, Tabora limepata stesheni ya *SGR* kwenye Kata ya Nzubuka, ninaomba Wizara ipandishe hadhi barabara ya kutoka Nzubuka kuja Tabora Mjini na ijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, ninaomba barabara ya kutoka Tabora Mjini – Mambali - Bukumbi mpaka Kahama iko chini ya *TANROADS* naomba itengewe bajeti ya kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, ninaomba barabara ya kutoka Tabora Mjini kuelekea Ulyankulu ina muda mrefu inaahidiwa lami, lakini haijawahi kutengewa bajeti hata mwaka huu wa fedha

haijapangiwa bajeti, naomba nisaidiwe maana wananchi waliiamini CCM kwa ahadi hizi.

Mheshimiwa Spika, kuna ahadi ya Rais wetu ya mwaka 2020 alipokuwa Mgombea Mwenza kwamba barabara ya kutoka Mwigelezi mpaka Mabama Centre kilometa tatu ambayo iko chini ya *TARURA* itajengwa kwa lami, lakini kwa kuwa *TARURA* haina bajeti ya kutosha, naomba Wizara ichukue hiyo dhamana ya kukamilisha ahadi ya Rais wetu kabla ya mwaka 2030 ili asibakie na deni ambalo litampatia doa mpendwa Rais wetu.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

MHE. EDWIN E. SWALLE: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kuunga mkono bajeti hii ya Ujenzi. Pili, nitumie nafasi hii kuipongeza sana Serikali na kipekee Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ya kutoa kipaumbele katika kuboresha miundombinu ya usafirishaji nchini ikiwemo barabara, vivuko, meli, viwanja vya ndege na ununuzi wa ndege.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Njombe ni mkoa wenye mvua nyingi sana kwa mwaka, hivyo changamoto ya usafiri hasa barabara ni kubwa sana. Tunaiomba Serikali kutoa kipaumbele kwa kutenga na kuongeza ukubwa wa bajeti ya kutosha kwa ajili ya barabara za Mkoa wa Njombe ili wananchi wetu waweze kusafiri kwa wakati na kusafirisha mazao ya chakula na biashara kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, aidha wananchi wa Jimbo la Lupembe wanaimba kujua ni lini Barabara ya Kibena - Lupembe hadi Madeke kilometa 126, itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami. Barabara hii ilitangazwa *tender* ya ujenzi tarehe 12 Februari, 2025 kwa kuanza na kilometa 42 (Kibena hadi Kidegembye), hata hivyo hadi leo mkataba huo haujasainiwa.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali iharakishe kusaini mkataba wa ujenzi wa barabara hii ili kuwanusuru wananchi

hawa na adha ya usafiri katika barabara hii kwani barabara hii ni muhimu kwa uchumi wa Mikoa ya Njombe na Morogoro hadi Tanga kupitia Kilosa. Aidha, barabara hii itafungua uchumi na uwekezaji mkubwa kwa Mkoa wa Njombe na Morogoro na kuchangia Pato la Taifa kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

MHE. LUCY D. S. KOMBANI: Mheshimiwa Spika, ninapenda kushukuru kwa nafasi hii ya kuweza kuwasilisha mchango wangu katika bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Morogoro, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuona umuhimu wa ku-*support* miundombinu katika mkoa wetu, hili kwetu ni kubwa sana kwani limekuwa linaturahisishia kwenye masuala mbalimbali hasa ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nishukuru kwa juhudi nzima ya kujumuisha mradi wa Barabara ya Nachingwea-Liwale-Ilonga-Mwaya-Mahenge (kilometa 345) kwenye mpango wa bajeti wa mwaka 2026/2027, mradi ambao utakapokamilika utaunganisha Mkoa wa Lindi na Morogoro, jambo ambalo Wana-Morogoro tunategemea kunufaika kwenye mahusiano ya kilimo hasa kwenye mazao ya korosho na ufuta na pia muunganiko wa kimasoko katika mazao hayo.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kushukuru pia kwa kutambua umuhimu wa Barabara ya Kidatu-Ifakara-Lupiro-Malinyi-Londo-Lumecha/Songea (kilometa 499) (ukurasa wa 29). Barabara hii inaenda kusaidia siyo tu wananchi wa Malinyi, bali inaenda kurahisisha mahusiano ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi wa Songea, kwa kurahisisha usafiri wa wananchi pamoja na mazao.

Mheshimiwa Spika, pia kwa sasa hospitali kubwa ya rufani ambayo inafanya matibabu hadi ya kansa inapatikana Ifakara, hii itawarahisishia wananchi wa mikoa ya jirani kusafiri kwa urahisi

na kupata matibabu kwa amani hasa pale wanapotakiwa kurudi mara kwa mara kwenye kliniki za *Chemotherapy*.

Mheshimiwa Spika, maombi yangu; Barabara ya Lupiro kuelekea Mahenge ambayo ni kilometa 40 tu ambayo ina milima na kona nyingi sana. Barabara hii imekuwa haipitiki kipindi cha masika jambo ambalo limekuwa likikwamisha sana shughuli mbalimbali za kijamii na za kiuchumi. Wilaya ya Ulanga imekuwa ikitegemea Ifakara kwenye mahitaji ya bidhaa mbalimbali ikiwa bidhaa za chakula, dawa, hata matibabu ya rufani na *operation* wananchi wa Ulanga wamekuwa wakitegemea kupata Ifakara.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi haya mahitaji yamekuwa ni magumu kupatikana kwani barabara zinakuwa hazipitiki hasa pale magari yanapokwama njiani hata siku tatu. Wilaya ya Ulanga imekuwa na utajiri mkubwa wa madini na pia wawekezaji wamekuwa wakishindwa kufika huko kwa kipindi chote cha masika. Wizara tunaomba muangalie hili jambo kwa ukaribu kwani tunaamini kama barabara itajengwa kwa kiwango cha lami na wawekezaji wataongezeka huko.

Mheshimiwa Spika, ombi la pili; hotuba imeainisha barabara ya Ifakara – Kihansi – Mlimba – Madeke – Kibena (kilometa 346.43); Ifakara – Mlimba (kilometa 62.5) na Mbingu - Chita JKT (kilometa 37.5) kwamba maandalizi ya kuanza kazi yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, tunaomba majibu ya lini hii kazi itaanza kwani kwa mhandisi kujiandaa tu, tutashindwa kufuatilia hili jambo kwani hakuna *time frame* ambayo Wizara imeji-*commit* kwenye hili jambo.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia napenda kuunga mkono hoja.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna Serikali ya Awamu ya Sita inajitahidi kuwekeza kwenye miundombinu ya barabara na sekta ya usafirishaji kwa ujumla, tumeona kuwa katika Awamu ya Sita imeweza kujenga

kilometa 1,495.45 ambapo inafanya jumla ya mtandao wa barabara za lami kuwa jumla ya kilometa 12,225.6 na kubakiza kilometa 25,508.8. Hii ni hatua kubwa sana ikiwa ni pamoja na ujenzi wa madaraja makubwa na ya kimkakati katika kujenga uchumi imara.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa Barabara ya Tarime - Mugumu kwa viwango vya kimkakati; baada ya pongezi naomba kuzungumzia Barabara ya Tarime – Mugumu kama kichocheo cha uchumi na utalii. Barabara ya Tarime – Mugumu isiangaliwe kama Mradi wa Mkoa wa Mara pekee, bali kama *strategic economic corridor* inayounganisha biashara, madini, utalii na usafirishaji katika ukanda wa Kaskazini. Hivyo lazima Serikali ione umuhimu wake kwa utalii wa Serengeti, usafirishaji wa madini, biashara ya mipakani na mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, miundombinu yenye tija ni ile inayozalisha uchumi, siyo inayounganisha maeneo pekee. Kwenye hotuba ibara ya 50 imeonesha hii barabara yenye kilometa 87.14 ni kipande cha Mogabiri hadi Nyamongo chenye kilometa 25 ndio pekee kimejengwa kna utekelezaji upo asilimia 61 tu. Lakini kipande cha Tarime Mjini hadi Mogabiri chenye kilometa 9.3 ni kimeharibika sana na mkandarasi ameshatoa *certificate* ya shilingi bilioni 7.99 lakini Serikali hadi leo haijapeleka fedha na iliahidi kupeleka fedha kabla ya mwaka huu wa fedha wa 2025/2026 kuisha.

Mheshimiwa Spika, hii barabara imepoteza maisha ya Watanzania wengi ikiwemo Diwani Philip, mfanyakazi wa halmashari na wengine wengi. Vilevile imesababisha ulemavu kwa wananchi wengi na kupunguza nguvu kazi ya Taifa letu, lakini pia kuna kipande cha Nyamongo hadi Mugumu chenye kilometa 48.15 na ile barabara ya mzunguko pale Mugumu yenye kilometa 3.6. Kwa masikitiko makubwa ibara ya 251 inaonesha hii barabara imetengewa shilingi bilioni saba tu kwa mwaka 2026/2027. Hii sio sawa, labda kama kuna fedha zinatoka kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha.

Mheshimiwa Spika, Serikali itambue kuwa barabara hii siyo tu ya wananchi wa Mara, bali ni mhimili wa biashara, utalii na usafirishaji kuelekea ukanda wa Serengeti. Kukamilika kwake kutapunguza gharama za usafiri, kuongeza mapato ya utalii na kurahisisha usafirishaji wa mazao na madini na mapato yatakayopatikana yatatumika kujenga barabara na miundombinu mingine kwenye maeneo ya kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madeni ya wakandarasi na athari kwa mfumo wa fedha wa ndani; kuchelewa kulipa wakandarasi wa ndani ni sawa na kuondoa ukwasi kwenye mzunguko wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, madhara ya kutolipa kwa wakati hupelekea wakandarasi hushindwa kulipa benki, riba huongezeka, ajira hupotea, gharama huongezeka kupitia *penalt* na riba na miradi kuchelewa kukamilika.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuepuka haya kuwepo na *Escrow/Payment Guarantee System, Predictable Payment Mechanism* au mfuko maalum wa kulipa madai ya miradi iliyokamilika.

Mheshimiwa Spika, kupunguza mikopo yenye riba kubwa katika miradi ya ujenzi; Taifa linaweza kujenga barabara kwa gharama nafuu, lakini likaingia hasara kupitia gharama kubwa za fedha za mikopo. Baadhi ya mikopo ya miradi ya miundombinu ina gharama kubwa za riba ambazo zinaongeza deni la Taifa bila sababu. Hivyo napenda kuishauri Serikali kuongeza matumizi ya *PPPs, infrastructure bonds, concesional financing* na mifuko ya ndani ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kuna wakati Taifa haliumizwi na gharama ya ujenzi, bali gharama ya fedha iliyokopwa kujenga. Hivyo ni vyema tuweze tumia *concesional financing, infrastructure bonds, PPP* na matumizi ya *local pension funds.*

Mheshimiwa Spika, *sustainability* ya deni la Taifa haitegemei ukubwa wa mkopo pekee, bali gharama ya fedha yenyewe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *maintenance economy* - kulinda miundombinu Iliyojengwa; tumejikita sana kwenye kujenga, lakini bado hatujawekeza vya kutosha kwenye uchumi wa matengenezo ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, ninashauri Serikali ione umuhimu wa *preventive maintenance,* matumizi ya teknolojia, *drainage systems* na *asset management systems.* Lazima tujue barabara nyingi haziharibiki kwa uzito wa magari pekee, bali kwa kukosekana kwa mfumo endelevu wa matengenezo.

Mheshimiwa Spika, hatua ya maendeleo ya Taifa lolote huonekana kwanza kwenye ubora wa miundombinu yake. Hata hivyo, miundombinu bora siyo ile inayojengwa kwa kasi pekee, bali ile inayojengwa kwa tija, inalindwa kwa weledi na inachochea ushindani wa uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya barabara inahitaji *maintenance,* lakini kuna changamoto ya kutolipwa Mfuko wa Barabara. Hasara ya kutotoa fedha hizi ni kubwa na zipo kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, ushauri zingatieni sheria, hakikisheni fedha hizi za mfuko zinatumika kadri zinavyokusanywa.

Mheshimiwa Spika, tunajisifu mafanikio ya bandari, lakini siri kubwa ya mafanikio haya ni Mfuko wa Huduma ya Bandari ambapo *TPA* anaruhusiwa kukusanya pesa na kumuwezesha kutekeleza miradi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wakandarasi wazawa kupewa kipaumbele kwenye miradi mikubwa ya ujenzi; wakandarasi wazawa wanakopa kwenye mabenki yetu kwa riba kubwa sana ukilinganisha na gharama ya fedha wanayoipata wakandarasi wa nje kutoka taasisi za kifedha za kimataifa. Jambo la kujiuliza ni hili, Serikali inapochelewa kuwalipa wakandarasi wa nje, madai yao yanaendelea kuongezeka kupitia *interest charges* na *contractual penalties,* wakati kwa wakandarasi wazawa wanapochelewesheshewa malipo huishia kulipwa *contractual*

penalties bila *interest charges.* Hii sio sawa na hudhoofisha wakandarasi wazawa na hata kupelekea kufilisika.

Mheshimiwa Spika, hivyo Taifa hupata *double financial exposure;* kwanza kupitia gharama kubwa za fedha kwa wakandarasi wazawa na pili kupitia *escalation* ya madai ya wakandarasi wa nje kutokana na kucheleweshwa kwa malipo na ikizingatiwa kuwa wakandarasi wa nje miradi yao ina gharama kubwa zinazotokana na mikataba yao hususani pale miradi inapofadhiliwa kwa mikopo yenye riba kubwa na masharti ya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa mapendekezo yafuatayo:-

(i) Serikali iweke mfumo wa *prompt payment* kwa wakandarasi ili kuzuia *escalation* ya *claims* na riba.

(ii) Benki za maendeleo na taasisi za fedha ziweke *special infrastructure financing window* kwa wazawa yenye riba nafuu.

(iii) Miradi mikubwa iwe na kiwango cha lazima cha ushiriki wa wakandarasi wazawa.

(iv) Serikali ifanye *contract risk assessment* kabla ya kuingia mikataba yenye *penalty clauses* kubwa.

(v) *Contractors Assitance Fund (CAF)* iongezewe kiwango toka dhilingi bilioni nne hadi walau shilingi bilioni 500.

Mheshimiwa Spika, ulinzi wa wakandarasi wazawa si suala la upendeleo bali ni mkakati wa kulinda mtaji wa ndani, ajira za Watanzania na uthabiti wa kifedha wa taifa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, lazima ujenzi wa barabara uendane na kasi ya maboresho ya bandari na ujenzi wa reli tunaona vituo vya *SGR* vimekamilika, *SGR* inafanya kazi, lakini hakuna barabara au zipo finyu. Hivyo kasi ya reli na barabara

zisipishane na kuna maeneo *TANROADS* ifanye kazi mgongoni mwa *TRC* kutokana na changamoto ya kifedha, kama kuna sehemu tunahitaji kuendeleza reli hatuna budi kuchagua wapi zitakutana na sio lazima zi-*run in parallel.*

Mheshimiwa Spika, katika hili tunawapongeza sana Uchukuzi kwa kuunganisha matumizi ya *SGR* bandarini mpaka Bahi na *MGR* toka Bahi mpaka Isaka. Sasa kutoka Isaka ni barabara, kwa mfumo huu itawezekana kuokoa barabara za Dar es Salaam - Morogoro - Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. RAMADHANI H. SINGANO: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa wasaa wa kuchangia katika Wizara ya Ujenzi kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati ya moyo wangu nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu kipenzi Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, kwa mapenzi makubwa naipongeza Wizara ya Ujenzi hasa Waziri Mheshimiwa Abdallah Hamisi Ulega pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya. Nawapongeza pia watumishi wote wa Wizara ya Ujenzi kuanzia Katibu Mkuu *Engineer* Balozi Aisha Amour, pamoja na Naibu Katibu wake.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nawapongeza kwa umakini mkubwa wa Mtendaji Mkuu wa *TANROADS* na *TBA* na watumishi wote katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, pongezi hizi kwa Wizara ni kwa sababu ya maandalizi makini ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi yenye maono, iliyoandaliwa kwa weledi na inayoakisi mahitaji halisi ya kila Mtanzania katika maeneo mengi nchini.

Mheshimiwa Spika, muhtasari wa ushauri wa jumla kwa Wizara ya Ujenzi juu ya changamoto mbalimbali za barabara Tanzania; Wizara ya Ujenzi ina jukumu muhimu katika maendeleo

ya miundombinu ya Taifa kupitia ujenzi wa barabara, madaraja, vivuko na usimamizi wa sekta ya ujenzi. Kupitia shughuli zake, Wizara hutekeleza mahitaji mbalimbali ya wananchi lakini pia hukutana na changamoto tofauti zinazohitaji suluhu maalum.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mahitaji ya Watanzania; Wizara hutekeleza mahitaji ya wananchi kwa njia zifuatazo; ujenzi na ukarabati wa barabara za mijini na vijijini; ujenzi wa madaraja na vivuko kwa ajili ya kurahisisha usafiri; kuboresha usafirishaji wa mazao, biashara na huduma za jamii; kukuza ajira kupitia miradi ya ujenzi; kusimamia ubora wa miundombinu na viwango vya ujenzi; na kuunganisha maeneo mbalimbali ya nchi kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, changamoto na suluhu zake; nianze na changamoto ya upungufu wa fecha; miradi mingi ya ujenzi huhitaji fedha nyingi, lakini mara nyingi bajeti huwa haitoshi kukidhi mahitaji yote ya ujenzi na matengenezo ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, suluhu ni kwa Serikali kuongeza bajeti ya sekta ya ujenzi; kutafuta mikopo na misaada ya maendeleo; kuvutia wawekezaji binafsi kupitia ubia kati ya Serikali na sekta binafsi *(PPP);* na kusimamia vizuri matumizi ya fedha za miradi.

Mheshimiwa Spika, pili, changamoto ya kuongezeka kwa gharama za ujenzi; kupanda kwa bei za vifaa vya ujenzi, mafuta na usafirishaji huongeza gharama za miradi.

Mheshimiwa Spika, suluhu ni kuimarisha matumizi ya vifaa vya ndani; kupunguza utegemezi wa vifaa vya kuagiza nje; kutumia teknolojia za kisasa zinazopunguza gharama; na kufanya mipango sahihi ya manunuzi mapema.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya uharibifu wa barabara na madaraja; mvua kubwa, mafuriko, magari yenye uzito mkubwa na ukosefu wa matengenezo husababisha uharibifu wa miundombinu.

Mheshimiwa Spika, suluhu ni kwa kufanya matengenezo ya mara kwa mara; kujenga mifereji bora ya maji; kudhibiti magari yenye uzito kupita kiasi kupitia mizani; na kutumia viwango bora vya ujenzi vinavyohimili hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya msongamano wa miji na foleni; ukuaji mkubwa wa miji unasababisha barabara kuwa finyu na kuongezeka kwa foleni.

Mheshimiwa Spika, suluhu ni kupanua barabara za mijini; kujenga barabara za mizunguko *(bypass);* kuboresha mipango miji; na kuimarisha mifumo ya usafiri wa umma.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya viashiria vya rushwa na usimamizi hafifu; baadhi ya miradi huathiriwa na matumizi mabaya ya fedha, kucheleweshwa kwa kazi au ubora duni.

Mheshimiwa Spika, suluhu ni kuongeza uwazi katika zabuni za miradi; kuimarisha ukaguzi wa miradi; kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya wahusika wa rushwa; na kutumia mifumo ya kidigitali katika usimamizi wa miradi.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya upungufu wa wataalamu na teknolojia; baadhi ya maeneo yana uhaba wa wahandisi, mafundi na vifaa vya kisasa vya ujenzi. Hivyo suluhu ni kuongeza mafunzo ya kitaalamu kwa wahandisi na mafundi; kuimarisha vyuo vya ufundi na teknolojia; kuwekeza katika vifaa na teknolojia za kisasa; na kutoa ajira na motisha kwa wataalamu wa ndani.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya mabadiliko ya tabianchi, mvua kubwa na mafuriko huharibu barabara na madaraja mara kwa mara, kwa hizo basi suluhu ni kujenga miundombinu inayohimili mabadiliko ya tabianchi; kuboresha mifumo ya mifereji ya maji; kutumia usanifu wa kisasa unaozingatia mazingira; na kufanya tathmini za mazingira kabla ya utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; Wizara ya Ujenzi ina mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa kwa kuboresha miundombinu na kurahisisha shughuli za kijamii na kiuchumi. Hata hivyo, ili kuongeza ufanisi wake, ni muhimu kuendelea kutatua changamoto zinazojitokeza kupitia uwekezaji, usimamizi bora, matumizi ya teknolojia na kuimarisha wataalamu wa ndani.

Mheshimiwa Spika, muhtasari wa ushauri wa njia za kuongeza mapato pamoja na kuboresha ili kuongeza ufanisi wa Mfuko wa Barabara Tanzania ni pamoja na tozo ya mafuta *(fuel levy);* tozo inayowekwa kwenye mafuta. Chanzo kikuu cha fedha za matengenezo ya barabara. Watumiaji wa barabara huchangia kupitia matumizi ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, pili, ni tozo ya mawasiliano (mfano shilingi 100); kiasi kidogo kinachokatwa kwenye huduma za mawasiliano husaidia kuongeza vyanzo vya mapato ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, tatu, ni *PPP – Public Private Partnership;* ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi; sekta binafsi hushiriki kujenga, kufadhili, kuendesha au kutunza barabara. Hupunguza mzigo wa serikali kwenye uwekezaji mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nne, ni Hati Fungani *(Infrastructure Bonds);* Serikali hukopa fedha kutoka kwa wananchi au taasisi kupitia *bonds.* Fedha hutumika kujenga au kuboresha miundombinu na hulipwa baadaye kwa riba.

Mheshimiwa Spika, njia nyingine za kuongeza mapato ya barabara ni pamoja na *road tolls* (ada za matumizi ya barabara); watumiaji hulipia kutumia barabara maalum na hutumika sana kwenye *express-ways,* madaraja na *highways.* Mfumo unaweza kuwa wa *electronic tolling.*

Mheshimiwa Spika, pPia *vehicle licensing & road user charges* (ada za leseni za magari na matumizi ya barabara); magari mazito huchangia zaidi kutokana na uharibifu mkubwa wa barabara.

Mheshimiwa Spika, kuna *betterment levy* (tozo kwa maeneo yaliyoongezeka thamani kutokana na mradi wa miundombinu) kwa mfano barabara mpya, kuongeza thamani ya viwanja na biashara. Aidha, kuna *property tax* maalum (kodi maalum) kwenye maeneo yanayonufaika moja kwa moja na mradi wa barabara. Fedha huelekezwa kwenye mradi husika.

Mheshimiwa Spika, *road assets monetization* (kutengeneza mapato kupitia mali za barabara) kwa mifano *billboards, parking, service areas, utility corridors.* Pia *utility corridor leasing* (kukodisha maeneo ya *road reserve* kwa *fiber optic,* mabomba, nyaya za umeme, *telecom infrastructure* hupunguza uchimbaji holela wa barabara.

Mheshimiwa Spika, *parking concessions* (kampuni binafsi kupewa haki ya kusimamia *parking);* Serikali hupata sehemu ya mapato. Hii huboresha ukusanyaji,usimamizi, *traffic flow*.

Mheshimiwa Spika, *freight & logistics levy* (tozo kwenye usafirishaji wa mizigo); *transit cargo* na malori makubwa huchangia zaidi.

Mheshimiwa Spika, aidha kuna *congestion pricing* (ada kwa magari yanayoingia maeneo yenye msongamano mkubwa - *CBD)*. Hii hupunguza foleni, uchafuzi na *pressure* kwenye barabara.

Mheshimiwa Spika, kuna *green financing/climate funds* (kupata fedha za kimazingira) kwa mfano *flood-resistant roads, drainage, and climate resilient infrastructure,* njia za kuboresha tija ya matumizi ya fecha, barabara zinazohimili mafuriko, *climate change, drainage improvements,* zinaweza kupata fedha kupitia *climate adaptation funds, green infrastructure financing, development banks* na *digital systems.*

Mheshimiwa Spika, ninashauri haya yaangaliwe kwa jicho la kitaalamu na kuona namna ya kuyafanya au kuyaboresha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *electronic tolling, smart parking, digital procurement, asset management systems and road maintenance endowment/sovereign infrastructure fund* sehemu ya madini, gesi, bandari, *transit trade,* iwe inaingia moja kwa moja kwenye *infrastructure reserve fund* ya muda mrefu. Nchi nyingi hutumia *resource revenues* kufadhili miundombinu ya kudumu.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya ushauri wa kuleta tija katika matengenezo ya barabara nchini ni pamoja na *preventive maintenance* (kufanya matengenezo mapema kabla ya barabara kuharibika sana), hii hupunguza gharama kubwa za *reconstruction.*

Mheshimiwa Spika, kwenye *performance-based contracts* (wakandarasi hulipwa kulingana na ubora wa huduma na matokeo), hii hupunguza pressure kwa barabara; kuimarisha reli, usafiri wa maji, *logistics alternatives* na hupunguza uharibifu wa *roads* na gharama za *maintenance.*

Mheshimiwa Spika, uwiano bora wa rasilimali za uhandisi *engineer:technician:artisan = 1:5:25;* hii ina maana ifuatavyo;

(i) *Engineer* (Mhandisi) mmoja.

(ii) *Technician* (Fundi Sanifu) watano.

(iii) *Artisan* (mafundi) 25.

Mheshimiwa Spika, uwiano huu hupendekezwa kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya miundombinu nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

MHE. TINNAR A. CHENGE: Mheshimiwa Spika, naomba niwasilishe mchango wangu kwenye hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwa kazi kubwa inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini

ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuboresha miundombinu ya barabara. Niishukuru Serikali kwa kutujengea barabara ya lami kutoka Lamadi, Bariadi, Itilima, Maswa hadi Mwigumbi ambayo inaunganisha Makao Makuu ya Mkoa wa Simiyu na Makao Makuu ya Mikoa ya Mara na Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukrani hizi niombe Wizara ione namna ya kuiimarisha barabara hii kwani ina mashimo mengi kwa sasa na huharibika mara kwa mara. Barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa Mkoa wa Simiyu na mikoa ya jirani ya Kanda ya Ziwa hasa ikizingatiwa kuwa Mkoa wa Simiyu ndio mzalishaji mkubwa wa zao la pamba (51%+ ya pamba inazalishwa simiyu).

Mheshimiwa Spika, sera ya Serikali ni kuunganisha makao makuu ya kila mkoa Tanzania Bara na makao makuu ya kila mkoa jirani kwa barabara ya lami. Wakati Simiyu ikiwa sehemu ya Mkoa wa Shinyanga, Mkoa wa Shinyanga ulikuwa uunganishwe na mikoa ya Mara kupitia Mwigumbi, Maswa, Bariadi na Lamadi na tayari kipande hiki kimekamilika, japo kinahitaji ukarabati wa hali ya juu. Barabara hii ni muhimu sana hasa kwa wafanyabiashara wa Mkoa wa Mara wanaohitaji kupeleka bidhaa zao makao makuu ya nchi yetu (Dodoma) na Mkoa wa Dar es salaam, kwani hawatahitaji kuzungukia Mwanza – Shinyanga. Njia hii ni fupi kwao kwani wakitoka Musoma wanapita Lamadi - Bariadi - Maswa Shinyanga - Singida – Dodoma – Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, hapo awali kuunganisha Mkoa wa Shinyanga na arusha kiunganishi ilikuwa ni kupitia Kolandoto – Mhunze – Lalago – Mwanhuzi – Sibiti- Matola – Mangola - Oldean Kisha – Mto wa Mbu – Makuyuni - Arusha. Ahadi ya kujenga barabara ya Kolandoto - Oldean imekuwa kwenye bajeti ya Serikali tangu Awamu ya Pili lakini mpaka tunavyozungumza bado haijajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali yangu sikivu ikamilishe ujenzi wa barabara hii muhimu ili kujenga imani kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianza kwanza na ujenzi wa Daraja la Mto Sibiti ambalo lilikamilika wakati wa Awamu ya Tano tayari Simiyu ikiwa ni mkoa unaojitegemea, ili kurahisisha mawasiliano. Baada ya Simiyu kuwa mkoa, kiunganishi na Mkoa wa Singida ni kutoka Bariadi - Lagangabilili - Mwanhuzi – Sibiti – Iguguno - Singida.

Mheshimiwa Spika, niombe sana Serikali yangu sikivu ione umuhimu wa kujenga barabara hii muhimu sana kwa uchumi wa hii mikoa miwili na hasa ukuzingatia kuwa ndio *shortcut* ya kufika Dodoma makao makuu ya nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa Mkoa wa Arusha kiunganishi ni Bariadi - Mwanhuzi – Matola - Mangola – Oldean – Arusha. Hivyo basi kwa Simiyu na Shinyanga bado barabara ya Kolandoto - Mwanhuzi- Sibiti – Mangola – Matola – Oldean – Arusha ni muhimu sana kwa uchumi wa mikoa hii mitatu. Hapa katikati kulikuwa na hoja ya wafadhili kutoafiki Mkoa wa Mara kuunganishwa na Mkoa wa Arusha kupitia Mbuga ya Wanyama ya Serengeti. Wafadhili walikuja na hoja kuwa Mkoa wa Mara kiunganishi kiwe barabara kutoka Oldean – Mangola – Matola – Sibiti – Mwanhuzi – Lalago – Maswa – Bariadi - Lamadi kwa maana ya *Serengeti Southern Bypass.*

Mheshimiwa Spika, ninaomba niunge mkono hoja hii kwa manufaa ya kulinda utajiri wa mbuga yetu ya Serengeti ambayo ina vivutio vya utalii kama vile *migration* ya wanyama kuelekea Kenya, Masai Mara. Kivutio adimu duniani kinachochochea utalii, na ni moja ya *World Heritage Sites.* Barabara hii ya *Serengeti Southern Bypass* ni muhimu kwa uchumi wa mikoa hii hvyo niiombe Serikali yangu sikivu iendelee kutenga pesa za ujenzi wa barabara hii kadri bajeti itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, ninatambua na kuheshimu mawazo ya wenzetu wa Mkoa wa Manyara unaotaka barabara ya kuunganisha Mara na Arusha isianzie Oldean bali ishuke kidogo kuelekea Karatu – Mbulu – Dongobeshi - Hydomu -Matola – Sibiti – Lalago – Maswa (badala ya Oldean – Mangola – Matola) na hapa niipongeze Wizara kwani kwenye bajeti hii nimeona kuna

ujenzi wa kiwango cha lami barabara kutoka Karatu – Mbulu – Hydom – Sibiti – Lalago – Maswa (kilometa 389).

Mheshimiwa Spika, pia kuna maandalizi ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Kolandoto – Kishapu – Lalago. (kilometa 64), lakini pia barabara ya Lalago – Ngoboko – Mwanhuzi (kilometa 74), na Iguguno Shamba – Mnolo (kilomita10). Hapa naomba kipande hiki kije kiunganishwe sasa na Mwandoya (Kisesa) – Lagangabilili – Bariadi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia nipongeze ujenzi wa Daraja la Simiyu ambalo limekamilika kwa 73% na hivyo basi kurahisisha ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine muhimu na ambayo ni *shortcut* ya kuunganisha Makao Makuu ya Mkoa wa Simiyu na Mkoa wa Mwanza ni barabara kutoka Bariadi - Ngulyati, Salama - Magu.

Mheshimiwa Spika, barabara hii ni muhimu sana, sio kiuchumi tu, bali pia katika kuokoa maisha ya wagonjwa mahututi wanaokimbizwa Hospitali ya Bugando katika jitihada za kuokoa maisha ya wagonjwa hawa. Hivyo kadri bajeti itakavyoruhusu niiombe Serikali ione umuhimu wa kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine muhimu pia ni ya kutoka eneo la Dutwa - Ngasamo – Nyashimo; eneo la Dutwa lina madini ya *nickel* na dhahabu pia. Barabara hii itafungua uchumi wa wananchi wa maeneo haya na kukuza pato binafsi, lakini pia pato la Taifa litakalotokana na tozo za madini haya.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ujenzi wa reli ya kisasa *(SGR)* unapita katika eneo la Malampaka, Jimbo la Maswa Magharibi, na kwa kuwa eneo hilo panatarajiwa kujengwa bandari kavu, niiombe sana Serikali ijenge kwa kiwango cha lami barabara kutoka Njia Panda kwenda Malampaka ili kurahisisha usafirishaji wa mizigo na barabara hii iambatane na taa za barabarani.

Mheshimiwa Spika, niombe sana na niungane na Wabunge wenzangu kuomba makusanyo ya *road fund* yaelekezwe kwenye ujenzi wa miundombinu ya barabara. Nimeona maoni ya Kamati ya Miundombinu kuwa Serikali ione namna ya kuongeza shilingi 100 kwenye miamala ya simu.

Mheshimiwa Spika, gharama za simu bado ni kubwa kwa mwananchi wa kawaida, hivyo kuweka ongezeko hili ni kumbebesha mwananchi mzigo, labda shilingi hii mia iwe kwenye *data* na sio kwenye muda wa maongezi. Ushauri wangu ongezeko hili liweke kwenye vinywaji ikiwemo bia, vinywaji vikali na kwenye sigara, kwani hivi sio *necessity* ni *luxury*.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Spika, Sera ya Ujenzi ya mwaka 2013 ilitambua ushiriki wa wanawake katika kazi za barabara na ni muda mrefu Wizara imekuwa ikiwezesha kufanyika kwa mafunzo kwa wakandarasi wanawake na wakandarasi wa madaraja ya *labour based* wamekuwa wakipata kazi ndogo ndogo.

Mheshimiwa Spika, matokeo makubwa ya wakandarasi wanawake kutekeleza barabara ya lami imetokea wakati huu ambao tuna Rais mwanamke. Tunaipongeza Serikali kwa kutenga miradi maalum inayotekelezwa na wakandarasi wanawake yenye thamani ya zaidi ya shilingi 40,000,000,000.

Mheshimiwa Spika, nitoe pongezi nyingi kwa *TANROADS* kwa kutenga na kusimamia miradi hii na kwa Katibu Mkuu - Ujenzi ambae kwa miaka mingi amekuwa akisaidia wakandarasi wanawake.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo sekta ya ujenzi ni sehemu ya sekta binafsi nchini inayochangia 12.5% katika pato la Taifa. Hali ya wakandarasi nchini wanaotekeleza miradi kwa sasa baada ya kupanda kwa bei ya mafuta ni hatarishi dhidi ya ukuaji wa sekta. Serikali itafute fedha za kuwa-*compensate* wakandarasi

kwa mujibu wa *conditions of contracts* za miradi. Uzuri sekta ilishatabiri hali hizi na kuelezwa vizuri kwenye mikataba.

Mheshimiwa Spika, Waziri atakapo-*wind up* aeleze mpango na mkakati wa Serikali kuwasaidia wakandarsi wa ndani wanaotekeleza miradi inayoendelea ili kuwanusuru dhidi ya kufilisika.

MHE. ALDONIS A. BITEGEKO: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na Serikali kwa ujumla kwa kazi kubwa na ya kihistoria iliyofanyika mpaka sasa ya ujenzi wa miundombinu inayosimamiwa na Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, ninashauri yafuatayo; kwanza kukamilisha mapitio ya Sera za Ujenzi na Usalama Barabarani. Serikali ikamilishe mapitio ya sera hizo na kuandaa mipango mikakati ya kuzitekeleza ili ziweze kuendana na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii yanayoendelea kutokea nchini na duniani ikiwa ni pamoja na kukidhi malengo ya Dira 2050.

Mheshimiwa Spika, pili, kuwalipa wakandarasi na wahandisi washauri; Serikali kupitia Wizara ya Fedha itafute fedha na kulipa madai ya wakandarasi na wahandisi washauri ili kuwezesha miradi ya barabara na vivuko kutekelezwa kwa wakati na kupunguza riba.

Mheshimiwa Spika, tatu, fedha za Mfuko wa Barabara ziingizwe moja kwa moja katika akaunti ya Mfuko wa Barabara *(RBF)* zilizopo Benki Kuu na zitumike tu katika ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Spika, Wizara kuleta fedha katika Mkoa wa Kagera zilizotengwa katika mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 kwa ajili ya ujenzi wa barabara. Nashauri Serikali ipeleke fedha katika bajeti za mwaka 2025/2026 katika Mkoa wa Kagera ili ujenzi wa barabara ufanyike. Barabara nyingi zimeathirika na mvua zilizonyesha.

Mheshimiwa Spika, uchache wa fedha zilizopo katika makadirio ya mpango na bajeti ya mwaka 2026/2027 kwa Mkoa wa Kagera. Fedha zilizotengwa takribani shilingi bilioni 14 ni chache kwa Mkoa wa Kagera kutokana uhitaji wa ukarabati wa barabara na madaraja na ujenzi wa barabara na madaraja. Serikali iangalie uwezekano kuongeza bajeti ya Mkoa wa Kagera ili iendane na mahitaji ya mtandao wa barabara wa Mkoa wa Kagera takribani kilometa 2156.

Mheshimiwa Spika, halmashauri zinunue na kutumie mitambo ya ujenzi wa barabara ili kupunguza gharama; na Serikali itoe kipaumbele katika kukamilisha miradi ya ujenzi na ukarabati barabara na madaraja badala ya kuanza miradi mipya.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Wabunge wengi kutoa ushauri unaohusiana na kutokuwepo kwa fedha za kutosha za ujenzi au ukarabati na barabara na madaraja ni vyema Serikali ikatoa kipaumbele na kufanya tathmini ya mfumo mzima wa upatikanaji wa fedha na ujenzi wa miundombinu hiyo ili tupate suluhisho la kudumu/muda mrefu ya changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Spika, kufanya pia ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Kata ya Nshamba mpaka Kata ya Mushabago katika Jimbo la Muleba Kaskazini na Kamachumu mpaka Hospitali ya Ndolage, Jimbo la Muleba Kaskazini, Wilaya ya Muleba.

Mheshimiwa Spika, vilevile, kufanya mapitio ya usanifu wa barabara ya lami ya Muhutwe-Kamachumu-Muleba kipande cha mteremko na kona ya Kyamalebe (kilichopo Kata ya Ibuga), Wilaya ya Muleba. Kipande hicho cha barabara kimekuwa na ajali ya nyingi za vyombo vya moto na watu kupoteza maisha.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Waziri wa Ujenzi atume timu ya wataalamu kufanya tathmini ya eneo na kufanya maamuzi ya kitaalamu.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

MHE. HAMOUD A. JUMAA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipatia nafasi hii kuchangia hotuba ya Waziri wa Ujenzi kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri ya kuandaa bajeti hii yenye dira ya kuendeleza miundombinu ya barabara nchini. Bajeti ya shilingi trilioni 2.47 ya maendeleo inaonesha dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuweka miundombinu kuwa *engine* ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa jitihada kubwa inazoendelea kuchukua kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi wa barabara maeneo mbalimbali nchini, aidha, pongezi kwa kuendelea kukarabati barabara zilizopo na za vijijini, kuhakikisha miundombinu hii inakuwa imara muda wote. Serikali kupitia Wizara wameendelea kujenga madaraja maeneo yote korofi, kukarabatiwa ama kujengwa upya ili kutatua changamoto. Miundombinu ya barabara ni sehemu ya ukuaji wa uchumi wetu, hivyo ni wajibu kuhakikisha inapitika muda wote katika hali nzuri. Mwelekeo mkuu wa bajeti ya Ujenzi ya mwaka 2026/2027 una mikakati mbalimbali mizuri yenye tija kwa Taifa letu hasa kwenye kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, barabara za kimkakati; kipaumbele kwa barabara za lami zinazounganisha mikoa na bandari, ikiwemo upanuzi wa Dar es Salaam - *Morogoro Highway* ni muhimu hasa ujenzi wa barabara njia 4/4 toka Kibaha Maili Moja hadi Chalinze.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matengenezo ya barabara za vijijini; *TARURA* iongeze fedha zaidi kwa matengenezo na ujenzi wa barabara za wilaya, vijijini na mitaani. Kwa upande wa madaraja na mifereji: fedha zilizotengwa kwa madaraja katika maeneo yanayokatika wakati wa mvua zitumike ipasavyo kuhakikisha wataalam wetu wanayatambua maeneo hayo kabla ya dharura kutokea na kusababisha madhara makubwa ya njia kufungwa.

Mheshimiwa Spika, tuhakikishe matumizi ya teknolojia kwa kuanzisha matumizi ya teknolojia ya "*cold mix*" *na* "*low-cost sealing*" kupunguza gharama za matengenezo ambazo zitasaidia kwa kiasi kikubwa Serikali kuipunguzia gharama.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla napenda kuzungumzia maeneo kadhaa ambayo Wizara inawajibu ya kuyazingatia kimkakati kwani maeneo hayo yana umuhimu kiuchumi kwa wananchi wangu, aidha, ni maeneo ambayo yana muda mrefu yamekuwa yakisahahulika ingawa nimeyasemea hapa Bungeni na Wizarani, maeneo hayo napenda kuyaelezea kama ifuatavyo; kwanza, naomba Wizara ielekeze fedha nyingi kwenye miradi mikubwa ya kimkakati. *Expressway* ya Kibaha – Mlandizi – Chalinze – Morogoro, upanuzi wa Kimara – Kibaha na Barabara ya Kisarawe – Mlandizi ni miradi ya kimkakati kwetu sisi Wana-Kibaha Vijijini.

Mheshimiwa Spika, miradi hii ikikamilika itapunguza gharama za usafirishaji na kuongeza ushindani wa bidhaa zetu sokoni. Pili, iendeleze utaratibu wa *PPP*. Kumpata mwekezaji wa sehemu ya Kibaha – Chalinze ni hatua sahihi ya kupunguza mzigo kwa Serikali na kuharakisha utekelezaji. Ninaomba Wizara ihakikishe mchakato huu unakamilika ndani ya mwaka huu wa fedha ili wananchi waone matokeo na kufaidika na mradi huu.

Mheshimiwa Spika, tatu, Serikali iendelee kutenga fedha kwa matengenezo kupitia Mfuko wa Barabara. Shilingi bilioni 1,047 kwa matengenezo ni muhimu kwa sababu barabara nzuri zinazoharibika haraka hazisaidii wananchi na kupelekea kudumaza uchumi.

Mheshimiwa Spika, sasa niruhusu nizungumzie Kibaha Vijijini. Kibaha Vijijini ni kitovu cha kilimo na biashara kati ya Dar es Salaam na Pwani, lakini kwa miaka mingi tumekuwa tukipata changamoto ya barabara zinazoharibika haraka na Daraja la Mto Ruvu linalokatika kila msimu wa mvua. Natoa shukrani kwa Wizara kwa kutambua umuhimu wa eneo hili kwenye hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, miradi ifuatayo ni habari njema kwa wananchi wangu; *Expressway* ya Kibaha – Mlandizi – Chalinze – Morogoro; shilingi bilioni 1.320 zimetengwa. Hii ni hatua kubwa ya kubadilisha uso wa Kibaha Vijijini. Ninaomba utaratibu wa ununuzi wa mwekezaji wa Kibaha – Chalinze ukamilike mapema ili ujenzi uanze ndani ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, pili, Barabara ya Kisarawe – Mlandizi kilometa 119; fedha zilizotengwa kwa maandalizi. Barabara hii itaunganisha wakulima wa Mlandizi, Kwala na Dutumi na soko la Pwani na Dar es Salaam. Niombe Wizara iharakishe usanifu ili ujenzi uanze mwaka huu wa fedha na kukamilika kwa wakati ili wananchi wangu waanze kufaidika na kukuza uchumi wao.

Mheshimiwa Spika, tatu; Kibaha – Kiluvya – Kisarawe kilometa 22; fedha zilizotengwa naomba ziende kwenye mradi kwa wakati. Hii itafungua kata za jirani kutokea Kibaha Vijijini na Kisarawe, kupunguza muda wa kusafiri.

Mheshimiwa Spika, nne, fedha zilizotengwa kwa mradi wa Makofia – Mlandizi kilometa 36.7: Hii itasaidia wananchi wa sehemu ya Kaskazini ya Wilaya kufika Mlandizi kwa urahisi na kusaidia wakulima kufikisha mazao yao kwa wakati. Naomba fedha hizi zilizotengwa kwenye miradi hii zifike kwa wakati na miradi hii ianze mwaka huu wa fedha ili wananchi wa Kibaha Vijijini washuhudie miradi hii ikianza kutekelezwa kwani ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Aidha, miradi ya Barabara ya Makofia, Mlandizi Mzenga takribani kilometa 102 na kwa umuhimu wake barabara hii itakwenda kuunganisha bandari itakayojengwa Bagamoyo na Bandari Kavu ya Kwala.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali ihakikishe miradi hii inakamilika kwa wakati kwenye mwaka huu wa fedha ili shughuli za kiuchumi kwa wananchi zianze mara moja na kuchangia pato kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, ingawa miradi hii ni mizuri, naomba nilete maombi matatu kwa niaba ya wananchi wa Kibaha Vijijini; moja, naomba Wizara iangalie upya Daraja la Mto Ruvu, Kijiji cha

Mlandizi, wananchi wangu wamechoka kukatika kila msimu wa mvua. Ikiwezekana mradi huu uingizwe kwenye bajeti ya dharura au *PPP* ili utekelezwe haraka.

Mheshimiwa Spika, mbili, naomba Wizara ihakikishe fedha za *TARURA* zinafika Kibaha Vijijini kwa wakati. Mwaka jana tulichelewa kupata awamu ya pili na miradi mingi haikukamilika. Wananchi wanataka kuona Barabara za Dutumi – Gwata, Mtongani – Soga na Kwala – Kijijini zinakamilika kwa wakati na kwa ubora.

Mheshimiwa Spika, tatu, ninaomba Wizara ianzishe utaratibu wa kudhibiti malori mazito yanayopakia mkaa na mchanga kwenye barabara za vijijini. Barabara zetu zinaharibika ndani ya miezi sita kwa sababu ya uzito kupita kiasi. Bila udhibiti huu, hata tukijenga leo, kesho tutarudi Bungeni kuomba fedha tena.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, naiunga mkono bajeti hii kwa 100%. Ni bajeti ya matumaini kwa Kibaha Vijijini na Tanzania kwa ujumla. Nawaomba Waziri na timu yake wakae karibu na Halmashauri ya Kibaha Vijijini ili kuhakikisha miradi hii inatekelezwa kwa ubora, kwa wakati na kwa gharama stahiki.

Mheshimiwa Spika, ahsanteni sana na Mungu ibariki Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

MHE. YANNICK I. NDOINYO: Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha mchango wangu kuhusu hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2026/2027, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, awali nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kwa juhudi zake na ujenzi mkubwa sana wa miundombinu za barabara, madaraja, usafiri wa anga na ardhini kwa kupitia *SGR*. Hata bajeti ya leo inadhihirisha dhamira njema

ya Mheshimiwa Rais ya kujenga barabara na madaraja nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, aidha nikupongeze Mheshimiwa Abdallah Ulega na timu nzima ya Wizara kwa utendaji bora na usio na mashaka ya kuwahudumia Watanzania. Pamoja na pongezi hizi, ninawaalika kutembelea Wilaya yangu hasa kujionea miundombinu na hali zake.

Mheshimiwa Spika, kupitia Wizara hii, naomba Serikali itenge fedha na kuanza ujenzi wa barabara ya lami kutoka Kigongoni/Mto wa Mbu hadi Wasso, Loliondo. Barabara hii ina umuhimu wa kipekee kwa wananchi wa Jimbo la Ngorongoro na Mkoa wa Arusha kwa ujumla, kwa kuwa ndiyo kiungo muhimu kinachoweza kufungua wilaya yetu kiuchumi, kijamii na kiutawala.

Mheshimiwa Spika, Ngorongoro (Loliondo) imebaki kuwa miongoni mwa maeneo machache na kwa mazingira ya Mkoa wa Arusha ni wilaya yenye uhitaji mkubwa ambayo bado haijaunganishwa kikamilifu na barabara ya lami kuelekea makao makuu ya mkoa. Hali hii imekuwa kikwazo kikubwa kwa wananchi, wafanyabiashara, wawekezaji, wakulima na wafugaji wanaotegemea barabara hii kwa usafiri, biashara na huduma mbalimbali za kijamii.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Kigongoni/Mto wa Mbu hadi Wasso, Loliondo, ni barabara ya kimkakati. Ujenzi wake utafungua fursa kubwa za uwekezaji katika sekta za utalii, mifugo, kilimo, biashara na huduma. Kwa sasa wawekezaji wengi wamekuwa wakilalamikia changamoto ya ubovu wa miundombinu na ugumu wa kufika Loliondo, jambo linalopunguza kasi ya uwekezaji na maendeleo katika eneo hili lenye fursa nyingi za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, barabara hii pia ina umuhimu mkubwa kijamii na kikanda. Itawezesha wananchi wa Loliondo, Sale, Ngorongoro, maeneo ya Kanda ya Ziwa, pamoja na wananchi kutoka nchi jirani ya Kenya, kufika Arusha na Dodoma kwa urahisi zaidi. Aidha, itasaidia wakulima na wafugaji kusafirisha mazao,

mifugo na bidhaa nyingine kwenda masokoni kwa gharama nafuu, kwa haraka na kwa usalama zaidi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kusisitiza kuwa barabara hii siyo ombi jipya, tayari Serikali ilishafanya tathmini na kuanza utekelezaji kwa kujenga kipande cha Wasso hadi Sale chenye urefu wa kilometa 49. Hivyo, ombi letu kwa Serikali ni kuendeleza hatua iliyokwishakuanza kwa kukamilisha ujenzi wa barabara hii muhimu hadi Kigongoni/Mto wa Mbu.

Mheshimiwa Spika, tarehe 3 Oktoba, nilipata nafasi ya kumweleza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu umuhimu wa barabara hii kwa wananchi wa Ngorongoro. Kwa heshima kubwa, naiomba Serikali sasa ichukue hatua mahsusi ya kuiweka barabara hii katika vipaumbele vya utekelezaji ili wananchi wa Ngorongoro waweze kufurahia matunda ya ukuaji wa kasi wa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara hii utakuwa siyo tu utekelezaji wa ahadi ya maendeleo, bali pia ni hatua muhimu ya kuunganisha wananchi, kupunguza gharama za maisha, kukuza uchumi wa ndani, kuongeza mapato ya Serikali na kuimarisha usalama wa kijamii na kiuchumi katika ukanda huu wa kimkakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, ninaomba kuwasilisha mchango wangu na ninaunga mkono hoja.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Spika, ninayo heshima kubwa ya kumpongeza sana Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anazoendelea kuzifanya katika kujenga miundombinu ya barabara na madaraja. Kipekee nimpongeze sana kwa uamuzi wake wa kuwapatia kazi wakandarasi wanawake ili kujenga Barabara ya Luanda Nyimbili kilometa 20 katika Wilaya ya Mbozi na Mkoa wa Songwe. Wakandarasi hawa wamefanya kazi kubwa na wanaendelea kufanya kazi nzuri sana katika ujenzi wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kilometa 20 kwa wakandarsi 12 *(joint venture)* ni chache sana. Lengo ni kuwajengea uwezo wa

kiuchumi na uwezo wa kujenga barabara. Hivyo ni muhimu Serikali ikaona uwezekano wa kuwaongezea eneo la kilometa 40 ili kila mkandarasi awe amejenga angalau kilometa tano. Chini ya kilometa tano wanaweze wasipate faida na kujenga uwezo wa kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wanafanyakazi nzuri ni vizuri wakaongezewa kilometa zaidi kwani wameonesha uwezo mkubwa sana wa kazi na kwa viwango vya kimataifa. Wanawake wanaweza. Hongera sana Mheshimiwa Rais na Waziri wa Ujenzi kwa kazi kubwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuwavutia wakandarasi hawa wanawake ni muhimu mkatoa motisha kuwa mkandarasi atayekuwa wa kwanza kumaliza kazi kwa viwango vinavyokubalika basi atapewa kilometa 20 zaidi ili aendelee na kazi.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Waziri naomba Serikali iangalie uwezekano wa kuanza ujenzi wa mizani pale Iboya ili kupunguza foleni ya pale Tunduma na kuwafanya wafanyabiashara kutumia muda mfupi zaidi ili kupunguza gharama za uendeshaji wa biashara.

SPIKA: Sasa namwita Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninaanza kwanza kwa kutoa shukrani zangu nyingi sana kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini katika nafasi hii ya Unaibu Waziri wa Ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatoa pia pongezi na shukurani nyingi sana kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa sana, ambayo ameifanya katika Nchi ya Tanzania, hasa sekta ya miundombinu. Tukumbuke tu kwamba, ametambuliwa kuwa, ni kati ya Marais bora katika Afrika ambao wamefanya kazi kubwa sana kwenye sekta ya miundombinu, hususan barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru sana wananchi wa Ileje kwa kuendelea kuniamini. Ninaishukuru familia yangu, ambayo inanipa ushirikiano mkubwa sana kuweza kutimiza majukumu yangu hapa, kama Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru wewe, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kazi kubwa ambayo mnaifanya, kuliongoza Bunge hili kwa kweli, kwa umahiri mkubwa, lenye viwango vya Kimataifa. Hongera sana Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru Kamati yangu ya Miundombinu chini ya Mheshimiwa Selemani Kakoso kwa miongozo mbalimbali, ambayo anaitoa. Ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge, ambao hakika lazima tukiri wametoa michango bora, yenye tija na ninasema tumeichukua yote na tutaifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, ninamwachia Mheshimiwa Waziri wangu aweze kuongea, lakini ninasema neno moja tu; mwaka huu tuna Mashindano ya *AFCON*. Moja ya eneo ambalo tunategemea kulifanyia kazi kubwa sana ni katika Mji wa Arusha.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa fedha kuanza kujenga miundombinu na hasa barabara, pale Mjini Arusha. Tunavyoongea mkandarasi ameanza kazi za *mobilization* kujenga; kwa watu wanaojua pale Arusha, kuanzia Mbauda, pale kwa Mrombo hadi Losiyani ambapo tayari, ataunganisha na ile Barabara ya Afrika Mashariki, njia nne.

Mheshimiwa Spika, pale *Tea Packers,* pale Moshono, kwenda Losiyani kuunganisha ile Barabara ya Afrika Mashariki. Pia, tunavyoongea tayari wametoa fedha, kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Barabara ya kutoka *Airport,* pale Kisongo kwenda Soko la Kilombero na kutoka Barabara ya *Airport* hadi *Technical College,* pale *TCA,* kwa njia nne. Hizo ndiyo barabara ambazo tunazijenga sisi *TANROADS,* zitakuwa zinaingiza watu katika uwanja ule wa Arusha. Pia, maelekezo yametolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu Barabara ya Tengeru kwenda Mererani ikiwa ni sehemu ya

bypass, ambayo sisi kazi tunayoifanyia hiyo barabara ni namna ya kuijenga kwa uharaka.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais, ametoa fedha nyingi sana na tulichojifunza ni kwamba, unaweza ukawa na fedha, ukajenga barabara moja ndefu sana ya lami, lakini pengine isiwe na tija kuliko ukaainisha maeneo ambayo ndiyo vikwazo vya barabara, kama alichofanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ametoa zaidi ya shilingi 800,000,000,000 kuainisha madaraja ambayo yalikuwa yanakwamisha na leo watu wanapita, kwa hiyo, tumepata somo kubwa sana. Ninawahakikishia Waheshimiwa Wabunge tayari iko mipango, ataelezea Mheshimiwa Waziri, kuunganisha mikoa yote ambayo hawa Wabunge wameisema.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, ninaomba nimwachie Mheshimiwa Waziri wangu, aweze kufafanua na kujibu hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge, wamezitoa. Ninaomba kuunga mkono kwa asilimia mia moja hotuba hii ya bajeti, lakini pia na hii Bajeti yetu ya Ujenzi. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mtoa hoja.

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi hii. Ninaomba niitumie fursa hii pia, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kufika katika hatua hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza ninashukuru sana kwa michango mingi sana iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kwa hakika tumepokea michango ya mazungumzo 95 na vilevile michango ya maandishi rasmi takribani mitano, iliyokwenda kwenye mfumo na bado kuna michango ya maandishi zaidi ya 10 kwa hivyo, unaweza ukaona namna ambavyo hoja yetu imepata wachangiaji wengi zaidi. Ninawashukuru sana kwa unyenyekevu mkubwa Waheshimiwa Wabunge na hilo ni deni la utumishi kwangu mimi na timu yangu. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Spika, katika jambo ambalo Wabunge wote wamelichangia humu kwa hakika ni juu ya kazi kubwa na nzuri

iliyofanywa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ni rekodi ya namna ya kipekee, ambayo ndani ya uongozi wake wa miaka mitano amekamilisha Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi, malengo na dira iliyowekwa na Serikali; Rais Samia amei-*champion* na ameonesha ya kuwa, yeye yupo tayari katika kuhakikisha anaipeleka nchi yetu mahali pazuri na pakubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuonesha ushahidi wa jambo hili katika miaka hii minne, mitano, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, pamoja na yote aliyoyafanya kwenye madaraja, pamoja na kilometa zaidi ya 1,400 za lami zilizojengwa nchi nzima, lakini utaona kwamba, tayari amesaini mikataba takribani 80 yenye thamani ya takribani shilingi 6,000,000,000,000, ambayo ipo kwenye *pipeline*. Hii ni *commitment* ya hali ya juu kabisa, ambayo ameonesha ni nini anakusudia na ni wapi anataka kulifikisha Taifa letu. Ndiyo maana nimekubaliana na hoja ya Kamati na ninakubaliana na hoja za Wabunge wote ya kwamba, tujikite katika kuhakikisha viporo vyote na miradi yote iliyosainiwa ni muhimu na ni lazima tuendelee nayo kwa nguvu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wachangiaji wengi wamezungumzia juu ya barabara kuu na ubovu wa barabara hizi. Ninawashukuru wote kwa ujumla, wapo waliosisitiza sana, hususan barabara kama vile ya Kusini. Ninawatoa hofu Waheshimiwa Wabunge na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wa kule Kusini, wakiongozwa na mtoa hoja namba mbili, kaka yangu, Mheshimiwa Nape, wala yeye asishike shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, ukweli ni kwamba, katika bajeti yetu ukisoma kitabu cha randama imeeleza wazi ukurasa namba 200, ukurasa namba 213, ukurasa namba 214, tumeeleza tutakavyokwenda kujenga vile vipande kutoka Mkuranga mpaka Kongowe, kutoka Ikwiriri mpaka Nyamwage mpaka Somanga, kutoka Somanga mpaka Nangurukuru na kutoka Nangurukuru mpaka Mbwemkuru, imeelezwa wazi katika bajeti ile. Vilevile, nimeshukuru kwamba, Waheshimiwa Wabunge wa eneo hili wameeleza kwa kina sana juu ya madaraja makubwa na mazuri yaliyojengwa katika maeneo yale.

Mheshimiwa Spika, ikaelezwa juu ya ile Barabara ya Mzunguko kutoka Mnazi Mmoja – Mingoyo mpaka Masasi. Masasi – Newala – Tandahimba mpaka Mtwara Vijijini na kurudi tena hapa Masasi. Pale Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeweka jumla ya fedha zaidi ya shilingi 600,000,000,000 zipo eneo lile peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, habari iliyo njema zaidi ni vijiji 30 vya kutoka pale Mnazi Mmoja kwenda Masasi, ambavyo takribani kilometa 70 zinapita katika Jimbo la Mtama peke yake, vyote vitawekewa taa. Eneo lile lina taa zaidi ya 3,000 kwa hivyo, ninaomba kwa heshima kubwa na taadhima hakutakuwa na sababu. Ninaomba kabisa ya kwamba, hii shilingi isishikwe kwa sababu, ikishikwa inaweza kusababisha pia, vilevile mradi ule usiendelee kule kwa hivyo, kwa heshima kubwa na tahadhima isishikwe hii shilingi, ili tuendelee kujenga nchi yetu katika eneo lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia, nieleze juu ya shukrani nyingi zimesemwa hapa kwa Mheshimiwa Rais. Mama yangu Mheshimiwa Salma Kikwete, Mheshimiwa Chikota, Mheshimiwa Zainab Kawawa, Mheshimiwa Nawanda, Mheshimiwa Katani na Mheshimiwa Mapalilo; wote wa barabara hiyo, wote wamezungumza vizuri na kumsifu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia, kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya.

Mheshimiwa Spika, hiyo pia, inaenda sambamba na zile barabara kuu nyingine. Kwa mfano Barabara ya kutoka Singida – Babati, dada yangu Mheshimiwa Asia Halamga ameizungumza vizuri na Mbunge wa Babati Mjini. Ninataka niseme, hii ni katika zile tulizoziweka kwenye mkakati wetu kwamba, tunakwenda kushughulika nazo, tena ni maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi, haturudi nyuma tunakwenda mbele. Hatuzungumzi juu ya *single carriage,* barabara moja ambayo magari yanapishana namna hii, barabara ni mbili, ilani imeelekeza, ni *dual carriage* na tunakwenda kufanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge pale waliposisitiza juu ya fedha za Mfuko wa Barabara. Mimi ninawasisitiza na kuwaomba sana kwamba, sisi katika Serikali tumejipanga vyema kutumia fedha hizo na tutakuwa na ile Hati Fungani, ambayo ninawahakikishia Wabunge wasiwasi wao na maoni yao, Serikali kwa upande wa Wizara ya Ujenzi na mwenzangu wa Wizara ya Fedha, tumeyachukua. Hatutafanya mchezo na fedha hizi hata kidogo na kwamba, labda hizi fedha zitatumika vibaya pindi mambo yatakapokuwa yameiva, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawapa *commitment*, ikiwa jambo hili limefanikiwa, litakwenda kufanya vizuri. Tunataka tufike mahali barabara hizi, ambazo ni za kiuchumi na zimechangiwa na Wabunge wengi humu, zitufikishe mahali zijengwe katika utaratibu ulio mzuri, ulio bora na tutoke kwenye kuzizungumza tena baada ya miaka michache ijayo. Tunataka miaka michache ijayo tuwe na mazungumzo haya ya akina baba Levo, ya kuwaombea watu wa Kigoma *flyovers*.

Mheshimiwa Spika, ninataka tufike mahali tusizungumze tena kukarabati. Tufike mahali kwamba, Mheshimiwa Musukuma akija humu Bungeni asizungumze mambo ya Barabara ya Nkome – Nzala, aje kuwaombea watu wa Geita *flyovers*, ndiyo tunataka tufike huko. Kwa hivyo, ninawaomba kwa heshima kubwa na taadhima watuamini na watuunge mkono. Ninawaomba kwa heshima kubwa na taadhima wasishike shilingi, tumejipanga, tunakwenda kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia kwa sababu, hoja ni nyingi sana, watu 100 kusema mmoja baada ya mwingine, ni lazima nikubali, na kwa ufinyu wa muda Wabunge waridhike kwamba, Serikali imejipanga vyema. Nimefurahi kwamba, katika mazungumzo makubwa na mazuri yaliyotokea hapa nimekaribishwa sehemu nyingi mara baada ya kusema kuwa, tutakapofunga Bunge na kwa kuwa, hela zimekwenda, Wabunge wamenikaribisha tupite majimboni.

Mheshimiwa Spika, mmoja katika Wabunge, aliyetia fora, amenialika niende jimboni, ni mtani wangu yule Mbunge wa Kahama, Mheshimiwa Benjamin Lukubha. Yeye kanipa na ofa, anasema uje Kahama, sisi tunataka uje kuiona Barabara ya Kakola na barabara nyingine, lakini tutakupa na jiko uongeze. Sasa ukipewa jiko na Wasukuma unakataa vipi?

Mheshimiwa Spika, hilo nimeliunga mkono, ninakuja huko na tutakwenda katika maeneo mengine pia. Tutahakikisha kwamba, tunakwenda kufanya kazi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa na taahadhima ninaomba Waheshimiwa Wabunge watuamini, watutume kazi. Tumejipanga, tunakwenda kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema haya, ninaomba kutoa hoja na ninaomba watuunge mkono kwa heshima kubwa na taadhima. Ahsante sana. *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Hoja imeungwa mkono.

Katibu.

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae.

Katibu.

NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:

KITABU CHA PILI

MATUMIZI YA KAWAIDA

FUNGU 98 - WIZARA YA UJENZI

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*……Sh. 2,545,368,220

MWENYEKITI: Waheshimiwa, kifungu hiki kina Mshahara wa Waziri na nina Wabunge kama watano. Tutaanza na Mheshimiwa Nape.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ninaanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri, yeye na watu wake, namna walivyofanya kubeba hizi hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninahitaji uthibitisho kutoka kwake na kwa kweli, nimetamka toka mwanzo sina mpango wa kushika shilingi. Uthibitisho mmoja ambao ninauhitaji kutoka kwake ni, baada ya Serikali kukubali kujenga hizi barabara na hasa hizi ambazo zimepigiwa makelele hapa, ikiwemo hii ya Lindi – Mtwara – Dar es Salaam na hii ya Singida – Dodoma na nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza huu mpango ambao zitajengwa kupitia Hati Fungani, tumekuwa na uzoefu wa jitihada za namna hii ambazo zimefanyika huko nyuma na zikashindwa. Ninachohitaji ni uthibitisho wa Wizara kwamba, mpango huu mpya wa Hati Fungani hautakwama kama zilivyokwama zile nyingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, nikipata sina matatizo na Mheshimiwa Waziri. Tunataka akatekeleze kazi ambayo tumempa, Wabunge, kuifanya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii na ninamshukuru sana ndugu yangu, kaka yangu, Mheshimiwa Nape. Ni kwamba, kwanza ukirejea kitabu chetu cha bajeti, Barabara ya Kusini imetamkwa vyema, ukurasa wa 200, 213 na 214, vipande vyote vile vimeelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mfano bora kwa wenzetu wa Kenya wametumia *infrastructure bond*, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge hii *infrastructure bond* tunayoizungumza hapa ya uhakika, sisi makusudio yetu mara baada ya kuwa tume-*ringfence* vyema fedha za Mfuko wa Barabara, kwa hivyo Mfuko utakuwa na uhakika wa hela, hapo matarajio yetu tutanguliza kuzichukua zile fedha. Barabara tutakazoanza nazo ni barabara kuu za kiuchumi kwa malengo na dhamira ya kwamba tuweze kumalizana nazo ili tuweze kupata fedha zaidi kupitia bandari na mizigo inayopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo nimhakikishie…

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ninaongeza muda mpaka tutakapomaliza kazi yetu.

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa hivyo, ninataka nimhakikishie tu kwamba tumejipanga vema, Waziri wa Fedha yuko hapa ameli-*champion* vizuri sana jambo hili na wataalam wetu kule Wizara ya Fedha liko vizuri, hili tunawahakikishia Waheshimiwa Wabunge.

MWENYEKITI: Ahsante. Kwa mujibu wa Kanuni Mheshimiwa Nape umesharidhika kwa sababu hukutaka kushika shilingi. Mheshimiwa Asia Halamga.

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri na nimeridhishwa na nimeridhika na maelezo yake, hivyo kazi iendelee. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Joseph Kasheku.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Ninataka kupata maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu tunao mpango wa muda mrefu wa hati fungani, lakini kutokana na ubovu wa barabara uliopo, ninataka kupata *commitment* ya Serikali kwamba zile fedha za *Road Fund* zinapelekwa lini angalau kuanza kuziba haya mashimo yaliyopo ambayo ni hatari kwa barabara zetu na wasafirishaji.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru tena kwa mara nyingine. Jana wakati niliposimama hapa kutoa hoja nililieleza Bunge kwamba tunamshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumepata fedha. Kwa namna ya kipekee niwashukuru sana watendaji na viongozi wote wa Wizara ya Fedha wakiongozwa na kaka yangu Balozi Khamis Mussa, siyo pekee yetu *TANROADS*, amepeleka pia fedha shilingi 20,000,000,000 upande wa TAMISEMI na *TARURA* kwa malengo ya kuweza kwenda kurekebisha barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kwamba ni lini tutaanza kuzipata hizo fedha imekwishaanza na tunakwenda kwa ajili ya kurekebisha mashimo yote nchi nzima na kusafisha zile za udongo na changarawe zilizoombwa na rafiki yangu Mheshimiwa Isack Copriano Mbunge wa Monduli kwamba angalau ziweze kupitika, au kwa mfano barabara moja kutoka Mabwekeni kule Tanga kwenda Korogwe imeharibika sana na Wabunge wa eneo lile la Tanga wote walilalamika. Watawaona wakandarasi wako huko wakifanya kazi ya kurekebisha ili kuwarahisishia wananchi usafiri na usafirishaji. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ulenge.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza niseme sikusudii kabisa kushika shilingi ya shemeji yangu, ninaiamini hii sekta imenikuza na kunilea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tu nipate ufafanuzi, kama ambavyo niligusia katika mchango wangu, sekta ya ujenzi inachangia kwa takriban 12.5% katika pato la Taifa. Wakandarasi wa Taifa hili ni watu muhimu kwa kuongeza ajira kama *private sector,* kwa mujibu wa dira tunahitaji waweze ku-*contribute* kwenye ile 70% iliyosemwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kupata ufafanuzi wa Serikali kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kuhusiana na sakata zima la mafuta namna ambavyo linaiathiri sekta hii na wakandarasi ambao wanaendelea na ujenzi sasa hivi. Ni ipi *commitment* ya Serikali kutafuta fedha ili kuendana na *conditions of contract* kama zilivyoelezwa katika *FIDIC* na katika mkataba wetu wa ndani kupitia *PPRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tu ufafanuzi kuhusu hilo namna ambavyo wataweza kuwa-*compensate* na kufanya *price adjustment* kwa mujibu wa *conditions of contract* ili sekta hii isiathirike na wakandarasi wa Taifa hili wasife. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba Mheshimiwa *Engineer* Ulenge amekuja na jambo *very technical* kwa sababu amezungumzia juu ya *price adjustments* na vitu vya namna hiyo, niseme tu amegusia namna ambavyo bei ya mafuta inaathiri na kwa hivyo hata *cement*, hata *bitumen* zote zinaathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu kwamba tumeichukua hiyo hoja sisi na wenzangu katika Wizara na hata wenzetu wa Wizara ya Fedha tutaifanyia kazi, kwa sababu tunaelewa mazingatio yake hapa ni kutaka kuona moja, wakandarasi hawaathiriki. Mbili, makusudio yake ni kwamba isije gharama za ujenzi wa barabara zikachumpa, zikaenda juu sana. Jambo hili tumelichukua na tunalichukua kama ni *homework*, tunakwenda kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba hata shilingi asiishike wala kuichukua. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Edwin Swalle.

MHE. EDWIN E. SWALLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi ambayo umenipa. Nami sikusudii kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu wahenga walitufundisha kwamba asiyeshukuru kwa yai hata ukimpa jogoo mzima hawezi kushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo moja tu ninataka ufafanuzi. Kumekuwa na sera ya Serikali ya muda mrefu ya kutoa kipaumbele kwenye ujenzi wa barabara za kuunganisha mikoa na mikoa. Ziko barabara nyingi hapa nchini ambazo Wabunge wengi tumesema ndani ya Bunge hazijaanza kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko Barabara ya Kongwa kwenda Kiteto Mkoa wa Manyara, ziko Barabara za Isyonje kule Makete kwenda Mbeya, ikiwemo na Barabara ya Kibena kwa maana ya Mkoa wa Njombe kwenda Mkoa wa Morogoro. Ninaomba *commitment* ya Serikali, mwaka jana Mheshimiwa Rais kwa mapenzi mema ya wananchi wa Lupembe ametangaza tenda ya Barabara ya Kibena kwenda Madeke, kilometa 42, lakini mpaka leo hii tenda hii haijasainiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba *commitment* ya Serikali tenda hii inasainiwa lini wananchi wangu wapate barabara ya lami. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Swalle, Mbunge wa Njombe. Ninamshukuru sana pale aliposhukuru, Mbunge wa Lupembe Mkoani Njombe na hii shukrani si ya bure. Kwa mfano, leo asubuhi kulitokea jambo hapa mchana huu ya kwamba barabara kule Njombe haina hata kilometa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba pale Njombe siyo kilometa moja, hiyo barabara iliyosemwa ya Itonyi - Lusitu ina takribani kilometa 50, katika hizo 50 zote tumeweka *rigid pavement* ya zege barabara nzima. Kwa hivyo hii shukrani ya watu wa Njombe ni halisi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo la kusaini huo mradi lisimnyime Mbunge usingizi, anayesaini mradi baada ya kupata kibali kwa Mheshimiwa Rais ni Waziri. Hilo ninakwenda kumalizana nalo rafiki yangu Swalle. Ahsante sana.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Katibu, *guillotine!*

NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:

Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*……Sh. 2,545,368,220
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……..Sh. 846,802,899
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*……Sh. 628,270,890
Kifungu 1004 – Government *Communication Unit*……..Sh. 283,708,850
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*…….Sh. 338,057,960
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*……Sh. 325,344,066
Kifungu 1007 – *Legal Services Unit*……..……Sh. 317,029,350
Kifungu 1008 – *Information & Communication Technology Unit*……Sh. 246,615,083
Kifungu 1009 – Monitoring *and Evaluation Unit*……Sh. 5,891,069,458
Kifungu 2002 – *Technical Services Division*…….Sh. 31,338,781,033
Kifungu 2005 – *Roads Division*……..…Sh. 90,628,157,859
Kifungu 5002 – *Safety and Environment Unit*……..Sh. 545,548,983
Kifungu 6001 – *Airport Construction Unit*……..Sh. 40,158,700

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya

Matumizi bila mabadiliko yoyote)

KITABU CHA NNE

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 98 - Wizara ya Ujenzi

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*……..Sh. 246,371,400
Kifungu 2002 – *Technical Services Division*……..….Sh. 53,105,214,000
Kifungu 2005 – *Roads Division*……Sh. 2,292,729,939,496
Kifungu 5002 – *Safety and Environment Unit*……...Sh. 1,370,147,000
Kifungu 6001 – *Airport Construction Unit*……..……..Sh. 119,884,807,104

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge Linarejea.

(Bunge Lilirejea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae. Mtoa hoja.

TAARIFA

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi yake, hivyo ninaomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niwahoji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Waheshimiwa Wabunge, walioafiki wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Yalipitishwa na Bunge)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, leo mpaka Mheshimiwa Ado kasema ndiyo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri hongera sana, pamoja na kuwa nimekaa hapa ile harufu ya ubani ninaipata mpaka hapa, ninaona umejifukiza sana leo, lakini kwa kweli mnafanya kazi nzuri sana wewe na Naibu Waziri wako na siyo peke yenu ni pamoja na Katibu Mkuu, *TANROADS* na wataalam wote ambao wanashirikiana na wewe. *(Kicheko/Makofi)*

Ninawashukuru Wabunge, mmewatimizia haki wananchi wenu kwa kuwasemea ndani ya Bunge na Bunge ndivyo linavyotakiwa liwe hivyo. Watu walifikiri Bunge labda Chama kimoja cha CCM wapo wengi, basi mambo yatakuwa yanateleza tu. Mambo yamekwenda kwa uhalisia, kwa hoja na Serikali imejibu kwa hoja, Wabunge mmeridhika na wananchi wameridhika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa ninapitia miradi ya kusini, shilingi 600,000,000,000 zilizotengwa na Serikali na Mkandarasi yupo *site*, madaraja yaliyojengwa, Waziri Mkuu ukienda na mimi nitakwenda kwa sababu hiyo njia ya Muhoro kule ndiyo kwetu.

Kwa hiyo Mheshimiwa Nape mambo yako yanakwenda vizuri na una wajibu, simama hivyo hivyo. Una wajibu wa kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu kazi aliyoifanya Rais Kusini ni ya kupongeza, sasa ushike *mic* umshukuru hapa.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Mtama, wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara, ninakushukuru kwa kunipa heshima ya kipekee ili nisimame hapa niishukuru sana Serikali sikivu ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kusikia na kuwa wasikivu wametutendea mema sana watu wa Kusini. Vilio vyetu kuanzia korosho, gesi, bandari ya uvuvi, miradi mbalimbali kwenye elimu na afya na leo tumehitimisha kwa kuhakikishiwa kwamba Barabara yetu ya Dar es Salaam – Lindi - Mtwara itajengwa kwa kiwango cha kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, nimesimama kumshukuru Rais, kuishukuru Serikali yake, kumshukuru mdogo wangu Mheshimiwa Ulega, pia ninakushukuru sana wewe pia kwa namna unavyoliongoza Bunge.

SPIKA: Basi sijakwambia utoe hotuba. *(Kicheko)*

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri bado hamna *appetite* ya *PPP*, bila *PPP* mzigo huu wa barabara ni mkubwa mno. Nchi zote watu wanaingia ubia Serikali na *private sector* na barabara inalipiwa *toll* nchi zote.

Mheshimiwa Waziri ninakuomba sana mzigo huu ni mkubwa sana, mahitaji bado ni makubwa sana, jaribuni sasa kuwa na *appetite* na kwenye *Vision 2050, 70%* ya miradi hii itafanywa na *private sector.* Bado hatuoni ile ari, sijui kwa nini mnang'ang'ania kufanya ninyi wenyewe, labda kuna kitu mtatuambia kuna nini huko. *Highways* zote ni road *toll*, wenzetu wamefanya miaka 20 iliyopita na sisi tuanze kuingia katika eneo hili.

Ubora wa barabara na gharama lazima mzitazame upya, tazameni Barabara ya Kibamba – Kibaha – Chalinze - Morogoro. Chalinze - Morogoro ni barabara ya zaidi ya miaka 15 sasa lakini bado safi kabisa. Jaribuni kutazama *where you are going wrong* na tutafuatilia. Kamati ya Miundombinu lazima ifuatilie ubora wa barabara kwa sababu hizi ni pesa za umma na ni lazima ziwe na uhakika.

Waheshimiwa Wabunge, sheria au kanuni ya kumlipa mkandarasi pesa za ziada kama *penalty* Serikali ikichelewa kumlipa muipitie tena upya, hiki kitu kinaitia hasara sana Serikalini na cha ajabu anayelipwa ni mkandarasi, Serikali hailipwi! Mimi sijawahi sikia hata siku moja Serikali inalipwa pesa. Fanyeni m-*revisit* hiki kitu ili kupunguza gharama na mzigo huu kwa Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno hayo, nimepata taarifa, fainali huko mambo yanakwenda vizuri. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

(Saa 7.54 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 22 Mei, 2026 Saa Tatu Asubuhi)